**27 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 27 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Salim Mussa Omar.

Na. 417

### Kima cha Chini cha Mshahara kwa Wafanyakazi wa Nyumbani

**MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kutengeneza Kanuni zitakazoweka kima cha chini cha mishahara ya Wafanyakazi wa Majumbani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Gando kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wafanyakazi wa nyumbani na hivyo imeendelea kuweka kanuni tajwa mwaka 2022. Kupitia Tangazo la Kima cha Chini cha Mshahara Na. 687, Serikali iliweka kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi ikiwemo sekta ya wafanyakazi wa nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria, tangazo hili linadumu kwa miaka mitatu, na hivyo kwa sasa Serikali kupitia Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara kwa Sekta Binafsi inaendelea kukamilisha utafiti wa kima kipya cha chini cha mshahara ambacho pia kitajumuisha sekta ya wafanyakazi wa nyumbani. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salim.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali yenye kutia matumaini. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba wafanyakazi wa ndani wanaendelea kunyanyasika sana kwa asilimia kubwa. Wafanyakazi hawa unakuta wanafanya kazi usiku, mchana, mwezi mzima na kiwango anacholipwa hakiridhishi, inafikia mahali mtu ambaye ana mfanyakazi huyo ana kipato zaidi ya shilingi milioni 20 kwa mwezi, lakini mfanyakazi huyo anapokea siyo zaidi ya shilingi 60,000. Huu siyo utu, hii ni biashara ya utumwa ambayo imekwishapitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako ninaomba sasa Serikali iangalie hili jambo *serious*, kwa sababu unyanyasaji unaoendelea nyumbani ni mkubwa sana na ndugu zetu wanaumia sana. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Mussa Omar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali hilo zuri na kuonesha kujali, hasa

kwenye manyanyaso ambayo yanafanyika kwa wafanyakazi wa ndani. Hata hivyo Serikali yetu imekuwa na sheria, ukiacha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzani, kuhusiana na haki na usawa wa kazi kwa mujibu wa Ibara ya 23, lakini pia kuzuia unyanyasaji na ubaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 12 na 13 ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, tunayo Sheria ya Kazi, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, ambayo inatoa mwongozo wa namna gani kazi ziwe za staha na pia kuwe na sehemu ya afya na usalama mahali pa kazi, kwa maana ya misingi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, kwanza kwenye eneo la malipo tunayo amri ya kima cha chini cha mshahara ambayo tuliitunga na kuitoa mwaka 2022 na pia sambamba nayo tuna utaratibu sasa ambao tumeanza kwenye hatua ya kusaini na ku-*ratify convention* Na. 189 ambao ni Mkataba wa Kimataifa, ambao utazungumzia kuhusiana na uwepo wa haki za wafanyakazi wa nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya haki zinazoangaliwa ni pamoja na masaa ya kazi, kuwa na mikataba ya kazi na pia kuhakikisha kwa wakati wote wanapata haki na stahiki zao na malipo yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya unyanyasaji yamekuwa yakijitokeza; wapo wafanyakazi wa ndani ambao wanapewa ujauzito na kufukuzwa, wapo wanaonyimwa chakula, na pia wapo wanaofanya kazi masaa yote. Hayo yote tumekuwa tukiyaangalia na kuyazingatia kwa kutumia Sheria yetu ya Kanuni za Adhabu Sura Namba 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua hii ya kwenda kufunga mkataba huu kupitia Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mheshimiwa Gwajima, pia nikitambua kazi kubwa inayofanywa na Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama cha Mapinduzi, kupitia Mheshimiwa Mama Chatanda na Wabunge Wanawake, wamekuwa *pioneers* wa kupigania haki za wafanyakazi wa nyumbani, wa kike na kiume, ni ili kuweza

kuhakikisha haki zao na stahiki zao wanazipata kwa mujibu wa sheria. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua haki za wafanyakazi hawa, siyo mishahara pekee, bali ni pamoja na haki nyinginezo, ikiwemo likizo, matibabu na kadhalika. Je, ni kwa kiasi gani Serikali inahakikisha kwamba haki hizi inazisimamia na kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanazipata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika haki ambazo nilizitaja hapo awali, zitakuwa ni haki ambatano za kimkataba wa Kimataifa, lakini pia na *domestic laws,* kwa maana ya sheria zetu za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya stahiki za haki hizi za wafanyakazi wa ndani, watakuwa na haki sawa kama wafanyakazi wengine tu kwenye sekta mbalimbali. Zitaangalia masuala pia hata ya umri wa kufanya kazi, masaa ya kufanya kazi, mazingira ya kufanya kazi na pia masuala ya likizo, ikiwa ni pamoja na matibabu, na kuchangiwa fedha zao kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, itakuwa ni haki ambatano ambazo zitakuwa tumezifanya na hasa tukishaingia katika mchakato huu wa kusaini na ku-*ratify* Mkataba wa Kimataifa Na. 189 na kuweza kubadilisha sheria zetu za ndani ili kuweza kuhakikisha kwamba tunasimamia kikamilifu haki zao. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magige, jiandae Mheshimiwa Neema.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Pamoja na kwamba viongozi wetu wa UWT Taifa

wakiongozwa na mama Mary Chatanda wamekuwa mstari wa mbele kupinga ukatili dhidi ya wanawake, watoto na hata wanaume, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha ukatili huu wa wasaidizi wa ndani unakoma kabisa, kwa sababu kuna wengine wanabakwa, wananyimwa chakula na hata kupigwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Catherine Magige, kwamba ni kweli mazingira hayo yamekuwa yakijitokeza katika nyakati tofauti, lakini tumeendelea kama Serikali kuchukua hatua kupitia sheria ya kanuni za adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa yoyote ya unyanyasaji, makosa yoyote ya kuvunja haki za binadamu, yanaelezwa na kusimamiwa na sheria ya kanuni za adhabu. Ikitokea imebainika mfanyakazi wa ndani amenyanyaswa kwa namna yoyote ile, hatua kali za kisheria zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba na kutoa rai kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwamba ikitokea kuna manyanyaso maeneo yoyote, ni wajibu wa jamii sasa kuripoti jambo hilo katika uongozi wa Serikali za Mitaa ama Polisi ili taarifa hizo ziweze kuchukuliwa na kwenda kufanyiwa kazi kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa na kudhibiti makosa hayo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Neema, jiandae Mheshimiwa Dkt. Ntara,

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema Tanzania tunajipanga kwenda kufanya *ratification* ya ule Mkataba wa Kimataifa *(ILO Convention* 189*)*, lakini *Convention* hii toka ipitishwe ni tangu mwaka 2011. Kwa hiyo, mpaka leo ni takribani miaka 22. Je, ni lini sasa mchakato huu utakamilika na Tanzania tutaridhia huu mkataba wa *ILO* 189 ili tusijikute tunasubiri tena miaka 22 mingine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Lugangira kwamba, kuna msemo wa wahenga, wanasema *what is common to others is not common to all*. Ni kwamba, ni kweli mkataba huu wa Kimataifa unaweza ukawa umepitishwa kwa nchi za wenzetu miaka ya 2011, lakini katika kuingia mikataba ya Kimataifa ambalo Mheshimiwa Mbunge anapaswa ajue kuna masuala mengi ya kuangalia *customs* zetu kwa maana ya mila, tamaduni na desturi, tunaangalia na pia *relevance* ya nchi na nchi, na pia tunaangalia masuala ya kiuchumi na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kwenye mambo yale ambayo yameingia kwenye mkataba ule, yapo ambayo tayari sheria zetu yanazitambua hata kabla ya wao kuingia mwaka 2011. Sisi tumeanza, ukiangalai kwa mfano Sheria ya Kazi iliyokuwepo ya Mwaka 1981, tayari ilikuwa inazingatia kazi za staha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna mambo mengi ambayo tayari kabla hata ya *convention* sisi tulikuwa tuko mbele zaidi, tumebakiza machache sana ambayo tunaendelea kuyafanyia kazi tuingie kwenye saini na *ratification*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Dkt. Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninarudia, ni miaka minne tumelizungumza hilo suala ndani ya hili Bunge, Mkataba wa C 189 mtauleta lini ndani ya hili Bunge?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Thea, tayari Serikali imeshalifanyia kazi na tumeshafanya uchambuzi kwenye ngazi ya Wizara, inaenda kwenye mamlaka nyingine kwa mujibu wa sheria

ili kuweza kuhakikisha kwamba mkataba huo, tuliokuwa tunatarajia kuuleta kwa Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Bunge hili, kwa hiyo, kama hatua ambazo tumezipeleka kwenye ngazi nyingine wakifanya haraka, basi tutaweza kuupitisha mkataba huo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, pamoja na sheria na kanuni za Serikali lazima tuweke utu na ubinadamu kwa watumishi wa ndani. Tujiulize wenyewe humu ndani, kila mtu ajiulize kwenye moyo wake, kweli tunawatendea haki watumishi wa ndani? Sisi humu ndani tuanze wenyewe, halafu ndipo tuulize sheria.

Kwa hiyo, utu na ubinadamu ndiyo msingi wa kuwatunza na kuwalinda watumishi wa ndani. Mtumishi wa ndani anakaa na mwanao, mtumishi wa ndani anakaa na mali yako, kwa hiyo, niwaombe sana, pamoja na sheria turudi nyuma na kumwogopa Mungu kwa kutoa haki kwa watumishi wa ndani.

Waheshimiwa, swali hili limechukua zaidi ya dakika 12, limechukua maswali mawili, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ahsante.

Waheshimiwa Wabunge sasa tunaendelea na Ofisi ya TAMISEMI, Mheshimiwa Mtinga, karibu uulize swali lako.

Na. 418

**Kukarabati Vituo vya Afya Mkalama na Kinyangiri**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ukarabati wa Vituo vya Afya Mkalama na Kinyangiri ambavyo ni chakavu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Afya vya Mkalama na Kinyangiri ni miongoni mwa vituo vya afya kongwe 203 ambavyo Serikali imeviainisha kwa ajili ya ukarabati na kuongeza miundombinu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakamilisha ukarabati wa hospitali 50 kongwe nchini na baadaye itafanya ukarabati wa vituo vya afya na zahanati kongwe kote nchini vikiwemo vituo vya afya vya Mkalama na Kinyangiri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yanayotia moyo kiasi ya Serikali, Kituo cha Afya Kinyangiri na Kituo cha Afya Mkalama nikisema vikongwe ni vikongwe kweli kweli, hata hadhi ya zahanati za sasa haina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makamu wa Rais, wakati huo ambaye sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, aliahidi ukarabati kwenye vituo hivi, akaja Katibu Mkuu wa CCM akawaahidi wananchi ukarabati wa vituo hivi, na wananchi wamekuwa wakisubiri kwa hamu sana muda mrefu mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali sasa haioni kwamba vituo hivi viwili vinapaswa kupewa udharura na vitolewe kwenye utaratibu huu alioujibu wa kusubiri kwanza hospitali 50 na viingizwe kwenye ukarabati angalau kwenye vituo vya afya vya sasa vya kimkakati, ipate angalau shilingi milioni 250 kila kituo ili kutimiza ahadi ya wananchi hawa ambao wamesubiri kwa muda mrefu sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Wabunge wako majimboni, kuna shida, hebu msaidieni jamani. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa, Francis Mtinga kwa swali lake linalolenga kuboresha sekta ya afya msingi katika jimbo lake. Kwa hakika amekuwa akipaza sauti. Ninaomba

nimhakikishie kwamba Serikali ya Awamu ya Sita ina dhamira ya dhati ya kuendelea kuimarisha sekta hii muhimu ya afya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uhitaji wake wa vituo hivi vya Afya vya Mkalama na Kinyangiri ambavyo ni chakavu, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwanza Bunge hili Tukufu limepitisha nyongeza ya bajeti, ambapo kuna shilingi bilioni 53.5 ambazo zinatoka kwa ajili ya kuhakikisha kwamba milioni 250 inaenda katika kila jimbo kwa ajili ya kuanza kujenga vituo vya afya vya kimkakati, na Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akisemea kwa upande huu. Kwa hiyo, ninaomba apate taarifa kwamba katika jimbo lake inakuja shilingi milioni 250 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya cha kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ukarabati wa hivi vituo vya afya viwili alivyovitaja, kwa sababu Serikali tayari imeanza kutenga fedha, imeanza kujenga vituo vya afya vya kimkakati, ninaomba nimhakikishie kwamba tayari hospitali kongwe zinafika mwisho wa kukarabatiwa na sasa tunaingia katika kukarabati vituo vya afya, na vituo vya afya hivi viwili tutavifikia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vinakarabatiwa na vinakuwa katika hali nzuri ili viweze kutoa huduma bora kwa wananchi wako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Vituo vyote vya afya, jibu ndilo hilo. Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo.

Na. 419

**Kukamilisha Ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Chato**

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa vituo vya afya Kata za Nyamilembe, Kasenga na Ilyamachele vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za Wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024/2025, Serikali imetoa shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *OPD* katika Kituo cha Afya Kasenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Kata ya Nyamilembe kipo kwenye Mpango wa kupokea fedha kutoka Mfuko wa *TASAF* katika mwaka 2024/2025, ambapo tayari Halmashauri ya Wilaya ya Chato imewasilisha maombi makao makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya vilivyoanza ujenzi kwa nguvu za wananchi katika Kata za Kimkakati kote nchini zikiwemo Kata za Nyamilembe, Kasenga na Ilyamchele katika Halmashauri ya Chato.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Medard.

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Pia, ninaomba nifikishe shukurani nyingi sana za wananchi wa Kasenga kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kutoa fedha shilingi milioni 250. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Ilyamchele, na Nyamilembe wana hamu sana na kujengewa vituo vya afya, lakini imechukua muda mrefu. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini fedha hizi za ujenzi wa vituo vya afya vya Kata ya Nyamilembe na Ilyamchele zitatolewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wana hamu na shauku kubwa kuona uhakika wa Serikali kwenye ujenzi wa vituo vya afya hivi viwili; ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri kama yuko tayari awahakikishie wananchi wa Nyamilembe na Ilyamchele, ni lini yupo tayari tufuatane mimi na yeye tukaone hamu yao na kuhakikisha kwamba vituo vya afya vitajengwa kwa haraka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, kwa kweli anapaza sauti yake kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora kabisa za afya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa kwenye ziara katika jimbo lake, kwa kweli alizungumza na nikamhakikishia na ninaomba niendelee kumhakikishia kwamba Serikali ya Awamu ya Sita ipo kazini na ndiyo maana utaona fedha tayari zimeshaanza kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa *(OPD)* katika Kituo cha Afya cha Kasenga, tayari imekuja, lakini kuna fedha nyingine kupitia Mfuko wa *TASAF* ambayo itaenda kwenye Kituo cha Kata ya Nyamilembe na yenyewe inakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuna shilingi milioni 250 ambayo inaletwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mwaka huu wa bajeti kwa ajili ya kujenga kituo cha afya cha kimkakati katika Jimbo lako. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ataona dhamira kabisa ya dhati kutokana na fedha hizi kwa kadiri zinavyokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wananchi wa Chato wasikie kwamba katika Kata ya Ilyamchele pamoja Kasenga, Serikali italeta fedha kwa ajili ya kuhakikisha vituo hivi vya afya vinajengwa na vinaweza kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili kwamba lini nipo tayari kuongozana naye katika Jimbo lake kwenda kuongea na wananchi wake, na kuonesha ni kwa kiasi gani Serikali ya Awamu ya Sita inafanya uwekezaji mkubwa sana katika upande huu wa afya msingi. Mheshimiwa Mbunge tutakaa tuzungumze tupange ili tuweze kufanya ziara hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kata ya Kala, Wilaya ya Nkasi wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwapatia shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya pamoja na gari la wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kituo ni kizuri sana na kimekamilika na gari lipo, ila hakijaanza kutoa huduma. Je, ni lini hasa huduma zitaanza kutolewa ili wananchi wapunguze adha ya kutembea kilometa 150 kufuata huduma makao makuu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Sylvia Sigula kwa swali lake hili zuri kabisa kwa maslahi ya wananchi wa Nkasi. Pia ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza Mkurugenzi akishirikiana na *DMO* na *RMO* waweze kufanya taratibu zote za Kiserikali ambazo zitawezesha vituo hivi kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna *compliance* yoyote, wafanye mawasiliano na Wizara ya Afya kwa ajili ya kituo hiki muhimu kabisa ambacho kimejengwa na ambacho tayari Mheshimiwa Rais ameleta gari la wagonjwa kianze kutoa huduma bora za afya kwa wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Anatropia

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninawapa pole wananchi wa Jimbo la Hai kwa kuondokewa na Baba Askofu Dkt. Emmanuel Lazaro, Mwasisi wa Kanisa la *TAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali ilituletea fedha shilingi milioni 250 tukaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Nkwansira na sasa kinatoa huduma. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta fedha shilingi milioni 250 awamu ya pili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambaye amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana kuhakikisha kwamba sekta ya afya msingi inaimarika katika jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilileta shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza majengo ya awali ya kituo hiki cha afya na tayari kituo hiki cha afya kimeanza kutoa huduma. Sasa kazi ya Serikali ni kuendelea kuleta fedha, tutaleta shilingi milioni 250 kwa ajili ya majengo ya awamu ya pili ili kituo hicho cha afya kiwe kina majengo yote yanayohitajika kwa ajili ya kutoa huduma bora kabisa ya afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Tumepokea barua za ujenzi wa vituo vya afya shilingi milioni 250, lakini mpaka sasa fedha hazijaja na Mfumo wa Serikali ni kama bado una wiki mbili tu usitoe tena fedha mpaka mwakani. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini sasa fedha hizo zitaachiwa ili tukimbizane na kujenga vituo vya afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Joseph Kasheku kwa swali lake hilo zuri kabisa lenye maslahi kwa ajili ya wananchi wake, lakini kwa ajili ya Wabunge wote waliomo humu. Ni kweli kabisa, Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipekee kabisa imetenga bajeti ya shilingi bilioni 53.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo 214.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe taarifa hii kwamba katika mwaka huu wa bajeti, fedha hizi zitaanza kutoka

kufika katika vituo hivi vya afya ili viweze kujengwa na viweze kutoa huduma bora ya afya kwa ajili ya wananchi. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Joseph Kasheku, kwamba kabla ya mwaka wa fedha haujaisha fedha hizi zitakuwa zimefika katika kituo hiki cha afya cha kimkakati katika jimbo lake kwa ajili ya kuanza kujenga majengo ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge pia na fedha hizo zitaanza kutoka kwa ajili ya majengo hayo ya awali katika hivi vituo vya afya ya kimkakati.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Abdallah Chikota; kwa niaba ya Mheshimiwa Hokororo.

Na. 420

**Kupatiwa Magari ya Wagonjwa Vituo vya Afya – Nanyamba**

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, lini Vituo vya Afya Kitaya na Majengo - Nanyamba vitapatiwa magari ya kubeba wagonjwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya na Nanyumbu mwaka 2023/2024 imepokea magari mawili ya kubebea wagonjwa ambayo yamepelekwa kwenye Kituo vya Afya Majengo na Hospitali ya Mji wa Nanyamba. Aidha, Kituo cha Afya Kitaya kinahudumiwa na gari kutoka Hospitali ya Mji Nanyamba, ambapo umbali kati ya vituo hivyo ni takribani kilometa 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa kwa awamu kwa ajili

ya vituo vya afya vyenye uhitaji kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya Kitaya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niweke Kumbukumbu za Bunge sahihi, ni Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba siyo Nanyumbu. Nanyumbu ni Halmashauri nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya masahihisho hayo, sisi wananchi wa Nanyamba tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupata gari katika Kituo cha Afya cha Majengo, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri Kituo cha Afya cha Kitaya kipo mpakani kabisa mwa Tanzania na Msumbiji na hayo maeneo ninadhani unayafahamu. Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kutupatia gari ya wagonjwa katika kituo hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Halmashauri ya Wilaya Nanyamba kwenye hospitali ile ya halmashauri na hivyo vituo vya afya tuna *x-ray machine* mbili, lakini katika hizo *x-Ray machine* mbili zote hatuna mtaalamu hata mmoja, hivyo kuwasababishia wananchi kwenda umbali mrefu kupata huduma ya *x-ray*.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa haraka kutupatia wataalamu ambao tumewaomba kwa muda mrefu ili wananchi wakapate huduma hiyo ya *x-ray* badala ya kusafiri umbali wa kilometa 100 ama 150? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Agnes Hokororo aliyeuliza swali hili kwa niaba na ninaomba nimtaarifu kwamba Serikali ya Awamu ya Sita tayari imenunua magari ya kubebea

wagonjwa 382, lakini imenunua magari 210, kwa ajili ya uratibu ambapo magari haya yamesambazwa kote nchini, lakini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu uhitaji mkubwa ambao Kituo cha Afya cha Kitaya inao na hasa katika kupata gari la wagonjwa, lakini ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kama vile ilivyoanza kutangulia kununua magari haya ya kubebea wagonjwa 382, itanunua magari mengine na kuyasambaza katika maeneo yenye uhitaji mkubwa ikiwemo katika Kituo hiki cha Afya cha Kitaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili kuhusu mtaalamu wa *x-ray machine,* Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, alifika katika Ofisi zetu na akawa ameeleza uhitaji huu mahususi kabisa, na ninaomba nimhakikishie kwamba tayari suala hili tunalifanyia kazi ili waweze wapatikane hawa watumishi wataalamu wa mashine hizi za *x-ray* ambazo zitawasaidia wananchi kupata huduma bora za afya. Tutaleta wataalamu ili waweze ku-*operate machine* hizi na kuweza kutoa huduma bora kwa Watanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Wilaya ya Kyerwa kijiografia ni pana sana na tuna vituo vya afya vitano, tukiwa na magari ya wagonjwa wawili Kata ya Murongo pia na Nkwenda. Ni kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa kuweka gari la wagonjwa katika kila tarafa yaani gari iongezeke katika Tarafa ya Mabira ili kurahisisha huduma ya wananchi wetu ambao eneo kijiografia siyo zuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge na ninaomba nimpe taarifa kwamba Serikali ya Awamu ya Sita tayari imenunua magari ya kubebea wagonjwa 382 na magari ya uratibu 210.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kuendelea kununua magari haya na kuyasambaza kote nchini kwa kuzingatia maeneo yenye uhitaji mkubwa. Ninaelewa kwamba katika Wilaya ya Kyerwa, kuna uhitaji mkubwa wa kupata magari haya ya kubebea wagonjwa na ninaomba nikuhakikishie kwamba Serikali italeta magari haya itatafuta fedha, itanunua magari haya, itayasambaza kote nchini ikiwemo Kyerwa kwa ajili ya kutoa huduma bora ya afya kwa Watanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Getere.

Na. 421

**Vijiji Kutopata Asilimia 20 ya Mapato ya Mnada**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, kwa nini vijiji vyenye maeneo ya mnada havipati mgao wa 20% ya mapato ya mnada?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa vijiji vinavyotoa maeneo kwa ajili ya shughuli za minada na mchango wake katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato yanayokusanywa kutoka kwenye minada huingizwa katika mfuko mkuu wa Halmashauri na kutumika kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo katika maeneo yote ya Halmashauri, ikiwemo vijiji vinavyohusika na minada. Vilevile, halmashauri zote nchini zina wajibu wa kuchangia kwenye miradi ya maendeleo kati ya 20% hadi 70% ya mapato ya ndani kulingana na daraja la Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha vijiji kugharamia shughuli ndogo ndogo za kiofisi Serikali imetoa maelekezo katika Mwongozo wa Bajeti kwa kila halmashauri kupeleka kati ya shilingi 100,000 hadi shilingi 200,000 kwenye vijiji kila robo mwaka kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi. Kiasi hicho cha fedha, hutegemea daraja la halmashauri husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu haya ya Serikali, Kijiji cha Mgeta kimekuwa na mnada kwa muda mrefu sana na kimekuwa na madai ya zaidi ya shilingi milioni 221. Sheria ya Halmashauri Na. 08 inataja wazi kwamba vijiji vyenye maeneo yanayotoa mradi wanapewa 20%, maana yake asilimia nne ya kata na 16% ya vijiji na itakwenda kwenye vitongoji. Sasa ni lini Serikali itatoa maelekezo ya Mnada wa Mgeta ili Wanakijiji wa Serikali ya Kijiji cha Mgeta kupewa fedha zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mnada wa Hunyari hauna uzio, ni lini sasa Serikali itajenga uzio kwenye mnada wa Hunyari? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Boniphace Getere kwa maswali yake haya mawili mazuri. Ninaomba nitumie nafasi hii kuendelea kuwakumbusha Wakurugenzi katika Mamlaka zetu za Serikali za mitaa kuzingatia Mwongozo wa Bajeti ambao unazitaka halmashauri kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kuzirudisha katika vijiji vyetu katika kata kwa kuzingatia daraja la halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mpaka wakati huu fedha za uendeshaji ambazo tayari zimetoka na kwenda katika Kata, Vijiji na mitaa ni shilingi bilioni 4.69, lakini tunataka tuendelee kuhakikisha kwamba vijiji vyetu hivi, kata, mitaa na vitongoji

havikosi fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nitoe msisitizo huo, Wakurugenzi wote wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa waweze kuzingatia mwongozo huu wa bajeti uliotolewa na warudishe hizi fedha katika ngazi hizo kwa ajili ya kuendesha shughuli zao. Maelekezo haya yanaenda pia katika Kijiji cha Mgeta na chenyewe kiweze kupelekewa fedha inazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na eneo la Mnada wa Hunyari, ninaomba pia nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri aweze kuweka katika mipango na bajeti kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ili waweze kuona namna gani wanajenga uzio katika eneo hili la mnada. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Ni bora kila Mkurugenzi awe na *TV* ili maelekezo yako ukiyatoa na Mkurugenzi huko alipo kwa Mheshimiwa Getere asikie na aone.

Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, Utawala Bora; Mheshimiwa Maganga.

Na. 422

**Ajira kwa Wahitimu wa Chuo**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ajira kwa wahitimu wa vyuo nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetoa nafasi 47,404 za ajira mpya kwa kada

mbalimbali ambazo utekelezaji wake unaendelea kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na mamlaka nyingine na wasailiwa kutoka vyuo mbalimbali waliofaulu wameweza wamepangiwa vituo vya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali inatarajia kutoa ajira mpya 45,000 kwa kada mbalimbali ambazo utekelezaji wake utafanyika kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imeidhinisha jumla ya nafasi 41,500 za ajira mpya kwa kada mbalimbali ili kuweza kuajiri wahitimu stahiki. Ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kuipongeza Serikali, kweli imejenga miundombinu ya elimu, na afya lakini mazingira wanayokaa watumishi hakuna nyumba na makazi. Serikali ina mpango gani wa kuwajengea maeneo ya kuishi ili kusudi hata wanapotoa huduma za kiafya wawe karibu na maeneo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ni mpya, kwa hiyo changamoto bado zipo nyingi sana ambazo zinawakabili watumishi wa Halmashauri hiyo ya Mbogwe. Je, kuna mpango gani wa kuwapiga *tough* ili na wao waweze kufanya shughuli zao vizuri waweze kuendelea na majukumu yao ya kiutumishi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Maganga, amekuwa mstari wa mbele kuja pale Ofisi ya Rais, Utumishi kufuatilia masuala ya watumishi wa Jimbo lake la Mbogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja juu ya mazingira ya makazi ya watumishi wa Mbogwe, na ukizingatia na halmashauri mpya, kwanza, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kujali maslahi ya watumishi wa umma. Amefanya hivyo siyo tu kuboresha maslahi na kuwapandisha madaraja, hata kujali suala la kujenga makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika halmashauri mpya 39 amejenga nyumba za Wakurugenzi, Wakuu wa Idara nyumba 58 wamejengewa, lakini nyumba za walimu zipatazo 1,700 zimejengwa, na wataalamu wa kada ya afya pia wamejengewa takribani nyumba 270. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe shaka Mheshimiwa Maganga, katika bajeti iliyopitishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI hapa, pia kuna bajeti ya kujenga nyumba kama zilivyojengwa katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba hili jambo litakuja kufanyika kwenye jimbo lake kwa kuwa pia ni sehemu ambayo tutaipa kipaumbele. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Mtanda.

Na. 423

**Upungufu wa Watumishi Newala Vijijini**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na upungufu wa watumishi hususan Walimu na Watoa Huduma za Afya - Newala Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali iliidhinisha kibali na kuajiri Walimu 12,015 na watoa huduma za afya 13,625. Kati ya nafasi hizo walimu 30 na Watoa Huduma

za Afya nafasi 42 waliajiriwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala ili kukabiliana na upungufu wa watumishi katika sekta hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kukabiliana na upungufu huo ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepanga kuajiri jumla ya walimu 10,652 na watoa huduma za afya 10,449 ambapo kati ya nafasi hizo, walimu wapya 49 na watoa huduma za afya nafasi 52 watapangiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri na pia katika ajira mpya ambazo inategemea kutangazwa, sisi wana Newala Vijijini tutakuwa wanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala, na halmashauri nyingi za pembezoni, watumishi wengi wanaoenda kuajiriwa, wanaenda kupata *cheque number,* baada ya kupata *cheque number* wanaanza uhamisho na kurudi. Kwa hiyo, unakuta upungufu ni mkubwa sana. Hali hiyo inaathiri utendaji kwa kiasi kikubwa. Nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni haja sasa kuchukuwa maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kwamba, watumishi wanaoajiriwa hasa maeneo ya pembezoni, basi wawe wale wanaotoka katika maeneo yale ili kuondoa hii kadhia ya hamahama ya kila siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa hamisho nyingi ni za kubadilishana, lakini unakuta wanaoathirika ni sisi wana Newala Vijijini kwa maana ya Halmashauri ya *Newala DC* wa kwetu wanaondoka, lakini mbadala wake hawarudi. Je, Serikali haioni haja sasa wanapotoa kibali cha ruhusa ya kuhama inatoa barua zote mbili ili kuondoa lile *gap* ambalo linajitokeza katika maeneo yetu na kutoathiri utendaji kazi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Maimuna Mtanda, kwanza nimpongeze, amekuwa na jitihada kubwa sana ya kufuatilia mambo ya watumishi kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiyajibu maswali yote mawili kwa pamoja, ni kwamba kuna mambo mawili ambayo tumefanya Ofisi ya Rais Utumishi, kwanza tunafanya jambo linaitwa *Human Resource Assessment* kuona mahali ambapo watumishi wapo wengi na kufanya msawazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili tumefikia mwishoni na tunakwenda kufanya msawazo hasa kupeleka maeneo yale ya pembezoni ambayo yana watumishi wechache. Kuna maeneo kama ya mjini kuna watumishi wamejaa, na bado majukumu yao mengine hawatekelezi ipaswavyo wakati mahali pengine haswa mikoa ya pembezoni watumishi ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uhamisho, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumeweka mfumo wa E-Uhamisho ambao kupitia mfumo huo huwezi kuhama. Kwanza kwa sasa mtumishi anayeajiriwa katika kituo kipya ni lazima ahudumu siyo chini ya miaka mitatu ndiyo aanze kuomba uhamisho. Ukiingia kwenye mfumo unakukatalia, unasema bado hau-*qualify* kupata uhamisho. Kwa hiyo, kwa sasa usumbufu uliokuwa unatokea huko nyuma, tatizo hili tumetafuta suluhisho la kudumu na watumishi wote watakaokuwa wanafika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa vijana wetu, wanapoomba ajira wanasema tupo tayari kufanya kazi mahali popote. Wanapopata tu barua ya kupewa kazi, wanaanza kulalamika kwamba tunataka twende mijini. Sasa hili jambo kama Serikali tumelidhibiti hasa kuokoa changamoto ya wafanyakazi kwa mikoa ile ya pembezoni ambayo vijana wengi wamekuwa wakiomba uhamisho kwenda mijini.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Biashara, Mheshimiwa Felix.

Na. 424

**Mkoa wa Kigoma kuwa Lango la Biashara**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya Mkoa wa Kigoma kuwa lango la biashara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kuifanya Kigoma kuwa lango la biashara ikiwa ni pamoja na kuimarisha biashara za mpakani ikiwemo Bandari ya Kigoma/Kibirizi katika kusafirisha bidhaa na abiria kwenda katika miji ya Momba na Kalemie nchini *DRC* pamoja na mipaka ya Manyovu na Mabamba katika Halmashauri za Wilaya ya Buhigwe na Kibondo ambayo inatumika na wafanyabiashara wengi kupitisha mizigo kwenda nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kuifungua Kigoma kuwa kitovu cha Biashara na Uwekezaji kwa kutumia fursa ya kijiografia kwa kuboresha miundombinu ya Barabara, Umeme, Afya, Elimu, Uwanja wa Ndege na Ajira, mfano barabara ya kutoka Kigoma kwenda Tabora.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya kuuliza. Moja, wafanyabiashara wa Mkoa wa Kigoma wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu juu ya tozo mbalimbali za ufanyaji wa biashara za mipakani. Upi mkakati wa Serikali wa kupunguza tozo hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Wizara ya Viwanda, Biashara na TAMISEMI wapo tayari kukaa pamoja na wafanyabiashara wa Kigoma ili waweze kusikiliza changamoto zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, swali la tozo unalo majibu yake? Kwa sababu halipo kwako, unayo majibu? Haya mpe basi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kavejuru kwa sababu amekuwa akifuatilia sana maendeleo ya Mkoa wa Kigoma mahususi kwa wafanyabiashara na kuhakikisha wananufaika kulingana na jiografia na mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili suala la tozo, kama Serikali kwa ujumla wake, tozo na kodi nyingine, kupitia mpango wa kuboresha wafanyaji biashara na wawekezaji nchini (MKUMBI), Serikali inaendelea kuangalia namna ya kupunguza kero mbalimbali ambazo zimeelezwa katika mpango ule na mojawapo ni hii ya tozo na ada na ushuru mbalimbali ambao siyo rafiki kwa wafanyabishara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa ujumla wake pamoja na kwa maana ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Serikali kwa jumla tunaangalia hilo ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili, Serikali tumekuwa tukikaa na wafanyabishara katika mikoa yote na huwa tunafanya hivyo ili kusikiliza; kwanza maoni yao, lakini pia kutatua kero zao. Wizara ya Viwanda na Biashara, mwenyewe nimekuwa nikipita katika mikoa mbalimbali, tunafanya vikao kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa maana ya TAMISEMI, lakini pia na wenzetu Wizara ya Fedha na taasisi zote ili kuhakikisha tunawasaidia wafanyabiashara waweze kuwa shindani, pia kutoa maoni namna ya kuboresha ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya hivyo na hasa Kigoma kwa sababu ni mkoa wa kimkakati, kama tulivyosema, tutaufungua ili uweze kuingia kwenye masoko haya makubwa ya *DRC*, Burundi na Rwanda na Afrika ya Kati ambako tuna hakika tuna soko kubwa la bidhaa za Tanzania. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Jesca.

Na. 425

**Tathmini ya Athari ya Pombe kwa Vijana**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza: -

Je, Serikali imefanya tathmini gani ya vinywaji ilivyoruhusu kama pombe kuona kama havina athari kwa wananchi hasa vijana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* hufanya udhibiti wa bidhaa za pombe kwa kupitia mifumo iliyowekwa ili kuhakikisha ubora na usalama wake. Mifumo ya udhibiti inahusisha uandaaji wa viwango; uthibitishaji ubora wa pombe zinazozalishwa nchini na zinazotoka nje ya nchi; ukaguzi, uchunguzi wa kimaabara; ufuatiliaji katika soko; na kutoa mafunzo na elimu kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hufanya Tathmini kupitia ufuatiliaji wa bidhaa za pombe na imekuwa ikifanyika mara kwa mara ili kuendelea kubaini na kusimamia ubora wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU**: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali

la kwanza, je, uthibiti huo wa kupata pombe zenye ubora wamepeleka mpaka kwenye pombe zile zinazotengenezwa za kienyeji?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna tathmini yoyote ambayo wameifanya kujua athari ya pombe hasa zile zenye *content* kubwa ya *alcohol* namna zinavyosababisha vifo nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Jesca Msambatavangu kwa kufuatilia na hasa kwenye afya na zaidi kwenye watumiaji wa vilevi au vileo ambavyo vinazalishwa katika nchi yetu na vingine vinaendelea kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya kazi kubwa sana. Moja, kuhakikisha kama nilivyosema tunadhibiti ubora wa pombe zinazozalishwa nchini na zile zinazoingia nchini. Kwenye eneo hili la pombe za kienyeji, nikuhakikishie kwamba Serikali tumeshaanza kufanya kazi kubwa moja, kwa kushiriki na taasisi zetu za *TBS*, *SIDO* na *TILDO*, tunafanya utafiti wa pombe za kienyeji ambazo tunaona zinakidhi viwango ili ziingizwe kwenye ubora na kuwasaidia wazalishaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tunavyoongea hivi sasa pombe za kienyeji kama rubisi, pia na ulanzi kule kwetu na pombe nyingine kama za ndizi nakumbuchi ambazo zilikuwa za kienyeji sasa tunazilazimisha kwa kuwapa viwango ili ziweze kuwa na ubora kupunguza athari kwa wanywaji ambao wakati mwingine wanaweza kunywa zaidi kuzidi kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na tathmini ya athari za pombe ambazo zimekuwa zimezidi au wanazokunywa zaidi ya viwango au zile zenye *content* ya *alcohol* kubwa, Serikali kupitia Wizara ya Afya hufanya hivyo na Waziri wa TAMISEMI, lakini na sisi kama Wizara ya Viwanda na Biashara kama nilivyosema, pale tunapobaini kwamba pombe fulani ina kileo kikubwa kuzidi viwango na nyingine kama tulivyosema za kienyeji kama gongo na nyingine huwa tunapiga marufuku, lakini pia kufuatilia ili

kudhibiti athari hizi ambazo zinaweza zikatokana na wingi wa kileo katika pombe za kienyeji na za viwandani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na majibu ya Serikali, ukifuatilia ripoti ya Muhimbili inaonyesha kwamba vijana wengi wamepata tatizo la *blood dialysis* kutokana na matatizo ya figo na vitu vingine kutokana na pombe feki na pombe ambazo zimezidi *content* ambazo zinazagaa mtaani. Je, Wizara mbali ya kuzingatia biashara, ina wajibu wa kulinda Taifa kwenye afya ya vijana; Wizara hii haioni kwamba kuwe na mkakati maalum, *operation* maalum kuondoa vinywaji ambavyo vimekuwa vikiangamiza nguvu kazi ya Taifa letu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Festo Sanga kwa swali hili muhimu sana. Ni kweli kama nilivyosema, moja ya changamoto ni hii ya matumizi ya pombe ya kuzidi kiasi na hasa kama alivyosema mfano kwa vijana na kumekuwa na changamoto hizo mbalimbali ikiwemo hiyo ya figo na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kama Serikali nimesema tunadhibiti ubora/viwango vya vinywaji hivi/vileo. Pili, pombe zile feki kupitia taasisi zetu ikiwemo *TBS,* lakini pia *Fair Competition Commission* huwa tunapita mitaani kusaka kwa kushirikiana na wazalishaji. Kwa mfano, kwenye suala la feki, kweli kumekuwa na pombe baadhi ni feki, mfano konyagi, baadhi ya wazalishaji na ambao sio waadilifu wanachukuwa zile chupa ambazo ni za pombe fulani, wanaweka pombe kali ambazo zina madhara, tumekuwa tukikamata. Tunashirikiana na wazalishaji kuhakikisha tunadhibiti hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi tunaendelea kutoa elimu kwa watumiaji. Sisi wote tunatumia vileo kuhakikisha tunatumia kwa kiasi, lakini pia kufuata viwango na kujiridhisha kwamba pombe unayokunywa ni ile ambayo ni nzuri na imetoka kwenye

wazalishaji halisi badala ya kufuata kwa sababu wengine wanafuata urahisi wa bei…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, maliza majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Ngonyani.

Na. 426

**Ujenzi wa Daraja la Mitomoni**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Daraja la Mtomoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa daraja la Mitomoni unatekelezwa kupitia fedha za dharura zilizotolewa na Benki ya Dunia kupitia dirisha la *Contingent Emergency Response Component (CERC)* kwa gharama ya shilingi bilioni 9.29. Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 1 Novemba, 2024. Hadi sasa utekelezaji wa mradi huu umefikia 21% na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuanza kujenga daraja lile

ambalo lilikuwa linaleta athari kubwa kwa wananchi wa maeneo yale.

(a) Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba daraja hili linakamilika kwa wakati?

(b) Je, Naibu Waziri yupo tayari kuongozana nami kwenda katika eneo la ujenzi wa daraja hilo pale Mitomoni ili aweze kupokea zawadi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri na kwa niaba ya Mheshimiwa Rais kwa sababu wananchi wamefurahi sana kuanzishwa kwa ujenzi wa Daraja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan nipokee pongezi za Mheshimiwa Mbunge, ninaamini hizi ni pongezi pia za Wanaruvuma wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuhusu swali lake la (a), kwamba mikataba tuliyosaini na tulivyokubaliana na wenzetu wa *World Bank,* miradi yote hii inatakiwa ikamilishwe ndani ya mwaka mmoja na hatutegemei kuwa na changamoto yoyote ya mtiririko wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulishakubaliana na wakandarasi, tunawasimamia tutahakikisha kwamba wanakamilisha hizo kazi kama tulivyokubaliana kwenye mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kupokea zawadi kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakubaliana tarehe sahihi na tutakuwa tayari kwenda kupokea zawadi ya Wanaruvuma kwa ajili ya Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kujenga hili daraja muhimu sana, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Aysharose kwa niaba yake Mheshimiwa Massare.

Na. 427

**Zao la Kitunguu Kuwanufaisha Wananchi wa Mkoa wa Singida**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y. MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Zao la Kitunguu linawanufaisha Wananchi wa Mkoa wa Singida?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwanufaisha wakulima wa zao la kitunguu….

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri sogeza hiyo *mic*.

**WAZIRI WA KILIMO:** Naam.

**NAIBU SPIKA:** Iweke *mic* vizuri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwanufaisha wakulima wa zao la kitunguu katika Mkoa wa Singida na maeneo mengine nchini, Serikali inaendelea kutoa mbolea ya ruzuku, mafunzo ya kanuni za kilimo bora cha vitunguu na kuwapatia Maafisa Ugani vitendea kazi zikiwemo pikipiki na vifaa vya kupima afya ya udongo ili kutoa ushauri sahihi wa matumizi ya mbolea na hivyo kuongeza tija na uzalishaji wa zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali inaendelea na ujenzi wa skimu za umwagiliaji zenye jumla ya hekta 7,300 katika Kata zinazolima zao la kitunguu za Msange, Masimba na Msingi.

Kukamilika kwa ujenzi wa Skimu hizo kutanufaisha wakulima 52,000 wa vitunguu katika vijiji 19 vilivyopo katika Kata za mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali katika mwaka 2025/2026 itaanza kujenga masoko kwa ajili ya zao la vitunguu katika Mkoa wa Singida na maeneo mengine nchini pamoja na kuandaa kanuni kwa ajili ya kuzuia ufungashaji wa lumbesa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri sana ambayo yana manufaa makubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Singida, lakini nina maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo ahadi ya Mheshimiwa Waziri katika eneo la Njiapanda ya Melia kujenga soko la vitunguu. Je ni lini ahadi hii utaitimiza?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Halmashauri ya Itigi tunalima vitunguu. Changamoto maeneo yanayozunguka Itigi yana changamoto ya oevu kipindi cha masika. Je, Serikali sasa ipo tayari kwenda kuyakusanya yale maji na kutengeneza bwawa kuzunguka katika Mji huo wa Itigi ili wananchi walime vitunguu kwa wingi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko alilolitaja, vile vile ilikuwa ni maelekezo ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbune kwamba ipo kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2025/2026, hilo soko litaanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo oevu la Itigi, ninataka na yeye mwenyewe amekuwa akifuatilia sana, wataalam wa Wizara ya Kilimo wameshaanza kufanya usanifu wa maeneo yote ambayo yanatuama maji katika Wilaya ya Bahi na Wilaya ya Manyoni. Kwa hiyo, maeneo yote haya yataingizwa katika mpango wa Serikali ili tuweze kuyafanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato.

Na. 428

**Kuboresha Huduma za Tehama katika Vyuo Vikuu vya Umma**

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma ya TEHAMA maeneo wanayotumia Wanafunzi kujisomea katika Vyuo Vikuu vya Umma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya maboresho ya Miundombinu ya *Internet*; Mifumo ya Kujifunzia Kidijitali *(LMS);* Maktaba za Kidijitali; Elimu kwa *Studio* za *Multimedia*; Mifumo ya Kiutawala Kidijiti na kununua Vifaa kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum katika Vyuo Vikuu vya Umma. Lengo ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wa elimu ya juu wanapata mazingira bora ya kujisomea yanayochochea ujifunzaji wa kisasa, jumuishi, na unaotumia teknolojia kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya maboresho haya ni hatua muhimu katika mwelekeo wa kuifanya elimu ya juu nchini kuwa ya kisasa, jumuishi na yenye ushindani wa Kimataifa ili kufikia ajenda ya mageuzi ya elimu ya juu hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Nahato.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri katika swali langu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa sasa hivi Serikali imeboresha sana TEHAMA katika vyuo vikuu. Je,

imejipangaje kuwajumuisha wafanyakazi wa TEHAMA katika vyuo vikuu ambao sio wataaluma kushiriki katika kuboresha TEHAMA katika vyuo vikuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Vyuo vikuu vya umma nchini vinaendesha masomo ya masafa *(distance learning)* kwa wanafunzi walioko mikoa mbalimbali. Je, Serikali imejipangaje kuwasaidia wanafunzi hawa hasa katika upande wa TEHAMA? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kumpa taarifa Dkt. Nahato kwamba, Serikali tayari imeanza mkakati wa maboresho ya vyuo vikuu vyote nchini, kupitia mradi wetu mkubwa kabisa ujulikanao kama *higher education for economic transformation* ambao una mawanda karibu sita au maeneo sita ambayo yanafanyiwa kazi. Eneo la kwanza ni ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya *campus* hizi zilizopo pamoja na *campus* mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ni kusomesha wahadhiri ndani pamoja na nje ya nchi; eneo la tatu, ni kutunga mitaala mipya pamoja na kuboresha ile mitaala iliyopo; eneo la nne, ni ushirikiano baina ya vyuo vyetu vikuu pamoja na viwanda; eneo la tano, ni uwezeshaji wa wenzetu wenye mahitaji maalum; na eneo la sita, ni hili eneo la TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika eneo la TEHAMA Serikali imejikita kufanya mambo yafuatayo ili kuboresha mazingira ya TEHAMA katika vyuo vyetu: ambapo eneo la kwanza, tutafanya upanuzi wa miundombinu mbalimbali ya *internet* kuhakikisha kwamba tunakuwa na *smart classes,* lakini tunakuwa na *smart campus a*mbazo zitakuwa sasa zinawasiliana siyo tu ndani ya nchi, bali hata kufikia vyuo vingine katika nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ni kutengeneza mifumo sasa ya kidijitali ile ya kujifunzia na kusomea. Eneo lingine ni kutengeneza maktaba za kimtandao au maktaba za kidijitali ili

kupata ile *e-Learning* kwa ujumla wake. Eneo la nne ni sasa hiyo elimu iliyozungumzwa kwa njia ya masafa, inazingatiwa kwenye eneo hili, lakini vilevile tunatengeneza sasa *studio* katika vyuo vyetu vyote vikuu ili kuweza kutengeneza vipindi ambavyo siyo lazima Mwalimu muda wote awepo darasani. Wanafunzi wanaweza ku-*access* kupitia maktaba zetu, lakini vilevile kuna ununuzi wa vifaa sasa kwa ajili ya kufanya mifumo hii iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mambo haya yote yanajumlisha vilevile watumishi wasio wanataaluma ili kuhakikisha kwamba mifumo hii inafanya kazi pamoja na kuwasomesha watumishi hawa wasio wanataaluma ili kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inakwenda kufanya kazi sawasawa na kwenye vyuo vyetu. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Tarimo.

Na. 429

**Utekelezaji wa Azimio la Bunge**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu ushirikiano kati ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Manispaa – Moshi Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imepanga kukutana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Maji na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya masuala ambayo yatawezesha utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu ushirikiano baina ya Manispaa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika shughuli za uokoaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea na ushirikiano baina yake na Manispaa katika masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa magari ya zimamoto na uokoaji, kupanga miji, upitishaji wa michoro ya ujenzi, usimikaji wa *fire hydrants* na upatikanaji wa viwanja vya ujenzi wa vituo vya zimamoto na uokoaji nchini ikiwemo Manispaa ya Moshi Mjini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu hayo mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa kuna Halmashauri kama Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ambayo imepata magari kutoka miji dada ambayo ni marafiki kutoka Ujerumani na kuna Halmashauri ambazo zimenunua magari haya, je, Serikali inaweza ikatoa kauli sasa kwamba umiliki wa magari haya uwe kwenye jina la Halmashauri husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Azimio lilipita mwezi wa Sita mwaka 2024 na bado kama siku kumi hivi tufikishe mwaka, Mheshimiwa Waziri anaweza kututhibitishia kwamba sasa wataharakisha kukutana na Wizara zile nyingine zote ili Azimio hili liweze kusonga mbele? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo Manispaa husika ama halmashauri imenunua gari la zimamoto na uokoaji, umiliki utabaki kwake kwenye Halmashauri husika au Manispaa husika, lakini matengenezo na uendeshaji utasimamiwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa sababu ndiyo wenye wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu Azimio, Serikali imekuwa ikiheshimu sana Maazimio ya Bunge na imekuwa ikiyatekeleza. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, hata Azimio hili pia Serikali itajipanga, itakaa kuhakikisha kwamba Azimio hili

linatekelezwa kwa ajili ya Manispaa ya Moshi na maeneo mengine hapa nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika Mkoa wa Manyara ambako Mheshimiwa Naibu Waziri anatoka kuna magari machache sana ya Zimamoto hasa maeneo ya Mbulu Vijijini, Mjini na hata Hanang, kuna tatizo, kukitokea kitu kinachoitwa ajali ya moto tunashindwa kupata hayo magari. Je, ni nini mpango wa Serikali katika kuyaokoa maeneo haya kwa kuletewa magari ya zimamoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeshanunua magari ya Zimamoto na Uokoaji kama tulivyoeleza mara nyingi hata kwenye hotuba yetu jana kwamba, magari 150 yameshanunuliwa na yatawasili nchini kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari awamu ya kwanza imeshaingia mwezi huu wa Tano; na yatakapoingia, kila Wilaya hapa nchini ikiwemo Wilaya ya Mbulu na Wilaya ya Hanang' kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge pia zitapata magari ya Zimamoto na Uokoaji kwa ajili ya shughuli za uokoaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza kwa niaba yake Mheshimiwa Kilumbe.

Na. 430

**Elimu kwa Wananchi Wanaolisha Mifugo Hifadhi za Reli**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wananchi hususan Wafugaji wanaolisha mifugo maeneo ya hifadhi ya reli? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* limeandaa mpango maalum wa kuhakikisha masuala ya mazingira na jamii yanatekelezwa kwa kuzingatia sheria za Kitaifa na Kimataifa. Aidha, *TRC* imeendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwemo wafugaji kupitia mpango maalum wa ushirikishwaji wa wadau yaani *"Stakeholders Engagement Plan"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu hii inatolewa katika shughuli za mradi za kila siku na kupitia kampeni maalum zinazofanyika kila baada ya miezi mitatu kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo usalama wa miundombinu ya reli kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ulinzi ni jukumu la kila mwananchi. Hivyo naomba kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuungana Serikali na *TRC* katika kutoa elimu ya usalama wa miundombinu ikiwemo ya reli kwa wananchi wa maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo nayapongeza, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Serikali imefanya kazi nzuri sana ya usafiri kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma wa *SGR* na wananchi wote Tanzania sasa wanatamani hatua hiyo wafikie. Nini hatua ya Serikali katika kutekeleza mradi wa *SGR* kwenye maeneo yote nchini ikiwemo kufika Kigoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwamba, reli ya kati kipande cha kutoka Kigoma kwenda Tabora kina changamoto

kubwa na kimeanza ukarabati. Nataka kujua ni lini ukarabati huo utakamilika na kuwawezesha wananchi kuendelea kutumia reli hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda kwa maelezo yake ya awali ya kuipongeza Serikali yetu pendwa kwa kazi kubwa ambayo imefanywa katika miaka hii minne kwenye sekta ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwarifu Mheshimiwa Kilumbe pamoja na Waheshimiwa Wabunge juu ya hatua mbalimbali ambazo Serikali imefanya katika kipindi kifupi cha miaka hii minne. Tukianza na kutoka Dar es Salaam - Morogoro mpaka Dodoma, hili halihitaji hata kulifafanua kwa sababu kila mtu anaona; tunapanda reli, tunafurahia usafiri salama na ulio mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumshukuru Mheshimiwa Rais wetu mpendwa ambaye ndiye anasimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM ambayo iliahidi kuhakikisha kwamba itaboresha usafirishaji katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza, naomba kumwarifu Mheshimiwa Mbunge, kutoka Makutupora – Tabora, Kilometa 368 mkandarasi yuko *site* tayari, na tuko asilimia 14.5, kutoka Tabora mpaka Isaka, Dkt. Samia Suluhu Hassan pia aliidhinisha na tulishasaini mkataba na mkandarasi ameshaanza kazi kilometa 165, tuko asilimia sita. Aidha, kutoka Mwanza mpaka Isaka kilometa 341, tuko 60%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, hivi karibuni mwaka jana pia Mheshimiwa Rais alikubali, tumeanza ujenzi wa reli ya kisasa, kilometa 506 na tuko asilimia sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu mwezi wa Tatu, tumesaini mkataba unaounganisha nchi yetu kutoka Uvinza kwenda Msongati kwenye madini ya *Nickel* ambapo ni kilometa

240. Hii ni hatua kubwa ambayo tumeshaifanya kama Serikali kwa upande wa *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, tupo kwenye maandalizi kwa sababu tunao mpango kama Serikali kuhakikisha tunajenga *SGR* (reli ya kisasa) kutoka Mtwara mpaka Mbamba Bay inayounganisha pamoja na matawi la Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunao mpango wa kujenga reli tena kutoka Tanga mpaka Musoma ili kuunganisha na maeneo yenye machimbo au madini ikiwemo na Engaruka ambako tuna Magadi Soda, pale Minjingu tuna *Phosphates* na kule Dutwa tuna *Nickel. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anataka kufahamu hatua ambayo Serikali imefanya katika ujenzi wa *Meter gauge* kutoka Tabora kwenda mpaka Kigoma. Kwanza, nimwambie Mheshimiwa Mbunge, Serikali tayari imeshasaini mkataba na mjenzi ameanza kazi kutoka Kaliua mpaka Mpanda kilometa 210, ambapo zaidi ya bilioni 379 zimeidhinishwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa ili kuhakikisha kwamba ukanda huo unakwenda kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninavyozungumza hapa, tumeshasaini mkataba wa reli kutoka Tabora mpaka Kigoma na tunasubiri mkandarasi aweze kuanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wa Kigoma wawe na subira, siyo muda mrefu neema inaendelea kuja kwao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Protas.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika Reli ya *MGR, Station* ya Goweko ilikuwa ina njia tatu, lakini mlitoa njia ya pili na ya tatu mkaacha njia moja, na pale tuna mizigo mingi. Ni lini mtarudisha reli ile ili wananchi wa Goweko wapate fursa ya kupakia mizigo yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikae na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kufuatilia jambo analolizungumza niweze kulifanyia kazi kwa ufasaha zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mahawanga.

Na. 431

**Kipaumbele kwa Wanawake katika Miradi ya Usafirishaji**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza: -

Je, mafunzo gani yanatolewa na Serikali kwa Wanawake kuhusu usimamizi wa biashara za uchukuzi na mbinu bora za usafirishaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara mbalimbali na taasisi zake imeendelea kutoa mafunzo kwa wanawake wajasiliamali kuhusu biashara za uchukuzi na mbinu bora za usafirishaji. Mafunzo haya yanatolewa kwa lengo la kuwezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika sekta ya uchukuzi ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikitawaliwa na wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya ujasiliamali yameendelea kutolewa kupitia taasisi zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *Small Industries and Development Organization (SIDO),* Tanzania *Women Chamber of Commerce (TWCC)* na *National Economic Empowerment Council (NEEC,* ambapo wanawake hupewa elimu ya namna ya kuanzisha, kuendesha, kukuza biashara za uchukuzi kama usafirishaji wa abiria, mizigo na usambazaji wa bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mafunzo haya ya udereva wa magari ya biashara yameendelea kutolewa kupitia taasisi zifuatazo: *National Institute of Transport (NIT)* na *Vocational Education and Training Authority (VETA)* ambapo wanawake wameendelea kufundishwa kuendesha magari makubwa (mabasi, malori, magari ya abiria, magari ya mizigo) pamoja na usalama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, hivi karibuni *LATRA* kupitia Vyuo vya *NIT* na *CBE,* wameanzisha mafunzo ya wahudumu wa mabasi ambao wengi wao ni wanawake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mahawanga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali madogo wawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Je, kuna ufuatiliaji au tathmini ya mafanikio haya yanayotolewa na Wizara kwa wanawake hawa wajasiliamali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kufuatia ufinyu na idadi ndogo ya wanawake wajasiriamali katika fursa zinazotokana na uchukuzi, je, Wizara inachukua hatua gani kukabiliana na changamoto hii hasa katika upatikanaji wa taarifa na mitandao ya biashara? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kwa kutambua umuhimu mkubwa wa nafasi ya mwanamke katika jamii, imeendelea kufuatilia na kuratibu kuhakikisha kwamba mwanamke kama kiongozi, kama mwanamama anakuwa sehemu muhimu ya kushiriki katika uendeshaji wa shughuli za usafirishaji katika nchi yetu. Hivi ninavyozungumza tayari kozi mbalimbali kama nilivyozungumza zinaendelea kutolewa na tathmini imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya ajira milioni 16.3, wanawake ni takribani 3,200,000. Ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kuhamasisha na kuhakikisha kwamba wanawake wanashirikishwa kikamilifu katika shughuli mbalimbali za usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali la pili kuhusiana na jinsi Wizara ilivyojipanga. Kwanza, tumejipanga kuhakikisha kwamba Ilani ya CCM, Toleo la 2025 ambayo imeelezea vilivyo katika Ibara ya 231, Kifungu cha *(g)* na *(h),* nafasi ya mwanamke na kuimarisha vituo vya mafunzo. Tutaendelea kukisimamia kifungu hicho kuhakikisha kwamba wanawake wanapata fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye upande wa Kanuni za Manunuzi ya Umma, imeeleza vizuri sana kwenye Kanuni Namba 35, jinsi mwanamke anavyopaswa kupewa fursa, ambapo imeelezwa kwamba takribani 30% ya kazi au bidhaa au shughuli zitolewe kwa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba mwanamke anashiriki ipasavyo katika kujenga uchumi wa Taifa lake kupitia sekta yetu ya usafirishaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni Mheshimiwa Anna Paul, Naibu Waziri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Yupo? Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar; Dkt. John Jingu, Katibu Mkuu; Wakili Evelyne Makala, Mkurugenzi Huduma za Sheria wa Wizara ya Maendeleo

ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa niaba ya Naibu Katibu Mkuu. Ahsante. Ndugu Felister Mdemu, Naibu Katibu Mkuu, Jinsia na Wanawake. *(Makofi)*

Pia wapo Ndugu Mary Chatanda, Mwenyekiti wa UWT Taifa. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Hajjat Mwantum Mahiza, Mwenyekiti wa Bodi ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Mjumbe wa Baraza Kuu UWT Taifa. *(Makofi)*

Pia, Dkt. Joyce Nyoni, Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Pia wapo Profesa Mohamed Makame Haji, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar; na Dkt. George Bakari, Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Sharifa Nabalang'anya, Mkurugenzi Halmashauri ya Gairo. *(Makofi)*

Ndugu Dogo Iddi Mabrouk, Makamu Mwenyekiti Wazazi Taifa. *(Makofi)*

Ndugu Sigilinda Mdemu, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mlele na Katibu wa Chama cha Wataalam wa Maendeleo ya Jamii Tanzania. *(Makofi)*

Ndugu Tunu Kondo, Naibu Katibu Mkuu UWT Zanzibar. *(Makofi)*

Ndugu Mohamed Andrea, Katibu wa CCM Itikadi na Uenezi Itakadi, Kusini. *(Makofi)*

Ndugu Halima Mamuya, Mjumbe, *M-NEC* na Mjumbe wa Kamati Kuu. *(Makofi)*

Jamani, naona Wajumbe wa Kamati Kuu mnawapigia sana makofi. *(Kicheko)*

Tunao pia, Ndugu Nicola Brennan, Balozi wa Ireland; *welcome to the Parliament*. Ndugu Oliva Kinabo, *Program Manager Gender*, Msaidizi wa Balozi wa Ireland; Ndugu Metrion Ndofi, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi Rasilimaliwatu wa Wizara; Ndugu Lilian Mtali, Mwenyekiti wa Kamati ya Majukwaa ya Uwezeshaji Kiuchumi; na Ndugu Victor Nkya, Mkurugenzi Sera na Mipango. *(Makofi)*

Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Dkt. Gwajima, ni Wakili Methusela Gwajima, mume wa Mheshimiwa. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Mwanaidi Khamis, Mbunge na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambaye ni Ndugu Seif Daudi Suleiman, mume wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Ali Mohamed Ali, mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri; na Ndugu Zeyana Ali Mohamed, mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge: kwanza ni wageni watano wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Ndugu Chihindi Ntwayo, mtoto wake kutoka Newala Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ghati Chomete, Ndugu Jane Mbulla, Mwenyekiti wa UWT kutoka Wilaya ya Butiama Mkoani Mara. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Amandus Chinguile, Wanafunzi wa Chuo cha Afya Kairuki kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Sanga, rafiki zake kutoka Mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Anastazia Wambura, ndugu zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Makada wa CCM kutoka Jijini Mbeya. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Taska Mbogo, watoto wake kutoka Marekani na Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Makada wa CCM kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Viongozi wa Kanisa la *Kingdom of Heaven on Earth Mission* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Kikundi cha *G11* Familia kutoka Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Taasisi ya Kupinga Ukatili kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Venant Protas, Wapigakura wake kutoka Igalula Mkoani Tabora. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Anatropia Theonest, Wamiliki wa *Day-care Centres* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Janeth Mahawanga, Kikundi cha *Women Vision Empowerment* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 70 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, *Narae Global School* kutoka Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: Wanafunzi 70 na Walimu watano wa Shule ya Msingi Doris iliyopo Kijichi Wilaya ya Temeke Mkoani Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wanafunzi 130 na walimu 10 wa shule ya Awali ya Msingi *Good Victory* kutoka Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwakumbusha wote kuwa, Wizara ya Nishati itaendelea na Semina kuhusu Gesi ya Petroli *(Liquefied Petroleum Gas - LPG)* inayoingizwa kutoka Nje ya Nchi kwa ajili ya kupikia hapa nchini na Gesi Asilia inayozalishwa nchini *(Natural gas)*. Semina hii itafanyika leo tarehe 27, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana, Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kuwajengea uelewa zaidi kuhusu *Liquefied Petroleum Gas (LPG)* na *Natural Gas*.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri. Ndiyo mganga wenu kakwambieni mfanye hivyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaomba kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kama kilivyo na yaliyomo yake yaingie kwenye *Hansard* za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,

Wanawake na Makundi Maalum, Fungu 53 kwa mwaka 2024/2025; na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2025/2026. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo, ili kuwasilisha hotuba yangu. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kutuongoza vyema kwa mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali kwa kipindi hiki cha miaka minne ya uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Ninatambua kuwa, Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa ya kuona hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini inaimarika na utoaji wa huduma za ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii na uwezeshwaji kiuchumi kwa makundi maalum unafanyika kwa kasi kubwa na ufanisi. Ninaahidi kwamba, Wizara itaendelea kutimiza majukumu yake kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Mgombea wa Kiti cha Urais kupitia Chama cha Mapinduzi. Tunawaombea mafanikio makubwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninapenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Mawaziri ya Maendeleo ya Jamii kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, kuhimiza usawa wa kijinsia, kutambua na kuratibu makundi maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo, uwezeshaji wanawake kiuchumi pamoja na kuzingatia haki za wazee, wanawake, wanaume na watoto katika jamii. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo anayoyatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 9 Aprili, 2025 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa jinsi ambavyo umeendelea kutuongoza vyema katika mijadala mbalimbali ya Bunge letu kipindi chote ambacho tumekuwa tukiwasilisha bajeti zetu na taarifa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninampongeza sana Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa uongozi wake wenye weledi na uliotukuka katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mungu ambariki na amfanikishie zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge; Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge; na Mheshimiwa

Najma Murtaza Giga, Mbunge, kwa umakini wao katika kusaidia kuongoza vikao vyetu vya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Mbunge na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ushirikiano mkubwa sana anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Sina shaka atarejea kwa kishindo mwaka ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge; na Makamu wake, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge; kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia wenye lengo la kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao unaiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mbunge, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa. Chini ya Uenyekiti wake, Kamati imeweza kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Profesa Mohammed Yakoub Janabi, kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. Kuchaguliwa kwake ni ushahidi wa heshima kubwa sana kwa nchi yetu na kuonesha kutambulika kwa michango ya wataalamu wetu katika kuimarisha Sekta ya Afya Barani Afrika na Dunia kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 27 Novemba, 2024 Taifa letu lilimpoteza Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika na Mbunge wa Jimbo la Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tarehe 7 Mei, 2025 Taifa lilipata msiba mwingine mzito kwa kumpoteza Mheshimiwa David Cleopa Msuya, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu. Kwa masikitiko makubwa, ninaungana na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, familia za Marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi hawa. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/2025, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vya wizara kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/2025, maelezo yako aya ya 15 hadi 21. Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Sheria, Mipango, Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa na Kitaifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii nchini, kama nilivyofafanua kwa kina kwenye aya ya 15 na 16. Katika kuboresha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii mwaka 2024/2025, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele saba ambavyo vimeainishwa kwenye aya ya 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato na matumizi ya fedha za Wizara, Fungu 53, katika mwaka 2024/2025, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi za Kitanzania 7,040,129,000 kwa mchanganuo kama unavyoonekana kwenye jedwali namba moja kwenye hotuba yangu. Hadi kufikia mwezi Machi, 2025,

Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 3,523,597,415 sawa na 50% ya makadirio ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa na Bunge shilingi 67,905,259,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 47,487,079,000 ni bajeti ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 20,418,180,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 25.8 ni fedha za Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 21.6 ni Mishahara. Aidha, kati ya fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 18.02 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2.3 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2025, Wizara imepokea jumla ya shilingi 35,206,488,106 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na 74.1%. Kati ya Fedha zilizopokelewa, shilingi 18,891,954,036 ni Matumizi Mengineyo na shilingi 16,314,534,070 ni Mishahara. Pia, Wizara imepokea Fedha za Maendeleo shilingi 12,525,746,891 sawa na 61.4% ambapo, shilingi 11,840,673,000 ni fedha za ndani na shilingi 685,073,891 ni fedha za nje, kama ilivyoonyeshwa kwa kina kwenye jedwali namba mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Fungu 53 kwa kina imeelezwa kwenye aya ya 22 hadi 150, ukurasa wa 13 hadi 80. Katika kutekeleza vipaumbele vya bajeti kwa mwaka 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali imetekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, eneo la maendeleo ya jamii, aya ya 23 hadi 34. Sekta ya Maendeleo ya Jamii ni mtambuka na ina jukumu kubwa la kufanya mageuzi ya kifikra na mitazamo ya jamii na kuifanya jamii kuwa kitovu cha maendeleo. Sekta hiyo inawajibika katika kuhamasisha na kuamsha ari ya wananchi kushiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo yao wenyewe na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ni kitovu muhimu katika ushirikishwaji wa jamii na wadau na kwa msingi huo, ina mchango wa kipekee katika mafanikio ya sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo katika Ngazi ya Msingi. Mpango huo unaoanza 2022 – 2026 unalenga kuwawezesha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo na kuchochea mageuzi ya kifikra, mtazamo na kiutendaji kwa timu ya wataalamu ngazi ya msingi ili kuboresha utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi, kama nilivyoeleza kwa kina kwenye aya ya 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuamsha ari ya jamii kushiriki katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii ambapo wamehamasisha utekelezaji wa jumla ya miradi 31,802, kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mila na desturi ni muhimu katika maendeleo na ustawi wa jamii yoyote. Hata hivyo, jamii yetu ni miongoni mwa jamii zinazokabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa kasi ya mmomonyoko wa maadili. Aidha, mila na desturi chanya zikitumika kwa ufanisi zina uwezo mkubwa wa kudhibiti mmomonyoko wa maadili na kujenga Taifa lenye maadili mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hilo, Wizara iliandaa Kitini cha Uwezeshaji wa Majadiliano ya Mila na Desturi Ngazi ya Jamii cha Mwaka 2023. Matumizi ya kitini hicho ni hatua ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya wananchi 20,211 wameshiriki mijadala hiyo katika Mikoa ya Mwanza, Mara, na Tabora. Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Wizara zote za kisekta katika kuhimiza uzingatiaji wa Miongozo hiyo. Miongozo yenyewe hiyo ni huo wa Maadili na Utamaduni wa Mwaka 2022 pamoja na miongozo mingine ya kisekta, hatua ambayo itaongeza kasi ya jamii kuziishi mila na desturi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu vyuo nane vya maendeleo ya jamii nchini vilivyotajwa kwenye aya ya 29. Maelezo mengine kuhusu eneo la maendeleo ya jamii yapo aya ya 30 hadi 34.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenda kwenye eneo la pili la uratibu na usimamizi wa shughuli za kiuchumi kwa wafanyabiashara ndogondogo, ambapo maelezo kwa kina yapo aya ya 35 hadi 42. Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia mipango ya kuwezesha na kuendeleza kiuchumi makundi maalum ya wafanyabiashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makundi hayo ni pamoja na wachuuzi wa bidhaa, yaani wamachinga, mama na baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji, wasusi, washonaji wa nguo na wafanyabiashara ndogondogo wenye mauzo ghafi yasiyozidi shillingi milioni nne kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imesajili kwenye mfumo wa kidigitali wafanyabiashara ndogondogo 54,999 kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Tarehe 8 Mei, 2025 na kufanya jumla ndogo ya wafanyabiashara ndogondogo waliosajiliwa kuwa 78,984; hapa wapo wa kike 50,283 na wakiume 28,701. Kati ya hao 28,287, sawa na 36%, wamepatiwa vitambulisho vya kidigitali vinavyowawezesha kupata huduma za mikopo ya Serikali yenye masharti nafuu kupitia Benki ya *NMB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuratibu na kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa ofisi za wafanyabiashara ndogondogo katika ngazi ya mikoa, ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 mikoa 17 kati ya 26 imekamilisha ujenzi wa ofisi hizo na taarifa zaidi ipo aya ya 42.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa Ofisi hizo ni juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwajengea mazingira mazuri wafanyabiashara hao katika kuratibu shughuli zao kiuchumi. Alitoa kiasi cha shilingi milioni 10 kwa kila mkoa mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze eneo la tatu la haki na maendeleo ya mtoto, kwenye aya ya 43 mpaka 60. Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia utoaji wa haki za msingi kwa mtoto, kama ilivyoelezwa kwa kina zaidi kwenye aya ya 43. Wizara imeendelea kuimarisha Mifumo ya Kisheria kwa kufanya marekebisho ya Sheria tatu ambazo ni Sheria ya Mtoto Sura ya 13, Sheria ya Makosa ya 24 Kimtandao Sura ya 443 na Sheria ya Msaada wa Kisheria Sura ya 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho hayo yamelenga kuondoa upungufu unaojitokeza katika utekelezaji wa masharti katika Sheria husika, ili kuimarisha ulinzi na maslahi bora ya mtoto. Aidha, kupitia marekebisho hayo, adhabu dhidi ya vitendo vya ukatili zimeainishwa kwa kina kwenye aya ya 44.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu mafunzo kuhusu sayansi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa maafisa 281, ambapo kati ya hao 215 walitoka mikoa na 25 halmashauri zote za Tanzania Bara. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuimarisha uwezo katika kusimamia na kuratibu Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, kifupi PJT-MMMAM ya miaka mitano, kuanzia mwaka 2021/2022 – 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imetoa mafunzo ya programu hiyo kwa waandishi wa habari 26 kutoka katika kila mkoa ambao ni vinara katika kutoa taarifa za programu hiyo, ili kuimarisha utoaji na elimu katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeratibu na kusimamia Kampeni ya Taifa ya Usalama wa Mtoto Mtandaoni, *Child Online Protection,* katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Kampeni ilikuwa na lengo la kuelimisha wazazi au walezi na watoto wenyewe kuhusu usalama wa mtoto anapokuwa anatumia mitandao. Kampeni ya usalama wa mtoto mtandaoni iliambatana na mafunzo ya wawezeshaji 516 kutoka ngazi za mikoa yote Tanzania Bara. Aidha, wazazi au walezi 821,098 walifikiwa na kampeni hiyo na wanafunzi 786,901 kutoka shule za msingi na sekondari walipata elimu ya usalama wakati wa kutumia mitandao. Wizara imeunda Kamati ya Taifa ya Ushauri ya Usalama wa Mtoto Mtandaoni kwa

lengo la kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu afua sahihi za ulinzi na usalama wa mtoto mtandaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende eneo la nne, kuhusu huduma za ustawi wa jamii ambazo maelezo yake yapo kwenye aya ya 61 mpaka 87. Wizara imeendelea kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa mtu binafsi, familia na makundi mbalimbali katika jamii kwa lengo la kuzuia matatizo na kutatua athari zinazotokana na changamoto mbalimbali. makundi hayo yameainishwa katika aya ya 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilifanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za matunzo, ulinzi, ushiriki wa wazee kwenye vyombo vya maamuzi katika jamii na taasisi mbalimbali. Sera hiyo iliidhinishwa na Baraza la Mawaziri Oktoba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Afya, ilifanya utambuzi wa wazee na wasiojiweza 4,975,473 na kutoa huduma za kiustawi katika mikoa 26 hadi kufikia Aprili, 2025. Kati ya hao, wazee wasiojiweza milioni 2.1 wakiwemo wanaume 1.01 na wanawake 1.18 wamepatiwa vitambulisho kwa ajili ya msamaha wa matibabu na bima ya afya, kwa ajili ya kugharamia matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya watoto 10,782 wa kiume 6,108 na wa kike 4,674 wanaoishi na kufanya kazi mtaani waliokolewa kutoka kwenye mazingira hatarishi ya mtaani. Kati ya hao, watoto 2,410 wameokolewa kupitia kampeni maalum inayoendelea kwenye mikoa yote nchini iliyoanza rasmi 7 Aprili, mwaka huu 2025 kuelekea Siku ya Kimataifa ya Watoto Waishio na Kufanya Kazi Mitaani iliyofanyika kwa mara ya kwanza Kitaifa Mkoani Mtwara na kampeni hii ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeshughulikia jumla ya migogoro ya ndoa 97,234 hadi kufikia Aprili, 2025 kupitia Kitengo cha Ustawi wa Jamii katika ngazi ya Halmashauri hadi Taifa ambapo, kati ya mashauri hayo, mashauri 81,820 yalipatiwa

ufumbuzi na mashauri 15,414 yalipelekwa Mahakamani kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara, kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta pamoja na wadau, imeendelea kuratibu huduma kwa manusura wa vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 jumla ya manusura 19,717 waliripotiwa, wakiwemo watoto 7,278 wa kiume 1,373 na wa kike 5,905 na watu wazima 12,439 ambao, wote walipata huduma katika Madawati ya Jinsia na Watoto ya Polisi Nchini, ambapo pia, Maafisa Ustawi wa Jamii huwa wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto, matokeo chanya, yakiwemo kupungua kwa vitendo vya ubakaji kutoka matukio 8,185 mwaka 2023 hadi matukio 7,670 mwaka 2024, ikiwa ni sawa na kupungua kwa 6.3%. Matukio ya ulawiti nayo yamepungua kutoka 2,382 mwaka 2023 hadi 1,930 mwaka 2024, sawa na kupungua kwa 19%.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wanawake. Wizara katika kutekeleza ajenda ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi inaratibu na kutekeleza programu na afua mbalimbali zenye lengo la kukuza usawa na kuimarisha wanawake na wasichana kushiriki katika nyanja zote za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu na afua hizo kwa kina zimeainishwa kwenye aya ya 88. Katika kuhakikisha kuwa, Sekta ya Umma na Binafsi zinajumuisha na kuzingatia masuala ya jinsia kwenye Sera, Mipango na Bajeti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imewajengea uwezo viongozi na watendaji wa ofisi hiyo kuhusu ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika ukaguzi wa Hesabu za Serikali, ili kuwa na taarifa ya kina ya sekta zinavyozingatia na kutekeleza masuala ya jinsia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kukuza haki na usawa wa kiuchumi, Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Tanzania ya Kizazi Chenye Usawa, ambayo inatekelezwa na wadau mbalimbali, kama ilivyoelezwa kwenye

aya ya 91 hadi ya 122. Kwa mara ya kwanza nchini kuelekea Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kuanzia Tarehe 01 – 08 Machi, 2025 Wizara iliratibu Makongamano ya Kitaifa katika Kanda Saba yaliyofunguliwa na Viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatua kubwa katika kusogeza karibu zaidi na wananchi, sauti ya wito wa wanawake kushiriki shughuli za maendeleo na mchango wao kusikika kwa sauti kubwa zaidi, maelezo ya kina yapo aya ya 107. Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Wanawake Duniani yalihusisha shughuli na huduma mbalimbali kama tulivyoeleza kwenye aya ya 108.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Wanawake Duniani kilichofanyika katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sheikh Amri Abeid Kaluta, Mkoani Arusha, tarehe 8 Machi, 2025 na Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Habari hii kwa kina ipo aya ya 109.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa shukrani kwa wadau wote waliofanikisha maadhimisho hayo, kama nilivyowataja na kuwafafanua kwa kina kwenye aya ya 110. Shukrani ziende kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kitaifa ya Uratibu wa Maadhimisho wakiongozwa na Bi. Sarah Masasi, Mwenyekiti wa Kamati na Mlezi wa Chama cha Wanawake Wachimbaji Wadogo wa Madini *(TAWOMA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika kuendelea kuimarisha uwezeshaji wanawake kiuchumi ilifanya maboresho ya Mwongozo wa Uundaji na Uratibu wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi wa mwaka 2022, ili uweze kukidhi matakwa ya sasa. Hadi kufikia Aprili, 2025, Wizara imewapatia mafunzo Viongozi na Waratibu wa Jukwaa katika mikoa 26, ili waweze kueneza na kufanya uhuishaji wa majukwaa kulingana na mwongozo huu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeunda Kamati ya Kitaifa ya Uhamasishaji wa Uundwaji wa Majukwaa inayoongozwa na Mwenyekiti Bi. Lilian Mtali, Mkurugenzi wa

Masoko wa Benki ya Taifa ya Biashara *(TCB)* na Mlezi wake Dkt, Judith Mhina kutoka Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ni ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi, ambapo imekuja na kampeni ya kuongeza kasi ya uundwaji wa vikundi na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi yenye kauli mbiu ya "Wanawake Inuka Imarika Tusua Kiuchumi" itakayotekelezwa kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu uandaaji wa Mpango wa Kitaifa wa Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama unaotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2024 hadi 2029 ambao Tanzania imeridhia utekelezaji wake kupitia Azimio Na. 1325 la Umoja wa Mataifa kuhusu Wanawake, Amani na Usalama. Utekelezaji wa mpango huu maelezo yake yapo aya ya 114.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye eneo la uratibu wa mashirika yasiyo ya Kiserikali, ambapo maelezo yake yapo aya ya 123 hadi 144. Usajili, uratibu na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unatekelezwa kupitia Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara imesajili mashirika 1,202, hivyo kufanya jumla ya mashirika yote yaliyosajiliwa kufikia 10,717. Serikali imejenga mfumo wa kidigitali wa utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo mashirika yote yaliyosajiliwa yameunganishwa, ili kuwawezesha wananchi kuyaona kupitia simujanja kiganjani, kama ambavyo tumeeleza kwa kina kwenye aya ya 133.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha uratibu na udhibiti wa masuala ya mmomonyoko wa maadili kupitia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara imeboresha Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wa mwaka 2020 na kutoa Toleo la Pili la Mwongozo huo la mwaka 2024, kama tulivyoeleza kwa kina katika aya ya 125 na 126.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia wasajili wasaidizi wa

mikoa na Halmashauri, imefanya ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuwasisitiza kutekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa, kama inavyosomeka kwenye aya ya 128.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia ufuatiliaji huo, ilibainika kuwa, miradi ya maendeleo inayotekelezwa na mashirika hayo imezingatia vipaumbele vya kisekta na kuwa na manufaa kwa jamii, kama inavyosomeka kwenye aya ya 130.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2023/2024 Wizara iliandaa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2023, kama ambavyo tumefafanua kwa kina kwenye aya ya 134 na 135. Taarifa ilionesha kuwa, jumla ya shilingi trilioni 2.61 zilipokelewa na kutumika na mashirika hayo katika utekelezaji wa miradi ya afua zilizoainishwa kwenye aya hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa yaliyopatikana kutokana na uendeshaji wa miradi mbalimbali ni pamoja na upatikanaji wa ajira za moja kwa moja 21,701 wakiwemo Watanzania 21,582 na wageni 119; tumeeleza zaidi kwenye aya ya 135.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuanzisha Tume ya Maboresho ya Kodi, kwa ajili ya kupokea maoni na changamoto za kikodi, ambapo kwa mara ya kwanza Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamepata fursa hii adhimu ya kuwasilisha maoni yao ya maboresho ya kikodi mbele ya tume hiyo. Fursa hii inaonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kujenga mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenda eneo la saba, kuhusu uratibu wa mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kifupi *(MTAKUWWA)*. Wizara imeendelea kuratibu Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya Pili, wenye lengo la kuzuia na kutokomeza vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Awamu ya Pili umeongeza mambo mapya kwa lengo la kuboresha uratibu na utekelezaji masuala yaliyoongezeka, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa vyombo vya usimamizi wa mpango huu, ikiwemo Kamati Elekezi ya Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wilaya kupitia Vikao vya Kamati za Ushauri za Mkoa na Wilaya kwa lengo la kupata msukumo wa kisera na kisiasa katika utekelezaji wa mpango huo ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kushirikisha wanaume na vijana wa kiume katika utekelezaji wa afua za kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia na kujumuisha afua za kupinga ukatili wa watoto mtandaoni. Ni hatua njema na kubwa kuwa, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/2026 uliotolewa na Wizara ya Fedha umesisitiza Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kujumuisha afua za mpango huu katika mipango na bajeti zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Wizara, aya ya 151 hadi 162. Kama nilivyoeleza hapa awali, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Maendeleo ya Jamii, Tengeru, na Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taarifa yake; ipo kwenye aya hizo nilizozitaja. Kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, miradi hii ipo mingi, ipo aya ya 163 hadi 170; nitaisoma baadhi kwa ridhaa yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kwa watumishi, Wizara inaendelea na ujenzi wa jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamiii Tengeru. Jengo hilo litagharimu shilingi bilioni 5.7, ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetoa fedha za ndani za maendeleo, shilingi bilioni 1.2, na kufanya jumla ya shilingi bilioni 2.7 zilizopokelewa. Hadi Aprili, 2025, ujenzi umefikia 70%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaratibu utekelezaji wa programu ya kizazi chenye usawa, ambapo Serikali imetoa shilingi bilioni moja zilizowezesha kuwajengea uwezo Maafisa Viungo wa Wizara za Kisekta, kuratibu ziara ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa, kujenga

uwezo kwa vikundi vya wanawake, ili kunufaika na zabuni kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 30%, ambayo inataka vikundi vijisajili kwenye mfumo wa manunuzi ya umma na ununuzi wa pikipiki 100 ambazo zipo katika taratibu za manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwezesha na kuendeleza makundi maalum, wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo, Serikali imetoa shilingi bilioni nane, ili kutoa mikopo kwa wafanyabiashara hao, kupitia Benki ya *NMB,* ili kuongeza kipato chao na kuwainua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2025, wafanyabiashara ndogondogo 601 wanaume 274 na wanawake 327 wamekopeshwa mikopo yenye thamani ya shilingi 1,101,650,000 na zoezi hilo linaendelea. Vilevile, maombi 2,092 yenye thamani ya shilingi 3,590,477,000 yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia unaojulikana kwa jina la "*PAMOJA PROJECT*'' ambao, uwezeshaji wake ni kupitia mkopo wa dola milioni 100 na ruzuku ya dola milioni nne kutoka Benki ya Dunia. Lengo la mradi ni kukuza fursa za kiuchumi, kuboresha huduma za kifedha kwa wanawake na pia, kuzuia na kupambana na ukatili wa kijinsia. Maelezo zaidi yapo aya ya 159.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye vipaumbele vya Wizara na Bajeti ya Mapato, Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026. Maelezo yapo aya ya 171 hadi 173.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake itatekeleza vipaumbele vitano kama ifuatavyo: -

(i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa katika ngazi ya msingi;

(ii) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii ikiwa ni pamoja na kukuza usawa wa kijinsia, kutokomeza vitendo vya ukatili, uwezeshaji

wanawake kiuchumi na upatikanaji wa malezi bora katika familia;

(iii) Kutambua, kuratibu maendeleo na ustawi wa makundi maalum wakiwemo watoto, wazee na wafanyabiashara ndogondogo;

(iv) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika taasisi na vyuo vya ustawi na maendeleo ya jamii; na

(v) Kuimarisha mazingira ya ushiriki na mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara kwa mwaka 2025/2026 imekadiria kutumia kiasi cha shilingi 76,057,153,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 49,115,697,000 ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo shilingi 22,646,148,000 ni fedha za mishahara na shilingi 26,469,549,000 ni fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, shilingi 26,941,456,000/= ni fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ambapo kati ya hizo shilingi 15,415,404,000 ni fedha za ndani na shilingi 11,526,052,000 ni fedha za nje. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2025/2026 tumeyaainisha kwa kirefu kwenye aya ya 162(i - vi).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijielekeze kwenye kutoa shukrani zangu; aya 174 - 184. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi rafiki zikiwemo; Japan, Ufalme wa Sweden, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Ufalme wa Norway, Ufalme wa Uingereza, Falme za Nchi za Kiarabu, Italia, Ujerumani, Ubelgiji, Ufaransa, Canada, Ufalme wa Denmark, Ireland, Jamhuri ya Uswisi, Bangladesh na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayashukuru mashirika na taasisi za Kimataifa ikiwa ni pamoja na *UNICEF, UNFPA, UN-Women, WHO, UNDP, UNEP, ILO, IOM, WFP, FAO, UNESCO* na *UNHCR*. Vilevile ninashukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki, Umoja wa Afrika,

Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Jumuiya za Umoja wa Nchi za Ulaya. Ninayashukuru mashirika ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *Mfuko wa Abbott Fund, Global Fund* na *Hilton Condrad Foundation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nashukuru taasisi za kifedha ambazo ni pamoja na Benki za *CRDB, NBC, NMB*, Benki ya Biashara Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Stanbic, Azania, Equity, Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki ya Akiba *Commercial*, *DCB Commercial Bank,* Benki ya Mkombozi na Benki ya Biashara Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayashukuru mashirika yasiyo ya Kiserikali na mashirika ya dini, *World Vision, PACT Tanzania, The Aga Khan Foundation, Foundation for Civil Society, Help Age Tanzania, Compassion International, Responsible Organization Tanzania, Both Ends Believing, Safe Society Platform Tanzania, Children in Crossfire, Care International Tanzania, Railway Children Tanzania, WiLDAF, ICS, TAWLA, TAYOA, LSF, SOS Children's Village Tanzania, BRAC Maendeleo Tanzania, Plan International - Tanzania*, Kivulini, *FSDT, WFT, TANLAP, Save the Children, Equality for Growth, Landesa, CAMFED, CSEMA; REPPSI, Amani Girls, Girls Effect, Pelum Tanzania, LHRC,* Haki Elimu, *TWCC, TECDEN, EGPAF, FAGDI, HJFMRI, TGNP, CRS* na MEWATA.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani kwa sekta binafsi ikiwemo, Mgodi wa Geita, *Barrick, State Oil, Bakhresa Group of Company, Total Energies, ASM technology, Asas Group of Company, Camal Steel Group, Afroil Investment Ltd, Oryx Gas, Great lakes, Fleight, Bulyankuru Gold Mine Ltd, Bowmans Tanzania Ltd* na *Highland Estate.*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu ziwafikie Baraza la Taifa la Ushauri la Wazee, Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Tanzania, Machifu na Viongozi wa Kimila Tanzania, Umoja wa Wanawake Tanzania *(UWT),* kwa Mheshimiwa mama Mary Chantanda ambaye leo yuko pamoja nasi hapa kwenye jukwaa kuu. Pia Chama cha Wanawake Wajane Tanzania, Jukwaa la ULINGO, Jumuiya ya Wazazi CCM, Baraza la Watoto la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, TAWIA, Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania na Umoja wa Mama na Baba Lishe Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizishukuru klabu za mpira wa miguu Tanzania hususan Yanga, Simba, *AZAM* na vikundi/kampeni za kijamii kama SMAUJATA, TFF, LeMaChu, SAWATA, *Malezi Bora Network* pamoja na vyombo vyote vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Wizara yametokana na ushirikiano wa wa wadau pamoja na Kamati tulizoziunda ambazo nimezieleza ambazo tumezipa majukumu ya kutekeleza. Nichukue fursa kuwashukuru sana Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchukua nafasi hii kumpongeza kijana Samson Mgelwa na kumshukukuru. Huyu ni mwandishi wa kujitegemea kipitia *Blog* ya Muungwana kwa makala yake ya 'Kwanini Wananchi Wengi Hawatoi Ushahidi Kwenye Kesi za Ukatili' ambayo iliyoshinda tuzo za '*Mama Samia Kalamu Award*', ahsante sana Mgelwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani zangu pia kwa Viongozi na Taasisi za Dini zikiwemo *CPCT, TEC, BAKWATA, CCT* na *CSDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekeze shukrani zangu kwenye menejimenti na wataalam wote wa Wizara ninayoiongoza ikiongozwa na Dkt. John Jingu, Katibu Mkuu Wizara hii ambayo yuko pamoja nasi na wasaidizi wake Wakili Amon Mpanju, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum na Bi. Felister Peter Mdemu, Naibu Katibu Mkuu wa Maendeleo ya Jamii na Wanawake upande wa Jinsia na Wanawake kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninamshukuru sana Katibu Wangu Bi. Shantali Mishako kwa ushirikiano wote aliyonipa kipindi chote cha utekelezaji wa majaukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwashukuru Bodi ya Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Bodi na Menejimenti za Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyama vya Kitaalamu *(CODEPATA* na *TASSO)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninawashukuru wakuu wa vyuo vyote nane vya Maendeleo ya Jamii, na hapa ninamshukuru sana Mama Mwantum Mahiza ambaye ndiye Mwenyekiti ya Bosi hii ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali kiufupi NaCoNGO, yuko pamoja nasi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ninawashukuru sana wakuu wa mikoa yote na wataalamu wote chini ya Ofisi zao na wadau wote wa sekta mbalimbali wanaohudumia katika maeneo yao pamoja na mwananchi mmoja mmoja na mitandao ya habari za kijamii ambayo imekuwa na chachu kubwa sana katika ufanyaji kazi wa Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba nichukue fursa hii pia kuishukuru sana familia yangu, hususan mume wangu kipenzi na mpendwa Wakili Msomi Methusela Gwajima ambaye nyuma ya mafanikio yote haya amekuwepo karibu sana na mimi. Mchango wa baba umeonekana katika maisha yangu. Ninaamini mchango wa wanaume wote pia utaonekana kwenye maisha ya wanawake wote katika Taifa letu, na watoto wetu wote pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu na wasaidizi wetu wa shughuli za nyumbani kwa uvumilivu wao wa kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze kuomba fedha kwa kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, aya ya 185 hadi 188. Kuhusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa 2025/2026, katika mwaka 2025/2026 Wizara imekadiria kukusanya kiasi cha shilingi 7,040,129,000 kutoka katika vyanzo mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 185.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya kawaida, katika mwaka 2025/2026 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha shilingi 49,115,697,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 26,469,549,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 22,646,148,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maendeleo. Kwa upande wa shughuli hizi za maendeleo Wizara inakadiria kutumia shilingi 26,941,456,000 kwa ajili ya miradi hii ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 15,415,404,000 ni fedha za ndani na shilingi 11,526,052,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2025/2026, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) tunaomba jumla ya shilingi 76,057,153,000 ili twende kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara yetu ya www.jamii.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia hapa, kwa heshima, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII,JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM,MHE. DKT. DOROTHY GWAJIMA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YAFEDHA KWA MWAKA 2025/26 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi

Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka 2024/25 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2025/26. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2025/26.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo ili kuwasilisha hotuba yangu. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kutuongoza vyema kwa mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali kwa kipindi hiki cha miaka minne (4) ya uongozi wake. Kipekee niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Natambua kuwa Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa ya kuona hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini inaimarika na utoaji wa huduma za ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii na uwezeshwaji kiuchumi kwa makundi maalum unafanyika kwa kasi kubwa na ufanisi. Ninaahidi kwamba Wizara itaendelea kutimiza majukumu yake kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu.

***3. Mheshimiwa Spika***, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuteuliwa kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais kupitia Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2025. Aidha, ninapenda pia kumpongeza **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi**, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Mgombea wa Kiti cha Urais kupitia Chama cha Mapinduzi. Tunawaombea mafanikio makubwa katika Uchaguzi Mkuu mwaka huu.

***4. Mheshimiwa Spika,*** pia, ninapenda kumpongeza na kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Mawaziri ya Maendeleo ya Jamii kwa kuendelea kuwa mstari wa

mbele katika jitihada za kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, kuhimiza usawa wa kijinsia, kutambua na kuratibu makundi maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo, uwezeshaji wanawake kiuchumi pamoja na kuzingatia haki za wazee, wanawake, wanaume na watoto katika jamii. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo anayoyatoa.

***5. Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.)**, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 09 Aprili, 2025 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2025/26.

***6. Mheshimiwa Spika****,* ninapenda kukupongeza wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa uongozi wako wenye weledi na uliotukuka katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.),** Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uchapakazi wake mahiri.

***7. Mheshimiwa Spika****,* vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.), Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.), na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) kwa umakini wao katika kusaidia kuongoza Vikao vya Bunge

***8. Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninamshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mb.),** Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake

na Makundi Maalum kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

***9. Mheshimiwa Spika***, kipekee ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya **Mwenyekiti Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq (Mb.)** na **Makamu wake, Mheshimiwa Riziki Said Lulida (Mb.)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia wenye lengo la kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii.

***10. Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao unaiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii. Wizara itaendelea kushirikiana nao ili kuhakikisha tunatimiza dhamira ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwa na jamii yenye ustawi na maendeleo jumuishi na endelevu.

***11. Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii, kumshukuru **Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb.)** ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Utekelezaji wa Ahadi za nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa. Chini ya uenyekiti wake, Kamati imeweza kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa (Tanzania Generation Equality Programme - TGEP, 2021- 2026) inayoainisha afua muhimu zinazotekelezwa na Wizara za Kisekta na kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeachwa nyuma katika maendeleo na ujenzi wa Taifa letu.

***12. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Profesa Mohammed Yakoub Janabi kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika. Kuchaguliwa kwake ni ushahidi wa heshima kubwa sana kwa nchi yetu na kuonesha kutambulika kwa michango ya wataalam

wetu katika kuimarisha Sekta ya Afya Barani Afrika na Dunia kwa ujumla.

***13. Mheshimiwa Spika,*** tarehe 27 Novemba, 2024 Taifa letu lilimpoteza **Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile (Mb.)**, aliyekuwa **Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika na Mbunge wa Jimbo la Kigamboni**. Aidha, tarehe 07 Mei, 2025 Taifa lilipata msiba mwingine mzito kwa kumpoteza **Mheshimiwa David Cleopa Msuya** aliyekuwa **Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu.** Kwa masikitiko makubwa naungana na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** familia za marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi hawa. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

***14. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/25, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2025/26.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Sheria Mipango, Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa na Kitaifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa Huduma za Maendeleo na Ustawi wa Jamii nchini. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2024; Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); na Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023). Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, katika kuandaa Mpango na Bajeti, Wizara pia imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya II (MTAKUWWA II, 2024/25– 2028/29); Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi wa Mwaka 2022/23 - 2025/26 (Bottom Up); Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM 2021/22 – 2025/26); Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (2021/22- 2024/25); Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals, 2030*); na Agenda ya Afrika Tuitakayo (2063). Aidha, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ahadi za Nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum – GEF, 2021 – 2026).

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kutekeleza Vipaumbele vifuatavyo: -

i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa Ngazi ya Msingi;

ii) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia na kutokomeza vitendo vya ukatili, uwezeshaji wanawake kiuchumi, upatikanaji wa haki, ulinzi na malezi chanya ya watoto;

iii) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za msingi za ustawi wa jamii;

iv) Kutambua, kuratibu na kuendeleza Makundi Maalum wakiwemo Wafanyabiashara Ndogondogo;

v) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na

vi) Kuimarisha ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.

**Mapato na Matumizi ya Fedha za Wizara (Fungu 53)**

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi za Kitanzania 7,040,129,000** inayotokana na ada za wanafunzi, uuzaji wa mitaala ya kufundishia fani za Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii pamoja na malipo ya hosteli katika vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Jamii Ufundi. Vyanzo vingine ni Mapato ya Usajili wa Wafanyabiashara ndogondogo, ada ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ada za mwaka na faini kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 pamoja na marekebisho yake na mapato mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2025, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,523,597,415** sawa na asilimia 50 ya makadirio ya mapato kama inavyoonesha katika ***Jedwali Na. 1.***

**Jedwali Na. 1:** Ukusanyaji Mapato ya Ndani kwa Kipindi cha **Julai, 2024 – April, 2025**

| Chanzo cha Mapato | Mapato Yaliyoidhinishwa | Makusanyo Halisi | Ufanisi (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 4,641,025,000 | 2,483,552,595 | 54 |
| Ada ya Malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 551,600,000 | 115,614,420 | 21 |
| Uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 40,000,000 | 15,000,000 | 38 |
| Usajili na Ada za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | 640,000,000 | 576,670,400 | 90 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Ustawi | 7,500,000 | 7,500,000 | 100 |
| Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo | 1,000,000,000 | 325,260,000 | 33 |
| Makusanyo Mengineyo | 160,004,000 | - | - |
| **Jumla** | **7,040,129,000** | **3,523,597,415** | **50** |

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** sababu ya kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ya mapato ni pamoja na kushuka kwa udahili wa wanafunzi kama ilivyokadiriwa, ambapo waliodahiliwa ni wanafunzi 5,166 kati ya 7,088 na hii ni kutokana na kukua kwa mchango wa sekta binafsi kwenye kuongeza idadi ya vyuo vya kati na vyuo vikuu vinavyotoa taaluma ya kada ya Maendeleo ya Jamii; Uhaba wa miundombinu katika Vyuo; Kutofautiana kwa mihula ya vyuo na Mwaka wa fedha wa Serikali; kuongezeka kwa fursa mbalimbali za mikopo zenye masharti nafuu kutoka sekta binafsi na sekta ya umma; na kupungua kwa ufadhili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutokana na mabadiliko ya sera za nchi wafadhili. **Wizara inaendelea na jitihada za kukusanya mapato katika kipindi kilichobaki ili kufikia lengo la makusanyo yaliyokadiriwa kwa mwaka 2024/2025.**

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara iliidhinishiwa na Bunge **Shilingi 67,905,259,000.00** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 47,487,079,000.00** ni bajeti ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 20,418,180,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 5,836,653,000.00** ni fedha za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 21,650,426,000.00** ni Mishahara. Aidha, kati ya fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi 18,025,673,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 2,392,507,000.00** ni fedha za nje.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2025, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 35,206,488,106.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 74.1. Kati ya

Fedha zilizopokelewa, **Shilingi 18,891,954,036.00** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 16,314,534,070.00** ni Mishahara. Pia, Wizara imepokea Fedha za Maendeleo **Shilingi 12,525,746,891.00** sawa na asilimia 61.4. ambapo, **Shilingi 11,840,673,000** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 685,073,891** ni Fedha za Nje, kama ilivyooneshwa katika ***Jedwali Na. 2.***

**Jedwali 2:** Fedha zilizopokelewa katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili 2025.

| **Matumizi ya Kawaida** | | | |
|---|---|---|---|
| **Eneo** | **Fedha zilizoidhinishwa** | **Fedha zilizotolewa** | **Asilimia** |
| Mishahara | 21,650,426,000 | 16,314,534,070 | 75.4 |
| Matumizi Mengineyo | 25,836,653,000 | 18,891,954,036 | 73.1 |
| **Jumla ndogo (a)** | **47,487,079,000** | **35,206,488,106** | **74.1** |
| **Fedha za Miradi ya Maendeleo** | | | |
| Fedha za Ndani | 18,025,673,000 | 11,840,673,000 | 65.7 |
| Fedha za Nje | 2,392,507,000 | 685,073,891 | 28.6 |
| **Jumla Ndogo (b)** | **20,418,180,000** | **12,525,746,891** | **61.4** |
| **JUMLA KUU** | **67,905,259,000** | **47,732,234,997** | **70.3** |

**C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA (FUNGU 53)**

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Vipaumbele vya Bajeti kwa Mwaka 2024/25, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake pamoja na Wadau mbalimbali imetekeleza yafuatayo: -

**ENEO LA 1: MAENDELEO YA JAMII**

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Maendeleo ya Jamii ni mtambuka na ina jukumu kubwa la kufanya mageuzi ya kifikra na mitazamo ya jamii na kuifanya jamii kuwa kitovu cha maendeleo. Sekta hiyo inawajibika katika kuhamasisha na kuamsha ari ya wananchi kushiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo yao wenyewe na

jamii kwa ujumla. Sekta hii ni kitovu muhimu katika ushirikishwaji wa jamii na wadau na kwa msingi huo, ina mchango wa kipekee katika mafanikio ya sekta mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa majukumu hayo kama ifuatavyo:-

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo katika Ngazi ya Msingi (2022/23 – 2025/26) ambao unalenga kuwawezesha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo na kuchochea mageuzi ya kifikra, mtazamo na kiutendaji kwa timu ya wataalam ngazi ya msingi ili kuboresha utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi. Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI imefanya mafunzo kwa Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata, Watendaji wa Mitaa/Vijiji, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Kilimo, Maafisa Mifugo, Maafisa Afya, Waratibu wa Elimu Kata na Wananchi katika mikoa 21 kuhusu utekelezaji wa mpango huo, ambapo idadi ya waliopata mafunzo imeongezeka kutoka 1,979 kwa mwaka 2023/2024 hadi 4,085, ambapo lengo ni kufikia Mikoa 26. Mafunzo hayo yataendelea kwenye mikoa mitano (5) iliyobaki ya Tanga, Simiyu, Mara, Shinyanga na Kagera.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imeendelea kuamsha ari ya jamii kushiriki katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye Mikoa 26 ya Tanzania Bara kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii wanaofikia **3,976** sawa na asilimia 75 ya waliopo nchi nzima, ambapo wataalam hao kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi mbalimbali nchini, wamehamasisha utekelezaji wa jumla ya miradi **31,802** ikiwemo miradi ya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya (Hospitali za Halmashauri **129**, Zahanati **1,158** na Vituo vya Afya **345**), ujenzi wa Madarasa ya Shule za Awali na Msingi **25,265** na Madarasa ya Shule za Sekondari **4,905**. Hakika, Wataalam wa Maendeleo ya

Jamii wamekuwa chachu ya kuhamasisha Wananchi kushiriki na kumilikishughuli za maendeleo katika maeneo yao**.**

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** mila na desturi ni muhimu katika maendeleo na ustawi wa jamii yoyote. Hata hivyo, jamii yetu ni miongoni mwa jamii zinazokabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa kasi ya mmomonyoko wa maadili. Aidha, mila na desturi chanya zikitumika kwa ufanisi zina uwezo mkubwa wa kudhibiti mmomonyoko wa maadili na kujenga taifa lenye maadili mema. Kwa kuzingatia hilo, Wizara iliandaa Kitini cha Uwezeshaji wa Majadiliano ya Mila na Desturi Ngazi ya Jamii cha Mwaka 2023. Aidha, kitini hicho kimetumika kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa Ishirini na Moja (21) ya Tanzania Bara kuhusu, namna ya kuendesha majadiliano kwenye jamii ili kuiwezesha jamii kujadili na kuibua mila na desturi zinazopaswa kuendelezwa na zile zinazopaswa kutokomezwa.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** matumizi ya kitini hicho ni hatua ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania wa Mwaka 2022. Mijadala hiyo ilihusisha pia elimu ya malezi na makuzi chanya kwa watoto ambapo mbinu zilizotumika kuendesha mijadala hiyo ni pamoja na kushirikisha watu maarufu wakiwemo Mashabiki wa Timu za Simba na Yanga na Wasanii mbalimbali.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Wananchi 20,211** wameshiriki mijadala hiyo katika Mikoa ya Mwanza, Mara na Tabora. **Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Wizara zote za kisekta katika kuhimiza uzingatiaji wa Mwongozo huo** wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania wa Mwaka 2022 pamoja na miongozo mingine ya kisekta, hatua ambayo itaongeza kasi ya jamii kuziishi mila na desturi chanya.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii nchini ambavyo ni Buhare (Mara), Mlale (Ruvuma), Monduli (Arusha), Rungemba (Iringa), Ruaha (Iringa), Uyole (Mbeya) na Vyuo viwili (2) vya Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi (Mwanza) na Mabughai (Tanga). Aidha, Wizara kupitia vyuo hivi imeendelea kuzalisha wataalam wenye maarifa na ujuzi unaoakisi mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Vilevile, katika kipindi cha mwaka 2024/25 jumla ya wanafunzi **5,166 (Me 1,747 na Ke 3,419)** wamedahiliwa katika vyuo vya maendeleo ya jamii na maendeleo ya jamii ufundi. Udahili huo umepungua kwa asilimia **6.45** ukilinganisha na udahili wa mwaka 2023/24 ambapo wanafunzi **5,499** (Me **1,966** na Ke **3,533**) walidahiliwa; na hii inatokana na kuongezeka kwa vyuo vya umma na binafsi vinavyotoa taaluma ya Maendeleo ya Jamii. Aidha, kwa mwaka 2023/24 wanafunzi **5,189** (Me**1,983** na Ke **3,206**) walihitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ujuzi, stadi na umahiri kwa Wahitimu wa Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Wizara imeendelea kutekeleza dhana tatu (3) ambazo ni uanagenzi (apprenticeship), ushirikishwaji jamii (community engagement) na vituo vya ubunifu wa kidigitali (digital innovation centres). Utekelezaji wa dhana hizi unalenga kumfanya mhitimu aweze kupata ujuzi zaidi wa taaluma aliyoisomea kwa vitendo utakaomwezesha kujiajiri na kuajirika.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** dhana ya uanagenzi ina lengo la kuwaunganisha wanafunzi/wahitimu na Makampuni, Mashirika na Taasisi mbalimbali ili kupata stadi, ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kuajiriwa, kujiajiri na kuajiri. Idadi ya waliojiunga imeongezeka kutoka **2,200** kwa mwaka **2023/2024** hadi **2,964** kwa mwaka **2024/2025**. Ongezeko hilo la wanafunzi **764** ni sawa na asilimia **25.7**. Vilevile, katika mwaka **2023/2024** Wanafunzi **1,104** wamehitimu mafunzo hayo ukilinganisha na Wanafunzi **1,174** waliohitimu mwaka **2024/2025 na**

ongezeko hilo ni sawa na asilimia **5.9.** Aidha, wanafunzi wamepata ujuzi katika maeneo ya: uongozi na utawala bora, ujasiriamali, ushirikishaji wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ngazi ya jamii, utatuzi wa migogoro, ujenzi wa barabara kwa kutumia nguvu kazi, usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya madaraja na majengo, upangaji na usimamizi wa miradi.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha dhana ya uanagenzi kwa wanafunzi na jamii zinazozunguka vyuo, Wizara kwa kushirikiana na Ubalozi wa China imegawa vyerehani 258 katika vyuo vinne (4) vya Maendeleo ya Jamii vya Ruaha (60), Rungemba (110), Monduli (60) na Mlale (28). Wataalam nane (8) walipata mafunzo ya ushonaji, ambapo kupitia karakana za vyuo zimewezesha jumla wanagenzi 85 kujifunza ujuzi wa kutengeneza taulo za kike, mikoba pamoja na ushonaji wa nguo mbalimbali. Aidha, Vitotoleshi 225 vimegawiwa katika Makao ya Watoto na Chuo cha Maendeleo Rungemba, ambapo kati ya hivyo 100 vimegawiwa kwenye Makao ya Taifa ya Watoto ya Kikombo, 100 Makao ya Watoto Kurasini na 25 Rungemba.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza programu ya ushirikishwaji jamii inayolenga kutatua changamoto zinazoikabili jamii kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yanayozunguka Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Katika mwaka **2024/2025,** jumla ya wananchi **7,797** walifikiwa na programu hiyo ikilinganishwa na wananchi **6,740** waliofikiwa katika mwaka **2023/2024** sawa na ongezeko la asilimia **13.4**. Wananchi hao walipata mafunzo mbalimbali yakiwemo: upandaji miti; ujasiriamali na masuala ya mikopo; uundaji na usimamizi wa vikundi; uhamasishaji wa kampeni ya makazi bora; elimu kwa jamii na kupiga vita ukatili wa kijinsia; uzingatiaji wa maadili; ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji; matumizi ya bima ya afya; uhamasishaji wa ujenzi wa vituo vya afya; utengenezaji wa mizinga ya kufugia nyuki; na tathmini ya faida za kilimo cha parachichi na ongezeko la kipato cha kaya.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali imeajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii 301 na kufanya idadi yao kufikia 3,976 sawa na asilimia 75 ya mahitaji. Nichukue fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuendelea kuimarisha sekta ya maendeleo ya jamii kwa kutoa fursa ya ajira. ***Natoa rai kwa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wote nchini kuendelea kutekeleza afua za maendeleo ya jamii kwa ushirikiano na Wizara za Kisekta.***

**ENEO LA 2: URATIBU NA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA WAFANYABIASHARA NDOGONDOGO**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia mipango ya kuwezesha na kuendeleza kiuchumi Makundi Maalum ya Wafanyabiashara Ndogondogo. Makundi hayo ni pamoja na wachuuzi wa bidhaa (Machinga); mama na baba lishe; waendesha bodaboda na bajaji; wasusi; washonaji wa nguo; na wafanyabiashara ndogondogo wenye mauzo ghafi yasiyozidi Shillingi Milioni 4 kwa mwaka.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imesajili kwenye mfumo wa kidigitali wafanyabiashara ndogondogo **54,999** (Me 20,140 Ke 34,859) kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi tarehe 08 Mei, 2025 na kufanya jumla ya wafanyabiashara ndogondogo waliosajiliwa kuwa **78,984** (Ke 50,283 Me 28,701). Kati ya hao, 28,287 sawa na asilimia 36 wamepatiwa vitambulisho vya kidigitali vinavyowawezesha kupata huduma za mikopo ya Serikali yenye masharti nafuu inayotolewa kupitia Benki ya NMB ambapo kufikia Aprili 2025, wafanyabiashara ndogondogo **601** (Me 274; Ke 327) wamekopeshwa mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 1,101,650,000** na zoezi hilo linaendelea. Vilevile, maombi **2,092** yanaendelea kuchakatwa yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 3,590,477,000.**

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuwawezesha

wafanyabiashara ndogondogo kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwenye taasisi za fedha, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa na kusambaza Mwongozo wa Utoaji Mikopo yenye Masharti Nafuu kupitia Taasisi za Fedha wa Mwaka 2024. Mwongozo huo unatoa masharti, vigezo na taratibu zinazotumika kutoa mikopo ya Serikali yenye masharti nafuu.

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina mfumo wa kidigitali wa utambuzi, usajili na utoaji wa vitambulisho (WBN-MIS) kwa wafanyabiashara ndogondogo ambao umeunganishwa na mfumo wa Benki ya NMB na hivyo unaondoa uwezekano wa wanufaika kukopa zaidi ya sehemu moja kwa wakati mmoja kwa kuwa mfumo huo unasomana na mifumo mingine na kubadilishana taarifa za walengwa wanaomba mikopo. ***Ninatoa rai kwa waheshimiwa wabunge kuwahamasisha wafanyabiashara ndogondogo katika majimbo yenu kutambuliwa na kusajiliwa ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali ikiwemo mkopo huo.***

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mikopo hii inaratibiwa na kuwanufaisha walengwa, Wizara imeshirikiana na OR – TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Shirikisho la Umoja wa Machinga na Benki ya NMB kuhamasisha na kutoa vitambulisho vya kidijitali ambavyo vinaendelea kuwawezesha wafanyabiashara ndogondogo kunufaika na fursa ya mikopo yenye masharti nafuu. Aidha, Vitambulisho hivyo vimeunganishwa na Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu za walengwa.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kiraia na Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) ilifanya mafunzo rejea kwa ajili ya kuwajengea uwezo viongozi 41 wa Shirikisho hilo kutoka

katika ngazi ya Taifa na Mikoa ili kuimarisha utendaji wao. Mafunzo hayo yalifanyika mwezi Oktoba, 2024.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa mikopo na elimu ya kifedha na ujasiriamali kwa wafanyabiashara ndogondogo kupitia Taasisi za kifedha. Jumla ya mikopo yenye thamani ya **Shilingi Trilioni 1.69** imekopeshwa kwa wafanyabiashara ndogondogo 87,984 katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025**.** Aidha, baadhi ya Madirisha yanayotumiwa kuwahudumia wafanyabiashara ndogondogo ni pamoja na mikopo ya kilimo na biashara kupitia benki ya NMB, mikopo ya vikundi kupitia Tanzania Commercial Bank (TCB); Kua Nasi Loan kupitia Benki ya NBC; IMBEJU ya *CRDB Foundation*; Jikwamue Loan Scheme kupitia Benki ya Azania; na mikopo ya tausi, sokoni, mikopo ya bajaji na bodaboda ya Benki ya Biashara Dar es Salaam (*DCB)*.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI imeendelea kuratibu na kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa Ofisi za Wafanyabiashara Ndogondogo katika ngazi ya Mikoa ambapo hadi kufikia Aprili 2025 mikoa 17 (65.4%) kati ya mikoa 26 imekamilisha ujenzi wa ofisi hizo tofauti na mwaka jana ambapo kipindi kama hiki mikoa tisa (9) tu ndiyo ilikuwa imekamilisha ujenzi huo. Aidha, Mikoa tisa (9) ambayo ujenzi unaendelea na umefikia hatua nzuri ni mikoa ya Iringa, Rukwa, Mtwara, Simiyu, Shinyanga, Singida, Kigoma, Kilimanjaro na Mwanza. Uwepo wa Ofisi hizo ni juhudi za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwajengea mazingira mazuri wafanyabiashara hao katika kuratibu shughuli zao kiuchumi ambapo alitoa kiasi cha **Shilingi Milioni 10** kwa kila mkoa mwaka 2022.

**ENEO LA 3: HAKI NA MAENDELEO YA MTOTO**

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia utoaji wa haki za msingi kwa mtoto ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi, kulindwa dhidi ya vitendo vya ukatili, kuendelezwa katika elimu na vipaji, kushiriki katika

masuala yanayomhusu mtoto kulingana na umri wake na kutokubaguliwa kwa sababu zozote zile kama zilivyoainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008. Aidha, Wizara inaratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya malezi chanya ya watoto na kundi la vijana balehe kwa wazazi au walezi na jitihada za kutokomeza vitendo vya ukatili kwa watoto. Utekelezaji wa majukumu hayo ni kama ifuatavyo:-

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya kisheria kwa kufanya marekebisho ya Sheria Tatu ambazo ni Sheria ya Mtoto, Sura ya 13, Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443, na Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21. Marekebisho hayo yamelenga kuondoa upungufu unaojitokeza katika utekelezaji wa masharti katika sheria husika ili kuimarisha ulinzi na maslahi bora ya mtoto. Aidha, kupitia marekebisho hayo adhabu dhidi ya vitendo vya ukatili zimeainishwa ikiwemo vitendo vya ukatili mtandaoni kifungu cha 13 (3) na (4) ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura ya 443 ambapo atakayebainika kushiriki vitendo vya ukatili mtandaoni atakabiliwa na adhabu ya faini isiyopungua shilingi million 50 au thamani mara tatu ya faida aliyoipata kupitia kitendo hicho au kifungo kisichopungua miaka 7 au vyote kwa pamoja au adhabu nyingine itakayoamriwa na mahakama ikiwemo kulipa fidia ya kiasi kitakachoamriwa na mahakama kwa manusura wa ukatili wa kimtandao.
Aidha, kifungu maalum cha 158A cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kinatoa adhabu kwa makosa ya ukeketaji ambapo atakayebainika kushiriki vitendo vya ukeketaji atakabiliwa na adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni 2 au kifungo kisichopungua miaka 5 na kisichozidi miaka 15 au vyote kwa pamoja au kulipa fidia ya kiasi kitakachoamriwa na Mahakama kwa yule aliyetendewa kosa hilo kwa maumivu aliyosababishiwa.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu mafunzo kuhusu Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa Maafisa 281 ambapo kati ya hao 215

walitoka Mikoa na Halmashauri zote za Tanzania Bara, 14 walialikwa kutoka Zanzibar na 52 ni Maafisa wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi hapa nchini. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuimarisha uwezo katika kusimamia na kuratibu Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM 2021/22 - 2025/26). Aidha, Wizara imetoa mafunzo ya MMMAM kwa Waandishi wa Habari 26 kutoka katika kila Mkoa ambao ni Vinara katika kutoa taarifa za MMMAM ili kuimarisha utoaji wa elimu ya MMMAM katika jamii.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025 jumla ya makala 1,798 kuhusu umuhimu wa MMMAM katika jamii ziliandaliwa na kusambazwa kupitia Magazeti, Redio na Runinga. Vilevile, Wizara imetoa elimu kuhusu Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa Madaktari Bingwa 150 wa Watoto ili kuimarisha afya ya mtoto ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa nguzo kuu tano za malezi na makuzi ya mtoto yaani afya bora. Nguzo nyingine ni lishe bora, ulinzi wa mtoto, elimu na uchangamshi wa awali na malezi yenye mwitikio. Mafunzo hayo yalitolewa wakati wa mkutano wa 25 wa Umoja wa Madaktari Bingwa wa Watoto Tanzania (Paedriatic Association of Tanzania - PAT) mwezi Novemba 2024.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu na kusimamia maandalizi ya Kadi ya Upimaji na Ulinganishaji wa Matokeo ya Utekelezaji wa Wadau wa Programu ya MMMAM (ECD Scorecard) na Dashibodi ya MMMAM kwa lengo la kuimarisha ufuatiliaji wa taarifa za utekelezaji wa PJT- MMMAM na utunzaji wa kumbukumbu za utekelezaji wake nchini. Katika kuhakikisha kuwa Dashibodi hiyo inaeleweka na inatumika katika kuchakata na kuhifadhi taarifa ngazi zote za utekelezaji, Wizara imeratibu mafunzo ya matumizi ya Dashibodi kwa Maafisa 89 kutoka Halmashauri 18 za Mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya katika kipindi cha 2024/2025. Mafunzo hayo yataendelea katika Halmashauri nyingine nchini mwaka ujao wa fedha.

**48. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu mafunzo kwa Maafisa wa Mikoa na Halmashauri pamoja na viongozi wa kidini yanayolenga kuimarisha uelewa wa Wazazi au Walezi kuhusu Wajibu wao kwenye Malezi na Matunzo ya Watoto na Familia kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii (52), Maafisa Ustawi wa Jamii (52), Wauguzi wa Afya ngazi ya Jamii (887), Viongozi wa Dini (84) kutoka Jumuiko la Madhehebu ya Dini Matano (5) ambayo ni Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Baraza la Waislam Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA) na Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT) katika mikoa 12 ya Tanzania Bara. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya Wazazi au Walezi 7,095 (Wanaume 3,497 na Wanawake 3,598) wakiwemo Watu wenye Ulemavu walielimishwa kuhusu wajibu wao katika malezi na matunzo ya mtoto.

**49. *Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mwongozo wa Taifa wa Wajibu wa Wazazi na Familia, Wizara imeendelea kutoa elimu ya malezi chanya kwa jamii kupitia vyombo vya habari, mikutano ya wazi na makongamano yanayohusisha wananchi na mitandao ya kijamii. Aidha, kupitia wataalam mbalimbali na viongozi wa dini (94) wa ngazi ya Taifa walipatiwa mafunzo kuhusu malezi chanya ya watoto kutoka jumuiko la Madhehebu ya Dini Matano (5) kama yalivyoainishwa kwenye aya ya awali. Elimu ya malezi chanya iliwezesha kuendeleza elimu hiyo kwa waumini 3,800,000 kwa njia ya mihadhara na mahubiri katika nyumba za ibada pamoja na warsha na makongamano. Wito wangu kwa wataalamu na viongozi wa dini ni kuendelea kutoa elimu ya malezi chanya ya watoto na familia na kusisitiza mahusiano mema katika ndoa ili kuimarisha huduma za malezi ya watoto katika familia.

**50. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu uanzishaji na uendeshaji wa Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika Shule za Msingi na Sekondari kwa lengo la kuwashirikisha watoto katika kutoa taarifa za viashiria na ukatili wanaofanyiwa. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Madawati 1,682 yalianzishwa ikilinganishwa

na madawati 2,400 yalioanzishwa mwaka wa fedha uliopita hivyo, kufanya kuwa na jumla ya madawati kuwa 4,082 yaliyoanzishwa hapa nchini. Aidha, walimu wa malezi na unasihi 4,700 wamepata mafunzo ya malezi na ulinzi wa watoto sambamba na uanzishaji na uendeshaji wa Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Watoto Ndani na Nje ya Shule.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mabaraza ya Watoto ni jukwaa la kuwakutanisha watoto katika ngazi tofauti kwa lengo la kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa watoto katika kujadili masuala yanayowahusu kulingana na umri wao. Katika kurasimisha Mabaraza hayo, Serikali imeyajumuisha katika Sheria ya Mtoto Sura ya 13 kifungu cha 96 A. Wizara imeratibu uanzishaji na kusimamia uendeshaji wa Mabaraza ya Watoto 595 kwa mwaka huu ikilinganishwa na Mabaraza 865 yaliyoanzishwa mwaka wa fedha uliopita hivyo, kufikia jumla ya Mabaraza 1,460 katika ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa Watoto katika kutoa maoni kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 mwezi Septemba 2024. Jumla ya Watoto 417 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Unguja walitoa maoni na kuyawasilisha Tume ya Taifa ya Mipango ambapo, yameshajumuishwa katika Rasimu ya Dira ya Taifa ya 2050;

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu utekelezaji wa Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza Katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (NAIA; 2021/22 – 2024/25) nchini. Katika kuimarisha uratibu huo, Wizara iliandaa Mkutano wa Mwaka wa Wadau wanaotekeleza Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza Katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe kwa lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa Ajenda hiyo kwa kipindi cha miaka 3 kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024.

Mkutano huo uliofanyika mwezi Oktoba, 2024 ulihusisha Washiriki 245 kutoka Wizara za Kisekta, Taasisi za Serikali,

Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali pamoja na Wawakilishi wa Vijana Balehe kutoka katika baadhi ya mikoa hapa nchini. Aidha, katika Mkutano huo, Wadau kwa pamoja walikubaliana/waliahidi kuongeza uwekezaji ikiwa ni pamoja na fedha na rasilimali zingine ili kuimarisha afuazenye vipaumbele itakazowezesha Vijana Balehe kukabiliana na changamoto za afya zikiwemo, Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na vikwazo vya maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

***54. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa Mwaka mwezi Oktoba, 2024 kwa nchi zenye Programu zinazolenga kundi la Vijana Balehe uliofanyika Duban nchini Afrika ya Kusini uliojulikana kwa jina la *Safeguard Young People Programe (SYP)* wenye lengo la kuchangia jitihada za Serikali za Afrika katika kushughulikia changamoto za Vijana Balehe wenye umri wa miaka 10 – 24. Mkutano huo ulilenga kujengeana uelewa katika maeneo mahususi ambayo ni Vikwazo katika Ustawi wa Vijana Balehe ikijumuisha elimu ya afya ya uzazi, mimba na ndoa za utotoni, maambukizi ya VVU na ukosefu wa usawa wa kijinsia.

***55. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu na kusimamia Kampeni ya Taifa ya Usalama wa Mtoto Mtandaoni (Child Online Protection - COP) katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Kampeni ilikuwa na lengo la kuelimisha Wazazi au Walezi na Watoto wenyewe kuhusu Usalama wa Mtoto anapokuwa anatumia mitandao. Kampeni ya Usalama wa Mtoto Mtandaoni iliambatana na Mafunzo ya Wawezeshaji 516 kutoka ngazi za Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Aidha, Wazazi au Walezi 821,098 walifikiwa na kampeni hiyo; na Wanafunzi 786,901 kutoka Shule za Msingi na Sekondari walipata elimu ya usalama wakati wa kutumia mitandao. Wizara imeunda Kamati ya Taifa ya Ushauri ya Usalama wa Mtoto Mtandaoni kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu afua sahihi za ulinzi na usalama wa mtoto mtandaoni.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa Kukabiliana na Ukatili dhidi ya Watoto Mitandaoni uliofanyika mwezi Desemba, 2024 Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kujadili na kuweka mikakati ya pamoja katika kutokomeza ukatili wa Watoto Mtandaoni. Maazimio ya kikao hicho yamejumuishwa katika Mpango Jumuishi wa Kisekta wa Usalama wa Watoto Mtandaoni (2024/2025 – 2027/2028) ambao utekelezaji wake unaendelea.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa Mawaziri wanaoshughulika na masuala ya watoto uliofanyika Novemba, 2024 Jijini Bogota, Colombia. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kujadili mikakati ya kutokomeza ukatili dhidi ya watoto sambamba na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Katika mkutano huo, nchi iliweka ahadi za vipaumbele ambazo ni kuimarisha ulinzi wa mtoto shuleni; kukabiliana na mila na desturi zenye madhara; na malezi na huduma za uangalizi wa familia. Ahadi hizo zitatekelezwa katika kipindi cha miaka 5 (2024/2025 – 2028/2029).

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za kupinga mila na desturi zenye madhara katika jamii ikiwemo ukeketaji ambapo kwa mujibu wa utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria ya mwaka 2022/2023 inabainisha kuwa, kiwango cha ukeketaji kwa wanawake na wasichana wenye umri wa miaka 15-49 kimeshuka hadi 8% kutoka 10% kwa takwimu za mwaka 2015/16. Aidha, vitendo vya ukeketaji vimepungua katika ngazi ya mikoa vinara ambayo ni; Manyara kutoka 58% hadi 43%, Mara 32% hadi 28%, Singida 31% hadi 20%, na Dodoma 47% hadi 18%.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na jitihada tofauti za kukabiliana na ukeketaji nchini, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Mtoto Sura ya 13 kwa kuingiza kifungu maalum cha 158A kinachotoa adhabu kwa

makosa ya ukeketaji ambapo atakayebainika kushiriki vitendo vya ukeketaji atakabiliwa na adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni 2 au kifungo kisichopungua miaka 5 lakini kisichozidi miaka 15 au vyote kwa pamoja. Vilevile, ataamriwa kulipa faini isiyozidi Shilingi Milioni 1 au vyote kwa pamoja na kulipa fidia ya kiasi kitakachoamriwa na Mahakama kwa yule aliyetendewa kosa hilo kwa maumivu aliyosababishiwa.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imesimamia Kampeni ya Kutokomeza Ukeketaji katika Mkoa wa Mara yenye kaulimbiu: **"Imarisha Ushirikiano; Kutokomeza Ukeketaji**", ambapo jumla ya Wananchi 2,325 wakiwemo Viongozi na Watendaji wa Serikali, Wazazi au Walezi, Watoto, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Kimila, Watu Mashuhuri, Ngariba na Maafisa kutoka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali walishiriki na kupata elimu kuhusu athari za ukeketaji kwa wanawake na wasichana katika kipindi cha 2024/2025. Aidha, Wizara imeratibu ujenzi na uzinduzi wa Kituo cha kuhudumia Manusura wa Ukatili ikiwa pamoja na ukeketaji katika Hospitali ya Wilaya ya Tarime, Mkoani Mara wakati wa maadhimisho ya kupinga ukeketaji Duniani mwezi Februari 2025**.**

## ENEO LA 4: HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa mtu binafsi, familia na makundi mbalimbali katika jamii kwa lengo la kuzuia matatizo na kutatua athari zinazotokana na changamoto mbalimbali. Makundi hayo ni pamoja na wazee na wasiojiweza, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, watoto wanaoishi katika kaya zenye umaskini uliokithiri; watoto waliopoteza mzazi au wazazi; watoto wanaoishi na mzazi au mlezi mwenye maradhi ya muda mrefu; watoto waliotelekezwa; watoto waliozaliwa nje ya ndoa; watoto walio katika familia zenye migogoro; watoto walio katika mkinzano na Sheria pamoja na watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Pia Wizara ina jukumu la kuratibu utendaji wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambayo ndio kitovu

cha utoaji wa elimu na wataalam wa fani za Ustawi wa Jamii nchini. Katika kufanikisha hayo, Wizara imetekeleza yafuatayo: -

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilifanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za matunzo, ulinzi, ushiriki wa wazee kwenye vyombo vya maamuzi katika jamii na taasisi mbalimbali. Sera hiyo iliidhinishwa na Baraza la Mawaziri tarehe 7 Oktoba, 2024 na jumla ya nakala ngumu 600 zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali na nakala tete imewekwa kwenye tovuti ya Wizara. Aidha, Wizara katika kuhakikisha wazee wanashirikishwa katika mipango ya Kitaifa iliwezesha ushiriki wa Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Wazee la Taifa kutoa maoni ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050;

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutoa huduma za matunzo kwa wazee na wasiojiweza 245 (Me 147, Ke 98) katika makazi ya Wazee Kibirizi (Kigoma), Njoro (Kilimanjaro), Kolandoto (Shinyanga), Bukumbi (Mwanza), Ipuli (Tabora), Fungafunga (Morogoro), Mwanzange (Tanga), Misufini (Tanga), Nunge (Dar es Salaam), Nyabange (Mara), Kiliima (Kagera), Sukamahela (Singida) na Magugu (Manyara) yanayosimamiwa na Wizara. Aidha, Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa utoaji wa huduma katika Makazi 15 yanayomilikiwa na Sekta Binafsi yenye jumla ya wahudumiwa 279 (Me 118, Ke 161);

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee tarehe 1 Oktoba, 2024 yenye Kauli Mbiu ya "**Kuzeeka kwa Heshima, Kuimarisha Matunzo na Mifumo ya Kusaidia Wazee**". Maadhimisho hayo yalifanyika katika mikoa yote Tanzania Bara ambayo yaliambatana na makongamano yaliyofanyika kitaifa na kimikoa; utoaji wa huduma za afya; huduma ya afya ya akili; na msaada wa kisaikolojia na kijamii. Aidha, maadhimisho ya Kitaifa yalifanyika Mkoani Tabora na kuhudhuriwa na Washiriki 951;

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) imekamilisha ujenzi wa Jengo lenye Ukumbi na Bwalo la Chakula (Multipurpose Hall) linalotumika kutoa huduma ya chakula, ukumbi wa kukodisha kwa shughuli mbalimbali na sehemu ya mapumziko kwa wazee katika Makazi ya Wazee na Wasiojiweza Fungafunga (Morogoro);

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Wizara ya Afya ilifanya utambuzi wa Wazee na Wasiojiweza **4,975,473** (Wanaume 2,293,263 na Wanawake 2,682,210) na kutoa huduma za kiustawi katika Mikoa 26 kufikia Aprili 2025. Kati ya hao, Wazee na Wasiojiweza **2,199,588** (Wanaume 1,010,076 na Wanawake 1,189,512) wamepatiwa Vitambulisho kwa ajili ya Msamaha wa Matibabu na Bima ya Afya kwa ajili ya kugharamia matibabu.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, jumla ya Watoto 10,782 (Me 6,108, Ke 4,674) wanaoishi na kufanya kazi mtaani waliokolewa kutoka kwenye mazingira hatarishi ya mtaani. Kati ya hao, Watoto 2,410 (Me 1,890, Ke 520) wameokolewa kupitia Kampeni Maalum inayoeendelea kwenye mikoa yote nchini iliyoanza rasmi tarehe 7 Aprili 2025 kuelekea Siku ya Kimataifa ya Watoto Waishio na Kufanya Kazi Mitaani iliyofanyika kwa mara ya kwanza Kitaifa Mkoani Mtwara na iliyokuwa na Kauli Mbiu ya Imarisha Ushirikiano Kuzuia Mtoto Kuishi Mtaani. Watoto waliookolewa wamepatiwa huduma mbalimbali mathalani kupatiwa makazi ya muda katika Makao ya Watoto, Nyumba Salama 17 zilipo nchini, Walezi wa Kuaminika (1,803) na kuwaunganisha na familia zao baada ya kufuatilia usalama wa familia hizo. Aidha, Watoto 1,346 kati ya waliookolewa walipatiwa Vifaa vya Shule na mahitaji mbalimbali huku 56 kati yao waliunganishwa na Vyuo vya Ufundi ambapo 43 wamehitimu.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mikoa inayoongoza kuwa na watoto wengi wanaoishi na kufanya kazi Mtaani ni Dar es

Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na Iringa huku Mikoa inayoongoza kuchangia maeneo ya miji kuwa na watoto zaidi ni Kagera, Geita, Kigoma, Dodoma, Mwanza na Shinyanga. Vilevile, Wizara imeandaa Kanuni za Utendaji (Standard Operating Procedure - SOP) za namna ya kushughulikia changamoto za Watoto waishio na Kufanya Kazi Mtaani;

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeanzisha Madawati mapya 11 kwenye Stendi za mabasi na Bandari kwa ajili ya kudhibiti usafirishaji haramu wa watoto na kudhibiti watoto kuishi na kufanya kazi mtaani katika Mikoa 10 ya Tabora, Mbeya, Dodoma, Kagera, Arusha, Morogoro, Ruvuma, Shinyanga, Njombe, na Dar-es-Salaam ambayo yatashughulikia Watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani. Hivyo, kufikia madawati 14 yakijumuisha madawati matatu (3) ya awali yaliyoanzishwa katika Mikoa ya Mwanza (2) na Dar es Salaam (1);

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imesimamia na kutoa mahitaji ya msingi ya huduma za afya ikiwa ni pamoja na kuwapatia bima za afya (NHIF) watoto 252 (Me 153 na Ke 99) waliopo kwenye makao ya Taifa ya Watoto ya Kikombo na Kurasini yanayosimamiwa na Wizara kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya. Aidha, Wizara imetoa huduma nyingine za msingi ikiwemo elimu, malazi, chakula, mavazi na msaada wa kisaikolojia na kijamii kwenye makao hayo;

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imesajili Makao ya Watoto 14 na kuhuisha leseni za Makao Binafsi 32 yenye jumla ya Watoto 834 (Me 409 na Ke 425) na kufanya jumla ya Makao 388 yaliyosajiliwa nchini. Makao hayo yamehudumia watoto 14,215 (Me 7,102 na Ke 7,113) walio katika mazingira hatarishi kwa muda maalum kufikia mwezi Aprili 2025. Vilevile, Wizara imekamilisha mapitio ya Mwongozo wa Taifa wa Uanzishaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Makao ya Watoto wa mwaka 2006 toleo la Mwaka 2024 kwa lengo la kuboresha huduma katika Makao ya Watoto;

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanzisha Kamati ya Kitaifa yenye Wajumbe 16 kutoka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi yenye lengo la kuratibu afua za Watoto Wanaoishi na Kufanya Kazi Mtaani ambapo, Kamati hii niliizindua tarehe 15 Novemba, 2024 kwa lengo la kuimarisha ushiriki na ushirikiano wa Sekta Binafsi kwenye utekelezaji wa Mipango na Mikakati ya Serikali. Kamati hii inaongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Kamishna wa Ustawi wa Jamii toka upande wa Serikali na Mwenyekiti Mwenza ambaye ni Shirika la Railway Children Africa (RCA) toka Sekta binafsi.

Kamati hii imeendelea kuongeza kasi ya uratibu wa utekelezaji wa afua za kudhibiti watoto kwenda kuishi na kufanya kazi mtaani ambapo kwa mara ya kwanza nchini imeratibu Wadau kushirikiana na Serikali kuadhimisha Kitaifa Siku ya Mtoto Anayeishi na Kufanya Kazi Mtaani tarehe 12 Aprili, 2025 Mkoani Mtwara. Maadhimisho haya yalienda sambamba na uzinduzi wa Kampeni Endelevu ya Kitaifa ya kudhibiti na kuokoa Watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani ambapo kama nilivyotangulia kueleza awali kwenye Aya ya 67, kufikia 28 Aprili, 2025 Watoto 2,410 (Me 1,890, Ke 520) wameokolewa kupitia kampeni hiyo inayoendelea.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru Wadau wote walioshiriki katika afua za kudhibiti wimbi la Watoto Wanaoishi na Kufanya Kazi Mtaani wakiwemo Railway Children Africa, SOS Children Village, Amani Centre for Street Children, Global Child Advocate, Compassion Tanzania, Amani Girls, Save The Children, UNICEF, IRC, United Help for Tanzania, African Women Aids Working Group, Kao la Amani, Umoja wa Bodaboda, SMAUJATA, Wamiliki wa Makao ya Watoto, Wamiliki wa Vituo vya Kulelea Watoto Mchana, Viongozi wa Dini, na vyombo vya habari ikiwemo Radio, Televisheni na radio za Kijamii. Pia napenda kuzishukuru Wizara za Kisekta, OR-TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Sheria na Katiba, Wizara ya Elimu na Teknolojia na Wizara ya

Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kuzitaja kwa uchache.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha uratibu wa Malezi Mbadala ya Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, ambapo jumla ya Watoto 103 wamepatiwa huduma ya Malezi ya Kambo na Kuasiliwa katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025. Kati ya Watoto hao, Watoto 41 (Me 19, Ke 22) waliasiliwa, 62 (Me 24, Ke 38) walipata walezi wa kambo. Vilevile, Jumla ya Watoto 586 (Me 279, Ke 307) waliwekwa chini ya uangalizi wa walezi wa kuaminika kutokana na changamoto za malezi na ukatili katika jamii na jumla ya watoto 1,310 (Me 702, Ke 608) waliopo katika makao ya watoto waliunganishwa na familia zao kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025;

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii walioko katika Halmashauri zote nchini pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria imeendelea kuhudumia kesi za watoto katika Mahakama za watoto 141 ambapo, jumla ya kesi za watoto 711 zilisajiliwa na kati ya hizo, kesi za watoto 597 zimesikilizwa na kufungwa na kesi 114 zinaendelea kusikilizwa katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025. Aidha, Wizara imetoa huduma za marekebisho ya tabia kwa watoto 104 (Me 102, Ke 02) waliokinzana na Sheria katika Mahabusu 5 za Arusha, Mbeya, Tanga, Moshi na Upanga. Watoto 34 wanaendelea kupatiwa huduma za marekebisho ya tabia katika Shule ya Maadilisho Irambo mkoani Mbeya.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Wizara za Kisekta na Wadau wa Maendeleo imefanya Mkutano Mkuu wa mwaka wa Maafisa Ustawi wa Jamii Tanzania kuanzia tarehe 18 hadi 20 Septemba, 2024 katika Ukumbi wa Chuo cha Polisi Mkoani Kilimanjaro. Mkutano huo uliwakutanisha Maafisa Ustawi wa Jamii 1,450 na Wadau mbalimbali wanaotoa huduma za Ustawi wa Jamii ambapo walijadili na kubadilishana uzoefu wa masuala mbalimbali katika kuboresha huduma za ustawi wa jamii;

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI imehudumia jumla ya watu 889,031 kwa kuwapatia msaada wa kisaikolojia na kijamii ikihusisha makundi yote wakati wa dharura na wakati wa utoaji wa huduma zote za Ustawi wa Jamii kuanzia ngazi ya kijiji hadi Taifa kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025. Wizara imetoa huduma ya afya ya akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii kwenye janga la kuporomoka kwa jengo la ghorofa katika eneo la Kariakoo Jijini Dar-es-Salaam, ambapo jumla ya waathirika 2,852 (Me 1,832, Ke 1,020) walihudumiwa. Vilevile, jumla ya waathirika 4,313 wa ugonjwa wa kipindupindu katika mikoa ya Simiyu, Kagera, Katavi, Mbeya, Rukwa na Mwanza walihudumiwa na kuunganishwa na huduma stahiki. Aidha, wahanga 342 wa mlipuko wa ugonjwa wa Marburg katika Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Biharamulo walipatiwa Makazi ya Muda na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii;

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa huduma za Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii kwa Wahudumiwa **22,998** (Me 11,553, Ke 11,445) katika Makazi ya Wazee, Makao ya Watoto, Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Mahabusu za Watoto, Shule ya Maadilisho na Watoto Wanaoishi na Kufanya Kazi Mtaani, ili kuimarisha hali ya afya ya akili na kutatua migogoro;

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshughulikia jumla ya Migogoro ya Ndoa 97,234 hadi kufikia Aprili, 2025 kupitia Kitengo cha Ustawi wa Jamii katika ngazi ya Halmashauri hadi Taifa ambapo, kati ya mashauri hayo mashauri 81,820 yalipatiwa ufumbuzi na mashauri 15,414 yalipelekwa mahakamani kwa hatua zaidi. Idadi ya Mashauri yaliyopokelewa imeongezeka ikilinganishwa na Mashauri 31,380 yaliyowasilishwa katika kipindi kama hiki cha mwaka 2023/2024 na ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa elimu kwa umma na uelewa wa jamii kuhusu kutoa taarifa za ukatili badala ya kuficha na hatua hii imechangiwa na kuendelea kuimarika kwa huduma za Ustawi na Maendeleo ya Jamii nchini,

kuimarika kwa mifumo ya hamasa na utoaji wa taarifa katika jamii kupitia kampeni zinazotekelezwa na Serikali na Wadau mbalimbali, kuongezeka kwa ajira za Maafisa Ustawi na Maendeleo ya Jamii mpaka ngazi ya kata na kasi kubwa ya Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid).

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshughulikia Mashauri 2,733 ya Watoto katika Mahakama za Watoto Dar es Salaam, Mbeya na Mahakama Jumuishi Temeke. Mchanganuo wa Mashauri hayo ni kama ifuatavyo: 1,038 matunzo, 975 amri ya malezi (custody), 615 amri ya kuona mtoto (access), 14 kuasili, 12 kupima vinasaba, 21 ulezi, 3 amri ya uangalizi, 41 kukazia hukumu (enforcement of order) na 14 nyinginezo. Aidha, mashauri ya watoto 6,556 (Me 2,781 na Ke 3,775) yalishughulikiwa na Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI katika mahakama za watoto 141;

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu na kusimamia utendaji wa Kituo cha Huduma kwa Wateja ambapo simu 917,804 zilipokelewa katika Kituo cha Msaada wa Simu kwa Watoto kupitia namba mahsusi ya bila malipo ya kutoa taarifa zinazohusu uhitaji wa msaada kwa Watoto ambayo ni namba **116** (Child helpline). Kati ya simu hizo hizo zilizopokewa, simu 916,758 zilihusisha uhitaji wa huduma ya ushauri na unasihi, masuala ya malezi na makuzi ya watoto, lishe, afya ya uzazi kwa vijana, msaada wa kisaikolojia, masuala ya elimu na maombi ya maelekezo ya kupata huduma za ustawi wa jamii na Simu 1,046 zilitoa taarifa za matukio ya ukatili dhidi ya watoto ambayo yaliunganishwa na wataalam na kuhudumiwa.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia (Kituo cha Wizara cha Mawasiliano ya Simu na Jamii) (*Call Centre)* jumla ya Mashauri 1,189 yalipokelewa na kushughulikiwa. Kwa upande mwingine, mwamko wa Wananchi kutumia mitandao ya kijamii na Vyombo vya Habari umeongezeka na Wizara imeendelea kupokea na kufanyia kazi taarifa hizo za Wananchi ambapo jumla ya

Mashauri 259 yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Tunawashukuru Wananchi kwa mwamko huu na pia, tunawahimiza pia kukumbuka na kuendelea kutumia mifumo yote iliyopo sambamba na namba **116** na namba za Kituo cha Wizara ambazo ni 0262160250, 0734986503, 0766400168, **0769608130 na 0774112233**.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta pamoja na wadau imeendelea kuratibu huduma kwa manusura wa vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya Manusura 19,717 waliripotiwa wakiwemo Watoto 7,278 (Me 1,373, Ke 5,905) na Watu Wazima 12,439 (Me 4,472, Ke 7,967) ambao, wote walipata huduma katika Madawati ya Jinsia na Watoto ya Polisi nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Wadau mbalimbali imeendelea kutoa huduma katika Vituo Jumuishi 30 katika Hospitali za Serikali na Vituo vya Afya ambapo jumla ya Wahanga wa Ukatili 256,797 wamehudumiwa. Vilevile, Wizara imeratibu uanzishwaji wa Vituo Jumuishi viwili (2) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Kishapu Shinyanga; hivyo kufanya vituo hivyo kufikia 32;

**84.** ***Mheshimiwa Spika;*** kufuatia jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kupinga ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, matokeo chanya yanaonekana yakiwemo kupungua kwa vitendo vya ubakaji kutoka matukio 8,185 mwaka 2023 hadi matukio 7,670 mwaka 2024 ikiwa ni sawa na kupungua kwa asilimia 6.3. Matukio ya Ulawiti nayo yamepungua kutoka 2,382 mwaka 2023 hadi 1,930 mwaka 2024 sawa na kupungua kwa asilimia 19. Aidha, matukio ya kutupa Watoto Wachanga yamepungua kutoka 183 mwaka 2023 mpaka 173 mwaka 2024 ambapo ni sawa na kupungua kwa asilimia 7. Wizara itaendelea kuongeza kasi ya kuratibu Wadau wengi zaidi wa sekta zote ikiwemo sekta binafsi ili kuendelea kuongeza kasi ya mapambano kwenye kutokomeza ukatili wa kijinsia na kwa watoto.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza Programu ya Kizazi Chenye Usawa (GEF) yenye lengo la kuimarisha uchumi wa mwanamke ili kuchangia maendeleo ya familia na Taifa kwa ujumla. Katika kufanikisha hili, Wizara kwa kushirikiana na Wadau inatekeleza afua za uanzishaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ili kumpatia nafuu mwanamke na muda wa kujishughulisha na uzalishaji mali. Wizara imehamasisha uanzishwaji na usajili wa Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana (Early Childhood Development Centers - ECD) 432 vyenye jumla ya Watoto 6,154 (Me 2,573 na Ke 3,581) na kufanya jumla ya Vituo kuwa 4,178 vyenye jumla ya Watoto 462,670 (Ke 232,613, Me 230,057) vilivyoanzishwa na kusajiliwa kati ya Vituo 4,400 vilivyopangwa kusajiliwa katika mikoa yote nchini ifikapo Juni 2025, ikiwa ni ongezeko la 6% ya watoto walioandikishwa ukilinganisha na watoto 397,935 (Me 175,517 na Ke 222,418) walioandikishwa kufikia Aprili 2024.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu Wadau katika utoaji wa Zawadi za Sikukuu za mwisho wa mwaka, Pasaka, Eid ul-fitr kwa Makundi Maalum katika Makao ya Watoto, Makazi ya Wazee na Wasiojiweza na Vituo vya Watu Wenye Ulemavu ikiwa ni juhudi za kuunga mkono jitihada za **Mheshimiwa Dkt. Samia Sululu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhudumia makundi Maalum. Katika kufanikisha hilo, Wadau walichangia Fedha na mahitaji mbalimbali yenye thamani ya **Shilingi 166,317,000** kwa ajili ya makundi hayo na kupelekwa katika Vituo vya kijamii 281 (275 Tanzania Bara na 6 Zanzibar).

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2024/25 Serikali iliajiri Maafisa Ustawi wa Jamii 178 na Maafisa Ustawi wa Jamii Wasaidizi 176 na hivyo kufanya idadi ya wataalamu hao kufikia 2,328. Nichukue fursa hii kuwapongeza Maafisa Ustawi wa Jamii wote nchini walioratibu na kutekeleza afua na kutoa huduma za ustawi wa jamii.

## ENEO LA 5: MAENDELEO YA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE

**88.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika kutekeleza Ajenda ya Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi inaratibu na kutekeleza programu na afua mbalimbali zenye lengo la kukuza usawa na kuimarisha wanawake na wasichana kushiriki katika nyanja zote za maendeleo. Programu na afua hizo ni Programu ya Kizazi Chenye Usawa, Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, Mpango wa Wanawake Amani na Usalama, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi na maamuzi.

**89.** ***Mheshimiwa Spika*** katika kuhakikisha kuwa sekta ya umma na binafsi zinajumuisha na kuzingatia masuala ya jinsia kwenye Sera, Mipango na Bajeti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imewajengea uwezo viongozi na watendaji wa ofisi hiyo kuhusu ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika ukaguzi wa hesabu za Serikali ili kuwa na taarifa ya kina ya Sekta zinavyozingatia na kutekeleza masuala ya jinsia nchini.

**90.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha majeshi yetu pia yanazingatia usawa wa kijinsia, Wizara imewezesha Jeshi la Magereza na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuandaa Mkakati wa ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika majeshi hayo ambao unatoa mwelekeo wa kimkakati wa utekelezaji wa afua mbalimbali ili kufikia usawa wa kijinsia.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kukuza haki na usawa wa kiuchumi, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta inaendelea kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Tanzania ya Kizazi Chenye Usawa 2021/2022 – 2025/2026 (Tanzania Generation Equality Programme - TGEP) ambayo inatekelezwa na wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Taasisi za Umma na Binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wadau wa Maendeleo.

Programu inatekeleza maeneo makuu manne (4) ambayo ni uwekezaji wenye mrengo wa kijinsia katika huduma na kazi za matunzo kwenye sekta za umma na binafsi, kazi zenye staha, upatikanaji na umilikishaji wa rasilimali za uzalishaji kiuchumi kwa wanawake, mipango ya uchumi jumuishi, maboresho ya kibajeti na vichocheo vya kiuchumi kwa kaya maskini vinavyozingatia jinsia. Matokeo ya maeneo haya yameainishwa katika utekelezaji wa sekta mbalimbali kama ilivyofafanuliwa kwenye aya zinazofuata.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wanawake kama mojawapo ya kundi linaloathirika kwa wingi kutokana na matumizi ya nishati isiyo salama, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanya uhamasishaji nchini kote kupitia makongamano, maonesho, vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii. Hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya mitungi ya gesi **402,000** na majiko banifu **206,713** yametolewa bure kupitia jitihada mbalimbali za Serikali na Wadau katika kutekeleza Mkakati wa Kitaifa ya Nishati Safi (2024-2034) ambao **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kinara wa kuwezesha nishati safi kwa wanawake Barani Afrika.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuongezeka kwa upatikanaji wa nishati ya umeme katika maeneo ya vijijini kumechochea wanawake kuanzisha miradi ya ujasiriamali ikiwemo viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yao, ambapo hadi kufikia Aprili 2025, vijiji *12,318* na vitongoji 33,657 kati ya vitongoji 64,359 vimefikiwa na huduma hiyo ya umeme. Aidha, uwepo wa nishati vijijini umeimarisha huduma za kifedha, masoko, mawasiliano ya simu, pamoja na kurahisisha upatikanaji wa habari kupitia runinga, redio na mitandao ya kijamii hivyo, kuwawezesha wananchi kufahamu mipango na maendeleo yanayofanywa na Serikali yao.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kumpunguzia mwanamke muda wa utafutaji maji na kushiriki katika shughuli za kiuchumi, programu hiyo imeendeleza jitihada za

usambazaji wa maji mijini na vijijini ambapo, upatikanaji maji safi na salama kwa maeneo ya vijijini ni asilimia 83 na mijini ni asilimia 91.6. Aidha, ushiriki wa wanawake katika vyombo vya utoaji huduma ya maji ngazi ya jamii (Community Based Water Supply Organization - CBWSO) umeendelea kuongezeka na kufikia jumla ya wanawake 1,915 kati ya watumishi 6,541 walioajiriwa. Ushiriki wa wanawake katika sekta hii ya maji umeimarisha utendaji wa vyombo hivyo katika kuzingatia mahitaji ya kijinsia.

**95. *Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye uvuvi na mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Wizara ya Mifugo na Uvuvi imehamasisha na kutoa boti 160 za uvuvi kwa vikundi vya wanawake vinavyojishughulisha na uvuvi ambapo kati ya wanufaika 3,163, Wanawake ni 1,008 (32%). Hii ikiwa ni mkakati wa kuweka mazingira wezeshi ya ushiriki wa wanawake katika sekta ya uvuvi.

**96. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kuwezesha fursa za upatikanaji wa elimu hasa kwa wasichana/wanawake, imeongeza udahili wa wanafunzi katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi ambapo hadi kufikia Aprili 2024, wasichana 66,588 kati ya 130,886 sawa na asilimia 50.87 walidahiliwa.

Vilevile, katika vyuo vya ufundi na masomo ya ufundi stadi jumla ya wasichana 191,794 kati ya wanafunzi 248,457 sawa na asilimia 77.2 wamejiunga na vyuo hivyo ikiwa ni hatua kubwa katika maendeleo ya ushiriki wa mtoto wa kike kwenye mafunzo ya ufundi stadi. Kwa upande wa elimu ya juu, jitihada za Serikali zimeimarisha uwiano wa wanafunzi wa kiume na kike ambapo kati ya wanafunzi 334,854 waliodahiliwa kwa mwaka 2024, wanafunzi pekee wa kike ni 150,543 sawa na asilimia 45. Uwiano huo unaashiria uelewa na mwamko wa jamii katika kutambua na kuthamini haki na maendeleo ya mtoto wa kike.

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha watoto wote wanapata haki ya elimu, Serikali inatekeleza mpango wa kuwarejesha wanafunzi waliokatiza masomo ya elimu ya msingi na sekondari kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujauzito na utoro ambapo jumla ya wanafunzi 10,864 (Me 5,722 Ke 5,142) walirejeshwa shuleni hadi kufikia Aprili 2024. Jitihada hizi kwa pamoja na uanzishwaji wa shule 26 za Sayansi za wasichana za bweni zilizojengwa mikoa yote Tanzania Bara zenye uwezo wa kusajili wanafunzi 1,000 kwa kila shule zitaimarisha elimu kwa mtoto wa kike hasa kwa mchepuo wa sayansi.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza Mpango wezeshi wa masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati (*STEM Outreach Program)* unaohamasisha wanafunzi wa kike kupenda masomo hayo na Programu ya (Structured Engineers Apprenticeship Program - SEAP) inayosimamiwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB). Programu hizo zimejikita kuwezesha wanawake na wasichana kujiunga, kujiendeleza na kupata ujuzi wa kazi katika fani zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi ngazi ya vyuo vikuu ili kuongeza wasichana wenye sifa, ujuzi na wanaoajirika katika sekta ya ujenzi. Wahandisi wanawake waliosajiliwa ni 1,044 kati ya Wahandisi Wataalam 9,832 sawa na asilimia 10.6 hivyo, Serikali itaendeleza jitihada za kusomesha wanawake na wasichana katika masomo ya STEM ili kuongeza idadi ya wanasayansi wanawake na wasichana.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara hii, Wizara ya Madini na Shirika la Madini la Taifa imewezesha upatikanaji wa vifaa na leseni ya uchimbaji madini kwa vikundi 43 vya wanawake vyenye wanachama 1,290. Pia, vikundi 20 vyenye wanachama zaidi ya 600 vimepatiwa vitalu vya madini kwenye machimbo ya madini ya Mbogo na Geita kwa lengo la kuimarisha uchumi kwa wanawake. Uwezeshaji huo umewezesha wanawake kushiriki katika sekta ya madini.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na vifo vya

wajawazito na watoto, Serikali inatekeleza Programu ya M-MAMA inayowezesha huduma ya Usafiri wa dharura kwa Mama Wajawazito na Watoto Wachanga. Hadi kufikia Aprili, 2025. Jumla ya akinamama wajawazito 110,722 na watoto wachanga 24,537 wamehudumiwa. Aidha, huduma za M-MAMA zimeongeza idadi ya kinamama kuhudhuria kliniki. Vilevile, utekelezaji wa elimu ya afya unaofanywa na Wataalam wa Maendeleo ya Jamii pamoja na Afya umechochea kuongezeka kwa mahudhurio ya wajawazito wanaohudhuria kliniki kikamilifu hadi kufikia wajawazito 3,143,332 mwaka 2024 ukilinganisha na 2,374,666 mwaka 2020.

**101.** ***Mheshimiwa spika,*** Kuimarika kwa huduma za uzazi, mama na mtoto kumepelekea kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga kwa kiwango kikubwa ambapo vifo vya wajawazito vimepungua kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 hivi sasa. Mafanikio haya yamepelekea dunia kutambua jitihada za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kuwa mfano bora Afrika katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na kupata tuzo ya ‘’**The Gates Goal Keepers Award’’**

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Tanzania *Women Chamber of Commerce* (TWCC) inatekeleza Programu ya iSOKO inayowezesha wanawake wajasiriamali kupata taarifa za masoko ya bidhaa na huduma ndani na nje ya nchi kwa njia ya kidijitali. Mfumo wa iSOKO unaratibiwa na TWCC na hadi kufikia Aprili 2025, idadi ya Wanawake wafanyabiashara 4,320 wamejisajili kupitia simu zao za mkononi na wanapata taarifa za masoko, idadi hii imeongezeka kutoka 11,500 kwa mwaka 2023/2024 na kufikia 15,820 Aprili 2025.

**103.** ***Mheshimiwa Spika***, Sheria ya Ununuzi wa Umma (2023), inaelekeza Taasisi kutenga asilimia 30 ya zabuni zote kwa ajili ya makundi maalumu wakiwemo Wanawake. Wizara katika kuratibu utekelezaji wa sheria hii inashirikiana na Wizara ya Fedha na Mamlaka ya

Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), ambapo hadi kufikia Aprili 2025, vikundi **231** vya wanawake vimenufaika na zabuni za umma zenye thamani ya **Shilingi bilioni 3.3** ikilinganishwa na vikundi 33 vilivyonufaika na zabuni za umma zenye thamani ya **shilingi bilioni 1.4** kwa mwaka 2023/2024. Kuwezeshwa kwa vikundi hivyo kumesaidia wanawake kujiajiri, kuwezesha utekelezaji wa shughuli za vikundi na kuongeza kipato chao. ***Natoa wito kwa wanawake walio katika vikundi nchini kutumia fursa hii ya kisheria kwa kuomba zabuni zinazotangazwa na Taasisi za Umma.***

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwapatia wanawake mitaji na mikopo yenye masharti nafuu ili kujiendeleza kiuchumi, Serikali inaendelea kuhamasisha Wanawake kujiunga na kujisajili katika vyama vya kuweka na kukopa zikiwemo SACCOS, VICOBA, Huduma ndogo za kifedha (CMGs), Mifuko na Programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Aidha, Mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi iliyopo chini ya Uratibu wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ni 75 ikijumuisha mifuko 63 inayomilikiwa na Serikali na Mifuko 12 iliyo chini ya Sekta Binafsi. Hadi Aprili 2025, mikopo yenye thamani ya Shilingi trilioni 3.5 imetolewa ambapo kiasi cha **Shilingi trilioni 1.7** sawa na 49% imetolewa kwa Wanawake na kwa upande wa Wanaume zilitolewa **Shilingi trilioni 1.8** sawa na 51%.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Kilimo katika kutekeleza Programu ya Kizazi Chenye Usawa imeendelea kuchochea ushiriki wa wanawake ikizingatiwa kuwa sekta hii imeajiri takribani wanawake kwa asilimia 65.6, ambao huchangia takriban asilimia 26.1 kwenye Pato la Taifa. Kupitia Programu ya *Building a Better Tomorrow* (BBT) kwenye kilimo, jumla ya wanawake vijana 255 kati ya vijana 716 wamewezeshwa ardhi zenye ukubwa wa ekari tano (5) kila mmoja kwa ajili ya matumizi ya kilimo cha kisasa ili kuongeza ajira na kipato.

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuwajengea uwezo wanawake wajasiriamali, Wizara kwa kushirikiana na

Chama cha Wanawake Wafanyabiashara (Tanzania Women Chambers of Commerce -TWCC) iliwezesha Wanawake Wajasiriamali 375 kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Saba Saba yaliyofanyika Dar es Salaam kuanzia 01 – 13 Julai, 2024. Aidha, wanawake wajasiriamali **163** waliwezeshwa kushiriki Maonesho ya Kilimo na Sherehe za Wakulima Nanenane yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Dodoma Agosti, 2024. Maonesho hayo yametoa fursa kwa wanawake kuongeza masoko na kukuza mitaji yao.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** **kwa Mara ya Kwanza Nchini,** kuelekea Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kuanzia tarehe 01 - 08 Machi, 2025 Wizara iliratibu Makongamano ya Kitaifa katika Kanda Saba (7) yaliyofunguliwa na Viongozi wa Kitaifa. Hii ni hatua kubwa katika kusogeza karibu zaidi na wananchi sauti ya wito wa wanawake kushiriki shughuli za maendeleo na mchango wao kusikika kwa sauti kubwa zaidi.

Makongamano haya yalifanyika Dodoma (Kanda ya Kati), Dar es Salaam (Kanda ya Mashariki), Geita (Kanda ya Ziwa), Lindi (Kanda ya Kusini), Kigoma (Kanda ya Magharibi), Mbeya (Kanda ya Nyanda za Juu Kusini) na Arusha (Kanda ya Kaskazini) na yalihusisha matukio mbalimbali ikiwemo ugawaji wa Mitungi ya gesi 6,000 na majiko banifu 800; na maonesho ya wajasiriamali yaliyoshirikisha waoneshaji 409. Aidha, Wananchi waliohudumiwa ni 30,102 (Me 13,797 na Ke 16,305); Vilevile, kulikuwa na uwasilishwaji wa Mada mbalimbali kulingana na kaulimbiu zilizochaguliwa kwa kila Kanda.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Wanawake Duniani yalihusisha shughuli na huduma mbalimbali ikiwemo hamasa, michezo na burudani, huduma za afya ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa magonjwa ya moyo kwa watoto walioko tumboni, uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na matiti, afya

ya akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii, magonjwa ya ndani, huduma za uzazi, huduma za lishe, uchunguzi wa kifua kikuu. Washiriki na wanufaika wa huduma zilizotolewa walikuwa 44,590 (Me 8,079 na Ke 36,511)

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** kilele cha maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Wanawake Duniani kilichofanyika katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sheikh Amri Abeid Kaluta Mkoani Arusha Tarehe 8 Machi, 2025. Mgeni rasmi alikuwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kaulimbiu ilikuwa **''Wanawake na wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji''**. Kaulimbiu hii ililenga kuhamasisha jamii katika kukuza usawa, haki na uwezeshaji wa wanawake na wasichana. Aidha, Maadhimisho hayo yalifanyika ikiwa ni sehemu ya kufanya tathmini ya miaka 30 ya utekelezaji wa Azimio na Ulingo wa Beijing ambapo Tanzania iliridhia maazimio hayo mwaka 1995. Jumla ya Wananchi 83,497 walishiriki.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatoa shukrani kwa Wadau wote waliofanikisha maadhimisho hayo wakiwemo NMB- Bank, CRDB – Bank, CRDB Foundation, BARRICK, AZAM, STATE OIL, AZANIA Bank Ltd, EQUITY, UN WOMEN, ASAS GROUP OF COMPANIES, NBC – Bank, Kamal, AFROIL, TOTAL Energies, TCB Bank, UNFPA, ESTATES TANZANIA, Kampuni ya Madini ASM – Tanzania na Bowmans Tanzania. Shukrani ziende kwa wajumbe wote wa kamati ya Kitaifa ya uratibu wa maadhimisho wakiongozwa na Bi. Sarah Masasi, Mwenyekiti wa Kamati na Mlezi wa Chama cha Wanawake Wachimbaji Wadogo wa Madini (TAWOMA). Vilevile kupitia OR-TAMISEMI shukrani ziende kwa Mheshimiwa Paul Christian Makonda Mkuu wa Mkoa wa Arusha ambaye alikuwa mwenyeji wa maadhimisho hayo. Shukrani kwa wananchi wote walioshiriki maadhimisho hayo.

Aidha, kutokana na muda, sio rahisi kumtaja kila mdau hivyo, shukrani ziende kwa wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya maboresho ya utaratibu wa utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na kuja na utaratibu mpya unaotaka kila mkoa kuwasilisha vikundi vya wanawake wajasiriamali vitakavyopatiwa mkopo. Lengo la maboresho haya ni kuhakikisha walengwa wa kila mkoa wananufaika na fursa hiyo. Kufuatia maboresho hayo, katika kipindi cha 2022/2023 hadi 2024/2025 Wizara ilitoa mikopo ya kiasi cha **Shilingi 704,500,000.00** na imeendelea na ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hiyo ambapo, **Shilingi 247,156,702.00** zimerejeshwa sawa na asilimia 37.2 ya marejesho hadi kufikia Aprili 2025. Mikopo hii yenye masharti nafuu ya riba ya asilimia 4 hutolewa kwa wanawake wajasiriamali waliojiunga kwenye Vikundi na Mwanamke mmoja mmoja kwa lengo la kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

Hivyo, baada ya maboresho hayo, Wizara inatarajia kuanza kutoa mikopo kwa mwaka 2025/2026 kwa waombaji wanaoipitisha maombi yao kupitia kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Halmashauri. **Hivyo, *ninapenda kutoa wito kwa wanawake wote waliokopeshwa na watakao kopeshwa kuzingatia masharti ya mikopo kwa kufanya marejesho kwa mujibu wa mikataba. Aidha, ninatoa wito kwa Vikundi na Wanawake mmoja mmoja wanaodaiwa fedha za Mfuko kurejesha mikopo yao kwa makubaliano yaliyowekwa ili kuuwezesha Mfuko kuwafikia wanawake wengi zaidi nchini.***

**112.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuratibu Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi kupitia Mikopo isiyo na riba ya asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Hadi

kufikia Aprili, 2025, Shilingi **bilioni 82.83** zilikopeshwa kwa Vikundi 8,275 vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 40.71 zilitolewa kwa Vikundi 4,557 vya Wanawake.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuendelea kuimarisha Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ilifanya maboresho ya Mwongozo wa Uundaji na Uratibu wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi wa mwaka 2022 ili uweze kukidhi matakwa ya sasa. Hadi kufikia Aprili 2025, Wizara imewapatia mafunzo Viongozi na Waratibu wa Jukwaa katika mikoa 26 ili waweze kueneza na kufanya uhuishaji wa Majukwaa kulingana na Mwongozo huu mpya.

Aidha, Wizara imeunda Kamati ya Kitaifa ya Uhamasishaji wa Uundwaji wa Majukwaa inayoongozwa na Mwenyekiti Bi. Lilian Mtali Mkurugenzi wa Masoko wa Benki ya Taifa ya Biashara (TCB) na Mlezi wake Dkt, Judith Mhina kutoka Sekta Binafsi. Kamati hii ni ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ambapo, imekuja na Kampeni ya kuongeza kasi ya Uundwaji wa Vikundi na Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi yenye Kauli Mbiu ya **Wanawake "Inuka–Imarika–Tusua Kiuchumi" itakayotekelezwa kwa miaka 5 kuanzia mwaka 2025**.

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliratibu uandaaji wa Mpango wa Kitaifa wa Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama unaotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2024 hadi 2029 ambao, Tanzania imeridhia utekelezaji wake kupitia Azimio Na. 1325 la Umoja wa Mataifa kuhusu Wanawake, Amani na Usalama. Utekelezaji wa mpango huo unaendelea kwa kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali ambapo Wakuu wa Mikoa nane (8) na Wakuu wa Wilaya nane (8) wa Mikoa ya Arusha, Tanga, Lindi, Mtwara, Mara, Kigoma, Kusini Magharibi na Pemba wameelimishwa kuhusu mpango huo. Zoezi hili litaendelea kwenye Mikoa mingine mwaka ujao wa fedha.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za usawa wa kijinsia na kutokomeza vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mashirika ya Kimataifa yakiwemo Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) imewezesha uanzishwaji na uimarishwaji wa Madawati ya Jinsia katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati.

**116.** ***Mheshimiwa spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Wizara imetoa mafunzo ya Mwongozo wa Uanzishaji, Uendeshaji na Ufuatiliaji wa Dawati la Jinsia katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati wa Mwaka 2021 kwa Wakuu wa Vyuo na Waratibu wa Madawati ya Jinsia katika Mikoa ya Mwanza, Simiyu na Shinyanga. Kupitia mafunzo hayo, Madawati 30 yameanzishwa hivyo, kufanya jumla ya Madawati yaliyoanzishwa mpaka sasa kuwa 360 kati ya Madawati 612 yanayopaswa kuanzishwa sawa na asilimia 59.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Madawati haya yameleta manufaa makubwa katika kutoa elimu ya masuala ya jinsia, ulinzi wa wahanga wa ukatili wa kijinsia pamoja na kushughulikia mashauri mbalimbali ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na vyombo husika. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, jumla ya matukio 171 ya ukatili wa kijinsia yameripotiwa. Kati ya hayo, matukio ya ukatili wa kingono (89) yalipewa rufaa kwenda Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo mbalimbali vya polisi hapa nchini. Aidha, ukatili wa kimwili matukio (31) na ukatili wa kihisia matukio (51) yameshughulikiwa kwenye Taasisi za vyuo husika husika.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** **Vilevile,** Wizara inatekeleza Mwongozo wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Dawati la Kutokomeza Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia katika Maeneo

ya Umma (2023), ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya madawati 134 yameanzishwa na Waratibu 60 kutoka katika Mikoa ya Katavi na Kigoma kupitia Halmashauri 13 za Mikoa hiyo wamepatiwa mafunzo. Aidha, hadi sasa toka kuanzishwa kwake, jumla ya Mikoa 16 kupitia Halmashauri 111 zimefikiwa na Waratibu 572 wamepatiwa mafunzo ya kuanzisha na kusimamia vyema madawati 238 yaliyoanzishwa katika maeneo ya umma hususan sokoni. Hata hivyo zoezi hili ni endelevu kwa Mikoa iliyobaki.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Madawati haya ya sehemu za umma, yanasaidia kuondokana na Ukatili wa Kijinsia unaofanyika kwenye maeneo ya masoko ambapo wanawake ni wahanga wakubwa wa matukio haya. Hadi kufikia Aprili 2025, Matukio 76 yaliyoripotiwa katika maeneo ya umma ambapo matukio ya ukatili wa kingono ni (14), ukatili wa kisaikolojia (25) na ukatili wa Kimwili ni (37). Kati ya hayo matukio 57 yalipatiwa ufumbuzi na matukio 19 yalipata rufaa kwenda vyombo vya sheria.

**120.** ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Ukatili wa Kijinsia kupitia Kampeni mbalimbali ikiwemo Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ambayo hufanyika tarehe 25 Novemba hadi tarehe 10 Desemba kila mwaka. Kwa Mwaka 2024 Kampeni hii ilifanyika katika mikoa yote nchini ambapo Kitaifa ilizinduliwa na Mhe. Palamagamba A.M Kabudi (Mb.) akiwa Waziri wa Katiba na Sheria tarehe 25 Novemba, 2024, Jijini Dar es Salaam.

**121.** ***Mheshimiwa Spika***, Kampeni hii iliambatana na Msafara wa Kijinsia uliopita katika Mikoa ya Pwani katika Halmashauri ya Chalinze na Bagamoyo, Mbeya na Songwe kwa lengo la kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia na msaada wa kisheria kwa Wananchi. Wananchi 8,408 walipata elimu kuhusu ukatili wa kijinsia, ambapo

wateja 76 walipokea huduma ya msaada wa kisheria, malalamiko 23 yalishughulikiwa hapo hapo, na mengine 53 kuelekezwa Taasisi nyingine za maamuzi kama vile Dawati la Jinsia la Polisi, Ofisi za Ustawi wa Jamii, Mahakama za Ardhi na Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa. Vilevile, Wanafunzi 4,383 katika shule za Mikoa hiyo walifikiwa kupitia programu za shule salama na kupewa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuhamasisha taasisi za Serikali na Sekta Binafsi nchini kuwa na Madirisha ya Wanawake na kuhamasisha Wanawake kupata mikopo yenye riba nafuu kupitia taasisi hizo na kuepuka mikopo isiyo rasmi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya Wanawake 30,273 walipata mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilion 197.5** kutoka kwenye baadhi taasisi za fedha nchini hususani benki za NMB, CRDB, TCB, DCB, NBC na Benki ya Azania. Mikopo hii imeendelea kuwapa uwezo wa mitaji wanawake katika kuinua vipato vyao na kuchangia pato la Taifa. Taarifa za utoaji wa mikopo kwa Wanawake kwenye baadhi ya mabenki ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Namba 3** hapa chini.

**Jedwali Na. 3:** Taarifa ya Utoaji wa Mikopo kwa Wanawake Kwenye Baadhi ya Benki - Julai 2024 Hadi Aprili 2025

| JINA LA BENKI | AINA YA MKOPO | IDADI YA WANAWAKE | KIASI CHA MKOPO |
|---|---|---|---|
| NMB | KILIMO | 1,350 | 30,334,847,477.00 |
| NMB | BIASHARA | 5,538 | 95,925,336,987.00 |
| TCB | BIASHARA NDOGO NA KATI | 959 | 22,784,577,438.34 |
| DCB | TAUSI LOAN | 11,734 | 12,500,000,000.00 |
| CRDB- | IMBEJU | 8,539 | 12,700,000,000.00 |
| NBC | BIASHARA | 153 | 3,261,900,000.00 |
| AZANIA | BIASHARA | 2,000 | 20,000,000,000.00 |
| **JUMLA** | | **30,273** | **197,506,661,902.34** |

## ENEO LA 6: URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

**123.** ***Mheshimiwa* Spika**, usajili, uratibu na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unatekelezwa kupitia Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanasajiliwa na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara imesajili Mashirika 1,202 ambapo Mashirika ya Kimataifa ni 42, Kitaifa ni 1,107, Kimkoa ni 29 na Kiwilaya Mashirika 24, hivyo kufanya jumla ya mashirika yote yaliyosajiliwa kufikia 10,717. Mashirika yaliyosajiliwa yanatekeleza afua mbalimbali katika sekta za elimu, afya, maji, nishati, kilimo, mazingira, uwezeshaji wa jamii, usawa wa kijinsia na utawala bora.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imejenga mfumo wa Kidigitali wa Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambapo Mashirika yote yaliyosajiliwa yameunganishwa ili kuwawezesha wananchi kuyaona kupitia Simujanja kiganjani kama nitakavyoeleza zaidi kwenye aya zinazofuata za hotuba yangu.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Udhibiti wa Masuala ya Mmomonyoko wa Maadili kupitia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara imeboresha Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wa Mwaka 2020 na kutoa Toleo la Pili la Mwongozo huo la Mwaka 2024. Mwongozo mpya umeainisha Majukumu ya Idara na Taasisi za Kiserikali katika uratibu wa pamoja wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, katika majukumu ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yameongezwa Majukumu Mahsusi ya Dawati linalosimamia Uratibu wa Mashirika hayo pamoja na majukumu kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Halmashauri kusimamia mwenendo na

utekelezaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maeneo yao. Vilevile, zimeongezwa Sura mbili (2) kuhusu Uratibu wa Mikutano ya Majadiliano na Jamii na uzingatiaji wa Mila na Desturi za Kitanzania (kwa kutumia Kitini cha Uwezeshaji wa Majadiliano ya Mila na Desturi Ngazi ya Jamii cha Mwaka 2023) pamoja na Sura ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mwongozo huo.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia maboresho hayo ya Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa sasa, Ajenda ya Mchango ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeingizwa katika Vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa (Regional Consultative Committee - RCC) na Vikao vya Kamati ya Ushauri ya Wilaya (District Consultative Committee - DCC). Aidha, Mwongozo huo utaenda sambamba na Utekelezaji wa Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania wa Mwaka 2022 ulioandaliwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao, umeweka misingi ya umuhimu wa kuzingatia Maadili ya Mtanzania kwa makundi mbalimbali na kukemea Mmomonyoko wa Maadili katika Jamii.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii, kuwapongeza Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kwa uratibu mzuri wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia vikao vya Kamati ya Ushauri za Mkoa na Wilaya. Uratibu huu utasaidia katika kuimarisha mahusiano, kujenga uelewa wa pamoja kupitia mipango na vipaumbele vilivyowekwa ikiwa ni pamoja na kupunguza mwingiliano katika utekelezaji wa miradi.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, OR-TAMISEMI kupitia Wasajili Wasaidizi wa Mikoa na Halmashauri imefanya ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuwasisitiza kutekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu

zilizowekwa. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili 2025, jumla ya Mashirika 507 yamefuatiliwa katika Mikoa 15 ya Iringa, Morogoro, Tanga, Dar es Salaam, Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Kigoma, Tabora, Simiyu, Njombe, Songwe na Rukwa kati ya Mashirika 8,052 yaliyomo kwenye Mikoa hiyo. Pamoja na ufuatiliaji huo, Wasajili Wasaidizi katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri zote nchini wamekuwa wakifanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa malengo ya Mashirika yanatekelezwa kwa ufanisi;

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, maeneo yaliyofuatiliwa yalihusu uzingatiaji sheria na miongozo katika utekelezaji wa miradi ya vipaumbele vya Wizara za Kisekta kwa mwaka huo vikiwemo vipaumbele vya kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, kuendelea na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali maji, kuongeza tija, uzalishaji na kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye kilimo pamoja na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032) kwa kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi ya kupikia.

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia ufuatiliaji huo, ilibainika kuwa, miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Mashirika hayo imezingatia vipaumbele vya kisekta na kuwa na manufaa kwa jamii. Baadhi ya miradi bunifu inayotekelezwa na Mashirika hayo ni pamoja na ujenzi wa nyumba kwa kaya maskini (271) katika Mkoa wa Iringa Wilaya ya Mufindi na Kilolo, matumizi ya nishati safi, ujenzi wa karakana za ufundi stadi (2) huduma za maji safi na salama kwa zilizotolewa kwa watu (38,798) na kuongeza thamani ya mazao kwa vikundi vya wakulima wakiwemo vijana na watu wenye ulemavu (5,000) pamoja na kutoa mikopo kwa wakulima. Aidha, Mashirika 46 kati ya 508 yaliyotembelewa yalibainika kuwa yanatekeleza **Mpango Mkakati wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/2023- 2026/2027)**

kwa kuwa na miradi mbalimbali yenye uendelevu inayowezesha Mashirika hayo kujiendesha. Miradi hiyo ni pamoja na vituo vya mafunzo, mashine za kusaga nafaka, miradi ya mashamba ya kilimo cha mbogamboga na mashamba darasa, mifugo, nyumba/hosteli za kulala wageni, kumbi za mikutano, ufugaji wa nyuki, umeme wa jua na visima vya maji ambayo imesaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa ofisi na kuendesha shughuli za Mashirika hayo kwa fedha za ndani.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufuatiliaji pia uliwezesha Mashirika 117 yaliyowekwa kwenye uangalizi kutokana na upungufu wa uzingatiaji wa sheria ikiwemo kulipia ada na kuwasilisha taarifa za kutekeleza matakwa ya Kisheria kwa kulipia ada na kuondolewa kwenye uangalizi maalum na Mashirika 94 yameendelea kubaki kwenye uangalizi. Aidha, katika kipindi cha ufuatiliaji huo, Mashirika hayo yalijengewa uwezo juu miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara Toleo la Pili la Mwaka 2024, Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) na Mwongozo wa Ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Bajeti ya Serikali.

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaratibu mikataba ya fedha za ufadhili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa Kanuni namba 609 ya Mwaka 2018 inayoweka misingi ya uwazi na uwajibikaji wa fedha hizo. Hivyo, Katika mwaka 2024/2025 Wizara imetoa idhini ya Mikataba 478 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 561.8 iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki ikilinganishwa na idhini ya Mikataba 192 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 205.8 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Fedha hizo zilizoidhinishwa, zililenga kutekeleza miradi katika sekta za afya, elimu, mazingira, kilimo, maji, haki za binadamu na utawala bora. Lengo ni kujiridhisha juu ya mfadhili anayetoa fedha, mpango wa utekelezaji unaoshirikisha

Wizara za Kisekta, wanufaika wa mradi pamoja na matumizi ya fedha hizo.

**133.** ***Mheshimiwa Spika**,* katika kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ramani ya kidigitali ya utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeendelea kuwa kitovu cha taarifa za Mashirika kiganjani na nyenzo ya kutambua Mashirika yalipo na miradi inayotekelezwa. Kupitia ramani hiyo, baadhi ya Mashirika yenye taarifa muhimu yamefanikiwa kupata wafadhili baada ya kujionea shughuli zao moja kwa moja kwenye Ramani. Mfano hapa ni Shirika la *Africa Academy for Public Health*, TAWLA na *World Vision*. Hadi kufikia mwezi Aprili 2025, mfumo wa Ramani ya kidigitali umeweza kuyatambua Mashirika yote 10,717 na kuweka taarifa kwenye Mashirika 9,460 mpaka ngazi ya Kata. Uwepo wa mfumo huu, ni hatua kubwa ya kuongeza uwazi na uwajibikaji katika shughuli za Mashirika. Aidha, kupitia mfumo huu, Mashirika yanaendelea kujenga imani miongoni mwa Wadau na Jamii ambapo, wananchi pia wanaweza kuona Mchango wa Mashirika katika Maendeleo ya Taifa kupitia shughuli zinazotekelezwa.

**134.** ***Mheshimiwa Spika**,* Wizara inaendelea kuandaa na kutoa taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kila mwaka. Kwa mwaka 2023/2024 Wizara iliandaa taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2023 ambayo, ilisambazwa kupitia Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali la mwaka 2024. Taarifa hiyo ilihusisha Mashirika 1,368 yaliyowasilisha taarifa za fedha zilizohakikiwa na Wakaguzi wa Hesabu kwa mwaka husika. Taarifa ilionesha kuwa, jumla ya Shilingi Trilioni 2.61 zilipokelewa na kutumika na Mashirika hayo katika utekelezaji wa miradi ya afua za afya, nishati, mazingira, uwezeshaji jamii, ulinzi wa jamii, elimu, kilimo, utawala bora, maji, haki za binadamu na usawa wa kijinsia.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** manufaa yaliyopatikana kutokana na uendeshaji wa miradi mbalimbali ni pamoja na upatikanaji wa ajira za moja kwa moja 21,701 (Me 9,748 na Ke 11,953) wakiwemo Watanzania 21,582 na Wageni 119. Vilevile, ajira za kujitolea 8,326 (Me 963 na Ke 7,363) wakiwemo Watanzania 7,888 na Wageni 438. Manufaa mengine ni pamoja kuchangia katika Pato la Taifa kupitia Kodi zinazolipwa na michango mbalimbali inayotolewa na Mashirika kwa mujibu wa Sheria.

**136.** ***Mheshimiwa* Spika**, Wizara kwa Kushirikiana na Mtandao wa maji na usafi wa mazingira (TAWASANET) chini ya usimamizi wa Wizara ya Maji, imeandaa Taarifa ya Mwaka ya Mapitio ya Utekelezaji Katika Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira kwa kuangalia mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Sekta ya Maji. Taarifa hiyo iliwasilishwa kwa Wadau wa Maendeleo ya Sekta ya Maji katika Maadhimisho ya Wiki ya Maji tarehe 17 Machi 2025. Kupitia taarifa hiyo, ilibainika kuwa Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Sekta ya Maji umeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 23.6 kwa mwaka 2023 na kufikia Shilingi Bilioni 24.6 kwa mwaka 2024.

**137.** ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara imeendelea kutanua wigo wa uratibu wa Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Sekta za Umma ambapo, mwezi Januari 2025, kilifanyika kikao kazi cha kisekta kati ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayotekeleza afua za elimu na kushirikisha jumla ya Mashirika 206. Lengo la kikao kazi hicho ilikuwa ni kuratibu mchango wa Mashirika ya Sekta ya Elimu ambapo, kupitia kikao hicho, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliazimia kuwezesha Wanafunzi wenye uhitaji kila mwanzo wa muhula wa masomo.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azimio hilo, iliundwa Kamati Maalum ya Uratibu iliyojumuisha Mashirika Saba (7) ambayo ni *Center for Women and Children Development (CWCD)*, Shirikisho la Vikundi vya

Ujasiriamali Tanzania (SHIVUTA), *The Tunu Pinda Foundation,* Mulika Tanzania, Haki Elimu, *Room to Read*, *Plan International* wakishirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO).

**139.** ***Mheshimiwa Spika****,* hadi kufikia, Aprili 2025 Kamati hiyo imefungua Akaunti ya Benki na kuweka kiasi cha Shilingi 500,000.00 zilizochangwa na Mashirika Matano (5) yaliyounda Kamati hiyo. Aidha, Mashirika pamoja na Wadau wengine wataendelea kuchangia ili kuwa na mfuko utakaoratibiwa na Mashirika yenyewe ambapo imepangwa kuwezesha watoto 5,200 kwa mwaka katika mikoa yote. **Hatua hii, ni utekelezaji wa Mwongozo wa Uratibu wa pamoja wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambao umeanzisha Madawati ya Uratibu wa Mashirika ndani ya Wizara zote.**

**140.** ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (National Council of Non Governemntal Organization - NaCoNGO) iliandaa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuanzia tarehe 4 hadi 6 Septemba, 2024 Jijini Dodoma, lenye Kauli Mbiu ya; ***"Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni Wadau Muhimu, Washirikishwe Kuimarisha Utawala Bora".*** Jukwaa hilo lilitanguliwa na Majukwaa katika Halmashauri na Mikoa ambapo kwa mara ya kwanza, mikoa yote nchini na Halmasahuri zake ziliendesha majukwaa hayo ambayo yalibeba na kujadili ajenda mbalimbali za Mashirika ikiwa ni pamoja na udhibiti wa vitendo vya mmomonyoko wa maadili. Katika jukwaa la Kitaifa, Washiriki 1,874 walihudhuria Jukwaa hilo ambapo, Mgeni rasmi alikuwa **Mheshimiwa, Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb**), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Serikali na Wadau wa Maendeleo walipata fursa ya kujadiliana na kutoa maoni na kuboresha maeneo mbalimbali yanayohusu uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini na masuala mbalimbali yanayohusu mkakati wa kupambana na rushwa, mapambano dhidi ya madawa

ya kulevya na mwongozo wa uwazi kifedha na sera mbalimbali za misaada ya ufadhili na ushirikiano.

**141.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia jukwaa hilo, wananchi 456 (Me 310 na Ke 146) walipatiwa huduma za msaada wa kisheria. Vilevile, Mgeni rasmi alizindua Kampeni ya Kutokomeza Utapiamlo kwa Watoto na kuyataka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa Mawakala wa Kampeni hiyo na kuifikia jamii kwa lengo la kuboresha lishe. Pia, yalizinduliwa Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Sekta Binafsi. Aidha, jukwaa hilo liliwezesha kubadilishana uzoefu na nchi za Uganda na Malawi katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia Sekta Binafsi hususani Mabenki.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** maazimio yaliyopitishwa kwenye jukwaa hilo ni pamoja na Mashirika kushirikiana na Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushughulikia changamoto za kikodi zinazoyakabili Mashirika hayo na kuhakikisha Waratibu wa Mashirika hayo katika ngazi za Mikoa na Halmashauri wanajengewa uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha Tume ya Maboresho ya Kodi kwa ajili ya kupokea maoni na changamoto za kikodi ambapo kwa mara ya kwanza Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamepata fursa hii adhimu ya kuwasilisha maoni yao ya maboresho ya kikodi mbele ya Tume hiyo. Fursa hii inaonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kujenga mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, naipongeza Mikoa na Halmashauri zote zilizojitokeza kuratibu majukwaa katika ngazi zao kwani, majukwaa hayo yanaimarisha uratibu wa pamoja na ushirikiano wa Mashirika kuanzia ngazi za msingi hadi Taifa. Aidha, natoa

rai kwa Mikoa kuendelea kuratibu majukwaa yatakayofanyika mwaka huu 2025.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa- TAMISEMI Zanzibar ambayo ina dhamana ya usajili na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya kiserikali imeendelea kuimarisha uratibu wa Mashirika kwa pande zote mbili za Muungano ambapo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Saba (7) kutoka Tanzania Bara yamepata kibali cha kutekeleza shughuli zake Visiwani Zanzibar. Ushirikiano huo umerahisisha mamlaka hizo za usajili kubadilishana uzoefu, utaalam na taarifa. Aidha, kupitia ushirikiano huo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayotekeleza afua ya utawala bora kwa pande zote mbili za Muungano yaliwezeshwa kushiriki katika utoaji wa elimu ya mpiga kura na usimamizi wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024.

***Ninatoa rai kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yatakayopata vibali vya kutoa Elimu ya Mpiga Kura na Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, 2025 kutekeleza majukumu hayo kwa weledi na kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayosimamia kazi hizo kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Aidha, niendelee kutoa rai kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika utekelezaji wa majukumu yao.***

**ENEO LA 7: URATIBU WA MPANGO KAZI WA TAIFA WA KUTOKOMEZA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO (MTAKUWWA).**

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya Pili (MTAKUWWA – 2024/25 – 2028/29) wenye lengo la kuzuia na kutokomeza vitendo vya ukatili. Mpango wa Awamu ya Pili uliozinduliwa mwezi Mei, 2024 umeongeza mambo mapya kwa lengo la kuboresha uratibu na utekelezaji kwa kulinganisha na

MTAKUWWA ya Awamu ya Kwanza. Masuala yaliyoongezeka ni pamoja na: kuongezeka kwa Vyombo vya Usimamizi wa MTAKUWWA ikiwemo Kamati Elekezi ya Mawaziri Wakuu wa Mikoa na Wilaya kupitia Vikao vya Kamati za Ushauri za Mkoa na Wilaya (Regional Consultative Committee - RCC na District Consultative Committee - DCC) kwa lengo la kupata msukumo wa kisera na kisiasa katika utekelezaji wa mpango huo ngazi zote; pia kushirikisha Wanaume na Vijana wa Kiume katika utekelezaji wa Afua za Kutokomeza Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia; na kujumuisha Afua za Kupinga Ukatili wa Mtandaoni.

**146.** ***Mheshimiwa* Spika,** ajenda ya MTAKUWWA imejumuishwa katika Vikao vya Kamati ya Ushauri ngazi ya Mkoa na Halmashauri kwa lengo la kuwapa nafasi Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kujadili ajenda hiyo muhimu.

Aidha, kabla ya Vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa na Wilaya (RCC na DCC), ajenda hii itakuwa imejadiliwa na Baraza la Madiwani, Menejimenti ya Mkurugenzi wa Halmashauri, Baraza la Maendeleo ya Kata (WDC) na Halmashauri za Vijiji ambapo, Kamati za Ulinzi za Wanawake na Watoto huwa wanatoa taarifa zikiwa na Wajumbe mbalimbali wakiwemo, viongozi wa dini, viongozi wa kimila na wadau wa maendeleo. Hatua hii itasaidia kutolewa maamuzi na kutekelezwa kwa mapendekezo yote katika ngazi zote yenye lengo la kuilinda jamii na kutoa huduma za msingi kwa wahanga wa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mpango huo unahusisha makundi yote muhimu katika jamii wakiwemo Viongozi na Watumishi wa Serikali, Viongozi wa Kimila, Viongozi wa Kidini, Wadau wa Maendeleo na Asasi za Kiraia na Jamii kwa ujumla. Aidha, mpango huu unasisitiza

ajenda ya MTAKUWWA kuwa Ajenda ya Kudumu katika Vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa na Vikao vya Kamati ya Ushauri ya Wilaya, Vikao vya Maendeleo ya Kata (Ward Development Committee – WDC) na Vikao vya Maendeleo ya Kijiji/Mtaa.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango huu una maeneo makuu nane (8) ambayo ni kuimarisha uchumi wa kaya; mila na desturi; mazingira salama katika maeneo ya umma na mtandaoni; malezi, familia na mahusiano; usimamizi na utekelezaji wa sheria; utoaji wa huduma za mwitikio kwa wahanga wa vitendo vya ukatili; ulinzi wa mtoto shuleni na stadi za maisha; na uratibu, ufuatiliaji na tathmini.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wadau wa Maendeleo wametekeleza afua mbalimbali ikiwemo:

i. Kufanya kikao cha Kamati Elekezi ngazi ya Mawaziri ambapo Mawaziri 16 wa Wizara za kisekta waliweza kutoa na kusaini matamko ambayo yamejumuishwa katika andiko la MTAKUWWA;

ii. Kufanya Kikao cha Kamati Elekezi ngazi ya Makatibu Wakuu ambapo Makatibu Wakuu walihimizwa kujumuisha afua za MTAKUWWA katika Mipango na Bajeti za Wizara zao;

iii. Kufanya Kikao cha Kamati Tendaji ambapo Wakurugenzi wa Wizara za kisekta walipitia taarifa ya utekelezaji ya MTAKUWWA kwa kipindi cha Julai – Desemba 2024. Taarifa hiyo iliandaliwa kuzingatia taarifa zilizoandaliwa na kuwasilishwa na wasimamzi wa maeneo nane (8) ya MTAKUWWA; na

iv. Kuratibu Uundwaji wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto 2,562 ngazi ya Jamii na

hivyo, kufanya Kamati hizo kufikia jumla ya Kamati 20,748. Kamati hizi zinalenga kuimarisha ulinzi wa wanawake na watoto dhidi ya vitendo vya ukatili.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni hatua njema  na kubwa kuwa, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/26 uliotolewa na Wizara ya Fedha umesisitiza Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kujumuisha Afua za MTAKUWWA katika Mipango na Bajeti. ***Nitoe wito kwa Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge kufuatilia utekelezaji wa mpango huu katika Wizara wanazozisimamia pamoja na majimbo yao ili kuongeza uwajibikaji na uwazi katika utekelezaji wa mpango huu kwa faida ya wananchi.***

## D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

**152.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeongeza idadi ya udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi **3,019** (**Me 1,052** na **Ke 1,967**) waliodahiliwa mwaka wa masomo 2023/24 hadi kufikia wanafunzi **3,219** (**Me 1,286** na **Ke 1,933**) katika mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la **7%.** Aidha, kwa mwaka 2024/25 mahafali ya 14 yalifanyika ambapo jumla ya wanafunzi **1,672** (**Me 554** na **Ke 1,118**) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,651 (**Me 575** na **Ke 1,076**) waliohitimu 2023/24. Taasisi inaendelea kuboresha mafunzo na kutoa wahitimu wenye weledi na uwezo. Ili kufikia lengo hili, Taasisi katika mwaka wa masomo 2025/2026 inatarajia kuanzisha jumla ya **mitaala mipya 15**.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** taasisi hii pia hutoa mafunzo ya muda mfupi na kushiriki katika masuala mbalimbali ya jamii ikiwa ni utekelezaji wa programu ya ushirikishwaji wa jamii. Katika eneo hili, Taasisi ya Tengeru ilitoa mafunzo ya elimu juu ya kujitambua, kufikia malengo na kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi **398 (Me 220 na Ke 178)** wa shule ya sekondari Arusha. Pia, Taasisi iliendesha mjadala (female students' dialogue) kuhusu masuala ya uongozi, haki ya kijinsia na changamoto za kijamii kwa **wanafunzi 400** kutoka shule za sekondari **sita (06)** za Makumira, Muungano Usa River, Kikwe, Poli, Sing'isi, na Arusha Day, chini ya kauli mbiu "**Kusisitiza Sauti za Wanawake Vijana; Uongozi kwa Haki ya Kijinsia**.' Matokeo muhimu yalikuwa ni kuanzishwa kwa Klabu za *She/He Brave* katika kila shule hizo ili kuongeza uelewa, kupambana na ukatili wa kijinsia, kukuza usawa wa kijinsia na kutetea mabadiliko katika jamii.

**154.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, inatekeleza programu ya kuchochea na kuendeleza ubunifu miongoni mwa wanafunzi kupitia Kituo cha Huduma Tandaa na Ubunifu wa Kidijitali (Jamii Outreach Digital Innovation Center – JODIC). Kituo hiki kinatumika kuratibu utekelezaji wa programu za ubunifu wa kidijitali, ushirikishwaji jamii na uanagenzi. Kupitia Programu hii, Taasisi imetekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kutoa elimu ya afya kuhusu magonjwa yasiyoambukiza katika kijiji cha Patandi. Jumla ya wananchi **125 (Me 45, Ke 80)** walipata elimu hiyo na kupata ushauri wa kiafya;

ii. Kutoa elimu kuhusu uundaji wa vikundi vya kiuchumi ili kuwezeshwa kupata fursa zinazotolewa na Serikali kupitia vikundi, ambapo vikundi **vinne (04)** vilisajiliwa katika kijiji cha Msomera kilichopo Wilaya ya Handeni kwenye mfumo wa Benki Kuu (BoT) kwa ajili ya kupata

mikopo ya ujasiriamali inayotolewa na Halmashauri;

iii. Katika kuadhimisha Wiki ya Sheria (Legal aid week), Taasisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, ilitoa elimu ya ardhi, migogoro kazini na masuala ya ukatili wa kijinsia kwa **Wananchi 130**. Aidha, Jumla ya **Wananchi 60** walipata msaada wa kisheria katika maadhimisho hayo;

iv. Taasisi imepeleka jumla ya **Wanafunzi 2,445** kufanya mafunzo kwa vitendo (apprenticeship) katika mashirika, taasisi na makampuni 30 ya Umma na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini. Mafunzo haya kwa vitendo yanawasaidia wanafunzi kukuza ujuzi wao na kupata uzoefu halisi wa kazi, hivyo kuwajengea uwezo wa kuajiriwa, kujiajiri na kuajiri wengine; na Pia, katika kuhudumia na kuboresha mawazo ya kiubunifu kwa wanafunzi, mwanafunzi mmoja (01) mwenye wazo la utengenezaji wa mashine ya kuvunia karanga alishinda kwenye mashindano ya uendelezaji bunifu yaliyoendeshwa na Shirika la StartHub Africa – Tanzania na kupata zawadi ya **Shilingi Milioni sita (6,000,000.00)** kwa ajili kuendeleza wazo lake. mwanafunzi huyo kwa sasa yupo katika mafunzo ya miezi sita (6) Wilayani Mpwapwa na Kondoa akifanya uchambuzi yakinifu kwa wakulima wa karanga.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kupitia Kituo chake cha Kitaifa cha Utafiti na Uhifadhi wa Machapisho ya Wanawake kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia - Dar es Salaam (DIT) na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, iliandaa Kongamano la mwaka la Wanawake lililofanyika Jijini Arusha tarehe 6

Machi 2025, lililoshirikisha Watafiti na Wadau 1,158 (Me 119, Ke 1,039). Kongamano hilo lilikuwa na kaulimbiu ya ***"Ushiriki wa Wanawake katika Utalii; na Mapambano Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia katika Miaka 30 ya Azimio la Beijing".*** Lengo mahususi la kongamano hilo ni kutathmini mchango, mafanikio, fursa na changamoto za ushiriki wa wanawake katika Sekta ya Utalii na Maliasili pamoja na kujadili mafanikio ya Azimio la Beijing katika kuimarisha usawa wa kijinsia.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la utafiti, ushauri elekezi na maandiko, Taasisi imetoa ushauri elekezi kwa Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) katika kufanya tathmini ya muundo wa mimea katika njia ya umeme Manyoni hadi Tabora pamoja na ushauri elekezi katika Wizara ya Maliasili na Utalii juu ya tathmini ya mimea ya kigeni iliyopo katika eneo la Pugu Kazimzumbwi, Dar es Salaam;

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili katika fani ambazo zinalenga Ustawi wa Jamii. Katika mwaka wa masomo 2024/25, Taasisi imedahili wanafunzi wapya 2,731 (Me 1,022 na Ke 1,709) ikilinganishwa na wanafunzi 3,039 (Me 904 na Ke 2,135) waliodahiliwa mwaka 2023/24 sawa na upungufu wa asilimia 10.1. Upungufu huo unatokana na kuongezeka kwa vyuo vinavyotoa programu zinazofanana na hivyo na kupelekea wanafunzi kuwa na uchaguzi mpana wa vyuo vya kwenda kusoma. Aidha, Katika mwaka wa masomo 2024/25 jumla ya wanafunzi 3,112 walihitimu masomo yao katika ngazi mbalimbali kati ya hao wanawake walikuwa 2,084 na wanaume 1,028.

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kutoa msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wanafunzi na Jamii kupitia kituo chake cha Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia. Hadi kufikia mwezi

Aprili, 2025 kituo hiki kimetoa huduma ya elimu, ushauri, msaada wa kisaikolojia, afya ya akili na namna bora ya kukabiliana na msongo wa mawazo kwa watu 1,862 ambapo, kati yao Wanawake ni 835 (45%) na Wanaume 1,027 (55%) katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Dodoma na Tanga.

Katika kuwawezesha na kuwainua wanawake kiuchumi, Chuo kwa kushirikiana Coca - Cola Kwanza kilitoa elimu kuhusu afya ya akili, huduma kwa wateja sambamba na elimu ya ujasiriamali na utunzaji wa kumbukumbu kwa wanawake wajasiriamali 487 Mkoa wa Tanga. Aidha, Chuo kimetoa huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii katika janga la kuporomoka kwa jengo la biashara katika eneo la Kariakoo Jijini Dar es Salaam;

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi inatekeleza programu ya uanagenzi ambayo inawapa wahitimu fursa ya kufanya kazi kwa kujitolea katika taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi ili kuboresha taaluma katika nyanja mbalimbali walizojifunza chuoni kwa kuwajengea uelewa na ufanisi katika utendaji wa kazi za Ustawi wa Jamii. Pia mpango huu unalenga kuondoa tatizo la muda mrefu la wahitimu kukosa ujuzi na uzoefu (soft skills) unaohitajika katika soko la ajira. Katika mwaka wa fedha wa 2024/2025, wahitimu 52 wameshiriki programu hiyo na kufanya jumla ya wahitimu 354 tangu programu ilipoanza 2019;

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi inaendelea na ujenzi wa hosteli ya wanafunzi awamu ya pili kwenye kampasi ya Kisangara yenye uwezo wa kuchukua Wanafunzi 104. Mradi huu utagharimu jumla ya **Shilingi 638,755,000.00** kwa kutumia mapato ya ndani ambapo hadi Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 534,972,587.00** zimetumika.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi inatekeleza mradi wa ujenzi wa Ukumbi wa Mihadhara wenye uwezo wa kuchukua Wanafunzi 419 katika Kampasi yake ya

Kijitonyama. Mradi huu utagharimu **Shilingi 626,405,368.00** unaotekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani na hadi sasa mradi umetumia **Shilingi 245,564,738.00** ambapo, ujenzi umefikia asilimia 40**.** Kutokana na ongezeko la wanafunzi, ukumbi huu unatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuboresha miundombinu ya elimu na kupunguza msongamano katika madarasa yaliyopo sasa.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kuboresha mitaala yake pamoja na kuanzisha programu mpya zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira. Taasisi imepata ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa ajili ya kutekeleza mitaala minne (4) ambayo ni Astashahada na Shahada katika Kazi za Jamii, Watoto na Vijana, Astashahada katika Saikolojia; Astashahada na Shahada katika Ukuzaji Ujasiriamali; Astashahada na Shahada katika Utatuzi Mbadala wa Migogoro Mahali pa Kazi na; Shahada ya Uzamili katika Masoko. Mitaala hiyo itaanza kutumika katika mwaka ujao wa fedha.

## E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya utendaji kwa watumishi, Wizara inaendelea na ujenzi wa jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamiii Tengeru lenye ofisi 44 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 94 na kumbi tano (5) zenye uwezo kuhudumia watu 545. Jengo hilo litagharimu **Shilingi Bilioni 5.7**, ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetoa fedha za ndani za maendeleo **shilingi Bilioni 1.2** na kufanya jumla ya **Shilingi Bilioni 2.7** zilizopokelewa. Hadi Aprili 2025, ujenzi umefikia asilimia 70**;**

**164.** ***Mheshimwa spika***, Wizara inaratibu utekelezaji wa Programu ya Kuondoa Vikwazo na Kuimarisha Usawa wa Kijinsia *(Gender Transformative Programme: Breaking the Glass Ceiling - GTAP)* ambapo kupitia programu hii, Serikali

inapokea fedha za ufadhili kutoka Jumuiya ya Umoja wa Ulaya na kujumuisha fedha hizo katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Katika kuratibu programu hii, Wizara imepokea **Shilingi Milioni 990.7** zilizowezesha kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo kusambaza na kujenga uelewa wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Jinsia na Wanawake (2023) kwa Wadau wanaotekeleza Sera; kukamilisha Mpango Kazi wa Taifa wa Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama; kuanzisha Madawati ya Jinsia katika maeneo ya Umma (Sokoni), Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati, na Madawati ya Ulinzi wa Mtoto Shuleni; kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996; kuwezesha majadiliano ya kujadili Mila na Desturi zenye madhara ngazi ya Jamii; kuimarisha Kituo cha Msaada cha Kijamii Wizarani *(Community Call Center);* kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Vitendo vya Ukeketaji na kufanya mapitio ya Mpango huo; na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatii Dhidi ya Wanawake na Watoto.

**165.** ***Mheshimwa Spika***, Wizara inaratibu utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa, ambapo Serikali imetoa **Shilingi Bilioni 1,** zilizowezesha kuwajengea uwezo Maafisa Viungo wa Wizara za Kisekta, Kuratibu Ziara ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa, kujenga uwezo kwa Vikundi vya Wanawake ili kunufaika na Zabuni kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 30% ambayo inataka vikundi vijisajili kwenye Mfumo wa Manunuzi ya Umma na ununuzi wa Pikipiki 100 ambazo zipo katika taratibu za manunuzi.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepokea fedha za nje kiasi cha **Shilingi Milioni 434.9** katika kuimarisha afua za kutoa elimu ya malezi chanya kwa watoto katika ngazi zote nchini zikiwemo kuratibu na kufanya Mkutano wa Wadau wanaotekeleza Afua za Vijana Balehe Nchini; Kugharamia maandalizi ya Mkutano wa Tano wa Nchi

Wanachama kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Afrika na Haki na Ustawi wa Mtoto; kufanya utekelezaji wa Afua za Ulinzi na Usalama wa Mtoto Mtandaoni; Kugharamia Afua za MMMAM na kupambana kuzuia aina zote za ukatili dhidi ya watoto ikiwemo ukeketaji na ukatili mitandaoni.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha na kuendeleza Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo (machinga), mama/baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji, wasusi na wanaoshona nguo, Serikali imetoa Shilingi Bilioni 8 ili kutoa mikopo kwa wafanyabiashara hao kupitia Benki ya NMB ili kuongeza kipato chao na kuwainua kiuchumi. Hadi Aprili 2025, wafanyabiashara ndogondogo 601 (Me 274; Ke 327) wamekopeshwa mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 1,101,650,000** na zoezi hilo linaendelea. Vilevile, maombi 2,092 yanaendelea kuchakatwa yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 3,590,477,000**.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kusimamia utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii, imepokea fedha za nje kiasi cha **Shilingi Milioni 172.3** zilizotumika katika kufanya tathmini ya kuboresha huduma za Malezi Mbadala; Kuandaa Mkakati wa Huduma za Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii na kutoa mafunzo kwa watoa huduma ngazi za jamii.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo, Wizara imepokea **Shilingi milioni 150** ambazo, zimetumika kufanya ufuatiliaji wa afua na utolewaji wa huduma katika Taasisi, Vyuo na Vituo vya Ustawi wa Jamii vilivyo chini ya Wizara.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia (Advancing Gender Equality in Tanzania) unaojulikana kwa jina la "PAMOJA PROJECT'' ambao, uwezeshaji

wake ni kupitia Mkopo wa Dola Millioni 100 na Ruzuku ya Dola Millioni 4 toka Benki ya Dunia (*World Bank)*. Lengo la mradi ni kukuza fursa za kiuchumi, kuboresha huduma za kifedha kwa wanawake na pia, kuzuia na kupambana na ukatili wa kijinsia. Mradi huu utatekelezwa kwa muda wa Miaka Mitano (5) kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, Mradi huu wa PAMOJA utatekelezwa katika Halmashauri 40 kwenye Mikoa 10 ambayo ni Mwanza, Arusha, Kagera, Mara, Shinyanga, Singida, Geita, Rukwa, Tabora, na Simiyu. Uchaguzi wa mikoa hii umezingatia viashiria vya hali ya ukatili na hali ya uchumi wa mikoa hiyo.

## F. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/26.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake itatekeleza vipaumbele vitano (5) ili kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo: -

i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa katika ngazi ya msingi;

ii) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii ikiwa pamoja na kukuza usawa wa kijinsia, kutokomeza vitendo vya ukatili, uwezeshaji wanawake kiuchumi na upatikanaji wa malezi bora katika familia;

iii) Kutambua, kuratibu maendeleo na ustawi Makundi Maalum wakiwemo watoto, wazee na wafanyabiashara ndogondogo;

iv) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na

v) Kuimarisha mazingira ya ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara kwa mwaka 2025/26 imekadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 76,057,153,000.00.** Kati ya fedha hizo**, Shilingi 49,115,697,000.00** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 22,646,148,000.00** ni Fedha za Mishahara na **Shilingi 26,469,549,000.00** ni Fedha za Matumizi Mengineyo.
Aidha, **Shilingi. 26,941,456,000.00** ni Fedha za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 15,415,404,000** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 11,526,052,000** ni Fedha za Nje.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2025/26 ni pamoja na**: -**
**174.**

i) Eneo la kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa katika ngazi ya msingi limetengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.5**;

ii) Eneo la kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii, kiasi cha **Shilingi Bilioni 10.3** zimetengwa. Miongoni mwa huduma hizo ni huduma kwa wazee, huduma za utengamao kwa watoto, huduma za usuluhisho wa ndoa, huduma katika mahabusu za watoto, shule ya Maadilisho na huduma za malezi ya kambo na kuasili;

iii) Eneo la kutambua, kuratibu na kuendeleza Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogo ndogo, kiasi cha **Shilingi Bilioni 12** kimetengwa;

iv) Eneo la kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, limetengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 8.5**;

v) Eneo la kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa, limetengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.5**; na

vi) Eneo la ufuatiliaji na tathmini, kiasi cha **Shilingi Milioni 90** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Taasisi, Vyuo na Vituo vya Ustawi wa Jamii vilivyo chini ya Wizara.

## G. SHUKRANI

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka Nchi Rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta Binafsi zinazosaidia na kuchangia katika huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Aidha, Ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za Nchi Rafiki zikiwemo; Japan, Ufalme wa Sweden, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Ufalme wa Norway, Ufalme wa Uingereza, Falme za Nchi za Kiarabu, Italia, Ujerumani, Ubelgiji, Ufaransa, Canada, Ufalme wa Denmark, Ireland, Jamhuri ya Uswisi, Bangladesh na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara ikiwa ni pamoja na: **Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo** UNICEF, UNFPA, UN-Women, WHO, UNDP, UNEP, ILO, IOM, WFP, FAO, UNESCO na UNHCR. Vilevile, ninashukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika

(SADC), na Jumuiya za Umoja wa Nchi za Ulaya (EU). Pia nayashukuru **Mashirika ya Kimataifa** ambayo ni: -Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfuko wa *Abbott Fund*, *Global Fund* na *Hilton Condrad Foundation*. Aidha, ninazishukuru **Taasisi za Kifedha** za hapa nchini zinazoshirikiana na Wizara ambazo ni pamoja na Benki za CRDB, NBC, NMB, Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Stanbic, Azania, Equity, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Akiba Commercial Bank (ACB), DCB Commercial Bank, Benki ya Mkombozi na Benki ya Biashara Tanzania.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali** na **Mashirika ya Dini** kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na; *World Vision, PACT Tanzania, The Aga Khan Foundation, Foundation for Civil Society*, *HelpAge Tanzania, Compassion International*, *Responsible rganization Tanzania, Both Ends Believing* (BEB)*, Safe Society Platform Tanzania*, *Children in Crossfire*, *Care International Tanzania, Railway Children Tanzania*, WiLDAF, ICS, TAWLA, TAYOA, LSF, *SOS Children's Village Tanzania*, BRAC Maendeleo Tanzania, *Plan International - Tanzania*, Kivulini, FSDT, WFT, TANLAP, *Save the Children, Equality for Growth (EfG)*, Landesa, CAMFED, C- SEMA; REPPSI, *Amani Girls*, Girls Effect, Pelum Tanzania, LHRC, Haki Elimu, TWCC, TECDEN, EGPAF, FAGDI, HJFMRI, TGNP, CRS na MEWATA.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe pia Shukrani zangu kwa Sekta Binafsi ikiwemo, Mgodi wa Geita (GGM), Barrick, State oil, Bakhresa Group of Company, Total Energies, ASM technology, Asas Group of Company, Camal Steel Group, Afroil Investment Ltd, Oryx Gas, Great lakes, Fleight, Bulyankuru Gold Mine Ltd, Bowmans Tanzania Ltd na Highland Estate. Shukrani zangu ziwafikie **jumuiya za makundi mbalimbali** ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Wizara zikiwemo: -

Baraza la Taifa la Ushauri la Wazee, Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Tanzania (CHAMWAPITA), Machifu na Viongozi wa Kimila Tanzania, Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Chama Cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT), Jukwaa la ULINGO, Jumuiya ya Wazazi CCM, Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TAWIA, Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) na Umoja wa Mama na Baba Lishe Tanzania. Pia, naomba nizishukuru Klabu za Mpira wa Miguu Tanzania hususan Yanga, Simba, AZAM na vikundi/kampeni za Kijamii kama (Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), Safe Society Platform Tanzania (SSPT), TFF, Lete Mabadiliko Chanya Ulipo (LeMaChu), Sauti ya Watoto Tanzania (SAWATA), Malezi Bora Network pamoja na Vyombo vyote vya Habari.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mafanikio ya Wizara yametokana na ushirikiano wa wa Wadau pamoja na Kamati tulizounda na kuzipa majukumu ya kutekeleza. Kamati hizo ni pamoja na Kamati ya Maandalizi ya Siku ya Wanawake Duniani 2025, Kamati ya kuhamasisha Wanawake kujiunga na Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi na Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Afua za Watoto Wanaoishi na Kufanya Mtaani. Nichukue fursa kuwashukuru sana Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizo. Wizara inaahidi kuendelea ushirikiano huo kwa msingi wa kukuza dhana ya ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza kijana Samson Mgelwa, muandishi wa kujitegemea kipitia Blog ya Muungwana kwa makala yake ya 'Kwanini Wananchi Wengi Hawatoi Ushahidi kwenye Kesi za Ukatili' iliyoshinda tuzo za 'Mama Samia Kalamu Award' kwa afua za Wizara ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu. Makala hii

imeelezea changamoto zinazoikabili jamii yetu na kutoa ushauri wa jinsi ya kukabiliana nazo.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe shukrani zangu pia kwa Viongozi na Taasisi za Dini zikiwemo Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA).

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yangu nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara. Naomba kipekee niishukuru Menejimenti na Wataalam wote wa Wizara wakiongozwa na **Dkt. John A. K. Jingu,** Katibu Mkuu na wasaidizi wake **Wakili Amon A. Mpanju,** Naibu Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum na **Bi. Felister Peter Mdemu**, Naibu Katibu Mkuu Maendeleo ya Jinsia na Wanawake kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninaomba kuwashukuru Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Bodi na Menejimenti za Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Pia, nawashukuru Wakuu wa Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wao mzuri unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu. Ninatoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao.

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kupitia OR – TAMISEMI nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote na Wataalam wote chini ya Ofisi zao na Wadau wote

wa Sekta mbalimbali wanao hudumia katika maeneo yao pamoja na Wananchi mmoja mmoja na ***mitandao*** ya habari za kijamii ambao wamekuwa wakifuatilia na kutoa ushirikiano mkubwa kwenye utekelezaji wa majukumu ya wizara yangu hasa kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia.

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru sana familia yangu, hususan M**ume wangu Mpendwa Wakili Msomi Methusela Gwajima** na watoto wetu wote pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu, kwa uvumilivu wao wa kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, nawashukuru W**ananchi wote wa Tanzania** kwa kuipatia ushirikiano Wizara ninayoisimamia wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu na pia kwa wao binafsi kuendelea kupambana kuhakikisha wanafikia maendeleo na ustawi wa jamii.

## H. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2025/26

### (i) Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/26

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara imekadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 7,040,129,000.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Vyanzo hivyo ni pamoja na: Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii; Ada ya malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Usajili; Ada ya usajili wa wafanyabiashara Ndogondogo na Ada za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Matumizi ya Kawaida

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 49,115,697,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 26,469,549,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na

**Shilingi 22,646,148,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

### (ii) Miradi ya Maendeleo

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 26,941,456,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,415,404,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 11,526,052,000.00** ni Fedha za Nje.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) inaomba Jumla ya **Shilingi 76,057,153,000.00** ili kutekeleza majukumu yake.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum *www.jamii.go.tz*

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** **Ninaomba Kutoa Hoja.**

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Ninaomba taarifa hii

ya Kamati yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(iv) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na

(v) Sehemu ya Tano na hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maelezo ya uchambuzi kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilizofanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara kwa ajili ya kukagua na kutembelea mradi wa ujenzi wa Hosteli za Wasichana Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Monduli, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii – Tengeru, Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama na Mradi wa Kituo cha Taifa cha Kulelea Watoto wanaoishi katika Mazingira Magumu – Kurasini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ujenzi wa Hosteli za Wasichana Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli; Kamati ilijulishwa kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 chuo hiki kilitengewa kiasi cha fedha shilingi milioni 500 ili kuendelea na ujenzi wa hosteli. Hadi kufikia tarehe ya ukaguzi chuo hakikuwa kimepokea fedha, na badala yake walikuwa wanaendelea na ujenzi kwa fedha zilizotengwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kuchelewa kuwasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo Kamati ilishuhudia hali ya kusuasua kwa ujenzi kutokana na mapokezi hafifu ya fedha kwa ajili ya kukamilisha mradi huo. Kwa upande mwingine Kamati inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuanzisha mradi huu wenye lengo la kupunguza kwa kiasi kikubwa kadhia ya makazi inayowakumba wanafunzi, hususan wanafunzi wa kike, ambao kwa kiasi kikubwa huathiriwa na mwingiliano wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kutoa rai kwa Serikali kuwa fedha inayotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi itolewe kwa ukamilifu na kwa wakati ili kukamilisha mradi huo kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 taasisi ilitengewa kiasi cha Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa jengo la utawala. Mpaka

**27 MEI, 2025**

Kamati inatembelea eneo la mradi shilingi bilioni 1.2 zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umetekelezwa kwa 70%. Aidha, imebainika kuwa mtiririko wa mapokeo ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ni wa kuridhisha na hivyo kupelekea mradi kutekelezwa kama ilivyopangwa. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuusimamia vema mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa mihadhara katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama. Kamati ilielezwa kuwa mradi huu una thamani ya shilingi milioni 626.4, ambapo hadi Kamati inatembelea mradi huu shilingi milioni 245.5 zilikuwa zimekwishatumika na kufikia 39.2% ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa baada ya kukamilika kwake ukumbi huu utakuwa na uwezo wa kubeba wanafunzi 400 kwa wakati mmoja. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuhakikisha kuwa taasisi zote zilizopo chini yake zinatekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia makusanyo yake ya ndani na hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa mradi wa kituo cha kulelea watoto walio katika Mazingira magumu Kurasini, Dar es Salaam. Kamati ilijulishwa kuwa katika kituo cha kulelea watoto Kurasini kiasi cha shilingi milioni 248.8 kilipokelewa na Wizara katika mwaka wa fedha 2024/2025 ili kuwezesha utekelezaji bora wa majukumu katika kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresho mbalimbali yaliyofanywa katika kituo hiki, Kamati ilishuhudia uchakavu wa miundombinu yakiwemo majengo mbalimbali kama vile mabweni, madarasa na ofisi. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itenge fedha ili kuboresha mazingira ya kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo ya uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza kwa umahsusi katika mambo makuu manne kama ifuatavyo: -

a) Makusanyo ya maduhuli;

b) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti ya kawaida;

c) Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

d) Uzingatiaji wa ushauri wa Kamati Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni saba kutoka vyanzo vyake vyote mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025 Wizara imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni tatu, sawa na 42.56%. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa jumla ya shilingi bilioni tatu sawa na 42.65% ya makusanyo yote ya Wizara hii yalikusanywa kwa kipindi hicho.

(ii) Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara hii imekusanya 42.65% tu ya lengo; ingawa kwa kipindi hicho ilitarajiwa angalau iwe imefikia 75% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa kwa miaka miwili mfululizo Wizara hii imekuwa ikikusanya maduhuli chini ya matajario. Mathalani katika mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia Februari ilikuwa imekusanya kwa 32.12% tu; halikadhalika katika mwaka wa fedha 2024/2025 imekusanya kwa 42.65% tu. Kufuatia hali hiyo, Kamati ilihoji ili kujua sababu za makusanyo kuwa chini ya matarajio ambapo ilielezwa kuwa ni kutokana na: -

(i) Vyuo kukisia kudahili wanafunzi wengi tofauti na hali halisi; ambapo vilikisia kudahili wanafunzi 7,088 na vimefanikiwa kudahili wanafunzi 5,166 tu.

(ii) Baadhi ya wazazi kushindwa kulipa ada za wanafunzi na wengine kutolipa kwa wakati;

(iii) Uchakavu wa majengo na Miundombinu katika vyuo vya maendeleo ya Jamii jambo linalopelekea wanafunzi kuhama kwenye hosteli na kuishi nje ya vyuo;

(iv) Uwepo wa idadi ndogo ya vyuo vilivyoanzisha programu ya maendeleo ya jamii jambo lililopelekea mauzo ya mitaala kushuka; na

(v) Mwitikio mdogo wa wafanyabiashara kulipia ada ya kuchapisha vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Kamati kuwa Wizara iweke mikakati madhubuti ya kukusanya kutoka kwenye vyanzo vya mapato ikiwa ni pamoja na kukarabati hosteli za vyuo kwa kutumia mapato ya vyuo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 47.5 kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 25.8 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 21.6 kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 25.42 sawa na 53.53 ya fedha

iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika Jedwali Namba mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwaajili ya mishahara na matumizi mengineyo ya Wizara pamoja na Taasisi zake siyo wa kuridhisha, kwani imepokea 53.53% ya fedha iliyoidhinishwa, jambo linalopelekea Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 20.4 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni18 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2.3 ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari 2025 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 11.9 sawa na 59% ya fedha zilizotengwa. Mchanganuo wa fedha umeainishwa katika Jedwali Namba tatu

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo kama ifuatavyo:-

(a) Kwa jumla mapokezi ya fedha za nje yapo chini ya kiwango kilichopangwa kupokelewa ambapo ilipokelewa 25.4% tu ya makadirio jambo lililoathiri utekelezaji wa miradi hiyo;

(b) Mapokezi ya fedha za ndani ni ya kuridhisha ambapo Wizara imepokea 63% ya fedha zilizotengwa;

(c) Mapokezi ya fedha kwenye baadhi miradi siyo ya kuridhisha, mathalani mradi namba 5,414 wa Uhai na Makuzi ya Mtoto umepokea 22% tu ya kiasi kilichotengwa na mradi namba 6,279 wa Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Kiuchumi kwa Wanawake ambapo umepokea 31% tu ya kiasi kilichotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kulikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 10.5

kilichoidhinishwa kwa ajili ya uratibu wa shughuli za wafanyabiashara ndogondogo ikiwemo kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu itakayowawezesha kuinua mitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 8,000,000,000 tu. Aidha, ilibainika kuwa kumekuwa na kasi ndogo ya utolewaji wa fedha hizo kwa wafanyabiashara ndogondogo kwani mpaka Kamati inapokea Taarifa hii ni kiasi cha shilingi milioni 197.5 tu kimekopeshwa kwa wafanyabiashara 119 kupitia Benki ya *NMB*. Ni rai ya Kamati kuwa Wizara ihakikishe kuwa fedha zilizotolewa na Serikali zinakopeshwa kwa wakati ili wafanyabiashara waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo yapo maeneo ambayo Kamati ilishauri na Serikali haikuyazingatia kwa namna ambayo ilitarajiwa na Kamati. Mathalani suala la kutoa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati ni jambo ambalo bado limeendelea kuwa changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ushauri mwingine ni kuandaa mkakati madhubuti wa kutoa elimu kwa wafanyabiashara ndogondogo kuhusu umuhimu wa kujisajili kidijiti na fursa zinazoambatana na zoezi hilo. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee kuzingatia ushauri huo ili kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, maduhuli. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni saba. Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa katika vyanzo mbalimbali. Mchanganuo wa

makusanyo hayo ni kama unavyoonekana katika Jedwali Namba nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa, makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yanalingana na mwaka wa fedha unaoisha. Kutokana na makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha uliopita kuwa chini ya matarajio, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuweka mikakati ya makusanyo ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa hosteli ili kuongeza mapato kupitia ada za malazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa matumizi ya kawaida. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 49.1 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 26.4 ni kwa matumizi mengineyo na kiasi cha shilingi bilioni 22.6 ni fedha za mishahara. Kiasi hicho ni ongezeko la shilingi bilioni 1.6 sawa na asilimia tatu ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mchanganuo huo upo katika Jedwali Namba tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 26.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.4 ni fedha za ndani, na shilingi bilioni 11.5 ni fedha za nje. Mchanganuo kama unavyoonekana katika Jedwali Namba sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo: -

(a) Bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa takribani shilingi bilioni 6.5 sawa na 31.95% ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha; na

(b) Bajeti ya Fedha ya Nje imeongezeka kwa 62.87%.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo kutoka nje, bado Kamati inaendelea kushauri kuwa Wizara isitegemee fedha kutoka nje kwenye miradi ya maendeleo kwani fedha hizo upatikanaji wake ni wa kusuasua na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MHE. FATMA H. TOUFIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni na ushauri wa jumla. Katika majadiliano yake na Wizara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatavyo: -

(i) Kutokana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kuwa mtambuka na ina jukumu kubwa la kuleta ustawi kwa jamii ya Tanzania jambo linalopelekea kuwa na uhitaji mkubwa wa fedha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuona umuhimu wa kuiongezea Bajeti ya Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kutekeleza azma yake ya kuleta ustawi kwa jamii;

(ii) Makusanyo madogo ya maduhuli kwa Vyuo na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara, yanatokana na baadhi ya Wazazi au Walezi kushindwa kulipa ada, na uchakavu wa majengo ya hosteli jambo lilipolekea Wanafunzi wengi kuishi nje ya chuo na idadi ndogo ya wanafunzi wanaodahiliwa na vyuo. Kamati inashauri vyuo na taasisi kukarabati majengo ya *hostel* za wanafunzi kwa kutumia mapato ya ndani ili kuongeza mapato na kuendelea kuvitangaza Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi za Ustawi wa Jamii ili kuongeza idadi ya udahili wa Wanafunzi;

(iii) Ujenzi wa Hosteli katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii Uyole, Monduli na Misungwi umesimama kwa muda mrefu jambo

linalopelekea wanafunzi wengi kuishi nje ya chuo na kupelekea wanafunzi hasa wa kike kupata changamoto za unyanyasaji wa kijinsia ikizingatiwa wanafunzi wengi wanaojiunga na vyuo hivi ni wa umri kati ya miaka 16 na 18. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya ujenzi wa hosteli hizo na kupunguza changamoto zinazowakabili wanafunzi wa kike katika vyuo husika. Kwa kufanya hivyo, Serikali itapata mapato ya kiasi cha shilingi milioni 305.6 kwa mwaka kutokana na ada ya malazi;

(iv) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kunasababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua, na mingine kutotekelezwa kabisa. Imeshuhudiwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 miradi miradi mingi ya maendeleo imetekelezeka kwa kasi isiyoridhisha na mingine kutotekelezeka kabisa kutokana na ucheleweshwaji wa fedha za maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikanaji wa fedha za nje umekuwa wa kusuasua;

(v) Mwenendo usioridhisha wa utoaji wa mikopo ya wafanyabiashara ndogondogo. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imepokea kiasi cha s hilingi 8,000,000,000/= kwa ajili ya kuwakopesha wafanyabiashara ndogondogo. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 24 Machi, 2025 Wizara kupitia Benki ya *NMB* ilikuwa imekopesha shilingi milioni 197.5 kwa Wafanyabiashara 119 tu, huku idadi ya maombi ikiwa ni wafanyabiashara 1,389 ambao wameomba jumla ya fedha shilingi bilioni 2.9 ambazo bado hawajakopeshwa kutokana na mchakato wa maombi kuwa katika hatua mbalimbali. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Benki ya *NMB* kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo hii ili kurahisisha mchakato wa ukopeshaji wa fedha ambazo tayari zimeshatolewa na Serikali ziweze kuwafikia walengwa kwa wakati;

(vi) Kasi ndogo ya utoaji elimu kwa wafanyabiashara ndogondogo juu ya kujiandikisha katika Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo. Kamati imebaini kuwa hadi kufikia Februari, 2025 wafanyabiashara ndogondogo 12,000 walipewa vitambulisho kati ya wafanyabiashara 40,000 walioandikishwa na hivyo kuwezesha Serikali kukusanya kiasi cha shilingi milioni 258. Jambo hili limetokana na wafanyabishara wengi kutokuwa na elimu juu ya uwepo wa usajili huo na manufaa yanayotokana na kujisajili. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mkakati wa kutoa elimu juu ya faida za kujisajili na manufaa yatokanayo na usajili huo, ikiwemo kuweza kukopesheka na taasisi za fedha na huduma nyingine za kijamii;

(vii) Kutokuwepo kwa mikakati madhubuti ya uhamasishaji na kufuatilia ulipaji wa Ada za Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa wakati kunaathiri kwa kiasi kikubwa makusanyo ya Mapato ya Serikali kupatikana kwa wakati. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya ufuatiliaji na uhamashishaji wa mashirika yasiyo ya Kiserikali kulipa ada kwa wakati ili kuongeza mapato ya Serikali yatakayowezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Aidha, Serikali ifanye mapitio ya kiasi cha ada inayotozwa ili kuona haja ya kuongeza kiasi cha Ada kwa Mashirika hayo;

(viii) Kutokana na udahili wa Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi za Ustawi wa Jamii kuwa chini ya makadirio. Kamati inashauri Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI iweke mikakati ya kuongeza idadi ya Wanafunzi wanaopangwa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi za Ustawi wa Jamii ili kuondoa tatizo la kudahili wanafunzi wachache na hivyo kuathiri makusanyo ya mapato; na

(ix) Kutokana na ujenzi wa hosteli za wanafunzi kuwa wa kusuasua kutokana na uhaba wa bajeti, Kamati inashauri Wizara kuona umuhimu wa kuingia ubia na sekta binafsi ili kushirikiana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa hosteli ili kuondoa uhaba uliopo na kufanya maboresho ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu za Kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, Mbunge na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Mbunge, kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. John Jingu na Naibu Makatibu Wakuu Bwana Amon Anastaz Mpanju na Bi. Felister Mdemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini sio kwa umuhimu, ninapenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha Shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**27 MEI, 2025**

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;
c) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;
d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na
e) Sehemu ya Tano ni hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ni Masharti ya Kanuni za Bunge, kifungu cha

6 (5)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inapaswa kabla ya kuchambua Bajeti, kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2024/2025 kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuishauri Serikali kuhusu mambo mbalimbali yaliyobainika katika ukaguzi huo.

Kanuni ya 117 (4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lako tukufu liijadili hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Malaam pamoja na Taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu inagusa **Fungu 53.** Naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi tarehe 25 Machi 2025. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kufanya ziara za kujiridhisha na hali halisi ilivyo katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya fungu lililotajwa hapo juu. Uchambuzi wa Kamati ulikuwa kama ifuatavyo;-

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ilifanya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha

2024/2025. Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara kwaajili ya kukagua na kutembelea Mradi wa Ujenzi wa Hosteli za Wasichana Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama na Mradi wa Kituo cha Taifa cha Kulelea Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu Kurasini.

### 2.1 Ujenzi wa Hosteli za Wasichana chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 chuo hiki kilitengewa kiasi cha **Shilingi 500,000,000** ili kuendelea na Ujenzi wa hosteli ambapo hadi kufikia tarehe ya ukaguzi, Chuo hakikuwa kimepokea fedha badala yake walikuwa wanaendelea na ujenzi kwa fedha zilizotengwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kuchelewa kuwasilishwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo Kamati ilishuhudia hali ya kusuasua kwa ujenzi kutokana na mapokezi hafifu ya fedha kwaajili ya kukamilisha mradi huo. Aidha ilibainika kuwa zipo changamoto nyingine zinazokikabili chuo hicho ikiwemo uhaba wa Watumishi hususan katika kada za ukufunzi na huduma saidizi, uhaba wa miundombinu mingine kama vile madarasa.

Kwa Upande mwingine Kamati inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuanzisha mradi huu wenye lengo la kupunguza kwa kiasi kikubwa kadhia ya makazi inayowakumba Wanafunzi hususan Wanafunzi wa kike ambao kwa kiasi kikubwa huathiriwa na mwingiliano na Jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kutoa rai kwa Serikali kuwa fedha inayotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi itolewe kwa ukamilifu na kwa wakati ili kukamilisha miradi hiyo kwa muda uliopangwa.

**2.2 Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru.**

**Mhedhimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Taasisi ilitengewa kiasi cha **Shilingi 2,000,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Ujenzi wa Jengo la Utawala ambapo mpaka Kamati inatembelea eneo la mradi **shilingi 1,200,000,000** zilikuwa zimetolewa kwaajili ya utekelezaji wa mradi huu. Jengo hilo linaundwa na kumbi za mikutano na ofisi za watumishi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilijulishwa kuwa mradi huu unapaswa kukamilika mwezi Juni Mwaka 2026 ambapo mpaka Kamati inatembelea eneo la utekelezaji mradi ulikuwa umetekelezwa kwa **asilimia 70** Aidha imebainika kuwa mtiririko wa mapokeo ya fedha kwaaajili ya utekelezaji wa mradi huu ni wa kuridhisha na hivyo kupelekea mradi kutekelezwa kama ilivyopangwa. Kamati inaipongeza wizara kwa kuusimimamia vema mradi huu.

**2.3 Utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa mihadhara katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa mradi huu unatekelezwa kwa mfumo wa *force account* ambapo ulianza kutekelezwa tarehe 22 Juni, 2024 na kutarajiwa kukamilika tarehe 22 Juni 2025. Mradi huu una thamani ya Shilingi 626,405,367.66 ambapo hadi Kamati inatembelea mradi huu Shilingi 245,564,738 zilikuwa zimeshatumika na kufikia asilimia 39.2 ya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa baada ya kukamilika kwake ukumbi huu, utakuwa na uwezo wa kubeba Wanafunzi 400 kwa wakati mmoja. Aidha Kamati ilihoji juu ya kasi ya ujenzi na ilielezwa kuwa kiwango kilichofikiwa ni kutokana na mpango kazi na hivyo ujenzi utakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuhakikisha kuwa taasisi zilizopo chini yake zinatekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia makusanyo yake ya ndani na hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

**2.4 Utekelezaji wa Mradi wa kituo cha kulelea Watoto walio katika Mazingira magumu Kurasini, Dar es Salaam.**

**Mheshimiwa spika,** Kamati ilijulishwa kuwa katika kituo cha kulelea Watoto Kurasini kiasi cha **Shilingi 248,883,884** kilipelekwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2024/2025 ili kuwezesha utekelezaji bora wa majukumu ya kituo hicho, majukumu hayo ni pampja na huduma za malazi, chakula, elimu,kukuza ujuzi pale inapobidi na huduma za kiutawala.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maboresho mbalimbali yaliyofanywa katika Kituo hiki, Kamati ilishuhudia uchakavu wa miundombinu yakiwemo majengo mbalimbali kama vile mabweni, madarasa na ofisi ni rai ya Kamati kuwa iendelee kutenga fedha ili kuboresha mazingira ya Kituo hiki.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 3.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza kwa umahsusi katika mambo makuu manne kama ifuatavyo;-

(a) Makusanyo ya maduhuli;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya kawaida;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na
(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni.

### 3.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 7,040,129,000** kutoka vyanzo mbalimbali kama vile Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 4,641,025,000** Uuzaji wa Mitaala ya

Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 40,000,000**; Ada ya Malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 551,600,000** Usajili na Ada za Mwaka za NGOs **Shilingi 640,000,000,** Ada ya Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo **Shilingi 1,000,000,000,** Uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **Shilingi 7,500,000** Mauzo ya Nyaraka za Tenda na Mapato mengineyo **Shilingi 160,004,000 .**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari 2025**,** Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 3,002,447,907** sawa na **asilimia 42.56** ya makusanyo yaliyokusudiwa. Makusanyo hayo yapo katika mchanganuo ufuatao**: -** Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 2,292,702,387** sawa na **asilimia 48.93,** Uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 16,500,000** sawa na **asilimia 41.25,** Ada ya Malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 105,849,420** sawa na **asilimia 19.19,** Usajili na Ada za Mwaka za NGOs **Shilingi 323,356,100** sawa na **asilimia 50.52,** Ada ya Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo **Shilingi 258,040,000** sawa na **asilimia 25.80,** Uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **6,000,000** sawa na **asilimia 80.00,** Mauzo ya Nyaraka za Tenda na Mapato mengine **Shilingi 0** sawa na **asilimia 0** Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekena katika **Jedwali Na. 1**.


**Jedwali Na. 1: Fungu 53 Makadirio na Makusanyo halisi katika Mwaka wa Fedha 2024/2025**

| MAELEZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ada za vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 4,641,025,000 | 2,292,702,387 | 48.93 |
| Uuzaji wa Mitaala ya Maendeleo ya Jamii | 40,000,000 | 16,500,000 | 41.25 |
| Ada za Malazi ya Wanafunzi wa vyuo vya Maendeleo | 551,600,000 | 105,849,420 | 19.19 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Usajili na Ada za Mwaka za NGOs | 640,000,000 | 323,356,100 | 50.52 |
| Uuzaji wa Mitaala vya Vyuo vya Ustawi | 7,500,000 | 6,000,000 | 80.00 |
| Ada ya usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo | 1,000,000,000 | 258,040,000 | 25.80 |
| Mapato mengineyo/Mauzo ya Nyaraka za Tenda | 160,004,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **7,040,129,000** | **3,002,447,907** | **42.65** |

***Chanzo: Randama ya Bajeti ya 2024/25***

**Grafu Na. 1: Fungu 53 Makadirio na Makusanyo halisi katika Makwa wa Fedha 2024/2025**




**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(a) Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa jumla ya **Shilingi 3,002,447,907** sawa na **asilimia 42.65** ya makusanyo yote ya Wizara hii yalikusanywa katika kipindi hicho.

(b) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 Wizara hii imekusanya **asilimia 42.65** tu ya lengo; ingawa kwa kipindi hicho ilitarajiwa angalau iwe imefikia asilimia 75 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kwa miaka miwili mfululizo Wizara hii imekuwa ikikusanya maduhuli chini ya matajario, mathalani katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi kufikia Februari ilikuwa imekusanya kwa **asilimia 32.12** tu halikadhalika katika Mwaka wa fedha 2024/2025 imekusanya **asilimia 42.65** tu. Kufuatia hali hiyo Kamati ilihoji ili kujua sababu za makusanyo kuwa chini ya matarajio ambapo ilielezwa kuwa ni kutokana na-

(i) Vyuo kukisia kudahili wanafunzi wengi tofauti na hali halisi. Ambapo vilikisia kudahili wanafunzi 7,088 na vimefanikiwa kudahili 5,166 tu.

(ii) Baadhi ya wazazi kushindwa kulipa ada za wanafunzi na wengine kutolipa kwa wakati;

(iii) Uchakavu wa majengo na Miundombinu katika vyuo vya maendeleo ya Jamii jambo linalopelekea Wanafunzi kuhama kwenye hosteli na kuishi nje ya vyuo;

(iv) Uwepo wa idadi ndogo ya vyuo vilivyoanzisha programu ya maendeleo ya jamii jambo lililopelekea mauzo ya mitaala kushuka; na

(v) Mwitikio mdogo wa Wafanyabiashara kulipia ada ya kuchapisha vitambulisho.

**Mheshimiwa Spika**, Ni rai ya Kamati kuwa Wizara iweke mikakati madhubuti ya kukusanya kutoka kwenye vyanzo vya mapato ikiwa ni pamoja na kukarabati hosteli za vyuo kwa kutumia mapato ya vyuo husika.

### 3.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 47,487,079,000** kwa matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 25,836,653,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na **Shilingi 21,650,426,000** kwaajili ya mishahara**.**


**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 25,421,397,639.57** sawa na **asilimia 53.53** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida**,** ambapo **Shilingi 13,008,606,854** ni fedha kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 12,412,790,785.57** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC). Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Fungu 53 Mapokezi ya Fedha Matumizi ya Kawaida 2024/2025**

| MAPOKEZI YA FEDHA MATUMIZI YA KAWAIDA 2024/2025 | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2024/2025** | **Fedha zilizopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | 21,650,426,000 | 13,008,606,854 | 60.08 |
| OC | 25,836,653,000 | 12,412,790,785.57 | 48.04 |
| Jumla | **47,487,079,000** | **25,421,397,639.57** | **53.53** |

**Chanzo: Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 53**

**Grafu Na. 2: Fungu 53 Mapokezi ya Fedha Matumizi ya Kawaida 2024/2025**




**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwaajili ya mishahara na matumizi mengineyo ya Wizara pamoja na Taasisi zake si wa kuridhisha kwani imepokea **asilimia 53.53** ya fedha iliyoidhinishwa, jambo linalopelekea Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

### 3.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ilitengewa jumla ya **Shilingi 20,418,180,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,025,673,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 2,392,507,000** ni fedha za nje.


Hadi kufikia Februari 2025 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 11,947,861,891.00** sawa na **asilimia 59** Kati ya fedha hizo **Shilingi 11,340,673,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 607,188,891** ni fedha za Nje. Mchanganuo wa fedha hizo umeainishwa katika **Jedwali Na. 3.**

**Jedwali Na. 3: Fungu 53 Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2024/2025**

| MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2024/2025 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Namba na jina la mradi** | **Bajeti iliyotengwa 2024/2025** | | **Mapokezi ya fedha hadi kufikia Februari 2025** | | Asilimia |
| | Fedha za ndani | Fedha za nje | Fedha za ndani | Fedha za nje | |
| **Na. 6290:** *Kuprogramu Mfumo wa Kompyuta na kuchakata Data* | 150,000,000 | 0 | 150,000,000 | 0 | 100 |
| **Na. 6330:** Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 2,000,000,000 | 0 | 1,200,000,000 | 0 | 60 |
| **Na.6279** Usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa Kiuchumi kwa Wanawake | 3,200,000,000 | 0 | 1,000,000,000 | 0 | 31 |
| **Na. 6259:** Mpango wa Rasilimali kwa Program za Jinsia | 1,175,673,000 | 0 | 990,673,000 | 0 | 84 |
| **Na. 5414**: Uhai na Maendeleo ya Mtoto | 0 | 1,977,597,000 | 0 | 434,898,000 | 22 |
| **Na.5451:** Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii | 1,000,000,000 | 414,910,000 | 0 | 172,290,891 | 12 |
| **Na.6280:** Uratibu wa Makundi Maalumu | 10,500,000,000 | 0 | 8,000,000,000 | 0 | 76 |
| **Jumla Kuu** | **18,025,673,000** | **2,392,507,000** | **11,340,673,000** | **607,188,891** | **59** |

**Chanzo. Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 53**

**Chati Na. 1: Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2024/2025**




**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo kama ifuatavyo;

(a) Kwa jumla mapokezi ya fedha za nje yapo chini ya kiwango kilichopangwa kupokelewa ambapo ilipokelewa **asilimia 25.4** tu ya makadirio jambo lililoathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

(b) Mapokezi ya fedha za ndani ni ya kuridhisha ambapo Wizara imepokea **asilimia 63** ya fedha zilizotengwa.

(c) Mapokezi ya fedha kwenye baadhi miradi si ya kuridhisha mathalani mradi namba 5414 (Uhai a Makuzi ya Mtoto) ambao umepokea **asilimia 22** tu ya kiasi kilichotengwa na mradi namba 6279 (Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Kiuchumi kwa Wanawake ambapo umepokea **asilimia 31** tu ya kiasi kilichotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kulikuwa na kiasi cha **Shilingi 10,500,000,000** kilichoidhinishwa kwa ajili ya uratibu wa shughuli za Wafanyabiashara Ndogondogo ikiwemo kuwapatia mikopo

yenye masharti nafuu itakayowawezesha kuinua mitaji yao, hata hivyo hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 8,000,000,000**. Aidha, ilibainika kuwa kumekuwa na kasi ndogo ya utolewaji wa fedha hizo kwa Wafanyabiashara Ndogondogo kwani mpaka Kamati inapokea Taarifa hii ni kiasi cha **Shilingi 197,555,000** tu kimekopeshwa kwa Wafanyabiashara 119 kupitia Benki ya NMB. Ni rai ya Kamati kuwa Wizara ihakikishe kuwa fedha zilizotolewa na Serikali zinakopeshwa kwa wakati ili Wafanyabiashara waweze kunufaika.

### 3.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ambao kwa kiasi kikubwa umeisaidia Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kuleta tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo yapo maeneo ambayo Kamati ilishauri na Serikali haikuyazingatia kwa namna ambayo ilitarajiwa na Kamati, Mathalani suala la kutoa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati ni jambo ambalo bado limeendelea kuwa changamoto, aidha ushauri mwingine ni kuandaa mkakati madhubuti wa kutoa elimu kwa Wafanyabiashara ndogondogo kuhusu umuhimu wa kujisajili kidijitali na fursa zinazoambatana na zoezi hilo. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee kuzingatia ushauri huo ili kuboresha utendaji kazi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 4.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 7,040,129,000**


sawa na kiasi kilichoombwa katika mwaka wa Fedha 2024/2025. Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo ni pamoja na**:** Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 4,641,029,000,** uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 40,000,000**; Ada ya Malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 551,600,000** usajili na ada za mwaka za NGOs **Shilingi 640,000,000,** ada za usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo **Shilingi 1,000,000,000,** uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **Shilingi 7,500,000,** ada za mwaka za vituo vya kulelea watoto **160,000,000,** Mchanganuo wa lengo la kukusanya kwa Fungu 53 unaonekana katika **Jedwali Na.4** hapa chini.

**Jedwali Na. 4: Fungu 53 Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli**

| CHANZO | 2024/2025 (Tsh.) | 2024/2025 (Tsh.) | Nyongeza/ Pungufu (Tsh.) | Nyongeza / Pungufu (%) |
|---|---|---|---|---|
| Ada za vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 4,641,029,000 | 4,641,029,000 | 0 | 0 |
| Uuzaji wa Mitaala ya Maendeleo ya Jamii | 40,000,000 | 40,000,000 | 0 | 0 |
| Ada ya Malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 551,600,000 | 551,600,000 | 0 | 0 |
| Usajili wa ada za mwaka za NGOs | 640,000,000 | 640,000,000 | 0 | 0 |
| Uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Ustawi | 7,500,000 | 7,500,000 | 0 | 0 |
| Ada za usajili wa Wafanyabiashara ndogondogo | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **7,040,129,000** | **7,040,129,000** | **0** | **0** |

**Chanzo. Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 53**

**Chati Na. 2: Fungu 53 Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuhuli**




**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yanalingana na mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha uliopita kuwa chini ya matarajio, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuweka mikakati ya makusanyo ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa hosteli ili kuongeza mapato kupitia ada za malazi.

### 4.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 49,115,697,000** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shlingi 26,469,549,000** ni matumizi mengineyo na kiasi cha **Shilingi 22,646,148,000** ni fedha za Mishahara. Kiasi hicho ni


ongezeko la **Shilingi 1,628,618,000** sawa na **asilimia 3** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mchanganuo huo upo katika **Jedwali Na. 5.**

**Jedwali Na. 5: Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026**

| **ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 53 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **2024/2025 (tsh.)** | **2025/2026 (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (%.)** |
| Mishahara | 21,650,426,000 | 22,646,148,000 | 995,722,000 | 1.7 |
| OC | 25,836,653,000 | 26,469,549,000 | 632,896,000 | 1.3 |
| **Jumla** | **47,487,079,000** | **49,115,697,000** | **1,628,618,000** | **3** |

**Chanzo. Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 53**

**Grafu Na. 3: Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026**




### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwaajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara, imetengewa jumla ya **Shilingi 26,941,456,000** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,415,404,000** ni fedha za ndani, na **Shilingi 11,526,052,000** ni


fedha za nje. Mchanganguo kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 6

**Jedwali Na. 6: Fungu Na. 53 Ulinganisho wa Bajeti ya Fedha za Maendeelo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026**

| **ULINGANISHO WA FEDHA ZA MIKRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Namba na jina la mradi** | **Makadirio kwa Mwaka 2024/2025** | | **Makadirio kwa Mwaka 2025/2026** | |
| | Fedha za ndani | Fedha za nje | Fedha za ndani | Fedha za nje |
| **Na. 6290:** *Kuprogramu Mfumo wa Kompyuta na kuchakata Data* | 150,000,000 | 0 | 90,000,000 | 0 |
| **Na. 6330:** Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 2,000,000,000 | 0 | 1,200,000,000 | 0 |
| **Na.6279** Usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa Kiuchumi kwa Wanawake | 3,200,000,000 | 0 | 1,920,000,000 | 0 |
| **Na. 6259:** Mpango wa Rasilimali kwa Program za Jinsia | 1,175,673,000 | 0 | 705,404,000 | 449,335,000 |
| **Na. 5414:** Uhai na Maendeleo | 0 | 1,977,597,000 | | 2,500,000,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ya Mtoto | | | | |
| **Na.5451:** Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii | 1,000,000,000 | 414,910,000 | 1,000,000,000 | 2,000,000,000 |
| **6252. Advanced** gender equality in Tanzania PAMOJA PROJECT | 0 | 0 | 0 | 6,576,717,000 |
| **Na.6280:** Uratibu wa Makundi Maalumu | 10,500,000,000 | 0 | 10,500,000,000 | 0 |
| **Jumla Kuu** | **18,025,673,000** | **2,392,507,000** | **15,415,404,000** | **11,526,052,000** |

**Chanzo. Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 53**




**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo; -

(a) Bajeti ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa takribani **Shilingi 6,523,276,000** sawa na **asilimia 31.95** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Ongezeko hilo limetokana na uwepo wa miradi ambayo inaanza utekelezaji wake tofauti na mwaka wa fedha unaoisha. Aidha ongezeko hilo limetokana na ongezeko la fedha za nje.
(b) Bajeti ya Fedha ya Nje imeongezeka kwa **asilimia 62.87.**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo kutoka nje, bado kamati inaendelea kushauri kuwa Wizara isitegemee fedha kutoka nje kwenye miradi ya maendeleo kwani fedha hizo upatikanaji wake ni wa kusuasua na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, katika majadiliano yake na Wizara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na makundi Maalum kwa Mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati inatoa maoni, ushauri na Mapendekezo kama ifuatavyo: -

(i) Kutokana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuwa mtambuka na ina jukumu kubwa la kuleta ustawi kwa jamii ya Tanzania jambo linalopelekea kuwa na uhitaji mkubwa wa fedha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuona umuhimu wa kuiongezea Bajeti ya Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kutekeleza azma yake ya kuleta ustawi kwa jamii.

(ii) Makusanyo madogo ya maduhuli kwa Vyuo na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara, yanatokana na baadhi ya Wazazi au Walezi kushindwa kulipa ada, na uchakavu wa majengo ya hosteli jambo lilipolekea Wanafunzi wengi kuishi

nje ya chuo na idadi ndogo ya wanafunzi wanaodahiliwa na Vyuo. Kamati inashauri Vyuo na Taasisi kukarabati majengo ya hostel za wanafunzi kwa kutumia mapato ya ndani ili kuongeza mapato na kuondelea kuvitangaza Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi za Ustawi wa Jamii ili kuongeza idadi ya udahili wa Wanafunzi.

(iii) Ujenzi wa Hosteli katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii Uyole, Monduli na Misungwi umesimama kwa muda mrefu jambo linalopelekea wanafunzi wengi kuishi nje ya Chuo na kupelekea wanafunzi has awa kike kupata changamoto za unyanyasaji wa kijinsia ikizingatiwa wanafunzi wengi wanaojiunga na vyuo hivi ni wa umri kati ya miaka 16 na 18. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kiasi cha **Shilingi 6,132,008,590** kwaajili ya kumalizia ujenzi wa Hosteli hizo na kupunguza changamoto zinazowakabili Wanafunzi wa kike katika vyuo husika. Kwa kufanya hivyo, Serikali itapata mapato ya kiasi cha **Shilingi 305,600,000** kwa mwaka kutokana na ada ya malazi**.**

(iv) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuna sababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua, na mingine kutotekelezwa kabisa. Imeshuhudiwa katika Mwaka wa fedha 2024/2025 miradi miradi mingi ya maendeleo imetekelezeka kwa kasi isiyoridhisha na mingine kutotekelezeka kabisa kutokana na ucheleweshwaji wa fedha za maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio. Aidha Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikanaji wa fedha za nje umekuwa wa kusuasua.

(v) Mwenendo usioridhisha wa utoaji wa mikopo ya Wafanyabiashara ndogondogo. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imepokea kiasi cha **Shilingi 8,000,000,000**

kwaajili ya kuwakopesha Wafanyabiashara Ndogo ndogo. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 24 Machi, 2025 Wizara kupitia Benki ya NMB ilikuwa imekopesha **Shilingi 197,555,000** kwa Wafanyabiashara 119 tu, huku idadi ya maombi ikiwa ni Wafanyabiashara 1,389 ambao wameomba jumla ya Shilingi 2,960,464,500 ambazo bado hawajakopeshwa kutokana na mchakato wa maombi kuwa katika hatua mbalimbali. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Benki ya NMB kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo hii na kurahisisha mchakato wa ukopeshaji ili fehda ambazo tayari zimeshatolewa na Serikali ziweze kuwafikia walengwa kwa wakati.

(vi) Kasi ndogo ya utoaji elimu kwa Wafanyabiashara ndogondogo juu ya kujiandikisha katika Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo. Kamati imebaini kuwa hadi kufikia februari 2025 Wafanyabiashara Ndogondogo 12,000 walipewa vitambulisho kati ya 40,000 walioandikishwa na hivyo kuwezesha Serikali kukusanya kiasi cha Shilingi 258,040,00. Jambo hili limetokana na wafanyabishara wengi kutokuwa na elimu juu ya uwepo wa usajili huo na manufaa yanayotokana na kujisajili. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mkakati wa kutoa elimu juu ya faida za kujisajili na manufaa yatokanayo na usajili huo, ikiwemo kuweza kukopesheka na taasisi za fedha na huduma nyingine za kijamii.

(vii) Kutokuwepo kwa mikakati madhubuti ya uhamasishaji na kufuatilia ulipaji wa Ada za Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa wakati kunaathiri kwa kiasi kikubwa Makusanyo ya Mapato ya Serikali kupatikana kwa wakati. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya ufuatiliaji na uhamashishaji wa mashirika yasiyo ya Kiserikali kulipa Ada kwa wakati ili kuongeza mapato ya Serikali yatakayowezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Aidha Serikali ifanye Mapitio ya kiasi cha Ada inayotozwa ili kuona haja ya kuongeza kiasi cha Ada kwa Mashirika hayo.

(viii) Kutokana na udahili wa Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisis za Ustawi wa Jamii kuwa chini ya makadirio. Kamati inashauri Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI iweke mikakati ya kuongeza idadi ya Wanafunzi wanaopangwa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi za Ustawi wa Jamii ili kuondoa tatizo la kudahili Wanafunzi wachache na hivyo kuathiri makusanyo ya mapato.

(ix) Kutokana na ujenzi wa Hosteli za Wanafunzi kuwa wa kusuasua kutokana na uhaba wa bajeti, Kamati inashauri Wizara kuona umuhimu wa kuingia ubia na Sekta binafsi ili kushirikiana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa hosteli ili kuondo uhaba uliopo na kufanya maboresho ya miundombinu.

## SEHEMU YA SITA

### 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Tamima Haji Abass, Mb.
4. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb.
5. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb.
6. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe. Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
8. Mhe. Katani Ahmadi Katani, Mb.
9. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
10. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.

11. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
12. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.
13. Mhe. Alli Hassan Omar King, Mb.
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
15. Mhe. Sanya Jussa Jafar, Mb.
16. Mhe. Khamis Yussuf Mussa, Mb.
17. Mhe. January Yusuf Makamba, Mb.
18. Mhe. Khadija Shaabani Taya, Mb.
19. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
20. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
21. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Doroth Onesphoro Gwajima Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri Mhe. Mwanaidi Ali Khamis, Mb kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. John Jingu na Manaibu Katibu Wakuu Bwn. Amon Anastaz Mpanju na Bi. Felister Mdemu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja**.**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Fatma. H. Toufiq, (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**
27 Mei, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa wasilisho lako zuri kwa niaba ya Kamati yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza uchangiaji na tutaanza na Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira na Mheshimiwa Munde Tambwe, ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum asubuhi ya leo na kwanza kabisa nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara ambao kwa kweli tangu Wizara hii imeundwa, wamefanya kazi kubwa sana hasa ya kuweka *awareness* katika mambo ya unyanyasaji wa kijinsia. Tunawapongeza sana na mwendelee kwa kazi hiyo njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bajeti yao pia ni shilingi bilioni 76 tu, ninaomba tu tuwape hiyo bajeti, na kwa hiyo, ninaunga hoja mkono ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi ya leo nitajikita katika maeneo mawili tu ambayo yote ni ya kujenga ustawi wa jamii yetu ya Kitanzania. Katika kusema hivyo, ninaelekea katika msingi muhimu sana wa ustawi wa jamii yetu ambao ni ujenzi wa familia iliyo bora. Ninaamini kwamba familia ikijengwa vizuri ndiyo msingi wa jamii ambao inaendeleo lakini pia ndiyo msingi wa ustawi wa Taifa zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maarifa ambayo yanajenga msingi huu wa familia bora hayawezi kupatikana shuleni tu, wala hayawezi kupatikana katika taasisi za dini tu, maarifa haya kimsingi yanapaswa kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi ndani ya familia yenyewe. Kwa maana ya kwamba watoto kadiri wanavyokua wanapaswa kupata haya maarifa kutoka kwa wazazi wao na kwa jinsi hiyo tutajenga jamii ambayo ina ustawi unaokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo, ninapenda kurejea kwamba sisi ambao tumebahatika kuwa wazazi tuna sababu ya kuchukua muda wa kutosha au kuutafuta huo muda wa kutosha kwa maana ya kwamba ni jukumu ambalo hatuwezi kulikwepa kwa kisingizio cha kazi nyingi, cha ufanisi wa mambo mengine yote isipokuwa kufundisha watoto wetu na tunapowafundisha watoto wetu katika familia tunajenga msingi wa kwamba familia inamhitaji baba, inamhitaji mama, inawahitaji watoto na kwamba hao wote ndicho kiungo ambacho kinaweza kikajenga familia iliyo bora na yenye ustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo ambalo mimi binafsi ukinichukua (Shukrani Manya) linalonikera, ni pale ambapo watoto wa kiume au akina baba tunatelekeza watoto wetu. Yaani ulipata mtoto kwa namna yoyote ile, halafu unamtelekeza, majukumu yote ya matunzo ya malezi anaachiwa mama. Hili jambo siyo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, sisi ambao ni wazazi, tuwafundishe watoto wetu, wanapokuwa wamefikia umri huo ambao wote tunaufahamu kwamba tendo la ndoa linapofanyika ndilo linaloleta watoto duniani, na kwa hiyo, kabla ya kuwaleta watoto duniani lazima watafakari kwamba kituo kinachofuata baada ya hapo ni malezi pamoja na matunzo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi hiyo, kama kijana wa kiume au wa kike huoni kwamba unayo nafasi au uwezo wa

kufanya matunzo na malezi ya mtoto, basi kwanza usishiriki tendo linalomleta huyo mtoto duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwafundishe watoto kwamba watoto wanapokuja duniani watahitaji muunganiko wa baba na mama katika kuwalea na kuwatunza. Kwa hiyo, mmojawapo na hasa baba au huyu kijana wa kiume asikwepe akakimbia majukumu yake na kumwacha mtoto wa kike akisota peke yake katika matunzo ya mtoto ambaye ameletwa. Kwa jinsi hiyo, ninadhani sisi kama wazazi, tunayo sababu ya kuchukua muda wa kutosha kuiweka hii elimu kwa watoto wetu ili wajue kabisa kwamba ili tuweze kuwa na jamii ambayo ina ustawi lazima malezi ya watoto yaanze na wazazi wawili ambao wametamani kuwa na familia. Ni katika familia hii hii ambapo tutakataa ukatili wa kijinsia. Ni katika familia hii hii ambapo tutatoa elimu ya kukataa ushoga, na ni katika familia hizi hizi tutaweza kukilinda kizazi hadi kizazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na kupendekeza kwamba elimu hii itolewe ndani ya familia tuna sababu ya kuviomba vyombo vyetu vya habari viweke vipindi maalum kwa ajili ya elimu ya familia, yaani utakuta *TV news media outlets* nyingi haziweki kipindi hata kimoja katika jambo hili la msingi ambalo ndilo linalojenga ustawi wa jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo langu Mheshimiwa Waziri asubuhi ya leo ni kwamba, tuviombe vyombo vyetu vya habari, elimu hii ya ustawi bora wa familia viwe na kipindi maalum kwa ajili hii ili elimu hii iendelee kutolewa kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hii itakapokuwa imekuzwa sana katika familia zetu, iwe ni nyumbani iwe ni katika taasisi za dini iwe ni katika *media outlets* maana yake ni kwamba itasaidia sana Taifa kupunguza watoto wa mtaani. Hakuna mtaa unaobeba mimba kwamba mtaa unazaa watoto wakawa wa mitaani, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, ni kwa sababu mzazi mmoja amekataa majukumu yake, hatimaye tunapata watoto wa mitaani. Kwa hiyo, hakuna mtaa wenye Watoto, watoto ni wa baba na mama; na elimu hiyo lazima ikuzwe katika familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ukiangalia nchi yetu ya Tanzania ukaitazama katika picha ya ujumla unagundua kwamba tatizo la udumavu wa watoto walio chini ya miaka 15 eti linapatikana katika Mikoa ya Kigoma, Katavi, Njombe, Songwe, na Rukwa, lakini mikoa hii ndiyo yenye utoshelevu wa chakula, yaani ni mikoa ambayo inapeleka chakula sehemu nyingine kwa wingi, lakini huko ndiko kuna udumavu wa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachopungua hapa ni elimu ya lishe bora na katika hili nimtaje Mheshimiwa Lugangira ambaye kwa kweli kila mara anaposimama huwa anaongelea juu ya lishe bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe uzoefu binafsi. Wakati fulani nilikuwa ninawafundisha watoto kati ya umri wa miaka tisa hadi 15. Siku hiyo nikawatania kidogo nikawauliza, ninyi chakula chenu mnachokipenda ni nini? Wakanijibu, "Piza na baga" halafu baadaye ndiyo wakaniuliza, "Kwani wewe mwalimu chakula unachokipenda ni nini?" Nikawaambia, ugali, dagaa na matembele, ndiyo *my best meal.* Watoto wale walicheka wakagaragara. Wakanambia Mwalimu, matembele na dagaa! Wao wanataja habari ya piza na baga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani Ukoloni Mamboleo mpaka kwenye chakula? Yaani piza na baga, vyakula vya watu wengine huko ndivyo vinaonekana ni vyakula bora ndani ya nchi ya Tanzania. Tuna sababu kama nchi, sasa tuna utoshelevu wa chakula kupeleka elimu bora ya lishe katika jamii ya Kitanzania kwa sababu hii habari ya kupenda chakula cha wengine tukaacha vyakula vyetu vya asili, siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kuna msanii mmoja alisema yeye hajala ugali sijui miaka 20, na anaona kwamba hiyo ni sawa kabisa na inafaa. Katika jamii za Kitanzania leo watu wengine wanaamini kwamba kula maharage ni chakula cha wafungwa na kwamba wewe unakuwa mfungwa na kwamba ukila mboga za majani ni dalili ya umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine hata wanaozalisha maparachichi wanaamini kwamba maparachichi na ndizi ni chakula cha biashara, wao hawali na kuna wengine ambao wanadhani kwamba ukila chipsi mayai kila wakati umekuwa na lishe bora kwa sababu chakula kile kina muonjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania tunapenda sana unga wa sembe, lakini sio wote tunajua kwamba sembe imeondolewa nyuzi nyuzi *(Fiber),* na *Fiber* siyo muhimu kwa ajili ya afya zetu? Ninatamani tuwe na mwongozo wa Kitaifa juu ya nini tule kama Watanzania kwa sababu tuna utoshelevu wa chakula, lakini bado tunakula hovyo kwa sababu hatuna mwongozo mzuri wa nini tule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie dakika moja. Ninaomba ni-*tease* kidogo hapa. Hivi ni jamii ya Watanzania wangapi kina akina mama ambao wanajua mwanaume anapokuwa katika *advanced age,* mbegu za maboga ni chakula anachokihitaji sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi hawajui na akina baba wengi hawajui kuwa mbegu za maboga ndiyo zenye madini ya *zink* na *selenium* kwa wingi ambazo ndiyo zimeondoka kwa sababu mwanaume amekua, lakini hatujui. Kwa hiyo, mbegu za maboga ukienda kule *supermarket* hazinunuliwi, maana walaji hawapo. Mwanamke hajui, na baba hajui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo sababu ya msingi sana ya kuimarisha elimu ya lishe bora katika Taifa letu na ninapendekeza pia kwamba vipindi vya lishe bora virudi katika *news outlet* kama ilivyokuwa katika Redio Tanzania zamani "Kuleni chakula bora

cha kuujenga mwili;" tulikuwa tunasikiliza sana hiyo *chorus.* Sasa hivi imeenda wapi? Hiyo, "Kuleni chakula bora cha kujenga mwili", hiyo *chorus* iko wapi katika *media outlets* leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Elisha Manya. Ninadhani mmesikia habari za mbegu za maboga. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe na Mheshimiwa Tarimba Abbas ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa kwa mchango mkubwa na mzuri kwenye eneo zima la lishe. Ni kweli kabisa lishe bora ni jambo la msingi na ndilo ambalo linapelekea kutuhakikishia kama Taifa kulinda rasilimali watu. Aidha, ninamshukuru sana kwa kutambua jitihada zangu binafsi na tutaendelea kushirikiana katika kusemea ajenda hii ya lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielekeze mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu sana ambayo kimsingi inabeba muktadha mzima wa maendeleo ya jamii, lakini pia masuala ya wanawake, jinsia na makundi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kuleta mageuzi makubwa katika sekta hii ya *NGO's,* halikadhalika kuimarisha ustawi wa sekta yetu hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Doroth Gwajimba, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Jingu, pamoja na viongozi wote wa Wizara hii. Kipekee kabisa, ninapenda kutambua jitihada kubwa sana ambazo zimefanywa na dada yangu Vicky, Msajili wa *NGO's* pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya *NGO's,* Mama yangu Mwantumu Mahiza

pamoja na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumesikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sekta hii ya *NGO's* kwa mwaka 2024 peke yake imechangia shilingi trilioni 2.61 katika kutekeleza afua mbalimbali za maendeleo hapa nchini kwetu. Pia, sekta hii ya *NGO's* imechangia moja kwa moja zaidi ya ajira 21,000 kwa Watanzania. Sasa pamoja na mafanikio haya ningependa kuishauri Serikali kupitia Wizara hii katika maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, kutokana na mabadiliko ya misaada au ya utoaji misaada ya fedha kutoka Serikali ya Marekani pamoja na Serikali nyingine ambazo zinaendelea kufanya mchakato huo, ni muhimu sana Serikali ifanye tathmini ya hali ya kifedha ya *NGO's* baada ya misaada hiyo kufutwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika hapa nimtambue na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kiongozi mwenye maono kwa sababu mwaka 2023 aliielekeza Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha mfuko wa *NGO's (NGO's Basket Fund)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa sana wakati Mheshimiwa Waziri unahitimisha utueleze bayana kuanzishwa kwa mfuko huo wa *NGO's* umefikia wapi hususan tukizingatia hali ya kiuchumi iliyoko hivi sasa kutokana na misaada mbalimbali kufutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kuwasilisha ombi maalum na ninafurahi leo Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, Jerry Silaa, yuko hapa kwa sababu katika Sheria ya Taarifa ya Ulinzi Binafsi hakuna *category* inayoitambua sekta ya *NGO's*. Kwa hiyo, hiyo inasababisha kwamba *NGO's* zinatakiwa zilipe kujisajili katika mfumo wa taarifa binafsi. Jambo ambalo linakwambisha jitihada za sekta ya *NGO's.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba niwasilishe ombi kwamba sheria ile ifanyiwe maboresho kidogo itambue *category* ya *NGO's* na ziweze kupata msamaha wa kulipa kiwango hicho cha usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa upande wa *TRA,* kwa maana *TRA* wanatambua *NGO's* kama vile ni biashara. Kwa hiyo, wanazitambua na kuzichukua *NGO's* na biashara kama ni kitu kimoja; kitu ambacho kinaleta changamoto kubwa sana kikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, niiombe sana Serikali, ninatambua tumeshapata fursa tumewasilisha kwenye Tume ya Kodi, lakini niiombe sana Serikali na Wizara hii itusaidie kuhakikisha kwamba *TRA* watofautishe kati ya *NGO's* na biashara kwa sababu *NGO's* hazifanyi biashara. Kwa hiyo, kuzichukulia kikodi kama vile nazo zinafanya biashara, ni jambo ambalo siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nikiwa kama Mbunge wa Viti Maalum kupitia Chama cha Mapinduzi ninayewakilisha kundi la *NGO's* ninaomba niwasilishe shukrani zangu za dhati kwa sekta nzima ya *NGO's* kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa tokea nimeanza kuhudumu nafasi hii na halikadhalika kunifanya nimekuwa Mbunge wa kwanza aliyehudumu katika nafasi hii kupata utambuzi na ushirkiano ambao wamenipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakishukuru sana chama changu (Chama cha Mapinduzi) kupitia Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake chini ya Mwenyekiti wetu bingwa kabisa, Mheshimiwa Mjumbe wa Kamati Kuu, Mama Mary Pius Chatanda pamoja na Makamu Mwenyekiti wetu bingwa kabisa m-*NEC,* Zainab Shomari kwa kuongeza nafasi ya Wabunge wa Viti Maalum wanaowakilisha kundi la *NGO's* kutoka nafasi mbili na sasa kuwa tatu ambapo kutakuwa kuna nafasi mbili upande wa Tanzania Bara na nafasi moja upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

**27 MEI, 2025**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaendelea kudhihirisha namna ambavyo chama changu (Chama cha Mapinduzi) kinatambua na kuthamini mchango mkubwa wa sekta ya *NGO's* kwenye kuchangia maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuahidi kwamba nitaendelea kufanya kazi kwa kujituma, ufasaha na ufanisi na ubunifu na weledi mkubwa kwa maslahi mapana ya maendeleo ya Taifa letu. Halikadhalika ninaendelea kuwategemea sana mama zangu na viongozi wangu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka kila kona ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninakipongeza sana chama chetu kwa kuwa chama ambacho kinaongoza na kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kinaimarisha mazingira wezeshi ya wanawake kuweza kushiriki katika ulingo wa kisiasa na demokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Chama cha Mapindizi kiko katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kuwa na sera ya jinsia ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Mwongozo wa Dawati la Jinsia la Chama cha Mapinduzi, jambo ambalo litakwenda kuimarisha ushiriki wa wanawake katika siasa. Kwa kufanya hivyo, ndivyo ambavyo tutakuwa tunatekeleza falsafa za *Four R's* za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kubwa pia kupitia Sera hii ya Jinsia ya Chama cha mapinduzi pamoja na Mwongozo wa Dawati la Jinsia la Chama cha Mapinduzi itapelekea kuwalinda na kuwawezesha na kuhakikisha kwamba Madiwani wa Viti Maalum na Wabunge wa Viti Maalum wataweza kutekeleza majukumu yao katika maeneo yao pasipo kupitia changamoto za kukwamishana kwa maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwashukuru sana viongozi wangu wa Serikali na Chama Mkoa wa Kagera na wilaya zote nane za Mkoa wetu wa Kagera kwa ushirikiano

mkubwa ambao wameendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hususan na kwa kipekee sana niwashukuru sana wananchi wenzangu wa Bukoba Mjini kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kunipa na niwaahidi ya kwamba tutaendelea kushirikiana kama ambavyo tumekuwa tukishirikiana, na niwatoe hofu kwamba tayari nimeshapata uzoefu wa namna ya kukabiliana na changamoto zenye mlengo wa kukwamishana kwa maslahi binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, nitumie fursa hii kuwatakia kila la heri wagombea wote wa Jimbo la Bukoba Mjini na niahidi nitatoa ushirikiano mkubwa kwa yule ambaye atateuliwa na chama chetu kugombea katika nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme kwamba ninaunga mkono hoja na tukutane *site,* na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema, pia kwa tutunzia muda, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Munde Tambwe atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Abbas na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge ninaomba kabla hajaongea Mheshimiwa Tambwe, tuna changamoto ya udhuru wa Wabunge. Wengi wangependa kuchangia mapema zaidi kuliko ambavyo wamepangwa. Tutajitahidi kwa kadiri tutakavyoweza, lakini ninaomba tusameheane pale ambapo itashindikana, Mheshimiwa Tambwe.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu. Awali ya yote nipende kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kusimamia na kulinda desturi za nchi yetu pamoja na utamaduni wetu. Siku zote amekuwa akikemea na kuonya na kuwasihi Watanzania tuendelee kubaki kwenye maadili na kuyasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hotuba aliyoitoa juzi, ametoa hotuba nzuri kabisa na ametoa *statement* nzuri ambayo sisi kama Wabunge wake tuko nyuma yake, tunaifuata. Tunajua kabisa tuna Rais mwanamke hodari, mkakamavu, shupavu na ni Amiri Jeshi Mkuu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kusimama na Rais wetu, kuungana mkono na Rais wetu. Niwaambie tu, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia tunaye na tunatamba naye. Mwaka 2030 ndipo tutakuja kuachana na Mheshimiwa Dkt. Samia. Kwa hiyo, niwaambie tu wale ambao wanajaribu kufanya majaribu tofauti tofauti ni kama wanapoteza muda wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu yuko vizuri, amefanya kazi kubwa sana kwenye nchi hii. Ndani ya miaka minne hakuna Kijiji, kata, wilaya, au mkoa ambao hauna alama ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ndani ya miaka minne amefanya mambo makubwa sana. Sisi Watanzania hasa Wabunge wake wa CCM tunaona fahari na tunayo mengi ya kwenda kuwaeleza Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kwa kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia maadili kwenye nchi yetu. Napenda kuongea kuhusu Asasi za Kiraia. Tunazo asasi nyingi za kiraia kwenye nchi yetu; tunazo asasi zinazokuja kwa kificho kuleta fedha kwa ajili ya kuchafua siasa zetu; tunazo asasi zinazokuja kwa ajili ya kuharibu watoto wetu kwenye shule zetu, zipo; tunazo asasi kwa ajili ya kuharibu maadili yetu na tunazo asasi nzuri

ambazo zinakuja kusaidia Watanzania kwa malengo yao wanayoyataka kuja kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumwomba Waziri wetu wa Maendeleo, dada yetu Mheshimiwa Dkt. Gwajima anayefanya kazi kubwa sana kwenye taasisi yake na Wizara yake hii. Namwomba atwambie ana mkakati gani sasa wa kuzichambua hizi *NGO's* kujua *NGO's* zipi ni bora na zipi siyo bora, na zipi zinaingia humu ndani kuharibu vizazi vyetu, zinaingia kuja kuharibu siasa zetu, zinaingia kupenyeza wanaharakati waje kuharibu siasa zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapa aje na mkakati aliokuwa ameupanga ili tuweze kuzichambua na kuzijua zipi bora na zipi ambazo siyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kuongelea suala zima la maadili. Kwenye Wizara hii pia kuna kitu cha maadili. Mimi naomba sana kwanza nianze kwa kukemea ukatili wa mtandaoni ambao unamdhalilisha mtu, utu wa mtu, na unampa fedheha mtu kwa kutoa siri au faragha zake kwenye mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naiomba *TCRA* pamoja na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, wakae pamoja kwanza kuleta sheria kali zaidi kuliko zilizopo na kwa kufuatilia hawa watu na kuwahukumu na tuone hukumu zao zinatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule China mtu akiiba wakimkamata wakichukua zile kamera zao wanatangaza kwenye vyombo vyao vyote vya habari jinsi alivyoiba mpaka walivyomkamata na mpaka alivyoenda kuhukumiwa kwa kuchomwa sindano ya sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi hao watu wanaochafua watu kwenye mitandao na wanaofanya ukatili kwenye mitandao watakapokuwa wanakamatwa tunaomba baada ya hukumu zao tuonyeshwe kwamba huyu alifanya ukatili huu, Mahakama

imefuatilia moja, mbili, tatu, ikathibitisha na imemchukulia hatua fulani. Labda itakuwa ni fundisho kwa wengine wenye kutaka kufanya tabia mbaya kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tunaamini hatua zinachukuliwa, lakini kwa sababu zinachukuliwa kisiri, labda watu wanajua kwamba, hizo hatua hazipo na wanaendelea kufanya hayo mambo kwenye mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu kwamba, nchi yetu ni nchi yenye maadili, nchi yetu ina misingi ya kimaadili, nchi yetu ina utamaduni wa kimaadili. Niombe, sisi kama viongozi wa nchi hii hususan Wabunge ni wa kwanza tuoneshe mfano wa kimaadili, sisi ndiyo tuwe wa kwanza kuweka maadili yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuwa Mbunge leo na mimi nikawa sina maadili, ninafundisha nini kizazi cha kule nje? Maaadili ni pamoja na kuheshimu mamlaka zilizo juu yetu. Wewe ukiwa na maadili lazima uheshimu mamlaka iliyo juu yetu. Vitabu vya dini vimesema vya Kiislamu na Kikristo kwa maana ya msaafu na biblia, mamlaka na ziheshimiwe. Tumeongozwa toka kwenye vitabu vya dini, lakini leo unakuta Kiongozi au Mbunge yaani anaona anastahili kusema lolote lile bila kuangalia maadili yetu yalivyo. Niombe sana viongozi tuwe wa kwanza kuonesha mfano wa kimaadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kiongozi mzima unakwenda unavi- *blast* vyombo vyetu vya usalama, halafu unasema una maadili, ni maadili gani? Bila vyombo vya usalama tusingekuwa hapa. Ninaomba tuchukue mfano, tutoe likizo ya mwezi mmoja, polisi tumewafungia mwezi mmoja, hakuna kituo cha Polisi, hamna Usalama wa Taifa, hakuna Jeshi, patakalika hapa? Hii nchi itakalika? Mimi ninaviheshimu sana vyombo vya usalama, ninaheshimu sana viongozi wote wa vyombo vya usalama, bila wao tusingekuwepo hapa, wanatulinda, wanafanya kazi ngumu na ndiyo maana leo tunajisifu, tunajidai kwamba Tanzania ni kisiwa cha amani, lakini kuna watu hawalali kwa ajili ya kutengeneza hii amani ambayo ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo sawa kwamba Wabunge tunajua kila kitu, tunajua *job instruction* za viongozi wote, tunajua *job instruction* ya vyombo vya usalama, siyo sawa, tuache vyombo vifanye kazi kama Katiba ya nchi inavyoelekeza, tuache vyombo vifanye kazi kama sheria zilivyo zinavyoelekeza na sisi kama viongozi tuendelee kuwatia moyo. Pia, sisi kama Wabunge hatuwezi kuingilia utawala wa kuteua viongozi, Katiba inaeleza wazi nani anamteua nani na nani anamteua nani. Kwa hiyo, yule anayeteua ndiyo anayejua amteue nani kwa wakati huo na kwa nini amtoe na kwa nini amuweke mwingine, sisi haituhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhusike kwenye kuwahudumia wananchi wetu kwenye majimbo yetu tuliyoomba kura. Tuhusike kuja kuwasemea, kuja kuomba matatizo yao ambayo yapo kwenye majimbo yetu, tuje tuiambie Serikali iwatimizie wananchi wetu, lakini tusiingilie kazi za Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia kwa kusema sisi kama Wabunge tutaendelea kumlinda Rais wetu, tutaendelea kumtetea, tutaendelea kumsemea, nimesema mwanzo tu, Mheshimiwa Rais Samia aliingia kuwa Rais kwa nguvu za Mwenyezi Mungu, ile nafasi aliipata na sasa hivi tunaenda kupiga kura. Niwaambie tu Watanzania wanaonisikiliza, niwaambie watu wote kwamba, tutamchagua kwa kura nyingi za heshima kwa kazi aliyoifanya, hatutampa kura kwa sababu nyingine yoyote, Samia amefanya kazi kubwa anastahili kupata kura za heshima, kwa kazi aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Watanzania tusimame na Rais wetu, lakini Watanzania pia maadili yetu yatufundishe tuheshimu Marais wote wa nchi za jirani, tuheshimu Serikali zote za nchi za jirani, lakini wale wachache wanaotuvunjia heshima na kuingia kwenye nchi yetu kutuvuruga hakika hatutakubali. Kwa hiyo, ninawaomba vyombo vyetu vya usalama viwe macho na vifuatilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tambwe.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mniruhusu nitambulishe wageni walioingia Bungeni muda huu. Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Kwanza, ni wageni wa Mheshimiwa Dorothy Gwajima Mbunge, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ambao ni Wakurugenzi Wakuu wa Vitengo kutoka Wizarani, Wakuu wa Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Wakuu wa Vyuo, Wadau wa Vyama vya Kitaalam, Maafisa wa Serikali, Wadau kutoka Taasisi za Fedha, Wadau kutoka Vyama vya Kijamii na Wadau kutoka vyombo vya Habari. Ninaomba wasimame kwa pamoja wote. Karibuni sana Bungeni, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Mwanaidi, ambaye ni Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na hao ni Ndugu zake kutoka Zanzibar, viongozi kutoka Baraza Kuu la UWT Taifa na Viongozi wa Umoja wa Wazazi CCM Taifa. Ninaomba kwa pamoja wasimame tuwatambue, ahsanteni sana na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, aidha, tunao wageni 60 wa Mheshimiwa George Simbachawene Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni Wenyeviti wa Vijiji kutoka Kibakwe, Mkoani Dodoma, ninaomba wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana Wenyeviti wetu kutoka Kibakwe Mkoani Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi ambaye ni Ndugu William Vedastus ambaye ni mtoto wake kutoka Musoma Mkoa wa Mara. Karibu sana kijana wetu, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, ambaye ni ndugu Rashid A. Rashid, Afisa Elimu Kata, kutoka Wilaya ya Moshi Mkoa wa Kilimanjaro karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni Watumishi wa Mungu na Wanamaombi kutoka Iringa. Ninaomba wasimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 28 wa Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, ambao ni Wanachuo wenzake kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni 80 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, ambao ni Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Kiteto Mkoa wa Manyara. Karibuni sana wadau wetu kwenye siasa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni pamoja na Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya *Zone of Hope* Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Frank Mapunda, karibu sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 35 na Walimu watano wa Shule ya Awali Rabi ya Mkoani Dodoma. Karibuni sana watoto wetu tumefurahi kuwaona, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni tunaendelea. Nilishamtaja Mheshimiwa Tarimba Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Thea Medard Ntara na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Awali ya yote ninapenda kusema kwamba, ninaunga mkono hoja hii iliyoletwa na Mheshimiwa

Dorothy Gwajima na ninampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mwanaidi Ally Khamis kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nitumie nafasi hii mapema kabisa kuendelea kumhakikishia Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari Samia Suluhu Hassan kwamba, sisi Wabunge wa CCM katika Bunge hili tutaendelea kuhakikisha yeyote yule hawezi akasimama na kumchafua Rais wetu na Serikali yetu, tutapambana naye kwa vyovyote vile itakavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia eneo moja, eneo linalohusiana na ukatili dhidi ya watoto. Nimekuwa nikisoma hasa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto *(UNICEF)* linasema nini kwenye eneo hili ambalo ni muhimu sana kwa watoto wetu. Taasisi mbalimbali zimefanya tafiti ili kugundua ni jinsi gani hali ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wetu mashuleni. Hali hii inavyokwenda na nikaangalia kwamba hakika Serikali imekuwa na juhudi kubwa sana katika kutafuta njia za kuwalinda watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na sheria kali kwa mfano, kama ile Sheria ya *Sexual Offences Special Provisions Act (SOSPA)* hakika sheria hii ni kali. Vilevile, kumekuwepo na mpango unaoitwa mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kumekuwepo na Dawati la Jinsia ndani ya Jeshi la Polisi, kumekuwepo, makongamano na maandiko mengi ambayo yote yanalenga kuhakikisha kwamba, visa vinavyowasibu watoto wetu vinapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametuambia katika hotuba yake kwamba visa hivi vinapungua, lakini ukiangalia katika maandiko ya *UNICEF* wanasema visa vinaongezeka na hakika tukiangalia takwimu zinatisha. Nisingependa nichukue muda wako mwingi sana kuelezea

takwimu ziko namna gani, lakini ningependa nizungumze juu ya hali ilivyo huko kwa wananchi hali ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 17 nilipata nafasi ya kutembelea Kata ya Tandale katika Jimbo langu na pale niliongozana na Diwani wa Kata ile anaitwa Abdallah Chifu, kuongoza maandamano ya amani kuanzia Shule ya Msingi Hekima. Shule hii ya Hekima iko ndani ya Kata ile na nililazimika kufanya maandamano kwa sababu ya kwenda kwa jamii kupaza sauti juu ya kuongezeka kwa vitendo vya ulawiti na ubakaji kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandamano yale tulikuwa tunapita maeneo yote yenye watu wengi na tulikuwa tukisimama na mimi nilikuwa nikihutubia na nikipaza sauti. Takwimu zinaonesha huko nyuma kila mwezi angalau kisa kimoja kinaripotiwa katika shule ile, sasa hivi imekwenda mpaka kila wiki haikosi kuna visa vinavyoripotiwa na Mwalimu Mkuu pale anasema hatashangazwa akiona kwamba visa vile sasa ni vya kila siku. Ni kwa sababu gani? Kwa sababu jamii pamoja na sheria kali inaona kana kwamba jambo hili halipewi uzito unaostahili, ninaomba Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa makini hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaofanya visa hivi wanasemekana wanaweza wakawa ndani ya jamii kwa maana ndugu, anaweza akawa baba mdogo, baba mkubwa, anaweza akawa kaka, anaweza akawa jirani, anaweza mpangaji, unajua nyumba zetu kule uswahilini, lakini yanapotokea mambo kama haya, jamii kwa maana ya ndugu wanakaa wanajadiliana na kumalizana. Mashauri mengine hayapelekwi mahakamani na kwa kuwa hayapelekwi mahakamani hata taarifa sahihi za matukio haya hatunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tulizonazo ni zile tu zinazoripotiwa katika dawati na nyingine zikapelekwa Polisi. Vilevile, hata zikipelekwa Polisi kesi hizi zinaahirishwa mara kwa mara kiasi kwamba jamii inapotea katika kujua kesi fulani imemalizika vipi, hivyo vitendo vinaendelea. Sasa wananchi

wanasemaje? Hapa ndipo ningependa niende moja kwa moja kwenye mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanasema kwamba, mashauri yote yanayohusiana na ukatili wa kijinsia iwe watoto wa kike, watoto wa kiume, wanawake, mashauri haya yasijadiliwe katika ngazi ya kijamii, kusiwe na mapatano na kama ikiwezekana ku-*criminalize* hatua yoyote ya watu kukaa kujadili kosa la jinai kulifanya kama vile ni kosa la madai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wakashtaki Polisi na Polisi kesi iende Mahakamani na kesi ikienda mahakamani, wananchi wanataka iwe *fast track* isiwe kesi ichukue miaka miwili, miezi sita, kesi iamuliwe mapema na watu wote wanaotuhumiwa watangazeni, kwamba kuna kesi inahusiana na masuala ya ulawiti, ubakaji visa vya ukatili dhidi ya wanawake, yaani zile kesi zake zikienda Mahakamani itangazwe kwamba fulani fulani anashtakiwa na Jamhuri kwa kosa la kubaka, wananchi wajitayarishe wasubiri. Endapo itahukumiwa kwamba yule kweli ni mbakaji kuwe na *list of shame* watu waandikishwe, kwamba huyu amelitia doa, huyu ni mtu mchafu na agopewe katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezunguamzia suala moja muhimu sana kwamba, wanaopelekwa mahakamani kwa makosa kama haya, wahakikishe Serikali wanafanya mabadiliko katika sheria ikiwezekana Sheria ya *SOSPA,* masuala yote ya ukatili wa kijinsia yawe ni makosa ambayo hayana dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa haya kama hayana dhamana watuhumiwa wakirudi mjini huko watashindwa kuingilia mwenendo wa kesi kwa sababu akiachiwa kwenda huko wao wanarubuni wazazi, wanarubuni hata yule aliyefanyiwa vitendo vile, hata mahakamani haendi, mwisho wake kesi ile inakufa. Kwani kuna taabu gani kama mtu akiamua kwenda kubaka, kulawiti na akakamatwa, akashtakiwa kwa nini kesi yake isiwe haina dhamana *(bond)*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho ninaomba hili dawati la jinsia, ninajua liko pale Polisi siyo sehemu yake, lakini yeye ni sehemu ya Serikali na Polisi ni sehemu ya Serikali. Ushauri wangu dawati hili liongezewe nguvu, ikiwemo liongozwe na Makamishna iwe kama ni Idara kwa sababu tatizo la visa hivi ni kubwa. Tupeni dawati hili lionekane kana kwamba ni moja ya sehemu ambayo itakuwa ni kimbilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia kusema kwamba, ninaunga mkono hoja hii na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Gwajima pamoja na Msaidizi wake Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi, wanafanya kazi nzuri sana sana hasa ya kufichua mambo na wakipewa tu taarifa wanawajibika, nimpongeze sana. Kwenye meza yake anawajibika kutoa yale yanayoonekana ni maovu na ukishayatoa yeye Mheshimiwa Bashungwa ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani naye pale anachukua nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kuna maeneo mengi ambayo mambo mabovu yanatendeka, lakini niombe Serikali kila Wizara ichukue nafasi kama jambo limetendeka mashuleni Waziri wa Elimu anahusika, Waziri wa TAMISEMI anahusika, Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwa hiyo, mambo haya yakitendeka maovu Wizara hizi nne zikishughulika pamoja basi hayo mambo yanaweza yakaisha haraka. Mara nyingi utaona Waziri Gwajima ameibua jambo, lakini linachelewa kufanyiwa

kazi, nikutie moyo endelea na hayo mambo kuyaibua yapeleke sehemu ili kazi ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na suala la ndoa za utotoni. Suala la ndoa za utotoni ninakumbuka wazi kwamba, wenzetu hawa walituambia wanakusanya maoni, wakakusanya maoni halafu likabaki kimya. Waziri Ndumbaro alisimama na ninakumbuka aliulizwa na Spika wanaleta Muswada au wanaleta maoni? Akajibu tunaleta Muswada, Sheria ya Ndoa za Utotoni ni lini itafika mwisho wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe elimu kidogo sana kuhusu suala zima la uzazi. Ninasikitika kusema kwamba wengi wanaelewa kwamba mtoto wa kike akishaona tu hedhi basi amekuwa anastahili kuolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisafiri na mama mmoja alikuwa anatoka Zanzibar. Wakati tunaongea akaonyesha ana machungu akasema mimi mtoto wangu ameona hedhi ana miaka 10; alilia sana. Sasa miaka 10 mnataka huyu mtoto akaolewe? Dalili za mtoto wa kike kukua ziko nyingi, wenzetu wanazitambua moja tu na wengi ni hao wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa kike kujua kwamba huyu sasa yuko tayari kuingia kwenye kuolewa au kuingia kwenye ndoa; kwanza unamwangalia kiuno chake tunaita *pelvic girdle* zipanuke. Lazima unaangalia hiyo ambayo pia tunaita nyonga. Kwa hiyo nyonga zinapanuka ndiyo dalili mojawapo. Pia dalili nyingine kwa mtoto wa kike ni sauti kubadilika kuwa nyororo, ngozi kubadilika na nywele kuota kwenye sehemu za kwapani na sehemu za siri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanachukua dalili moja kwamba mtoto akiona hedhi ndiyo amekua; siyo kweli. Kwa hiyo niwaombe sana wale wanaofikiria kwamba mtoto akifikia ameona hedhi miaka 10 au 12, (watoto wa siku hizi wanapata hedhi mapema) basi aolewe. Juzi mliona kwenye magazeti baba

mmoja amemchukua mtoto wa miaka tisa akamharibu mtoto aka-*bleed* mpaka akafariki; ndicho mnachokitaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wanaosema eti sheria zinasema mtoto akipata hedhi aolewe, watoto wao wako shuleni wanasoma; hakuna aliyempeleka mtoto wake akaolewe. Mheshimiwa Waziri watuletee ushuhuda hapa watoto wao wameolewa na miaka 12 au 13? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Sheria ya Ndoa irudi. Mheshimiwa Esther Matiko aliliongea sana jambo hili, lakini bado tunaangalia tu. Wewe mtoto wako wa kike miaka 10 unampeleka kwa mwanaume kweli? Hivi kwa nini tunashindwa kufanya maamuzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maoni waliyokusanya Mheshimiwa Gwajima na Mheshimiwa Ndumbaro yamefikia wapi? Kwa nini bado tunashindwa kufanya maamuzi kama nchi? Hawa wachache waliokuja sijui wanasema hapana sheria; kuna tamaduni lazima tuziondoe. Watoto wanahitaji kusoma, kwa hiyo hilo Wizara ilisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka majibu, mtoto kuona hedhi siyo kwamba ndiyo yuko tayari ni kama mahindi wakiona yale mahindi yanapotoa zile nyuzi pale juu ndiyo mhindi umekomaa? Si bado unaona kwamba lazima ukae, ukomae ndiyo ule. Huwezi ukauvunja ule ukala, mahindi yale yanatoa maziwa maziwa tu. Tujipange kwenye hilo, ninamwomba Mheshimiwa Gwajima asimame kwenye nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumza ni kuhusu suala zima la ukatili na maadili. Yaani ni ukweli usiofichika ukatili ndiyo umezidi, ubakaji upo, wamesema wenzangu kulawiti watoto kunaendelea na sisi tulisema walete Muswada hapa tubadilishe sheria. Mtu analawiti mtoto wako ni kwa sababu wakati mwingine hayatugusi. Mtoto analawitiwa halafu wanasema huyu mtu anapelekwa kule? Tulisema walete tubadilishe sheria tuweke sheria kali kama wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaume hao wanaobaka wahasiwe. Pia, niliwaomba wakipelekwa kule; jana tumewasifia sana Polisi hapa. Wakipelekwa huko kabla hawajafika Mahakamani washughulikieni. Kuna dawa wawape, wawahasi wale wakae hivyo hivyo watatumia lile eneo lao kwa ajili ya kutoa haja ndogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tunaliona hili suala kama ni la mchezo lakini haya mambo yanaendelea. Hebu tulete sheria sasa haya mambo ya kubakana na ya kulawitiwa tulete sheria kali. Tukifanya hivyo mara moja watu watashika adabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye haya mambo ya maadili ya kawaida. Mavazi sasa hivi hovyo. Niwapongeze sana wasanii ambao mpaka sasa wao mavazi yao ni ya heshima akiwepo Darassa, Lady Jaydee na Ben Pol wanavaa mavazi mazuri, lakini nyimbo mbaya na mavazi mabaya kwa wengine wote, Wizarz wachukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi, ni aibu kuna wanawake wanacheza vigodoro na Dar es Salaam ndiyo inaongoza. Hivi kweli wanacheza nguo zile, ninasikia zile nguo wanazilowesha maji halafu wanavaa ili sehemu zao zile zitingishike. Jamani tunaona hayo kwenye ma-*clip,* Serikali iko wapi? Wakamate hao wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanavaa nguo za hovyo na hii singeli; singeli imekuja vizuri ila wameibadilisha wanacheza hovyo. Mheshimiwa Bashungwa asaidiane na Mama Gwajima wawakamate wale wanawake wote wanaocheza, wanatuaibisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanacheza unaona kabisa hii ni sawa. Ali Kiba anavaa vizuri, tunataka wanamuziki wanaovaa vizuri, tunataka wasanii wanaovaa vizuri. Kuwa msanii au kuwa maarufu siyo kuvaa nguo za ajabu na siyo kuimba

nyimbo za matusi. Sasa haya mambo tukiwa *serious right from the beginning* watu watajua Tanzania sasa iko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine maadili hayo hayo wamesema hapa. Tunawafundisha nini watoto kama kuna dhehebu la dini linafundisha vitu vya ajabu? Fungia! Wakati ule Mheshimiwa Sagini amempeleka yule Mchungaji, Hakimu akamwachia. Mtu anawafundisha watoto wetu eti mimi ni Mungu ndani yangu kuna Mungu, wanamwachia! Mheshimiwa Bashungwa anamwachia? Hapana, wafanye sasa hivi, ninaomba wa-*review* madhehebu yote ya dini ya hovyo hovyo yanayosema uongo tuyafungie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wanaona yule wa madhehebu mmoja ametoka Kongo, wameona alivyotutukana? Yule wa Kongo anasema ametuibia hela ametudanganya alikuwa anaitwa nani yule? Nani…

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo huyo…

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo huyo. *(Makofi/Vicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kiboko ya wachawi…

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, anaitwa kiboko ya wachawi. Kiboko ya wachawi anatamba alivyotufanyia Tanzania na ndiyo hayo hayo yanayoendelea kwa Mama Zumaridi. Hivi vitu kwa nini tunaviangalia? Yaani ni aibu kweli halafu Mchungaji mzima unahubiri mbele unakatakata viuno kweli? Halafu mnasema huyo ni Mchungaji? *No*…

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwongezee mchangiaji kwamba kwa kweli kuna umuhimu sana wa kuangalia maadili yetu; leo kuna vijana wanasuka kama wanawake. Kwa nini isichukuliwe hatua ya kuwanyoa nywele tunapokutana nao barabarani? *(Makofi/Vicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea hiyo taarifa na ndiyo maana nimempongeza mwanamuziki mmoja. Wewe hujamwona yule mwanamuziki ametoboa masikio, anavaa vaa hereni. Ali Kiba anaishi katika maadili, lakini wengine wanavaa suruali wanaimba muziki, wameishusha chini lichupi linaonekana; nani anataka kuona? Nani anataka kuona chupi yako? Kwani nani asiyevaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuangalie hivyo vitu jamani. Hebu tusimame kwenye maadili tuwe kama Wakorea jamani tusimame kwenye maadili. Wanapaka; yaani ni vitu vya ajabu. Wasimamie na hapo niwaombe sana. Mama Gwajima wasaidiane na Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Bashungwa hayo ndiyo maeneo yake, awakamate tutengeneze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niombe sana Mheshimiwa Gwajima kama anavyofanya kuna hawa wanafunzi wetu wenye ulemavu hasa ulemavu wa ngozi na ulemavu wa miguu, vile vifaa tukisema wavifuate hospitalini au sijui kwenye *sectors* hawapati. Mafuta ya watu wenye u-*albino* ninaomba wagawiwe shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vya watoto wenye ulemavu viende kwenye vyuo au mashuleni, hapo tutakuwa tumetengeneza. Hawana uwezo! *Please,* hebu viende mashuleni wagawiwe; kwanza ni wachache. Wagawiwe kama

wanavyogawiwa wengine vidonge vile vya *TB,* vidonge vya *HIV,* wagawiwe pia mafuta mashuleni na vyuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara. Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru kunipa fursa hii ya kuchangia. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika jamii yetu hususan kwa umaalum wao waliokuwa nao maana Wizara yao inagusa moja kwa moja wanawake, watoto na jamii nzima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee sisi tukiwa kama Wabunge Wanawake hatuna namna na hatuna maneno mazuri, ushirikiano wao kwetu umekuwa mkubwa na wamekuwa wakifanya ufuatiliaji wa karibu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri maana yeye ni Waziri kwa wanawake kati yao ni wa mwendokasi. Pia, nimshukuru kwa namna anavyokwenda na Naibu Waziri wake. Naibu Waziri wake muda mwingi anakuwepo Bungeni, msikivu, mtulivu, mtu ambaye anatusikiliza, anasikiliza na kufanya papo kwa papo kutatua matatizo ya wanawake tunapomletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nina mambo matatu ambayo nitakwenda kuyazungumza. Wanawake wa Zanzibar, Mkoa wa Magharibi wameniteua kunileta hapa Bungeni kuzungumza zaidi mambo yanayowahusu wanawake na kero za watoto na Tanzania kwa ujumla. Kwa hiyo sitosita kufanya hivyo kila nitakapopata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara na Watumishi wote kwa namna

wanavyofanya kazi vizuri na Waziri na Naibu Waziri na ndiyo maana Wizara imepata ufanisi mzuri wa kufanya kazi. Niwapongeze Wakuu wa Mikoa wote Tanzania na Wakuu wa Wilaya. Mara nyingi shughuli nyingi za kijamii na matatizo mengi ya wanawake na watoto, utatuzi wake huanzia kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Wamekuwa wakichukua fursa hii kila inapobidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani niseme mambo mengi ninayojua kupitia Wakuu wa Mikoa wetu na Wakuu wa Wilaya. Mheshimiwa Rais wetu hakuwahi kukosea namna anavyoteua Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Tumeona kwa namna ya kipekee nilitamani kuyasema yale wanayoyafanya lakini ninafikiri Mheshimiwa Waziri na Naibu wake ni mashahidi hata kuna watoto wanaotelekezwa mitaani au kutupwa; Wakuu wa Mikoa bado wanawachukua kuwaweka ndani ya nyumba zao na Wakuu wa Wilaya. Niwapongeze, tunawaona kwenye mitandao namna wanavyoihudumia jamii. Hakika Mungu alipitisha roho ya kuwateua kupitia Mama yetu Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, 2024/2025, zaidi ya shilingi bilioni 67 ndiyo zilikuwepo kwenye Wizara hii, lakini kwa sasa tunaongea ni shilingi bilioni 76; ongezeko la shilingi bilioni nane. Tunamshukuru Rais wetu kwa kuupa umuhimu wa kipekee kwamba Wizara hii ni Wizara iliyobeba wanawake, watoto na kero zote zilizokuwepo ndani ya jamii. Tunasema ahsante na tunamshukuru Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ambayo sisi kama Wabunge tunapaswa kuyawasilisha kwa Wizara ili kuona tunaboresha vipi na kuweza kufanya kazi vipi ndani ya Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni mifumo ya uchangishaji wa fedha kwa watu wenye matatizo. Mheshimiwa Waziri ni Mama jasiri, hatuna mashaka na uongozi wake, angalia mifumo sahihi ya uchangishaji wa fedha. Kuna watu binafsi mara nyingi wanajitokeza labda kuna mtoto anaumwa na jamii yetu ya

Tanzania ni watu wanaoishi kwa huruma na kuhurumiana, wanaishi wakiwa na nguvu ya pamoja ya kusaidiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa wanaweka mitandaoni namba za simu wanasema changia mgonjwa ni huyu. Mheshimiwa Waziri hili tunalileta kwako, mtu yeyote ndani ya mtandao anapoweka namba ya simu ya kuchangia iwe imepata kibali kutoka ndani ya Wizarani. Mheshimiwa Waziri alichukue hili wawe wanakata vibali na namba hiyo wawe wanaitoa wao ikiwa ni namba ya simu iwe imesajiliwa chini ya Wizara yenu na ikiwa ni namba ya Benki iwe imetoka kupitia Wizara yenu. Ikiwezekana kufanya hivi kwa mtu, wako wanawake wengi wanajitolea ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wana vyombo binafsi vya *TV* wanaenda kuibua kero za wananchi na wananchi wengi na jamii yetu ya Tanzania huwa wanaguswa wanachangia. Mheshimiwa Waziri alichukue hili na namna ya pekee ya kulitatua, mtu anapotaka kuchangisha jamii ya Tanzania, kibali kiwe kimetoka chini ya Wizara yake. Atafute namna ya kuliweka ili likae vizuri liende. Maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba mtu huyo wakati anachangisha watamfuatilia mwisho wa kufunga mjadala wa kuchangisha alichangisha shilingi ngapi? Je, zilikwenda kwa mhusika? Bado liko chini ya dhamana ya Wizara. Ninadhani tuweke mambo yetu yaende sawa ili Watanzania wanufaike na Tanzania yao na michango inayotolewa na Watanzania wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo kwangu lilinifanya leo nisimame ni mwenendo mzima wa wanafunzi katika shule zetu. Mheshimiwa Waziri muda mwingine kama hakualikwa ataalikwa Naibu Waziri au Waziri mwingine yeyote na muda mwingine Wabunge wa Viti Maalum au Wabunge wa Majimbo tunaalikwa mahafali ya shule watoto wa *nursery* wadogo mpaka watoto wa *primary*. Mheshimiwa Waziri nimesimama hapa kwa masikitiko makubwa, watoto wale sasa hivi kwenye mahafali zao kutoka shule za *nursery* kwenda *primary* wanafungwa kanga za

kiuno wanafungwa tena ili kiuno kikaze wanafungwa kanga mbili Waziri atoe tamko tena atoe tamko kali kwa walimu na kwa shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa kwamba kuna Wizara ya Elimu lakini suala la malezi ni juu ya Wizara hii. Haiwezekani watoto wetu wa kiume, watoto wa kike wadogo tena baya zaidi mtoto wa kike akishafungwa ile kanga kiunoni na macho anapeleka juu anakata viuno laiti ni kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, kuna watoto wetu wa kiume wanakata viuono mpaka inafika wakati unasema imekuwaje? Mheshimiwa Waziri hili halihitaji fedha, hili hatuna sehemu ya kuwaambia Mama Samia aongeze fedha, inahitaji karipio lake na tamko lake; wasituchezeshee watoto wetu viuno. Kuna michezo shuleni ya watoto wanapofanya mahafali wawape *debate* za kushindana juu ya kujibu, maswali itatufurahisha zaidi. Kengele imelia, hiyo ni ya kwanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la watoto kuamshwa alfajiri. Mheshimiwa Waziri mtoto anakwenda *nursery* anaenda kujifunza kushika kalamu siyo kuandika, kushika penseli anaenda kujifunza (a) inaandikwaje? Hivi mtoto unamkuta anasubiriwa na basi la shule? Haya tumeamua kuyaleta kwa Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Elimu tumeshasema tumechoka tunalileta kwake kwa ujasiri wake hili asijadiliane nao; tunamtaka atoe tamko. Wanawake wa Tanzania tupo nyuma yake kwenye matamko haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini mtoto wa *nursery* anasubiria basi la shule. Amka alfajiri fanya mazoezi, saa 10.30 mfikirie mtoto yule kutoka saa 10.30 alipokwenda barabarani kusubiri basi, ameamka saa ngapi kujiandaa? Wakati huo anamwacha mama yake na baba yake wamelala kitandani; huyo mtoto anaenda kutafuta nini? Tusaidiane kurekebisha muda wa mabasi kuchukua watoto kwenda shuleni. Mheshimiwa Waziri hili tunatumia nguvu kubwa kama Serikali na tunatumia nguvu

kubwa kama Wabunge kuona vitendo vya ubakaji vinaondokaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya vitu vinavyoleta ubakaji ni pamoja na mifumo mibovu ya usimamizi wa watoto wetu juu ya kwenda shule. Mheshimiwa Waziri hili ni dogo lifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la watoto waliopata matatizo ambapo wazee wao wamekorofishana na mama akaamua kuchukua begi kwenda nyumbani kwao. Mheshimiwa Waziri kuna tatizo kubwa na katika sehemu ambayo tunapaswa kutunga sheria iwapo mtoto akapotea, akababakwa, lakini mazingira yale kama wanatuhusisha sisi kama walezi au wazazi tuna sehemu ya kuwajibishwa kwenye sheria ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mama amekorofishana na mume wake ametoka; mama anakaa Kariakoo baba anakaa Tabata. Kwa hiyo mtoto yule anaenda kuishi na mama Kariakoo, shule Tabata. Kwa hiyo, bado yule mtoto ule mfumo wa kuamshwa saa 10 za usiku aende shule mbali. Mheshimiwa Waziri katika kesi zinazokuja lazima tuangalie kwa kina chanzo cha tatizo la mtoto limesababishwa na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya matatizo tunasababisha sisi wazazi tuliowazaa watoto. Mtoto unamtengenezea mazingira magumu. Wewe umekorofishana na mume wako, ni wewe, lakini ushindani wako na mumeo unatengeneza kumuadhibu mtoto. Waziri, shule zimejengwa mpaka chini ya nyumba zetu. Mheshimiwa Rais anaendelea kujenga shule, hakuna sababu ya watoto wetu kupata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia hayo machache ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tauhida.

Mheshimiwa Waziri hili jambo la watoto kwenda kuamshwa saa 11, watoto wa chekechea na *nursery,* mwaka jana 2024 lilizungumzwa. Ninadhani ni vizuri Waziri akalifafanua hapa, kama haiwezekani kulifanyia kazi kwa sasa ni vizuri Watanzania wakajua kwa nini?

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara muhimu sana. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema, imempendeza leo nisimame kwenye Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyofanya kazi nzuri na njema sana kwenye Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inahusu wanawake pia. Ninapenda kuchukua nafasi hii nimpongeze sana Mwenyekiti wa Wanawake Tanzania, Mheshimiwa Mary Chatanda, pamoja na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Zainab Shomari, amekuwa akipita kila mkoa kuhakikisha anaongelea wanawake, watoto na makundi ya watu maalum. Hongera sana Mheshimiwa Mary Chatanda pamoja na timu yake yote kwa ujumla. Mungu asimpungukie kwa muda wake na nafasi kubwa anayoitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimempongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa, kwetu Mkoa wa Mbeya amefanya mambo makubwa kwa maana ya kwamba, kila Wizara inaposimama hapa kuchangia michango yake, kila mahali anaongelewa ambavyo amefanya kazi kubwa na njema kwenye Wizara hiyo. Kwenye wizara hii Mheshimiwa Rais ametusaidia sana, kwa Mkoa wa Mbeya amewajali pia, wanawake ambao wanajifungua, kwa maana ya Jengo la Mama na Mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wilaya ya Kyela amejenga Majengo ya Mama na Mtoto manne, Mbarali majengo manne, Rungwe pamoja na Busokelo majengo tisa, Chunya majengo sita, Mbeya Jiji majengo saba, lakini Mbeya Jiji hapa amejenga jengo kubwa sana, pale Meta, ambalo limegharimu fedha kiasi cha shilingi 11,300,000,000; pamoja na hayo, amenunua vifaa muhimu sana, kwa ajili ya wanawake na watoto, vya zaidi ya shilingi bilioni tano. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa, amekuwa akijali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Wizara hii. Ninampongeza Mheshimiwa Gwajima, Waziri, Naibu Waziri wake na Wizara yote kwa ujumla, wanafanya kazi njema sana. Ninaomba jambo moja, wawatazame wazee wa Taifa hili. Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, ni msikivu, ana busara na hekima, kwa majengo haya yote ambayo ameyajenga, kwa ajili ya afya za wanawake na Watanzania wote kwa ujumla, hawezi kushindwa kujenga angalau kila wilaya moja *hostel,* ili kuwatunza wazee pale kwa sababu, kuna wazee wengine ambao hawana msaada wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, Serikali inatoa hizi Fedha za *TASAF,* lakini mzee yule anakuwa hana mtu yoyote wa kumsaidia, yamkini hata kwenda kuzifikia fedha zile! Fedha zile zinachukuliwa na wajanja; anakosa fedha, lakini kama kuna viongozi ambao wana roho ya huruma wakamfikishia fedha zile, akapewa, anapita mtu anamwomba akamnunulie japo sukari kwa sababu, yeye hana uwezo. Matokeo yake kijana anaweza akapotea na fedha na ndani hamna kuni, maji, sukari na kitu chochote cha muhimu. Kwa hiyo, niombe sana kwenye Wizara hii wawajali wazee. Pamoja na kwamba, wameonesha kuwajali, lakini angalau *hostel* ijengwe katika kila wilaya moja, litakuwa jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania Baba yetu wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alituachia misingi imara sana ya amani, upendo na mshikamano. Misingi hiyo ni ambayo Watanzania tunaendelea kukua nayo, ninaomba kutoa

angalizo jambo moja; katika misingi hiyo kwa upande wa wazazi, baba na mama, mke anapokuwa mjamzito, awe baba awe mama, anategemea apate mtoto ambaye ni mwenye busara na hekima na awatii wazazi vile ambavyo wamemwongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine maadili yameporomoka sana. Maadili hayo ni sisi wenyewe wazazi ambao tunatakiwa tuyalinde. Natamani nishauri jambo moja kwa Watanzania, unajua kiumbe tangu kinaingia ndani ya tumbo, tunapaswa kuombea watoto wetu kuanzia akiwa ni kiumbe kipo ndani ya tumbo. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu mtoto huyo aje atoke na awe ni mtoto wa aina gani, vile ambavyo mzazi yeyote anapenda mtoto wake atoke akiwa salama na afuate yale anayofundishwa na wazazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulizuka maneno mbalimbali kwamba, Wabunge wakisimama Bungeni kazi yao ni kumpongeza Mheshimiwa Rais. Sisi Wabunge tunasimama hapa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uhalisia wa kazi zake nzuri anazozifanya. Mheshimiwa Rais, pamoja na kazi nyingine tunazoziongelea, angalia miradi mikubwa ambayo ilikuwa imeachwa Awamu ya Tano; Bwawa la Mwalimu Nyerere lilikuwa 32% tu, lakini Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kadri anavyoweza zikatolewa fedha zaidi ya shilingi trilioni 6.58 likakamilika na sasa umeme upo wa kutosha. Nani kama Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo *SGR* sasa hivi imekuwa ni mtelezo tu. Tunakwenda Dar es Salaam, Morogoro; wanakwenda wanafanya kazi na wengine wanarudi kufanya kazi hapa. Yote hiyo ni kwa sababu, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesimamia hayo. Kipindi cha Awamu ya Tano zilitolewa karibu shilingi trilioni nne, lakini sasa hivi miradi inayoendelea kwenye *SGR* Mheshimiwa Rais ametoa zaidi ya shilingi trilioni saba, ujenzi wa *SGR* unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuongea jambo moja muhimu na makini sana. Kuna maneno ambayo yalikuwa yakipita

kwenye mitandao, Mheshimiwa Rais wetu ametwezwa sana utu wake. Ninatamani kukemea sana hili jambo. Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni mama mnyeyekevu, ana busara na hekima na ni msikivu sana. Mheshimiwa Rais wetu tunampenda sana, hatutaki mtu yeyote aguse mboni ya jicho lake. Maana kwa kutweza utu wake kwenye mitandao wanagusa mboni ya Mheshimiwa Rais na wamegusa mboni ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa, majirani zetu wa Kenya, wanapata wapi ujasiri wa kumtukana Mheshimiwa Rais wetu hapa nchini? Wanapata wapi ujasiri wa kusema watakuja hapa Tanzania wafanye wanavyotaka? Wao wakiwa na misukosuko kwao kule hawajawahi kuona Mtanzania yeyote ametoka hapa kwenda kufanya vurugu kwao, wao wanaingiaje hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara husika, ambayo inashughulikia watu ambao ni watovu wa nidhamu, kuwakamata haraka mara moja na kuwadhibiti, ili wajue Tanzania tupo imara na macho. Hakuna kitendo kimeniuma na kimewaumiza Watanzania, kama mtu kumtukana Mheshimiwa Rais wetu. Ninajua hata sasa hivi wanaweza kuhamia kwenye Bunge hili ili waweze kututukana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeshazoea, Wabunge, watukane wanavyotaka, lakini Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, wamwache mama wa watu. Wamwache aendelee kufanya kazi, maana tunajua anafanya kazi nzuri, anafanya kazi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi tumempitisha kwa mara nyingine tena, ili awe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia kipindi hiki mpaka miaka mitano ijayo na atakuwa Rais hata wafanye nini, hakuna mtu wa kupinga. Tunakwenda kwenye kampeni, tukutane *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayupo mtu wa kumsemea vibaya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mimi na Watanzania wote tutakuwa mstari wa mbele. Tunampenda na tunamtegemea Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, ni mama bora, mwema na amefundishwa maadili, watu wamemtukana kwenye mitandao, amenyamaza kimya ni kwa sababu, ni mstaarabu. Ni mama mwema sana na ni bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Ninaamini ujumbe umefika kwa ndugu zetu hao Wakenya na hata hawa ambao Watanzania wanagusagusa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Suma ikenda Fyandomo. Ninaona leo umetumia sauti ya zege. Ahsante sana, hongera sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea ninaomba tuwatambue wageni wengine ambao wapo:-

Tunao wageni 64 wa Mheshimiwa Dorothy George Kilave, ambao ni Wanachama wa Taasisi ya Sisi Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam. Tunaomba wasimame tuwatambue, kama wapo. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 25 kutoka Chuo cha Dar es Salaam, Tumaini *University*. Karibuni sana, tunafurahi kwa kutembelewa nanyi. *(Makofi)*

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Tunaye Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana. Niwapongeze Waziri na Naibu wake. Ninamwona

Waziri anajitahidi sana, lakini bado tuna changamoto kubwa kwenye hii Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubakaji na ulawiti bado sana Tanzania. Hapa ninapoongea, kule Tarime, Halmashauri ya Mji wa Tarime, ndani ya mwezi mmoja kuna mtoto wa darasa la tatu ana miaka kumi tu; walivamiwa nyumbani kwao wakamfunga mama yake usoni wakampiga sana mama yule, ambapo amefariki na amezikwa siku kama nne hivi, wakambaka yule binti wa miaka 10. Haikuishia hapo, kuna dada mmoja anaitwa Esther Gaustine, huyo ni wa Kinyamanyoli; yule mama anaitwa Schola Magabe, ambaye wamemzika hata siku nne hazijapita, mtoto wake alibakwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Tulwa, Mtaa wa Kwa Kiogoma, kuna mama mmoja pia alibakwa, anaitwa Esther Gaustine. Wakamchoma visu, wakambaka akafariki. Mwenzake walimchoma visu, wakambaka, lakini akapona; siwezi ku-*disclose* jina lake hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo bado yanaendelea. Tunaomba sana, sheria zipo, lakini inaonekana *enforcement* haipo kabisa! Wanatoa elimu, lakini bado hayo majanga ni makubwa sana kwenye jamii yetu! Achilia mbali watoto wadogo ambao wanalawitiwa na kubakwa, haya mambo hatuwezi kuendelea kuyavumilia kwa Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na maswali, walishauliza hata Wabunge hapa. Wale akinamama ambao unakuta wamebakwa wamepata ujauzito, *at a time* inawa-*affect* kisaikolojia. Anabeba yule mtoto, wengine wanashindwa wanatoa mimba, lakini wengine wakizaa bado wanakuwa wanam-*hate* yule mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali hapa Bungeni; ninawaza kwa kina sana, kama ambavyo wameanzisha madawati ya jinsia kwenye vituo vya polisi, labda waanzishe tena

madawati kwenye vituo vya afya, zahanati na hata hospitali. Kitengo maalum kabisa cha saikolojia kwa akinamama wajawazito ambao wanaweza waka-*estimate* ambao wamebakwa waweze kufanyiwa *counselling* wakiwa wajawazito, ili wasifanye *abortion*. Pia, hata wakishakuwa wamejifungua, kama wametelekezwa, waone jinsi gani wanawasaidia wasiweze, wengine, kutupa wale watoto au kuwanyanyapaa kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri inaweza ikasaidia wakati tukiangalia *measures* nyingine za kukomesha hili wimbi la ubakaji na ulawiti ambao unafanywa na ndugu zetu. Sijui ni kwa sababu ya *depression* ama kitu gani kingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru pia kwa Mji wa Tarime, tulikuwa tunapiga kelele Maafisa Ustawi wa Jamii na Maendeleo, lakini sasa hivi tunao wa kutosha. Changamoto ambayo tunaipata ni, tunashukuru wametupatia Maafisa Maendeleo ya Jamiii 11 wameenda kwenye kata zote nane na wengine wamebaki pale Halmashauri ya Mji, lakini hawana vitendea kazi kwa maana ya gari na pikipiki katika halmashauri ya mji, ili kuweza kuzunguka. Wapewe sasa kila kata, ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi, kama vile ambavyo kwenye Wizara ya Kilimo wameweza kuwapatia Maafisa Ugavi, basi na hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wapewe kwenye kata zao ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni changamoto ambayo inajitokeza sasa kwenye hii mikopo ya 10%, ambapo tunawapa vijana asilimia nne, wanawake asilimia nne na watu wenye ulemavu asilimia mbili. Kule kwetu Tarime watu wenye ulemavu wamepata changamoto sana kwa sababu ya kile kigezo ambacho wamekiweka kwamba, ni lazima awe na shughuli fulani, ambayo anaifanya au biashara, unakuta hawana, kwa hiyo unakuta ile asilimia mbili haiendi kwa walengwa. Kwa hiyo, pale tunawaza, aidha hiki kigezo kiondoke au waboreshe waweze kutoa *specific amount,* kama ruzuku kwa hawa watu, ili sasa hata wawe na *initial capital* ya kuweza kufanya hizo shughuli

kwa sababu, unakuta wengi, nikitoa *sample* ya pale Tarime, hawawezi kupata hii mikopo na inapita tu bila kunufaika wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwenye mikopo hii ya 10% ni, watu wanaopewa, sheria iliyopo sasa hivi, wengine hawafanyi marejesho kabisa, hawarudishi na hatua ukichukua kali unasema umempeleka Mahakamani. Ukimpeleka kule ni kesi ya madai, anachoambiwa sana sana anapewa utaratibu upya wa kulipa. Wengine unakuta wanakiuka hata hiyo Amri ya Mahakama hawalipi. Kwa hiyo, unakuta fedha zinapotea, zinashindwa ku-*revolve* wengine waweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, labda wataangalia upi utaratibu mpya bora; aidha, watafanya mtu asipoleta afunguliwe kesi ya jinai, kama amechukua fedha kwa kudanganya, maana mtu kama amechukua kwenda kujiendeleza kiuchumi, ni lazima atafanyia kazi aweze kurejesha na wengine wapate, lakini ukichukua kwa ajili ya udanganyifu huwezi kupata hata hiyo ya kurejesha. Kwa hiyo, tuboreshe, wasiporejesha wafunguliwe jinai watu waogope, waweze kuleta marejesho ukizingatia kwamba, hizi fedha zinatolewa bila riba yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo, kwenye halmashauri ambazo hazina fedha nyingi. Kwa mfano, mapato ni shilingi bilioni mbili, nilishawahi kusema hata hapa Bungeni, 10% yake ni shilingi milioni 200 tu. Sasa, hii unakuta haitoshelezi ukilinganisha na halmashauri nyingine unakuta wanapata mapato ya shilingi bilioni 70 au 80, hapo10% yake ni shilingi bilioni saba au nane. Kwa hiyo, waangalie ile Mifuko mingine ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ipewe kipaumbele kwenye hizi halmashauri ambazo zina mapato madogo, ili wale wananchi na wenyewe waweze kunufaika, kama wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kule kwetu, Halmashauri ya Mji Tarime, mapato yetu ni madogo sana hayafiki hata shilingi bilioni tano. Kwa hiyo, wahakikishe hizi zinaangaliwa, wakiwemo wazee ambao hawapati 10% zile kwenye hii Mifuko ya uwezeshaji

waweze kunufaika, wazee wetu nao waweze ku-*move* mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu 2025 ni mwaka wa uchaguzi. Nipo kwenye Bunge la *IPU* na wewe mwenyewe ni Mjumbe, unajua kabisa tulikuwa tunaadhimisha miaka 40 kule, Bunge lililopita. *IPU* pamoja na *UN Women* waliweza kufanya tafiti za uwakilishi wa wanawake kwenye Mabunge; Wanawake Marais, Spika, Naibu Spika na Mawaziri, nitaenda kusoma hizi takwimu kabla sijaweka hoja yangu, ikizingatia mwaka huu 2025 Tanzania ni mwaka wa Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia idadi ya Wabunge wanawake Tanzania, Kidunia tunashika nafasi ya 39, Kiafrika tunashika nafasi ya tisa na kwa *East Africa* Tanzania tunashika nafasi ya tatu. Kidunia nchi ya kwanza ni Rwanda na Kiafrika pia, ni Rwanda, wenyewe wana *lower chamber* na *upper chamber*. Kwa wastani wanakuwa wana 59% uwakilishi wa wanawake Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuja *South Africa,* kwa Afrika wana 44% wenyewe ni wa pili, wa kwanza ni Rwanda. Ethiopia wana 36% ya wanawake Bungeni. Kwa *East Africa* sasa Rwanda ya kwanza 59%, wanafuata Burundi 38%, hii ni kwa mujibu wa Januari; ninajua kuna baadhi ya nchi zimefanya uchaguzi, kama Namibia. Wanafuata Burundi 34.2%, sisi Tanzania tunafuata kwa 37.2% wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwa upande wa Mawaziri wanawake, Tanzania kidunia ndiyo tupo 65, Kiafrika tunafika nafasi ya 15, ya kwanza ni Ethiopia ina 45% ya wanawake Mawaziri. *South Africa* ina 43% ya wanawake Mawaziri, Madagascar ina 42% ya wanawake Mawaziri. Kwa *East Africa* Tanzania sisi ni wa nne, Burundi ni ya kwanza 33%, Kenya na Uganda walipata 30% wote na Tanzania tuna 28.6%. Mawaziri kwenye sekta nyeti, kama *defence,* Tanzania tumo, kidunia ni wanawake 21 tu ambao ni Mawaziri. Pia, ikasisitiza sekta, kama *finance*, madini, nishati na sekta nyingine nyeti *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye Maspika ni 23.7%. Tanzania tunashukuru sisi tuna Spika wetu mwanamke na ndiyo Rais wa *IPU,* Naibu Spika ni 32%. Kwenye Marais *(Heads of State)* 11%, *Heads of Government* ni 8.3%. *Heads of State and Government* ni Marais sita tu dunia nzima, kwa Januari. Kwa Afrika ni Rais mmoja tu, ambaye ni Dkt. Mama Samia, *by then,* kwa Januari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tunajua kwenye uchaguzi huwa kuna unyanyasaji wa aina nyingi. Ninashukuru Tanzania tumetunga sheria ile, kama wakati wa kampeni wakifanya *violence* yoyote *against women,* watachukuliwa hatua. Pia, kuna hizi *cyber bullying* na ndiyo maana hata ukiona watu wana-*react* na mimi, *in particular,* jana nili-*react* sana kwa Rais kushambuliwa kwa *cyber bullying* ambazo zinamvua nguo kwa sababu, kwanza ni *image* siyo tu kwa Tanzania, kwa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanamke pekee ambaye ni *Head of State and Government* kwa dunia katika wanawake ni sita tu. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe tusiwafanye wanawake wajitoe kwenda *front* kwenye nafasi ya udiwani, ubunge na urais. Nimeona *ACT* wametangaza kuna mwanamke atasimama kupitia *ACT* nafasi ya Urais. CCM wameshampitisha Mheshimiwa Dkt. Samia kusimama kugombea nafasi ya urais. Lazima tuhakikishe mtu ukimpinga mtu, m-*criticize* kwa hoja na sera, siyo kumtweza utu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana…

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa. Mheshimiwa Mpembenwe.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na mchango mzuri sana anaochangia

Mheshimiwa Mbunge, *Senior,* ninataka nimwambie tu; anachosema ni sahihi. Wanawake wanapaswa wapewe nafasi ya uhakika, lakini kwa Tanzania nafasi ya Urais tayari tunaye Mama Samia. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Esther! hii ni Taarifa au *approval?*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unilindie muda.

**MWENYEKITI:** Unaipokea hii Taarifa?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa yake ninaipokea kwa sababu nina imani. Nimesema hapa *ACT* wameweka mwanamke, CCM wamesimamisha mwanamke; mama anaweza kuwa na *advantage* zaidi kwa sababu, yupo kwenye mamlaka, ataenda atauza alichokifanya, wananchi watapima. Wakiridhika na yale ambayo amefanya watamu-*endorse*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, atakuwa Rais baada ya uchaguzi kufanyika, Tarehe 28 Oktoba, 2025. Kwa hiyo, niwaombe sana, tunaposimama kukemea *cyber bullying*, mimi jana nilisema ni *activism* wa haki za binadamu na wazungu wanasema, *two wrongs don't make right;* mimi nikikukosea huwezi uka-*revenge* kwa kunifanyia ubaya, ndiyo eti unajilipiza niliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote ambaye anahisi amefanyiwa mabaya na Mamlaka ya Tanzania kuna mambo mbalimbali; kuna Mamlaka ya Kitaifa na Kimataifa, tuna mpaka Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, kama unahisi *there is no justice,* nenda, *file*. Hata hapa Tanzania tumeona kuna

mtu alishawahi kufukuzwa kazi, akahisi hakutendewa haki, mawakili kutoka kwenye chama changu wakaenda Mahakamani ku-*file*, ili aweze kupata haki yake. Ukifanyiwa kosa usirudishe kosa kwa kumtweza mtu mwingine, hiyo mimi nitapinga, leo, kesho, mpaka ninaingia kaburini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, kwa mchango wako.

Ninawshukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumepata nafasi ya kuchangia asubuhi ya leo. Ni bahati mbaya kwa baadhi yetu, wale ambao tulikuwa na dharura tumeshindwa kuchangia asubuhi, tutajitahidi mchana tutoe nafasi za mapema. Mchana wa leo watakaofuatia nitawasoma baada ya tangazo ambalo ninaenda kulisoma sasa.

Waheshimiwa Wabunge tunakumbushwa, tangazo hili lilishatoka jana; tunakumbushwa Wabunge wote kuwa, Wizara ya Nishati itaendesha semina kuhusu gesi ya petroli inayoingizwa kutoka nje ya nchi, kwa ajili ya kupikia hapa nchini na gesi asilia iliyozalishwa hapa nchini.

Semina hii inafanyika leo, Tarehe 27 Mei, 2025 mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge, Saa 7.00 Mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu, ili kuwajengea uelewa zaidi kuhusu *Liquified Petrol Gas* na *Natural Gas.*

Waheshimiwa Wabunge tutakaporejea mchana, tutaanza na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, atafutiwa na Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa Christina Christopher Mnzava, Mheshimiwa Profesa Patric Alois Ndakidemi, Mheshimiwa Joesph George Kakunda na Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila.

Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha Bunge mpaka Saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

**27 MEI, 2025**

*(Saa 7.03 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Waheshimiwa tunaendelea na ratiba yetu ya uchangiaji. Nilishawatamka wachangiaji wetu wa asubuhi. Tutaanza na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Asya Sharif Omar na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kufungua jioni kuchangia Wizara pendwa ili tuweze kutoa maoni.

Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri, dada yetu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mwanaidi kwa kazi nzuri ambayo kiukweli wameitendea haki Wizara hii. Wamekuwa na matamko mengi, wamekuwa na ufuatiliaji wa karibu sana kwa matukio mbalimbali ambayo yanaathiri maisha ya mwanamke na mtoto kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia maeneo makuu matatu. La kwanza kabisa, ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ninaomba uketi. Ahsante.

Katibu.

**27 MEI, 2025**

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Majadiliano yanaendelea. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama nilivyosema hapo awali ninawapongeza viongozi, lakini nisimsahau Katibu Mkuu Jingu ambaye yeye ndiye anayeendesha Wizara, kwa maana ya utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa Wizara hii ni Wizara muhimu sana kwa kuweka Taifa letu la sasa, la kesho na kesho kutwa. Tusipokuwa na msingi kwa kumsaidia Wizara hii basi tutakuwa hatuna Taifa hapo mbele kwa sababu tunapozungumzia mwanamke, tukizungumzia mtoto na jamii nzima, basi tunakuwa tumeweza kujua ni namna gani tunaweza tukaandaa Taifa letu kuwa bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninapenda kuzungumzia suala la bajeti. Tusipoipatia Wizara hii bajeti ya kutosha; kwa sababu tunafahamu hapa walipata fedha za maendeleo 31.95% hii ni namba ndogo sana. Bunge linapopitisha bajeti kimsingi bajeti zile zinaenda kusaidia Wizara kufanya mambo yale ambayo tumewaambia wafanye. Tunapowapa chini ya 50% utekelezaji wao hasa wataalam unakuwa mbovu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kuwa Wizara hii inaendesha vyuo vya ustawi wa jamii. Tunafahamu na hata Kamati imeeleza hapa, kwamba mabweni, vyuo, bado ni

chakavu. Tunahitaji kujenga na kuwapatia fedha za kutosha na tukifahamu kabisa kwenye mabweni tunakuwa tumemsaidia mtoto wa kike. Anapokuwa anasoma katika mazingira mazuri, basi yale mambo yasiyomfaa hawezi kuyafirikia kwa sababu yuko katika eneo ambalo linamsaidia aweze kusoma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba Wizara hii ndiyo inayotengeneza wanawake wa kesho, mama wa kesho, viongozi wa kesho. Basi tunaomba tuwapatie fedha sawasawa na jinsi walivyoomba na kuwafanya ndugu zetu hawa wataalam waweze kufanikisha yale ambayo wameyapanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna eneo la mikopo ya wafanyabiashara ndogo ndogo. Tunaomba sana ninajua kwamba bajeti anaisema na sisi tunapitisha vifungu hapa, lakini utekelezaji wake unakuwa mdogo. Mwisho wa siku hawa watu wanaanza kuona Serikali kama haifanyi kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Rungwe sijaona, labda aje aniambie anapotoa majibu; kwamba kuna Wamachinga wamepata mikopo. Kwenye takwimu zake inaonyesha kwamba aliomba bilioni nane, lakini watu waliopata tu ni milioni 197. Tunaomba basi, kama bajeti inataka bilioni nane basi *at least* isogee ili watu hawa wafanyabiashara ndogo ndogo waweze kufanikiwa, maana hao ndio wengi wanaofanya uchumi wetu, hasa kwenye halmashauri zetu, uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudi tena kwenye suala la maadili. Sisi kama Taifa, kwanza sisi viongozi tunaamini kwamba tukitengeneza familia bora kwenye ngazi ya familia, basi Taifa linapata viongozi bora. Leo hii tukianza na sisi viongozi, hatujui watoto wetu wanacheza na nani, hatujui watoto wetu wanaongea na nani, tuko bize na siasa, kwa sisi wanasiasa. Viongozi mbalimbali maofisini unatoka nyumbani saa 11 asubuhi unarudi nyumbani saa tano usiku, hujui mtoto wako anaongea na nani, amekula nini na anafanya nini. Nimesema tunatengeneza viongozi wa kesho. Tusipowasimamia sisi tukasema kwanza Serikali ije, tunaanza kwanza sisi Serikali inafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna maadili mabovu kabisa kwenye jamii zetu. Tunaona jinsi ambavyo watoto wetu wanaishi na wadada wa kazi ambao hata huyo dada maskini ambaye tumesema hapa na wenzangu waliotangulia asubuhi, hata mishahara yao tunawakopa hatuwapi. Si tu kuwakopa tunawapa pia mishahara midogo sana; na elimu zao wengine ni ndogo kabisa kuliko hata watoto wetu. Unategemea huyo ndiye ahakikishe mtoto wako amekula vizuri, uhakikishe mtoto amempeleka shule, wala huwezi kujua mtoto amerudi shule saa ngapi. Tunakuja kupata kizazi ambacho tunakilaumu, tunasema watoto hawatusikii sisi, kumbe watoto ni watoto wa kinadada. Mtoto analelewa na dada asubuhi mpaka jioni, mzazi hujihusishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia masuala ya shule za *boarding*, tunafahamu kabisa kwamba ni vyema watoto wasome shule zote, ni haki, lakini mtoto ambaye ana miaka mitatu anawekwa *boarding,* hili ni suala la hatari sana kwa kiazi kijacho. Mtoto anaangalia *TV channels* ambazo hatuzifahamu asubuhi mpaka jioni bila kuangaliwa na wazazi wala walezi ambao wamepewa. Hiyo siyo sawa. Matokeo yake sasa ndiyo tunapata hao watukanaji wa kwenye mitandao. Niseme tu kwamba, tusipokuwa na maadili mema kama Taifa tutalaumiana, tutalaumu Serikali, lakini mwanzo wa ujenzi wa familia ni wewe mzazi ambaye umetengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa Mbunge hapa amezungumzia suala la akinababa wanaozalisha wanawake na kuacha watoto. Hili ni suala ambalo sasa limekwishakuwa kama mazoea na *single mothers* imekuwa kama ni jina la uhalali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafahamu kwamba tumekuwa tunamrushia Mheshimiwa Waziri, ma-*message* mbalimbali akinamama wakiteseka kabisa. Mtu anazaa na mtu kwa makusudi. Anajua kwamba yeye ni mume wa mtu, anazalisha halafu anafanya siri. Akina dada waliozalishwa waseme waume zetu walikowazalisha ili wawe wazi, ili watoto hao waweze kutunzwa kwa sababu kosa siyo la mtoto. Mapenzi

wamefanya wao wawili, lakini watoto hawapelekwi shule, watoto wanapata shida hawana bima za afya, akinababa wazima kabisa na vyeo maofisini wanazalisha watu na kujificha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri alisimamie hilo, kwa sababu hatimaye tunaacha watoto wenye vinyongo vikubwa kabisa na kuja kutiliana sumu na watoto tuliowazaa kwenye ndoa kwa sababu tu wana uchungu waliofanyiwa na baba zao ambao hawakutaka kuwatunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia akinamama ambao pia wanawaza vibaya. Mama anazaa mtoto nje halafu anatupa mtoto. Kwani alipokuwa anazaa kwa nini hukuwa na kinga? Kwa sababu kuna sayansi zinaendelea na wakati mwingine wanawapeleka kwenye vituo vya kulelea watoto, ninafikiri si sawa. Tupeleke watoto kwenye vituo wale walioshindikana kabisa, ambao wamepata bahati mbaya ya kufiwa na amebaki na bibi ambaye ni mzee, tuwapeleke basi kwenye hivyo vituo. Lakini wamezaa kwa mapenzi yao kwa makusudi wanakuja kuwaweka watoto katika hali mbaya na hatimaye tunawaita watoto wa mitaani. Mtaa haujawahi kuzaa mtoto hata siku moja. Tuhakikishe tunawalinda hawa watoto kwa nguvu zote, maana hilo ndiyo Taifa la kesho *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mitandao; haki za watoto kwenye mitandao. Kuna watu wanapiga picha bila hata kuziba nyuso za wale watoto. Sheria ipo; uwezi kum-*expose* mtoto kwenye mtandao hata kama unataka apewe matibabu, hata kama unataka asaidiwe. Ni lazima ufiche sura yake kwa faida yake na kwa ulinzi wake na usalama wake. Ninaomba kwa picha kama hizo azitolee matamko. Tumemwambia tangu asubuhi atoe matamko. Awe tu mama matamko, tunamruhusu kabisa. Kwa sababu hatimaye tunahitaji usalama wa hawa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna *cyber crime* na *bullying* kwenye mitandao. Hili suala si la Mama Samia kwa kwa sababu ni Rais wa Tanzania, ni suala la haki ya mwanamke

kulindwa. Leo hii tunakwenda kwenye uchaguzi, tulitunga sheria hapa, kwamba tunahitaji kulinda haki ya mwanamke. Leo hii unawezaje mwanamke mwenzetu akamtukana mwanamke mwingine? Hii haitakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala wala si suala la kisiasa, ni suala la hifadhi na hadhi ya mwanamke anayotakiwa kulindwa nayo. Wanawake wenzetu wengi wengi wengi; wewe fikiria kama Mheshimiwa Rais anaweza akafanyiwa vile nini mtu wa kawaida anashindwaji kufanyiwa hivyo? Anafanyiwa vitu vibaya, anaweza akafanyiwa masuala ya ngono na yakarushwa kwenye mtandao na hao wanaume wanaofanya hivyo wapo, lakini pia wanaotukana kwenye mitandao wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema vizuri sana kiongozi mmoja hapa asubuhi, kwamba Wizara ya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na Wizara yake Mheshimiwa Waziri, ni lazima tusimamie haki za wanawake wote akiwemo na Rais wetu ambaye ametukanwa. Hili nimeliona kwenye mitandao wakiendelea kusema, kwamba nyinyi mnaosema mna njaa. Suala la njaa lipo katika haki na staha ya mwanamke yeyote katika Taifa hili. Tunaomba tulindwe kama wanawake. Tusipokuwa wakali mwisho wa siku tutajenga Taifa ambalo kitu kikifanyika kidogo tu unarushwa kwenye mtandao. Kitu kikikosewa kidogo tu unarushwa kwenye mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sheria zichukue mkondo wake kwa kulinda hadhi ya mwanamke yeyote anayesemwa vibaya kwenye mtandao. Hata kama umegombana na mume wako, hana mamlaka ya kurusha chochote, kwamba huyu mwanamke nimemwacha kwenye mtandao. Tunahitaji *privacy* ya ndoa, tunahitaji *privacy* ya wanawake, kwa sababu tunajua mwanamke akilindwa Taifa linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia mambo mengi sana. Mwaka jana nilizungumzia suala la ombaomba, hasa wale wazee wanaotembea na vijana wadogo. Muda wa saa za shule mzee ameshika fimbo na anavutwa na mtoto wa darasa la pili au

la tatu au la nne kwenda kuomba kwenye baa. Ninaomba watoto hawa na wazazi hawa wapigwe marufuku; na tutoe tamko kabisa, kwamba, hakuna kutoa fedha kwa mzee huyu kwa sababu zile fedha hazimsaidii yule mtoto. Hiyo ni biashara ya yule mzee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa wana *future* yao ya kesho. Leo hii saa saba mchana anatembea na mtoto baa anakwenda kuomba fedha. Huyu mtoto atasoma lini, anapata afya gani? Watoto ni wachafu, unaona kabisa watoto ni wadhaifu. Ninaomba litolewe tamko kwa watoto hawa. Nilisema mwaka jana na mwaka huu ninarudia. Ninaomba Mheshimiwa Waziri alichukulie hatua suala hili *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, tunaomba kabisa Mheshimiwa Waziri asimamie nafasi yake kama Waziri. Tuko nyuma yake kuhakikisha kuwa haki ya mtoto wa kike pamoja na wanawake viongozi na wanawake wa kawaida inalindwa sawasawa na sheria na kanuni la Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaunga hoja katika bajeti hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea ninaomba tutambue uwepo wa mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum, ambaye ni Ndugu Yusuph Kileo, Mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Ukatili Mtandaoni. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Asya Sharif Omar, atafuata Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ajiandae.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na akanipa afya njema jioni hii leo nikaweza

kusimama katika Bunge letu hili Tukufu na kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia kumpongeza kwa kazi nzuri ambazo anaendelea nazo za utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi. Aya inasema, "*Man la yashkurin-nasa la yashkurillah.!*". Mtu yeyote ambaye hatamshukuru binadamu mwenziwe basi hata Mwenyezi Mungu hataweza kumshukuru. Mimi ni nani, wao ni nani hata wasiweze kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia kwa mazuri ambayo ametufanyia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kuendelea kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoendelea kuletea maendeleo Taifa hili. Aliyekuwa haoni hataki kuona, asione, lakini sisi tulio wengi tunaiona kazi kubwa anayoifanya Mama Samia. Ni kazi ambayo imetukuka; ni kazi ambayo inaleta imani kubwa kwa Watanzania, hasa wanyonge, tukiwemo sisi wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anatokea mtu kibaraka aliyekuwa tayari amepigwa na laana na Mwenyezi Mungu anamkosea Mama Samia, anamkebehi. Tunasema Mwenyezi Mungu hatasimama nao watu kama hao. Hatutowapa nafasi watu madhalimu na wabaya ambao hawaoni jitihada ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeumia sana. Ninachangia Wizara hii ya Maendeleo na haya ninayazungumzia kwa ukali. Tumekerwa sana na watu hawa. Tunasema wakome! Mama Samia amezaliwa, ni mtoto ana wazazi wake kama walivyozaliwa wao. Haiwezekani na tunaiomba sana Wizara inayoshughulika na Mambo ya Ndani, Wizara yetu ya Ulinzi na Usalama, ihakikishe kwamba inachukua sheria mara moja kwa vibaraka wale ambao wamekosa nidhamu na utu. Ninathubutu kusema kuwa hawana hofu ya Mwenyezi Mungu. Haiwezekani! Wao ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi ni mtu ambaye ameshushwa na Mwenyezi Mungu. Uongozi hakujitengenezea, amepewa. Leo inakuwaje anakuja mtu anamchafua Rais wetu? Halikubaliki. Kama kuna vibaraka wanaona wana nafasi katika nchi hii kumchafua Mama Samia, wamechelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, salamu ziwafikie wale majeruhi wote ambao wanajaribu kuichezea nchi yetu. Tuko macho Tanzania, hatuchezewi na Mama Samia yuko vizuri, na jeshi lake ndiyo kina sisi hapa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze mchango wangu kwa Wizara hii, hizo zilikuwa ni salamu tu. Mchango wangu leo utajikita kwa vijana wetu Wamachinga. Bado tutaendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ndugu zetu Wamachinga hawa ambao ni wafanyabishara ndogo ndogo, wakiwemo Mama Lishe, Baba Lishe, wale ndugu zetu ambao ni wajasiriamali washonaji wa nguo, pia bodaboda ambao ni vijana nguvu kazi ambayo Taifa inalitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nampongeza Mama Samia na kumshukuru sana kwa kuyaona makundi haya, kuyafikia, lakini pia kuyarahisishia maisha yao ya kila siku katika kujitafutia riziki. Hongera sana kwa Mama Samia na Mungu atamsimamia amtie nguvu. Wale wote waliokuwa na nia mbaya Mwenyezi Mungu atawalaani, *Insha Allah*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia ameweza kutoa fedha kwa ajili ya kuwekea mazingira mazuri ya kufanya kazi makundi mbalimbali yakiwemo kama haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameweza kujenga ofisi kila mkoa ndani ya Tanzania hii. Kama haitoshi, amewapa mtaji wa milioni 10 kila mkoa. Tunataka nini Watanzania? Tunataka nini kama si kumtia nguvu Rais wetu na kumshukuru kwa upendo wa dhati, lakini anafanya kwamba ni wajibu wake. Halafu watokee

wachache tu waseme ooh Mama Samia! Nyie, hee; mshindwe na mlegee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi za mikoa 17 tayari ziko katika matengenezo ya kukamilika ili na wao sasa waweze kufaidika na zile shughuli zao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Rais wangu, Mama Samia kwa kuendelea kuwaona machinga hawa, bodaboda, baba lishe, mama lishe lakini wale mafundi wa nguo, na bodaboda kwa kufikia zile nafasi za mikoa. Kama haitoshi, ninampongeza Rais wetu sana kwa sababu Ilani hii ameitekeleza 99% na sasa tupo mwezi Juni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mpaka nina furaha kwa kweli, amewapatia mtaji wa shilingi milioni 10 kila mkoa, lakini sasa ofisi za mikoa 17 zimekamilika na wengine wapo mbioni kukamilishiwa.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja nimalizie, kwa sababu kuna mambo mazuri. Sasa hivi watu 78 ambao wamesajili kupitia mfumo wanasomeka kwenye mfumo, lakini kama haitoshi 601 tayari wameshakopeshwa tunataka nini? Kama siyo kumpa kura ya ndiyo Mama Samia, ikifika 2025. Mama Samia huyu huyu sasa hivi tayari kuna shilingi bilioni 1.1 hizo hela tayari zimeshaenda kwa hao ndugu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengine 2,000 wanatarajiwa kupata mkopo wa shilingi bilioni 3.5 kwenye bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2024/2025. Haya ndugu zangu ndio maendeleo, halafu waje wengine hapa wawavunje moyo. Ndugu zangu machinga ninataka nitoe rai kwao, niseme Mama Samia ni kioo lakini Mama Samia mtu tena mwenye utu, tumshikilie, tumng'ang'anie na tumwombee kwa Mwenyezi Mungu, aendelee kumtia nguvu.

Ninakuahidi Mama Samia tutaendelea kukutetea na hatakugusa mtu yeyote, Mwenyezi Mungu atakulinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zetu hawa machinga pia, wamebahatika sasa kazi zao kuingia kwenye mfumo wa kidijiti na kwa sasa hivi wameweza tena kuingia ndani ya mifumo hiyo kupitia vitambulisho vyao vya *NIDA*, lakini wameenda kuingia kwenye mifumo ya benki. Mwanzo hawa walikuwa mambo ya kukopa ni magumu, lakini sasa masharti ni nafuu, kwa sababu mtu mwenyewe anaweza kukopa na kujidhamini, nani kama Mama Samia? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, baada ya maelezo hayo ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asya Sharif Omar, kwa mchango wako tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako saa hizi. Nimesimama hapa katika Bunge hili Tukufu ili kuweza kuichangia hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ninapenda sana kuichangia hii, maana ina mambo mbalimbali, hii Wizara tamu kama nini. Wale viongozi wangu kule mbele walipo na wao ni wazuri, watamu sana. Maana Mheshimiwa Waziri wangu pale na Naibu wake, Mheshimiwa Mwanaidi, wanafanya kazi kubwa. Ninasema siku zote Mheshimiwa Mwanaidi, saa zote ukimwita; leo ukimwita anakwambia mimi sasa hivi sina nafasi niko huku.

Anaangalia Wizara yake, jinsi anavyofanya kazi pamoja na Waziri wake. Akija hapa anatoa maswali asubuhi kisha anatoka anakwenda kufanya kazi zake za wanawake. Kwa hiyo, ninawapongeza sana, waendelee kuifanya kazi vizuri katika Wizara yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi Mheshimiwa huyu alivyokuwa ana maono. Ninasema huyu kaanza kuyaona maono toka huko anakotokea Mheshimiwa Rais. Tupo pamoja kipindi kile Mbunge na Mwakilishi Jimbo la Makunduchi, tunafanya kazi basi yeye ana maono, hapa nikifanya hivi itakuwa hivi yanakuwa kweli na hapa nikifanya hivi inakuwa hii, inakuwa kweli. Sasa hivi ameshakuwa Rais anafanya vitu kweli. Kwa hiyo, ninampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wanaombeza, waache wambeze na yule sisi kwetu kazaliwa hana matatizo, tena kazaliwa mtoto wa tumbo, mjukuu wa mbavu. Mwenyezi Mungu amwondolee shari, ampe heri, amjaalie kila la heri ndugu yangu, aendelee na kazi zake vizuri na viongozi wenziwe waliomzunguka Mheshimiwa Dkt. Samia. Mheshimiwa Dkt. Samia ana imani toka huko anakotokea, mpaka hivi sasa anaendelea na kazi. Ninasema haya kwa sababu mimi mwenyewe ninamjua *A to Z,* ninamjua Mheshimiwa Dkt. Samia. Kwa hiyo, waache wao wabeze, wafanye maneno yao wanayomsemesha yeye mwenyewe katulia na anaangalia, siyo kama hajui kusema yule, anasema tena akisema neno lake moja utatafuta uvungu ujitie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuchangia sasa. Kuna suala hili la akinababa wale ambao wanabaka watoto huko nje au kuwalawiti, wanaume hawa wanawalawiti watoto wetu wale ambao hawana akili, maana akili hawana. Wanawaona hawa mbumbumbu basi huyu mimi ndiye atakayenifaa. Maana anaona yule mwenye akili yake, anaona mimi pale nitaenda chukua mzigo wa UKIMWI au maradhi mengine, lakini ninakwenda kwa huyo uliokuwa mbumbumbu hajafanywa chochote. Anakwenda kule anamsemesha na yule analaghaiwa,

anacheka tayari anamwingilia na kisha pengine kashamjaza mimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba ile aliyokwisha kumjaza sasa, siyo yule kama atamshughulikia, atashughulikiwa na wazee wake, baba au mama au familia. Mtoto yule atazaa atakwisha na kama ataulizwa basi anasema, mimi kanifanya jambo hili Fulani, lakini akiendewa yule mwanaume tayari na yeye anakataa au kama hakukataa ndiyo lile tulilolisema la kuhusu familia. Familia wakae wazungumze ili yule apate kumwoa, hamwoi. Anangoja mtoto akue, aje tena kumfanyia kitendo kingine, anamtia mimba nyingine na hili lipo mimi ninaliona, limo ndani ya nyumba yangu nitasema. Akisha kumtia mimba ile nyingine yeye yule anakimbia haonekani kabisa. Sasa pale tayari tushakuwa na mizigo miwili, baada ya yule mtu tunayemlea (mwathirika) yule halafu na yule mtoto wake wa mwazo uliyelea, aliyezaa na hivi sasa hivi tunalea mimba nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili aweze kulea, ninamwomba Mheshimiwa Dorothy na ninaiomba Wizara yako ifanye kazi juu ya suala hili la hawa watoto wanabakwa huko mitaani na wanaume waliokuwa hawajitambui (hawajijui). Hawa wanaume hawa wapo na ninasema hili siyo kama wale wanaume waliokuwa wana akili zao tuliokaa humu Bungeni kuzungumzia sheria zetu humu Bungeni. Wanaume hawa wapo huko mitaani wanafanya vitendo vibaya kwa watoto wa wenzao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, wakae kitako, pamoja na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wapange jinsi mtu kama huyu anayemlawiti mtoto au kumbaka, kisha akamwachia na ulezi kama huo. Kwa hiyo, hilo ndilo ninalolisema kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili, ninasema hivi katika taarifa yako, taarifa yako nimekaa nimeiangalia kwa kina nzuri, haina mbambamba nitasema, tena ile inasema tukutane *site* na *site* yenyewe ndiyo hii hapa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba kuna kampeni ya watoto wanaozurura mitaani. Watoto hawa wapo, wanazurura mitaani tena na wazee wao, mtoto anaachiwa anaambiwa nenda kwenye gari ile pale,

mzazi kajificha nyuma na mambo hayo yapo sana sehemu za Dar es Salaam. Anakwenda kwenye gari anakwenda kuomba akishapata ile pesa anampelekea mzazi, wale watoto bado wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mpaka hivi sasa hii kampeni hii tuliyonayo kama haijafanyika basi ifanyike, imefanyika izidi kufanyika ili hawa watoto waache kuombaomba kwenye magari, mitaa na barabara. Utaogopa wewe binafsi mtoto anavyokujia utaogopa, ninasema huyu mtoto akipigwa na gari huyu, kweli huyu mtoto ana mzee? Kumbe ana mzee wake anamwangalia, kakaa huko, yeye huku anakwenda kuombaomba. Mheshimiwa Waziri, hili suala lipo kwa hiyo hii kampeni ifanyike, tena ifanyike kampeni ya kitaifa, wanaoweza tushirikiane twende ili hili suala liweze kutoka. *(Makofi)*

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa, tafadhali.

## TAARIFA

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpongeze mama yangu kwa mchango wake mzuri, nilitaka kumpa taarifa tu, siyo tu kwamba wazazi ndiyo wanawasindikiza watoto kwenda kuomba, lakini kuna watu wapo Dar es Salaam biashara yao ni hiyo. Wana nyumba, watoto wanaishi kwenye nyumba hizo, mchana wanawapeleka kwenda kuomba, usiku wanawafuata wanakusanya zile fedha, ndiyo mradi wao. Kwa hiyo, ni vizuri akapata taarifa hii ili aishauri Serikali vizuri juu ya kudhibiti uhalifu huu wa kutumia watoto kufanya biashara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unapokea Taarifa ya Mheshimiwa Saashisha?

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa ya mwanangu, huyo yeye ndiyo kazi yake kunipiga mataarifa nikizungumzia katika Wizara hii, kwa hiyo mimi ninapenda sana anipe taarifa halafu niendelee. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kampeni hii iendelee kufanyika ili tuweze kuwadhibiti hawa watoto wetu pamoja na wazee wao, waweze kukaa katika majumba yao wafanye shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubakaji na ulawiti umepungua na haya unasema wewe katika taarifa yako ya kazi kwamba haya masuala yamepungua. Haya masuala Mheshimiwa bado hayajapungua, hayajapungua yapo (ubakaji na ulawiti). Juzi tu hapa nchi hii yetu hii ya Tanzania, kalawitiwa mtu, alivyokwisha kumlawiti mbele na nyuma kisha wakamuua, wakaenda wakamtupa mwituni, baadaye wao wakakimbia. Mtoto yule mwanamke amekutwa mwituni amefariki katika Tanzania hii na nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bado hili suala lipo, tuzidi kupanga sheria. Nilisema humu ndani, sheria hii tuipange iweze kupatikana japo wanaume wawili tu wanaobaka wale, wawili tu wakahasiwa hawa, wakishahasiwa hawa watu wawili, wakajulikana na wanaume wenzao hili suala litaachwa. Sheria imeletwa tumeitunga humu Bungeni, lakini ninasema hii sheria wala sikuifurahia sana, kwa sababu sikuijua, na hii sheria ilikuwa tuipitishe kwa uzuri ili hawa wanaume wanaobaka wakamatwe watiwe ndani miaka 30. Wakishatiwa ndani miaka 30, wapigwe shindano, wakishapigwa shindano wamekwisha wanarudi majumbani mwao wanaenda kulala, ndilo lililobakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama si hivyo hapa kila siku tutakuja hapa tukaizungumzia Wizara hii, tukaisema Wizara hii, lakini hili suala bado lipo na linafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wangu, Mheshimiwa Mwanaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ni suala la kikanuni, ninaomba nirejee kanuni, kwenye kanuni zetu kuna hoja ya taarifa ambayo inaweza ikatolewa na Mbunge yeyote ambaye hayupo Bungeni wakati mwingine anachangia na yule ambaye anachangia ana hiari ya kuipokea taarifa au kutokuipokea taarifa, lakini kumekuwa na *tendency* wakati mwingine tunatoa taarifa ambayo inam-*distract* mchangiaji au haimwongezei kitu chochote na haichangii kwenye hotuba ya mchangiaji.

Waheshimiwa Wabunge, ninataka tu-*make reference* kwenye mchango wa Mheshimiwa Saashisha, kwa namna alivyotoa taarifa inachangia vizuri sana kwenye hoja ya Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mwantumu Dau na tu-*encourage* taarifa kama hizi zinatusaidia Bunge na zinaisaidia Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na uchangiaji, tunaye Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na ninamshukuru Mungu pia kwa kuwepo leo tena na kupata fursa hii ya kuchangia. Kabla sijaenda mbele sana unajua hii ndiyo Wizara kwetu ina-*deal* na *NGOs* na kuna mambo ya wanaharakati humu ndani. Nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru ndugu zetu wale Wakenya na niliwaambia kabisa saa hizi wanisikilize, nilikata kidogo maana tume-*chat* mpaka saa tisa, kwa hiyo nilikata kidogo nipo *busy* Bungeni, lakini niwaombe sana tukitoka hapo tutaendelea tena na mjadala wetu kama kawaida, kwa wale wote tu ambao wanatutukana, wale ambao wanatusifu lakini hoja inapingwa kwa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninawashauri wale rafiki zangu wale *Gen Z* wale ambao tumeanza mazungumzo m-*create*

*group* la *WhatsApp* waniinginze humo nitakuwa *busy* kidogo leo na kesho kwa sababu kuna rafiki yangu mwingine Mkenya yupo hapa anataka parachichi, kwa hiyo yupo shambani tutakuwa tunashughulika naye ili achume aje nazo huko. Kwa hiyo, ninaomba wanipe muda, kwa hiyo Jumamosi nitawajibu *live*, tutaendelea. Wakenya ni ndugu zetu, ni rafiki zetu, ni majirani zetu na hatuna namna ya kuwakwepa. Kwa hiyo tutaendelea, cha msingi hoja ijibiwe kwa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kwenye mchango wangu sasa. Ninakushukuru sana na nimeisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nilisimama hapa mwaka jana nikaongea kuhusiana na mipango yetu, jinsi ambavyo inatakiwa iwaunganishe wanaume. Tutaongea hapa kutunga sheria kali, tutaongea hapa sijui Polisi waingilie kati, tutaongea hapa mipango yote tunayoipanga, tuta-*inject* fedha tunavyotaka kuweka katika kulea maadili. Kama familia hazijawa *strong* hili suala litatusumbua sana. Tunapoongelea familia ni somo dogo tu ambalo ukienda kule shule ya msingi wanafundishwa *Family Tree* ni nini. Wanasema pale anakuwepo babu, atakuwepo bibi, anakuwepo baba, anakuwepo mama, wanakuja watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutaweka msingi kwenye familia, hili suala la maadili litaendelea kutusumbua kama ambavyo Mheshimiwa Waziri, anasema kwenye Ibara ya 29 kwamba ni mmomonyoko wa maadili kwenye nchi yetu umezidi na taarifa ya *UN* ameisema vizuri Mheshimiwa Tarimba, inasema kabisa kwamba vitendo vya ukatili vinaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilisema mwaka jana kwa uchungu hapa na nikafikiri labda nimeeleweka lakini ninaona mambo ni yaleyale. sasa kama *we are serious* tunataka kubadilisha hii jamii na tumeshasema hii Wizara ni mtambuka na kazi yake kubwa ni kujenga fikra mpya, tunaomba nyinyi wenzetu wa Maendeleo ya Jamii kwanza wenyewe wabadili fikra mpya. Mwalimu Nyerere alisema, tunajenga usawa wa kibinadamu, lakini kutokana na mambo ya mwingiliano wa dunia kwenye ule

usawa wa kibinadamu tukaja kwenye usawa wa kijinsia, usawa wa kijinsia ni sehemu ndogo ya usawa wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kusoma hapa Sera ya Maendeleo ya Jinsia ya kwetu sijaona, pale palipoandikwa Sera ya Maendeleo ya Jinsia uki-*click* unapata Sera ya Maendeleo ya Watoto na uki-*click* ya watoto unapata Sera ya Maendeleo ya Watoto, kwa hiyo wakaliangalie hili ili tuweke taarifa sahihi. Nikaenda kwenye Sera ya Maendeleo ya *East Africa* ambayo sisi tumeridhia, inasema kabisa ili tuweze kuimarisha hizi haki za binadamu, tuweze kujenga usawa, usawa wa kijinsia, kuleta maendeleo endelevu lazima tuwahusishe wanawake na wanaume mabinti na vijana wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 76 *para* ile ya 145 mfano kwenye taarifa bado inasema mkakati wa kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na sehemu nyingine kwa watoto, umemalizia kwa kusema, lakini mpango huu mpya tulichokiongeza ni kuunganisha au kuongeza zile Serikali za Mikoa, Wilaya ili ziweze kuwa *part and parcel* ya kutekeleza mpango huu. Pia, unasema: "Pia tunaongeza wanaume na vijana wa kiume katika kutekeleza afua hizi za ukatili wa kijinsia." Hawa watakuwa mpango wa utekelezaji, mpango wao wa kuwalinda uko wapi? Wa kutokomeza ukatili kwa wanaume uko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watakuwa mpango wa utekelezaji, mpango wao wa kuwalinda upo wapi wa kutokomeza huo ukatili kwa wanaume upo wapi? Sielewi labda mimi ndiyo ninayefikiria tu sijui nyinyi wenzangu Wabunge humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi, labda mimi ndiyo ninayefikiria, sijui ninyi wenzangu Wabunge humu ndani? Labda hivi ninavyofikiria kwamba katika *society* yetu leo, wanaofanyiwa ukatili ni wanawake pekee yao wanaume hawafanyiwi? Nami ninafahamu unapokuwa unategeneza mpango lazima utatengeneza malengo ambayo yatafikika yatakuwa na *timeline,*

utayawekea *resource* utaweka mkakati, utaweka tunasema *goals* za ku-*achieve* ndiyo maana ya mpango. Maana yake ni kwamba sasa hapa mipango yetu au mpango wetu wa ukatili wa kijinsia ume-*base* kwa wanawake na hauna wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaweka mipango utaweka mikakati utaweka malengo utaweka *goals* za ku-*achieve* kwa upande wa wanawake, hawa wanaume ni vipi? Lawama imekuwa kubwa mitaani jamani sisi ni Wabunge tunakwenda tunafanya mikutano tunaomba tusikilizwe. Lawama imekuwa kubwa kwa sababu hawa wanaume wanasema kabisa hata wakienda dawati la jinsia wanaoangaliwa na kushughulikiwa ni wanawake zaidi wao hawasikilizwi ndiyo malalamiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukubaliane, hivi hiyo familia unayotaka mama tu atetewe na mama ni malaika yeye hawezi kufanya kosa akamtendea kosa mwenziye. Huyu anakwenda wapi kujieleza? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote *riot* imekuwa ni kugombania nafasi, lakini usawa wa kijinsia hakuna mwanamke anayetaka kuwa mwanaume na hakuna mwanaume anayetaka kuwa mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alivyoongelea usawa wa binadamu aliongelewa utu kama binadamu kwenye mahitaji ya muhimu wote tunatakiwa tupewe fursa sawa. Ni kweli Serikali imewekeza sana kwa wanawake kwa sababu waliachwa nyuma, lakini *trend* ilivyo sasa hivi Serikali mmefanya kazi kubwa mno ya kum-*empower* mwanamke, *thank you very much*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke, sasa mwanaume anaachwa nyuma jamani watoto wa kiume wanaachwa nyuma. Moja ya usawa tunaosema ni kuwawekea miundombinu itakayowasaidia kuchangia maendeleo endelevu ikiwepo na elimu, lakini leo tunajenga shule zote tunazojenga mabweni na

shule kubwa tulizozijenga nchi nzima mikoa 26 ni za watoto wa kike za bweni wa kiume hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu shule zilivyojengwa zile za wakoloni ni shule moja tu iko Mtwara ya wanaume ndiyo imejengwa tena ya bweni. Hatari imekuwa kubwa sana kwa watoto wa kiume kuliko hata hao wa kike: wa kike wamefungiwa kwenye *hostels,* wamefungiwa kwenye mabweni wa kiume wanarandaranda ndiyo wanaingiliwa kinyume cha maumbile, ndiyo wanalawatiwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mimi sielewi, *me I don't understand* ndiyo maana siku ile niliwaomba kama haiwezekani kwani hawa wanaume nao kwa sababu *population* yetu 50% ni wanawake *of course* na wanaume wanaweza kuwa wanaangukia huko huko. Kwa nini, tusiwe na watu wengine watakaowaangalia wanaume au taasisi au wizara nyingine? Kama tunafikiri hatuwezi kuchanganya au Waziri kwa nini asiwabebe wanaume wake kwenye wizara hii halafu tuwatoe hawa watu makundi mengine yaingie biashara ya umachinga ili a-*relax* kutujengea maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamna namna kwa sababu hawa wanaona wanaonewa wanaamua kutekeleza ndiyo maana sasa hivi *single mothers* tuko wengi! Kwa sababu sheria inawalinda wakienda dawati wanatetewa wanaume wanaamua. Kwanza, *after all* wao moyo wao ni mdogo sijui *I don't know*, sijui tusema ni mdogo au vipi wanaweza tu wakakimbia mtoto na asiumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ule mzigo mzito wa akinamama wanaachiwa watoto pekee yao inakuwa shida kuwalea. Akinamama muda wote wanakosa muda wanatafuta hela wawalee watoto asimamie maadili kwenye familia alipe gharama zote za kulea mtoto *is impossible.* Wakati kuna mtu tu alitakiwa kukaa hapa kwa sababu hajatendewa haki hajaheshimiwa binadamu yeyote anataka utu wake uheshimiwe. Hajasikilizwa ameamua ku-*avoid* ameondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani huu uwezeshaji haya hawa wanaume kwenye mikopo ya 10% tumewaweka wanawake tumesema na vijana *ok,* ukienda *in real sense* ukiacha ile Halmashauri moja sijui ni ya Bumbuli huko ndiyo iliyofanya muujiza wa vijana wengi wa kiume kukopa kwenye mikopo ya vijana. Ukija hizi halmashauri nyingine zote ni kwamba mikopo mingi ilipelekwa kwa wanawake zaidi ya asilimia nne tulizopanga wa kiume hawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hawa wapo kwenye biashara ndogo ndogo za machinga wako kwenye bajaji wapo kwenye boda. Hao ndiyo tulisema wakopeshwe hii mikopo ambayo wametenga bilioni nane wamekopesha milioni 159. Uwezeshaji wa hawa wanaume kiuchumi upo wapi kwenye mipango hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri akisimama asitujibu kiwepesi kwamba jamani wote wanabebwa humo humo kivipi? Kama wote wanabebwa humo humo kwa nini huyu awe na mpango kamili halafu yule mwingine kwenye mpango hayupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani tuwaangalie watoto wa kiume ni *species* ambayo ni *endanger* kama *species* ya tembo wanatafutwa kila mahali wanaathiriwa kila mahali. Kwenye vita ikitokea wanaenda wao wanaisha ndiyo maana hata *population* yao ni ndogo kuliko tuwalinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ukisimama ninaomba unisaidie huo mpango wa wanaume, uwezeshaji wao, ukatili na mpango wao kuwawezesha kiuchumi upo wapi? Wewe ndiyo Waziri wa Maendeleo yetu ya Jamii, Jinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashukuru sana sitakuwa na maneno mengi. Ninachomwomba Mheshimiwa Waziri hilo ndilo nilitaka kumwambia na ninaomba akisimama nisishike shilingi aniambie. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Yale makofi ya wanaume sijayasikia jamani. Ahsante sana, Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Kwanza, kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na nchi kutujalia afya njema sote tukiwa wazima tukiendelea kutimiza majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya kutetea, kulinda na kutupigania Watanzania kama Amri Jeshi Mkuu. Tunamtia moyo tunamwombea na tunamhakikisha kwamba tupo bega kwa bega na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana pia Wizara hii ikiongozwa na dada yangu Mheshimiwa Dkt. Dorothy pamoja na Naibu Waziri lakini Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa ambayo mmekuwa mkiifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Gwajima, mara nyingi amekuwa aki-*respond* kwenye mitandao matukio ambayo wananchi wanayaripoti wanaya-*post* wanakuwa wakiku-*tag*. Kwa kweli umekuwa ukiitikia kwa haraka sana na kufanya ufuatiliaji, hilo nikupongeze, lakini haitoshi kwa Mheshimiwa Dkt. Gwajima pekee yake kufanya hii kazi. Sisi sote kama Watanzania kama wazazi ni wajibu wetu kulinda maadili kulinda mila zetu, kulinda tamaduni zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mmomonyoko wa maadili, mmomonyoko wa tamaduni zetu unaanzia kwenye ngazi ya familia. Familia nyingi tumekuwa aidha hatutimizi wajibu wetu kutokana labda na kazi nyingi ambazo tunazo au kutokana labda na uzembe au kutokana na utandawazi ambao umekithiri duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika ukiangalia watoto wengi ambao wako mitaani hawana makazi wanafanya kazi wengine wanarandaranda ni watoto ambao wamezaliwa na baba na mama. Kutokana na sababu mbalimbali zikiwepo magovi kati ya baba na mama au ikiwemo na malezi ambayo watoto hawa wamepatiwa tunajikuta kuna watoto ambao hawana makazi maalum, tunawaita watoto wa mitaani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ni jukumu letu sisi kama wazazi kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwalinda watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na vitendo sisi wote ni wazazi, sisi sote ni walezi, lakini utandawazi unatupelekea hata malezi ya watoto wetu yanakuwa magumu. Sasa hivi watoto tunawalea kwa katuni, haki za watoto kila mtu anazitambua, mtoto ana haki ya kuishi, mtoto ana haki ya kupata elimu, mtoto ana haki ya kupata matibabu, mtoto ana haki ya kwenda shule, mtoto ana haki ya kupata mlo kamili na malazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haki nyingine ambazo tunataka kuziiga kutoka kwenye nchi za wenzetu. Mtoto wa miaka mitatu, mtoto wa miaka mitano unakuta anam-*control* mzazi wake mtoto anashinda kwenye *TV* yeye ndiyo anaamua aangalie kipindi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu unakwenda kwenye familia nyingine unataka hata kuangalia taarifa ya habari wewe ni mgeni mtoto ndiyo ana mamlaka ya ile *remote* na mzazi wake anakwambie, enhee! Yaani unajua anapenda kweli kuangalia katuni hayo ni malezi kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wetu humu tumelelewa na wazazi ambao wamekwenda na walikuwa ni wafanyakazi, lakini tulikuwa hatuna malezi ambayo tunayo sasa hivi ya kumdekeza mtoto anakuwa kama yai. Mtoto hata kumkaripia hata Biblia inasema kiboko ni haki ya mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na malezi ambayo mimi kwa kweli, mtoto analilia simu eti mpe achezee anataka kuangalia sijui nini, mtoto anajua na ku-*download* hivi kama mtoto anajua ku-*download* hizo katuni atashindwa ku-*download* vitu vingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watoto wetu sasa hivi wamekuwa *so creative,* wanajifunza vitu vingi wepesi wa kunasa. Watoto toka shule wanafundishwa kutumia kompyuta leo wewe mama unamwachia mtoto simu achezee. Mtoto unaweka *password* anakuangalia unavyofungua anaifungua badala ya kuangalia katuni anakwenda ku-*search* vitu vingine. Hayo ndiyo malezi ambayo sasa hivi sisi kama wazazi tumewalea watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huu mmonyoko wa maadili unasababishwa kwanza kabisa na ngazi ya jamii ngazi ya familia. Kwa hiyo, sisi kama wazazi tutimize wajibu wetu hawa watoto wa mitaani, mtaa unazaa kama alivyosema Mheshimiwa Jesca, pale mtaa unazaa? Mtoto anazaliwa na baba na mama, lakini kwa sababu hatuna malezi mazuri, ukiondoka leo duniani mtoto akaenda kwa mtu mwingine hawezi kukaa na ile familia kwa sababu malezi ambayo umempa siyo malezi ambayo anaweza mtu mwingine akayavumilia. Kila anachokitaka mtoto unafanya! Uzungu mwingi, tunaacha mila na desturi zetu, tunaacha mila ambazo tulikuwa tunafundishwa sisi na wazazi wetu, tunafuata utandawazi, utandawazi hatuwezi kuukwepa, lakini kuwe na mipaka kwenye familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto anataka kitu, je hiki kitu kina manufaa? Mtoto anakwambia mimi leo siendi shule mimi leo mtoto sitaki kula ugali ninataka kula *burger,* sitaki hiki na mama

unafuata baba unafuata baba anavyotaka. Sasa kama sisi wazazi tunakuwa *driven* na watoto wetu unategemea tutakuwa tunamlaumu mama Mheshimiwa Dkt. Gwajima, hapa tutakuwa tunalaumu Serikali, lakini malezi sisi kama wazazi tumewajibika kwa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana wazazi niwaombe sana wanawake na akinababa wote Tanzania tutimize wajibu wetu kuwalea watoto wetu katika misingi ambayo sisi tulilelewa. Hatuwezi kufanana sana kwa sababu hatukuwa na teknolojia kubwa kipindi kile hatukuwa na mambo ya mitandao, lakini walau basi vile vitu vya msingi tuwapatie watoto wetu kitu kikiwa kibaya mwambie asikifanye kikiwa kizuri mwambie akifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kwenye hatua ya pili, kwenye mchango wangu wa pili, tumeona kuna tafiti ambazo zimefanywa kuna utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka wa Fedha 2022/2023 imebainisha kwamba ukeketaji kwa wanawake na wasichana miaka 15 mpaka 45 umepungua kutoka 10% mpaka asilimia nane kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaona kwamba vitendo hivi vinafanyika, kuna mikoa ambayo bado vitendo hivi vipo. Kwa mfano; Kwa Mkoa wa Dodoma imepungua kutoka 47% mpaka 18%, hawa wanaweza kusema kwamba wamefanya vizuri sana. Singida kutoka 31% mpaka 20%, Mara kutoka 32% mpaka 28%, lakini Manyara bado kuna tatizo kutoka 58% mpaka 43%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi na Mheshimiwa Waziri ukeketaji wa wanawake unafanyika kwa watoto wadogo. Mtoto mdogo amezaliwa anakeketwa bila yeye kujua. Kwa hiyo, ninaomba sana, mamlaka ambazo zinazidi kusimamia kuendelea kuelimisha umma wa Watanzania ambao bado mila hizi zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kumnyima haki lakini pili ni kumpa maumivu, ni kumtengenezea maumivu baadaye atapata uzazi pingamizi atakapokuwa mtu mzima vitendo hivi

havikubaliki. Kumekuwa na taasisi mbalimbali Asasi za Kiraia ambazo zinaelimisha ambazo zinapigana kupinga ukatili huu wa ukeketaji kwa sababu huu ni ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe sana zile Asasi za Kiraia ambazo zinajishughulisha na masuala mazima ya kupinga mila potovu zisizofaa kuendelea kuelimisha jamii ambazo bado zina utamaduni huu kwa sababu huo ni ukatili kama ukatili mwingine. Mtoto hajui lakini hata kama ni msichana wa miaka 15 hana hiari ya kufanya kile kitendo cha kukeketwa. Tunaomba waendelee kuelimisha, kuhamasisha katika jamii ambazo ukeketaji bado unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tumeona kuna unyanyasaji katika mitandao wanawake wengi wanadhalilika kwenye mitandao, wanaume wengi wanadhalilika kwenye mitando. Tumekwenda mbali Watanzania mpaka tunafikia ya kudhalilisha hata viongozi wetu wa kitaifa kwenye mitandao hili halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kabisa sheria zipo *TCRA* Mheshimiwa Jerry afuatilie watu ambao wanadhalilisha viongozi wanatweza utu wa viongozi wetu hatutakubali kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kupigana, tunaendelea kupambana kuhakikisha kwamba staha ya mtu inaendelea kulindwa, staha ya Mheshimiwa Rais wetu inaendelea kulindwa tutapambana kwa hali na mali kuhakikisha kwamba mtu hatwezi utu wake kwa sababu anastahili heshima hata vitabu vitakatifu vimesema mwenye mamlaka na apewe heshima yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Christina. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi,

atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Robert Maboto, wajiandae kwa dakika tano tano.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana na nianze kwa mpongeza sana Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima na msaidizi wake Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kusema ukweli wanatutendea haki wanafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza kwa sababu chache niseme tu chache. Kwanza, kabisa tulikuwa tunapiga kelele tupate ile Sera ya Wazee irekebishwe ile ya 2003 tuwe na toleo jipya. Niwapongeze kwa sababu wameshafikia hilo na tunawaomba baada ya hii sera sasa twende tukarekebishe sheria ya wazee ili mambo ya wazee yaende sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana Shirika *Help Age,* hili ni Shirika linalo-*deal* na wazee hapa nchini, kusema ukweli ninawashukuru na ninawapongeza. Serikali pia ninaipongeza kwa sababu kuna vitu vichache wamefanya nimshukuru sana mama yangu Mheshimiwa Jesca, Mbunge wa Iringa ameongea sana kuhusu watoto wa kiume nami pia nitakazia kwenye wazee, akinamama na wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona kuna vitu vizuri wamefanya kwenye zile kambi za wazee kuna kambi 13, bado wanawahudumia na *private sector* ina kambi 15 ambayo inahudumia hawa wazee. Kwa hiyo, mchango wangu mkubwa utahusiana na suala la wazee hapa nchini kwa sababu ni balozi wa wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee ni watu muhimu mno sana kwenye jamii yetu na ni kwa nini ni muhimu, wazee ni watu wenye hekima sana wazee ni watu wenye uzoefu na wameshatoa mchango mkubwa kwenye maendeleo ya Taifa hili ikiwa ni

pamoja na kuziendeleza familia zao na jamii ya Kitanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye kitabu kitakatifu ambacho ninakiamini mimi cha Biblia nimesoma kuna mistari kama 100 inayotuambia kwamba wazee ni muhimu na tutumie hekima zao na kwenye kitabu kimoja. Kwa mfano; nitatoa tu mfano, Musa alivyozidiwa na ubishi wa wana Israeli alipokuwa anawapeleka kwenye nchi ya ahadi yalitokea matatizo pale baba mkwe wake alimwambia akachague wazee 78 wamsaidie kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa inaonesha umuhimu wa wazee kuanzia zama hizo kwenye vitabu vitakatifu tunaambiwa, kwenye kitabu cha Ayubu 12:12 inasema "Hekima ipo kwa watu wazee, maarifa kwao walioishi muda mrefu" kwa hiyo hata kwenye vitabu vya *Quran* nina hakika tunaelekezwa kwamba tutumie hekima ya wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, wazee siyo watu wa kubeza, wazee ni watu muhimu sana, hata huku Bungeni tusije tukabeza wazee. Kwa mfano, kuna Mzee Profesa Muhongo utambeza umekuwa nani? Kuna Prof. Kabudi, kuna Mama Ishengoma, kuna wazee na mimi Mzee Ndakidemi utanibeza na uzee wangu huu kwamba mimi sifai. Kwa hiyo, tuwe makini wazee wanahitajika, mwendo ni mdogo, lakini wana mambo mengi wanayoweza kusaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme, pamoja na umuhimu wa wazee hapa nchini, lakini bado wana changamoto nyingi kubwa ambazo nitaiomba Serikali itusaidie kwa sababu hizi changamoto zinaathiri ustawi na maisha ya hawa wazee wetu hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza kwa wazee wetu hapa nchini ni ukosefu wa kipato cha uhakika na kutegemea familia. Wazee wengi wakishazeeka kama mzee hana *pension*, kama mzee ametoka kwenye familia maskini, sasa

hukuwaandaa watoto ukiwasomesha vizuri, ukawatafutia kazi nzuri, kwa vyovyote kutakuwa na shida ya kipato. Kwa hiyo kuna changamoto ya hawa wazee kupata kipato cha kuwasaidia, ndiyo pale tunakuja sasa tunapiga kelele tunasema familia hizi *TASAF* tumepeleka kule iwasaidie, lakini tunatakiwa tufanye vitu vya ziada ili kuwasaidia wazee wanaotoka kwenye familia maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano hapa hata Mheshimiwa Jesca ameongea hapa, Nne vijana, Nne akinamama, haya wamenisaidia, sasa mtu ambaye amewajibika kuliko mtu yeyote kwenye familia zetu za Kiafrika hapa Tanzania ni baba, mwanaume mzee, anapokuwa ameishiwa nguvu husaidiwa na Serikali kwamba naye awe kwenye hili kundi la watu maalam kwa sababu hii Wizara pamoja na Makundi Maalum na Wazee wapo pale, mimi sioni kama tunawatendea haki hasa hizi familia ambazo ni maskini, ambazo huwa hazina kipato badala ya kuwasaidia ili nao wawe kwenye lile kundi, wa-*generate income* ya kuwasaidia waishi, tunawaacha unawapa akinamama, vijana na watu wenye ulemavu, mimi ninafikiri hapa kuna kitu tunatakiwa tubadilishe kwenye sera zetu na sheria zetu ili tuwasaidie na hawa wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ni ya wazee kukosa *pension*. Huku kwetu Tanzania Bara wazee hawapati *pension* na hii ni changamoto, kule Tanzania Zanzibar wamejiongeza vizuri sana. Rais wa Zanzibar hata juzi aliongeza *pension*, walikuwa wanalipwa ukishafikia miaka 70 ulikuwa unalipwa shilingi 20,000 sasa hivi Mheshimiwa Rais Mwinyi kule Zanzibar amesogeza kidogo anawapa shilingi elfu 50. Sasa jamani hawa wazee siyo wengi, wazee wa hapa Tanzania Bara siyo wengi kiasi hicho, ni nini kinaishinda Serikali yetu kila siku tunapiga kelele hapa tusiwape hawa wazee ambao hawajiwezi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameshafanya kazi nzuri, wamefanya kazi nzuri, wame-*identify* watu ambao hawajiwezi na tunajua namba yao. Sasa inatushinda nini hao watu karibu 5,000 kuwapa *pension* ili nao wawe na maisha, waweze kupata pesa

ya kununua sukari, aweze kujikimu, aweze kupata pesa ya kumpatia dawa? Ni nini kinatushinda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kushindwa hawa wazee ambao hawajiwezi, ambao hawana bima ya afya, wengi wanashindwa kulipia matibabu, akiugua hana namna ya kwenda hospitali ili apate tiba. Sasa ninaomba hawa wazee wanahitaji wasaidiwe bima ya afya na wameshafanya kazi nzuri, wame-*identify* watu ambao hawajiwezi, katika hao 46% wameshawapa vile vibali vya kupata tiba, 54% hawajapata hivi vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, nashauri Serikali tujitahidi wazee wote wapatiwe bima za afya ili wakienda hospitali waweze kupata misaada kwa magonjwa kama *pressure*, kisukari, kansa, miwani, hivyo ni vitu ukishazeeka lazima unavaa miwani, wengine wakishidwa kutembea yale magogo wanatakiwa wapate pesa ya kuwasaidia kuyanunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mwisho ambayo ni ya kawaida ni msongo wa mawazo. Wazee wengi wakishazeeka, watoto wameondoka wameoa wameenda kujitafutia kazi huko waliko, bahati mbaya unabaki wewe na mama, mama akitangulia au baba akatangulia, mzee utabaki kule ndani huna wa kukusaidia, huna wa kukufulia nguo, huna wa kukuletea kuni, huna wa kukupikia, unapata msongo wa mawazo na mara nyingi wanaishia kupoteza maisha hao wazee kwa sababu ya msongo wa mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali tuhamasishe vijana wetu, tuwafundishe kupenda wazee wao, kama mzee amezeeka angalau tumpelekee hata mtoto akae naye kule, mashirika ya dini, dini zetu zote hizi mbili ziwashauri vijana, sasa hivi kumetokea mtindo mbaya vijana wanazaa mtoto mmoja, wawili, usitegemee kama kijana wako ana mtoto mmoja ama wawili atakupa mtoto Hapana! Wewe utabaki hivyo hivyo maana na yeye ana hamu ya kukaa na mtoto wake. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali tuwe na program maalum za kusaidia hao wazee, kwa

mfano, tunaweza kupata watu wanaowafundisha kisaikolojia, kuwatibu kisaikolojia, wawashauri namna ya kuishi, namna ya kushiriki katika jamii na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee ni watu muhimu sana, wazee bado wanahitaji sana huduma za watu ambao wanawazunguka, tukiwepo wananchi wote kwenye jamii tunatakiwa tuangalie wazee. Niendelee kushauri, Waziri aweke nguvu kwenye wazee, kwenye bajeti yake ametenga bilioni 12 kwa ajili ya yale makundi maalum, anaratibu vitu vyao ikiwa ni pamoja na siku ya wazee duniani, lakini nina wasiwasi kwenye hizi bilioni kumi ni kiasi gani….

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa malizia.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa ninamwita Mheshimiwa Kakunda, wajiandae Mheshimiwa Festo na Mheshimiwa Maboto.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ndiyo huwa tunaiimba kwenye Wimbo wa Taifa pale tunaposema wake kwa waume na Watoto, kwa hiyo Wizara hii ni Wizara muhimu sana katika maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yao kwa jinsi ambavyo wamejiandaa hadi wametuletea taarifa nzuri kwenye hotuba na tumeielewa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakiri kabisa kwamba jina la Wizara hii linasadifu kabisa maendeleo ya Taifa letu. Ninaomba nianze kwa kutoa tafsiri rahisi za baadhi ya maneno machache. Jamii ni watu wanaokaa pamoja kwa kushirikiana na Watanzania

wanaishi kwa kushirikiana ndani ya Taifa letu hata kwenye harusi, kwenye misiba tunasheirikiana na hili halina ubishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa maana yake ni muunganiko wa watu wenye utamaduni, mapokeo na historia yao, umoja wa Taifa hutegemea sana lugha na lugha yetu ya Kiswahili imetujengea umoja ambao hautikisiki. Umewasikia baadhi ya watu katika nchi jirani wanajivunia Kiingereza, sasa ningependa kuwauliza hawa ndugu zetu, hivi Wachina Taifa ambalo linapambana kimkakati wa kibiashara na Marekani leo lipo katika dunia ya kwanza kimaendeleo, hivi Wachina wote wanazungumza Kiingereza? Hao wenzetu bado wapo nyuma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana ya nchi ni eneo la ardhi pamoja na eneo lililofunikwa na maji ambalo lipo ndani ya mipaka rasmi. Mipaka yetu hii tulirithi kutoka kwa wakoloni na ndiyo maana ili tushirikiane vizuri na nchi jirani tumekuwa tunapambana, tunajitahidi kuanzisha mitangamano ili tuweze kushirikiana kimataifa, tuweze kufaidika kibiashara na mambo mengine. Sasa hawa ndugu zetu ambao wanaanzisha chokochoko ambazo zinataka kutuvunjia umoja wetu ambao wa ushirikiano na nchi jirani wana maana gani, wanatupeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nilivyokuwa ninaangalia jinsi wanavyozungumza, wanambeza Rais wetu, kiongozi wetu, wanazungumza maneno machafu, matusi na nini, ninasikitika na ninashangaa. Ninatoa wito kwa viongozi wao, wawaite hao watu wawafokee, wawaweke katika tabia ambazo zitakuwa ni nzuri. Labda katika jambo hilo ninaomba nimsikitikie Ndugu yetu mmoja ambaye amevamia mada ambazo hazielewi vizuri kwa sababu hata Serikali yenyewe bado hajaijua vizuri kwa sababu yeye mwenyewe hajawahi kufanya kazi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, amehoji mambo mengi ambayo hayaelewi vizuri. Tafsiri yangu kwa kweli kwa yale aliyoyasema ninahisi anahitaji zaidi kuelimishwa, watu wakae naye,

wamwelimishe hatua kwa hatua, ninaamini ataelewa. Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imempa Rais mamlaka yenye kinga katika kuongoza nchi yetu na kuteua wasaidizi wake kwa kadri anavyoona inafaa na anapoteua au kutengua hahojiwi na chombo chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana, nimpe mfano kwa nyakati tofauti tangu tupate uhuru, wamekuwepo kwa mfano, Wakurugenzi wa Usalama wa Taifa ambao wamekaa kwa miaka 10 -15 katika Madaraka, lakini wapo ambao wamekaa muda mfupi, hiyo ni hiari na muono wa kiongozi wetu mkuu wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mifano michache, tangu tupate uhuru mwaka 1961 nchi ilikuwa na Mkurugenzi wa Usalama anaitwa Emidio Mzena, alikaa miaka 15, lakini mwaka 1975 akateuliwa Dkt. Laurence Gama akakaa miaka mitatu tu, mwaka 1978 akateuliwa Dkt. Hassy Kitine tena alikuwa kijana mdogo wa miaka 35 akakaa miaka mitatu tu na mwaka 1980 akateuliwa Dkt. Augustine Mahiga ana miaka 33 wakati ule anateuliwa, Mheshimiwa Rais aliona kwamba hawa watakuwa ni wasaidizi wangu ambao watanisaidia kazi. Kwa hiyo, kwa muda ambao anaona Mheshimiwa Rais kwamba huyu anafaa kunisaidia kazi hawezi kuhojiwa na chombo chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nilishangaa sana nilipokuwa ninamsikiliza Ndugu yetu, lakini nikajiuliza maswali mengi, hivi *motive* ilikuwa ni nini? Nchi hii ilimruhusu Ndugu yetu akazunguka kwa helikopta majimbo yote Tanzania, hivi kulikuwa na *motive* gani kwenye hiyo ziara? Labda kulikuwa na mambo fulani ambayo yanaandaliwa ambayo pengine angependa kuyafanya katika mwaka 2025. Ninadhani niachie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye Wizara. Wizara hii kwa jina lake lilivyo ndiyo inayostahili kuratibu mikopo yote ya makundi yote ya jamii. Mikopo ambayo inatolewa na halmashauri ile ya 10%, mikopo ambayo inatolewa na Idara ya Vijana pale Ofisi ya Waziri Mkuu, kuna mikopo mingine ipo Ofisi ya Rais sijui kwenye Mradi wa *SELF* na mikopo mingine ipo kwenye Wizara

nyingine na Mashirika mengine. Hii mikopo yote, fedha yote ile ilitakiwa ipelekwe kwenye Majiji yetu, kwenye Halmashauri zetu, kwenye Miji yetu ili wale Madiwani na zile Kamati za mikopo za Halmashauri ambazo zinawajua vizuri zaidi watu kuliko wao watu ambao wapo kwenye Wizara, Makao Makuu huku ndiyo wangehusika kutoa hiyo mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaishauri Serikali nzima wakakae waweze kuiweka mikopo yote kwenye Mfuko mmoja na mikopo hiyo itolewe kwenye Halmashauri na taarifa ziratibiwe kupitia kupitia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Tukifika hapo tutakuwa tumesaidia nchi yetu kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tuitetee sana hii Wizara, hii Wizara ni miongoni mwa Wizara ambazo zina bajeti ndogo, lakini vilevile niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuitetee sana Serikali. Pia ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kukitetea Chama Cha Mapinduzi ambacho kimetuleta humu ndani, bila vikao vya Chama Cha Mapinduzi wengi wetu tusingekuwemo humu ndani. Tunafahamu, wapo watu hapa waliongoza kura za maoni, lakini wapo ambao hawakuongoza kura za maoni, lakini waliteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuja humu ndani, tukitetee sana Chama Cha Mapinduzi ili nchi hii iendelee kuongozwa na chama ambacho kimeendelea kuihakikishia nchi hii amani, usalama na utengamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutakikosa Chama Cha Mapinduzi inawezekana kabisa nchi hii ikaingia kwenye matatizo makubwa sana kama ambavyo yameanza. Watu wa nje wametoa macho, 2025 hii wametoa macho kutaka kuisambaratisha nchi hii. Kwa hiyo, ninaomba kila mtu awe makini anachozungumza, anachowasilisha kwenye jamii, awe makini sana nacho kwa sababu nchi yetu sasa hivi mpaka tuvuke Mwezi Oktoba tumalize uchaguzi mkuu tutakuwa tumepitia misukosuko mikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Festo, jiandae Mheshimiwa Maboto.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Jambo la kwanza niseme ninaunga mkono hoja Wizara ya Mheshimiwa Gwajima na jambo la pili nimpongeze kwa uwasilishaji mzuri. Pia nimpongeze kwamba vijana mtandaoni wanasema anafikika, kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri amekuwa aki-*attend* kwa wakati matukio ambapo yanatokea hususan mambo ya ukatili na mambo mengine, tunampongeza na nadhani wanafanya jambo zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache tu ya kushauri kwenye Wizara hii, kwanza tufahamu kwamba Wizara hii haya yote tunayozungumza suala la maadili ya watoto au maadili ya watumishi au mmomonyoko wa maadili ni matokeo tu, ni matokeo ambayo yanatokana na malezi kutoka kwenye ngazi ya familia. Kwa hiyo, tunaweza tukazungumza mambo mengi kumhusu Mheshimiwa Gwajima na Wizara yake, lakini kiuhalisia ni Wizara nyingi ambazo zinahusika kuweza kumsaidia Mheshimiwa Gwajima kwenye suala la malezi kwenye Taifa letu. Yeye kama yeye ni matokeo tu ambayo anakutana nayo, lakini kuna suala la TAMISEMI, kuna Wizara ya Mambo ya Ndani, kuna Wizara tofauti tofauti zinahusika kwenye hili jambo kuhakikisha kwamba kama nchi inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri, kwanza ninatamani sana, kwa sababu tu kwanza kama Taifa lazima tukiri kwamba kuna mmomonyoko mkubwa wa maadili, sasa kama kuna mmomonyoko mkubwa wa maadili nini kifanyike na sisi inawezekana ndiyo *generation* ambayo Mungu ametupa nafasi ya kufanya *turning point* kwenye kubadilisha haya ambayo tunayaona yaende kwenye mambo mema ambayo tunayataka. Kwa sababu kama unazungumza mmomonyoko wa maadili unazungumzia mtoto wako kwamba,

mimi mtoto wangu yupo salama, lakini nikuhakikishie hutaweza kumzuia mtoto wako kuolewa na mtu ambaye hana maadili. Kwa hiyo, ni lazima wote tushikamane kuhakikisha kwamba tunapata Taifa jema na tunapata viongozi wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwepo kwenye mjadala mmoja na wenzangu kwamba, kama tutafikia hatua hatuzuii hili suala la mmomonyoko wa maadili, tunaomba sasa hivi *financing* za fedha kutoka nje, kuna wakati tunaomba mikopo tunapata, kuna siku tutaanza kuomba na viongozi wa kusimamia hii mikopo, kwa sababu uwezo kama Taifa la kusimamia kuwa na viongozi wazuri baadaye tumeshindwa kuzoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Gwajima huyu wa leo ambaye tunamzungumza siyo Gwajima aliyelelewa kwa haya ambayo sisi tunawalea watoto wetu, ni Gwajima ambaye amelelewa kwa misingi ya maadili na taratibu zote. Sasa ninaomba jambo moja, tunapozungumza suala la TAMISEMI, tunatamani wenzetu TAMISEMI wana mfumo kutoka nyumba kumi ambao unaweza kudhibiti mmomonyoko wa maadili kuanzia ngazi ya chini, kama familia haipo tayari, lakini kuna wajibu wa Balozi, kuna wajibu wa mtu wa nyumba kumi kusimamia kuhakikisha kwamba je, kuna jambo gani linaloendelea katika jambo husika, TAMISEMI wakasaidia kuhakikisha mtu anakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mtoto kuanzia ngazi ya shule akipewa elimu nzuri akaenda akakua hadi Chuo Kikuu, ni vyema tukawa na mitaala mizuri ambayo inazingatia kulijenga Taifa letu lakini pili Mheshimiwa Waziri kuwa na *special program* kwa ajili ya mashule kuanzia shule *level* ya msingi, *level* ya sekondari lakini level ya vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mashule mengi kwa mfano, ninakupa sehemu ambapo unakuta kama Taifa tumemeguka. Mtoto amelelewa vizuri kwenye *seminary school* kuanzia yupo shule ya msingi na yupo sekondari, akishaingia chuo mtoto anakutana na uhuru. *Lifestyle* ya wanafunzi wengi wa vyuo

ambao tunategemea baadaye waki-*graduate* ndiyo waende maofisini wamegeuka kuwa msiba kwenye Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ninaliomba Mheshimiwa Waziri, wewe pamoja na Maprofesa wa nchi hii, kwa sababu Wizara ya Elimu ni Wizara mtambuka kwenye suala la maadili, lazima tukae chini kama Taifa tuzungumze, tuwe na *modality* yetu kama Taifa na mataifa mengine yaweze kuiga, *product* gani tunaizalisha kutoka kwenye chuo kikuu husika, kuanzia kwenye maadili hadi uwezo wa mwanafunzi. Kwa sababu, mtu anaweza akawa na uwezo darasani lakini hana maadili na baadaye tukampeleka kwenye ofisi ndiyo haya Mheshimiwa Rais juzi alikuwa anazungumza, uzalendo kwa Watanzania na watumishi wa Serikali umepungua. Ni muhimu sana tuusimamie huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama Mheshimiwa Waziri lazima kuwe na *program*, kuwe na mkakati maalum wa kutoka kwenye Wizara kuhusisha Wizara ya Elimu kwa ajili ya kuweza kusaidia Taifa letu. Tuangalie *product* tunayoitoa vyuoni kuja kwenye kuihudumia jamii ni *product* ambayo inaendana sawa? Mambo ya kusema mtu akifika chuoni ana uhuru wa manyani wa kufanya anachojisikia *results* yake ndiyo hii, *generation* hii haitutaki tufanye hivyo! Tunahitaji kama Taifa tujifunge mkanda, kuzalisha kitu ambacho kitaenda kuwa na faida kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba tena Mheshimiwa Waziri kitu kingine, tunatamani kuwa na azimio lazima tuwe na *declaration* kama nchi kwamba *this is the turning point* kwenye suala la maadili twende kwenye moja, mbili, tatu. Kama tulishawahi kuwa na Azimio la Arusha na sisi kama Wizara lazima wakubaliane na wazazi wa nchi hii, wewe utazuia leo huyu kabakwa, utazuia yule kalawitiwa, huwezi kufanikiwa kwenye nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima sasa tuweke mkanda na mshikamano wa nchi yote kukubaliana kwamba ni kipi tunakifanya kwa ajili ya watoto wetu. Kwa hiyo, ni lazima kuwe na *declaration* (azimio la kitaifa) kwamba kuanzia viongozi wa dini,

vyuo, taasisi mbalimbali, Bunge na *NGOs* zote tuwe na kauli ambayo huu ndiyo mwelekeo wa Taifa letu kuanzia sasa kwenye suala la maadili. Mtu asiyeenda hivi tutafanya moja, mbili, tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizo Wizara ni Wizara hii, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya TAMISEMI na nyingine nyingi ambazo zinahusika kwenye kutengeneza *declaration* kama nchi tukaamua kutoka hapa na kwenda hatua nyingine. Ninatamani sana hayo yafanyike kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Tofauti na hapo tutaendelea kulalamika kwa sababu unaongelea *issue* ya *TCRA* kwamba kuna changamoto kwenye mitandao, lakini yale yote ni matokeo ya jinsi mtu anavyolelewa kuanzia ngazi ya chini. Huku juu tutahangaika na kizazi ambacho tayari kimeshakomaa na tayari ni kizazi ambacho imekuwa sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu pia hata asubuhi nimezungumza hapa kwamba, kwa mfano vijana wanatumia pombe ambazo zimezidishwa *content* au wengine wanazidisha kunywa pombe wakiamini kwamba labda ndiyo njia ya kutoa *stress* kutokana na aidha amekosa ajira au kutokana na kesi zao zingine ambazo ni *social interaction*. Tunatamani kuwe na darasa kubwa sana la kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Mheshimiwa Waziri ninaiunga mkono (shilingi bilioni 76 alizoomba), lakini ninatamani *investment* kubwa ambayo inatakiwa aiweke ni kwenye kuelimisha jamii kwenye *TV,* redio na madarasa. Afanye namna awezavyo kuielimisha jamii wakati huo tunaunda *modal* tofauti kama Taifa la Tanzania kwa ajili ya kuijenga hii nchi yetu katika mfumo mpya kwa maana tuwe na *declaration* yetu ya maadili kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na hapo, kama ambavyo tunajuta ukame kwenye maji, tunajuta ukame kwenye mazao na hali ya hewa; ndivyo ambavyo kuna siku tutajuta kwamba Taifa halina viongozi kwa sababu watu wote wamekuwa ni *corrupt* kwa

sababu Mheshimiwa Waziri hatuwezi kukubaliana. Macho yako yanashuhudia watu wana *Instagram account* wanatangaza ushoga; macho yako yanashuhudia kuna hawa wanavaa nguo zisizokuwa na maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tutabaki kuzuia huyu mmoja mmoja? Ni lazima tutafute mfumo ambao uta-*unify* Taifa kuhakikisha kwamba wote tunakuwa ni wamoja, lakini tunaisaidia nchi kuja kuzalisha Mawaziri na Marais ambao wana *integrity* kama ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anayo na kama ambavyo Marais wengine wamepita na kama Mawaziri wengine ambavyo wapo. Hatuwezi kupata Mawaziri kama nyie kama hatutakuwa na umoja wa kitaifa au azimio la kitaifa kuelekea kwenye suala la maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa muda. Nilikuwa na mambo mengi ya kuzungumza kwa ajili ya kuchangia, lakini mwisho kabisa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele, Mheshimiwa Festo yaandike.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nisisitize kama Taifa ni lazima tumlinde Mheshimiwa Rais kwa wivu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama vijana, tuko tayari kuhakikisha kwamba tunamlinda Mheshimiwa Rais na hatuko tayari kuona mtu mwingine anaenda kinyume na kile ambacho Mheshimiwa Rais anafanya. Kazi kubwa anaifanya na amefanya kazi kubwa kwenye maendeleo ya nchi yetu. Sisi kama Watanzania, lazima tuwe na wivu na Mheshimiwa Rais wetu. Wao wa-*deal* na Rais wao pamoja na nchi yao na sisi tu-*deal* na nchi yetu. Watuachie nchi yetu ibaki kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote, ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii jioni hii ya leo, lakini ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa letu kwa namna ambavyo ameendelea kusimamia Taifa na linakuwa na utulivu mkubwa. Pia, Mheshimiwa Rais kwa mambo ambayo anayapitia kwa kipindi hiki ni mambo magumu na hasa ukizingatia ni mambo ambayo yanatoka nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninajiuliza, kumbe mmomonyoko wa maadili huu ni karibu mataifa yote yamepata mmomonyoko wa maadili? Kwa sababu mtu wa kawaida tu kumzungumza Mheshimiwa Rais au mtu mzima, lazima uwe unaelewa unazungumza jambo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata hawa ambao bado wanaendelea kujadili jambo hili, ninaamini kwamba ni mmomonyoko wa maadili na wao inawezekana huko walikoanza hawakulelewa vizuri. Wangelelewa vizuri, saa zingine hata ukitaka kuzungumza jambo lazima ujue jambo hilo unataka kumweleza nani na amekukulia kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, ndiyo Wizara ambayo inatengeneza sheria kwa ajili ya kulea watoto wetu. Hao watoto wa leo tunaowazungumza ndiyo watu ambao tunawategemea miaka ya baadaye waweze kuwa watu salama na watu sahihi ambao wanaweza kusimamia Taifa hili ambalo leo linatengenezwa katika miundombinu mikubwa na yenye gharama kubwa. Hata hivyo, matarajio yetu ambayo tunatarajia kuwarithisha miundombinu hiyo ni hao watoto wetu wa leo ambao tunawalea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa kwa sababu hali ya leo, malezi ya leo ambayo yanawalea watoto ni malezi ambayo yamechanganyikana. Malezi

yamechanganyikana kwa sababu watoto wetu wa leo mambo wanayoyapitia katika mitandao na kwa sababu sehemu kubwa ya muda wao wanautumia kupita kwenye mitandao, kwa hiyo inakuwa ni vigumu sana kuelewa wazazi walitaka watoto wafanye kitu gani kwa sababu wazazi nao wamekosa nafasi nzuri ya kukaa na watoto wao kuwaelewesha, kuwaambia nini wakifanye na nini wakiache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wamewaachia mitandao ili watoto wajifunze maisha ya kuishi duniani kupitia mitandao. Kitu hiki mwisho wake tunachokuja kukivuna ndicho hiki ambacho leo tunakiona kwamba, mtu yeyote yule mwenye umri wowote ule anaweza kumweleza mtu yeyote yule kitu chochote kile bila kujali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama angekuwa amepitia maadili mazuri, kila unapotaka kumweleza mtu jambo ambaye amekuzidi umri, lazima wewe mwenyewe ujitathmini na uone hiki ninachotaka kumweleza huyu, kwangu mimi kinawezekana nikamwambia au siwezi kumwambia? Kama hulijui hilo na umepitia kwenye mitandao, umelelewa na mitandao hutajali. Chochote kile kitakachokuja kwenye kinywa chako utakisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii ndiyo Wizara ambayo inatunga sheria kwa ajili ya kulea watoto. Leo hii ukipita katika nchi yetu, kuna watoto ambao wamezaliwa hawana baba, hawana mama na ni yatima lakini wanaishi katika maisha yao hayo hayo wanayoyaishi; ya misukosuko, wanasoma kwa shida, wanakula kwa shida, wanalala kwa shida lakini wanaishi. Pia, muda huo wa kusema watapitia mitandao ya kijamii hawana kwa sababu hata uwezo nyumbani kwao wa kununua hizo simu ambazo zinaweza zikamfanya aweze kupita kwenye mitandao ya kijamii, hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu ambao wataendelea kusumbua Taifa hili sana kwa muda mrefu ni wale watu ambao muda wao mwingi wamekaa kupita kwenye mitandao ya kijamii

au watoto wale ambao watalelewa, analelewa na wazazi wake lakini sehemu kubwa ya maisha yake analelewa na mitandao ya kijamii. Jambo analokutana nalo mle kwenye mitandao ya kijamii ndilo jambo analolichukua mtoto kulileta kwa mzazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli pamoja na sheria ambazo tunazitengeneza hapa kwa ajili ya kulea watoto wetu, lazima tuangalie sheria hizo zitawafikisha wapi watoto wetu. Tukiwapa haki watoto zikazidi umri wao badala yake madhara yake tutakuja kuyapata sisi wenyewe wazazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa imani yangu ninavyoamini...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maboto, muda wako umekwisha maana mlipewa dakika tano tano tu, ambao hamkuwa kwenye orodha mlipewa dakika tano... *(Makofi)*

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uchapakazi wake; hakika Taifa letu la Tanzania linamtegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninachukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa jitihada zao za kuendelea kupambana na ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara pamoja na jitihada zote bado tatizo la ukatili ni kubwa sana. Wizara ikae na ije na mkakati mpya wa kuendelea kukabiliana na matendo ya kikatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kutoa hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nipende kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini katika Wizara hii na kunipa nafasi ya Unaibu Waziri. Pia, niwashukuru watendaji wote ambao wako katika Wizara hii kwa ushirikiano ambao wananipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye anatuongoza katika Bunge hili. Pia, nimshukuru Mheshimiwa Spika na wewe pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote ambao wanatuongoza katika Bunge hili Tukufu kwa miongozo mizuri ambayo wanatupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii ambayo inaongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Fatma Toufiq kwa miongozo mizuri na maelekezo mazuri ambayo wanatupa katika Wizara yetu hii hadi tukafikia hii leo na tukawa na miongozo na sera mbalimbali ambazo zinawasaidia wananchi kuhakikisha tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kumsahau Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ambaye ananiongoza vizuri sana kuhakikisha Wizara hii tunaifanyia kazi. Hatulali usiku na mchana, tunapokea simu za wananchi na tunazijibu kwa umakini kabisa kuhakikisha kwamba wananchi wanaiamini Wizara yao, lakini wanamwamini Mheshimiwa Rais kama alivyotuamini sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Mume wangu ambaye ananiongoza kwa miongozo mbalimbali na kunistahimilia katika kazi hizi za kujenga jamii, lakini na yeye kama mzazi basi tunashirikiana pamoja kunisaidia kuhakikisha wananchi nao wanaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa UWT pamoja na Wajumbe wote wa UWT Taifa kwa kunichagua na kuhakikisha ninaendelea vizuri katika kazi zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niupongeze Mkoa wangu wa Kusini na Wajumbe wote wa Mkoa wa Kusini kwa kunielewa na kunifahamu kazi ambazo Mheshimiwa Rais amenipa na wao kuwa wananikosa kwa mambo mengi ambayo yanafanyika katika Mkoa wangu, lakini tunakuwa tunashirikiana pamoja pale ninapopata wasaa wa kushirikiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru familia yangu kwa ujumla, lakini pia niwashukuru Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa kutupa nafasi nzuri na miongozo mizuri, ushirikiano ambao tunafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha Wizara hii inakwenda vizuri na inakwenda salama na tunahudumia wananchi kama tulivyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini ninapenda sasa nichangie hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia wote na ambao waliochangia kwa maandishi na pia wale ambao wana fikra za Wizara yetu hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea hoja zenu na hoja zenu ni nzuri sana ambapo ninaamini kwamba Wizara hii sasa wameanza kuielewa. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipopata Urais aliona kwamba Wizara hii ilikuwa ndani ya Wizara ya Afya, lakini kwa vile yeye ni mama na vile yeye ni mzalendo na

anajua uchungu wa akinamama na anajua uchungu wa watoto, akaona Wizara hii aiunde Wizara kamili ili vitendo vyote vinavyoonekana yale machungu yote ambayo wanawake wanayapata pamoja na watoto yaweze kuonekana na kufanyiwa kazi kuhakikisha kwamba watoto wa nchi hii na wanawake wa nchi hii, lakini wakiwemo na wanaume wanakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia mambo mengi sana. Tukija kwenye hoja, mimi nitajikita katika hoja tatu katika mambo ya ukatili, mmomonyoko wa maadili lakini nitajikita katika wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Profesa Shukrani hapa, alieleza kuhusu malezi na makuzi ya watoto. Ni kweli kila mmoja ana familia katika nchi hii na familia ni taasisi katika kuleta ustawi wa jamii na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, yapo madhara makubwa ya watumishi wenza kuishi mbali na watoto ambao wanapata madhara. Madhara haya ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya watoto kuongezeka vitendo wa ukatili, kuingizwa katika vitendo vya kiudhaifu, kukosa malezi na kuathirika na mambo mbalimbali. Haya yote tunasema, mtoto anapozaliwa na mzazi wanapoungana kila mtu anatarajia mtoto na kila mtu anatarajia mtoto awe mtoto mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto ambazo zinawafika wazazi zinasababisha kutengana lakini jukumu kubwa anaachiwa mama na mama huyu ndiyo kila kitu. Anategemewa alifanikishe jambo hili, kwa hivyo anapata mzigo mkubwa sana na mama anahangaika kulea mtoto huyu hadi anapompa mahitaji yote ambayo yanastahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, sisi sote ni walezi humu ndani, lakini sisi

sote tuna watoto na sisi sote tuna maadili ambayo ni ya Mtanzania na Utamaduni wetu wa Mtanzania. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan yeye ni mama, lakini ni mlezi. Siku zote anaposimama majukwaani anahimiza mila na desturi ya mtoto wa Kitanzania, lakini anahimiza tushikamane kuendeleza utamaduni wetu. Haya ndiyo yatatusaidia hapo mbele na mtoto wa Kitanzania tunamtegemea kuwa kiongozi wa kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipomlea sasa hivi tukampa maadili mema, basi hapo baadaye tutakuwa na Taifa ambalo halina miongozo mizuri. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, Serikali hii Mheshimiwa Hayati Nyerere, alipoianzisha aliandaa miongozo, sera, na kanuni katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kila nchi au tuseme mtaa kuna kanuni zake au kuna miongozo yake ambayo amepewa mtu aweze kujuana katika kijiji kile. Sasa ile miongozo tujitahidi tuifuate. Sisi ndiyo viongozi, kama vile tunavyohangaika kutafuta kura basi tuhakikishe ile mitaa na wale watu ambao wanaishi katika mtaa ule basi tunawajua na tunafahamu tabia zao ili tukimuona mtu ambaye ana ripoti mbaya, turipoti katika vyombo husika ili kukomesha ukatili na kukomesha udhaifu ambao unatokea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie katika kipengele cha wazee. Wazee ni tunu katika Taifa letu na wazee ndiyo waliosababisha hadi leo tuko hapa tunaendesha Taifa hili kwa umakini. Wazee wetu tumewaundia sera kwa vile tunawajali. Tulikuwa tuna Sera ya Mwaka 2013, lakini tumeiboresha sera na tumeunda Sera ya Mwaka 2024. Sera hizi zinawawezesha wazee kupata haki zao zote stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anawajali sana wazee na kila *time* anapopata nafasi utamkuta anawatembelea wazee na kuwafariji. Hivi ndiyo tunavyotakiwa tuishi na kila mtu ana mzee wake. Kwa vile mtu ana mzee wake, haina haja ya mtu kumbeza mzee wake. Umlee kama yeye aliyokulea wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mtu ambaye anashindwa na kitu hiki. Mzee hahitaji makubwa kwa nini umtupe kwa maisha ambayo unaendelea nayo sasa hivi wakati yeye ndiye aliyekuwezesha hadi ukafika sasa hivi? Kwa hivyo, tuheshimu sana wazee na tuwajali sana wazee, tusiwabeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiona mambo yanazidi tutaunda sheria. Kwa nini watoto hawalei wazee wao? Sheria hizi ziwakamate, ili tusione wazee wanahangaika wakapata taabu katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuhakikishe katika majirani zetu, tuwaelimishe. Sisi ndiyo viongozi na ni mabalozi ambao tunatoa elimu mbalimbali kuhakikisha wananchi wetu wanafaidika na matunda ya Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo mama yetu ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Yeye ni mama na ni mlezi ambaye ana uchungu wa Serikali hii na ndiyo maana kila mara anahimiza upendo, uzalendo, ukakamavu, uhusiano mzuri katika mataifa na katika nchi yetu. Pia, anapoona jambo ambalo linamkasirisha basi utamwona sura yake inavyobadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mama hapendi kusema, lakini likimkera ndani ya moyo wake, neno lake moja tu na yeye anakwambia mtu anajua mwenyewe vya kum...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kabla hatujaendelea kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Yupo Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Ndugu Samson Mgelwa, Mshindi wa Tuzo ya Samia Kalamu *Awards* ambaye ameandika matukio kuhusu ukatili wa kijinsia. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Jerry Katende, Mwenyekiti wa Wanawake Wajane wa Mkoa wa Dar es Salaam na Ndugu Emakulata Mkwabi, Mjumbe wa Wanawake Wajane Kata ya Kibaha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kuwa mahali hapa siku hii ya leo nikiwasilisha bajeti yetu kama nilivyofanya awali asubuhi na sasa ninahitimisha. Ninaomba kuhitimisha hoja yangu ili bajeti hii iweze kupitishwa kwa ajili ya kwenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kuniamini na kuniamini pakubwa sana kuja kuanzisha hii Wizara ambayo awali haikuwepo, lakini akaona umuhimu wake kwenye majira ya nyakati za sasa. Akasema ianzishwe na akanileta mimi na nimeweza kwenda nayo miaka minne, akiendelea kuniamini hadi muda huu ambapo ninakuja kuwasilisha bajeti hii kwa mara ya nne hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kazi yangu pekee yangu ni kazi yetu sote. Tumekuwa tukija humu, tukipata miongozo na maelekezo yenu Waheshimiwa Wabunge. Tumekuwa tukipata maelekezo ya kamati pamoja na wadau wengi wa maendeleo hadi kuipambanua na sasa inaeleweka pakubwa kiasi kwamba, ninajivunia kupata maswali mengi tunapokuwa tunakuja kuwasilisha hotuba zetu hapa, kinyume na miaka iliyopita ambapo maswali yalikuwa machache sana.

**27 MEI, 2025**

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwashukuru viongozi mbalimbali asubuhi. Ninaomba nisirudie, shukurani zangu zisajiliwe, kama ambavyo niliwasilisha kwenye muhtasari wa bajeti yangu asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba kipekee niwashukuru Wabunge wote waliotoa michango yao siku hii ya leo jioni, ningeweza kuwasoma wote, wako 17 wamezungumza na wengine wamenipatia kwa maandishi. Inawezekana nisiweze kuhitimisha kujibu hoja zao zote na kufafanua, lakini niseme tumezipokea na tutazifanyia kazi. Ninawahakikishia tutazileta kwa maandishi, ili ziweze kuwa kumbukumbu sahihi za michango yao kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Kamati yangu, ambayo imeleta hoja karibu 10 za Kamati. Vilevile nazo tutazifanyia kazi na kuziwasilisha kwa maandishi, endapo sitafanikiwa kuzijibu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kama utangulizi, hoja ambazo zimewasilishwa hapa ni nyingi. Mheshimiwa Naibu Waziri ameanza kuzizungumzia nyingine awali, ninamshukuru sana na ninaunga mkono majibu aliyoyatoa. Ninampongeza sana kwa ushirikiano wake. Nitapita kwenye baadhi ya hoja, ninaweza nikarudia alizozisema kwa nia njema ya kuendelea kuongeza, kujazia na kufafanua zaidi yale yote ambayo yamesemwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kubwa ambayo imejitokeza kwenye mjadala wetu huu wa jioni ni suala zima la maadili. Hii ni hoja ambayo imeendelea kujitokeza kila tunapokuja hapa kuwasilisha hotuba zetu na Wabunge wamekuwa wakitupatia miongozo, maelekezo na michango mizuri sana, ambayo imekuwa ikitusaidia kwenda kuboresha utendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda tu ni mdogo. Awali ya yote ninaomba, kupitia Bunge lako Tukufu, niweke kumbukumbu sahihi, ili tuweze kwenda vizuri na hoja yetu hii ninayoihitimisha. Huu mmomonyoko wa maadili ambao tumekuwa tukiusema kila siku;

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme machache kupitia Mwongozo wetu wa Taifa wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania, ambapo kuweka kumbukumbu sahihi, mwongozo huu Wizara yenye dhamana ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kwa sababu maadili yetu ni zao la tamaduni na mila zetu tulizozirithi, hivyo wamefanya kazi kubwa na nzuri. Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Wizara nyingine, sisi sasa ni washirika katika kuhakikisha kwamba, jamii inapata mwongozo huu na kuutumia, lakini haiwezi kupata mwongozo huu, kama hauwezi kupita kwenye *machinery* za Serikali ambazo sisi wote humu pia, ni wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema vizuri kuhusu *machinery* hizo, maadili yametafsiriwa hapa kwamba, ni "tabia njema, misingi, kanuni na taratibu zinazofuata mienendo inayokubalika katika jamii, ambayo inaongoza uhusiano katika makundi ya jamii husika na maadili yanamtaka mtu kufanya kitu kilicho sahihi, mahali sahihi, kwa wakati sahihi. Kimsingi maadili ni zao la mila na desturi za utamaduni wa jamii inayohusika", mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo kisa na mkasa cha suala zima la maadili kumomonyoka ni malezi ya watoto wetu huko kwenye familia, tunawaleaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote ni wazazi. Kwa bahati mbaya tumekuwa na watoto ambao hawana malezi mazuri na wenyewe wamebarikiwa kuzaa watoto, wameendeleza kukata ule mnyororo wa maadili. Kwa sababu, hawakuruthishwa na wenyewe hawawezi kuendelea kurithisha, lakini dalili zake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili zake sasa ni mabaya yote tutanayoyalalamikia sasa hivi humu ndani na siku zote; ubakaji, ulawiti, sanaa mbalimbali mbaya, hizi *cyber bullying* ambazo zimekuja na utandawazi zinazompa mtu asiye na maadili, ambaye hakuruthishwa tabia njema, ujasiri wa kufanya vitu vibaya, ambavyo hawezi kumfanyia baba na mama yake waliomzaa. Hapa pamebaki tu wawachukue wazazi wao

waliowazaa wawafanyie *cyber bullying,* kama wamekuwa na ujasiri wa kwenda kufanya *cyber bull* kwa viongozi hadi wa Taifa na kiongozi namba moja wa Taifa. Huu ni ujasiri mkubwa utokanao na malezi mabovu kwa baba zao, mama zao, babu zao na bibi zao, hili hakika ni janga.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya masuala ya mavazi mabaya na watoto kunengua viuno yametajwa hapa. Huduma za mafundisho ya baadhi ya dini au baadhi ya viongozi wa dini, ambayo yamekuwa ni tata, yote haya ni zao la mmomonyoko wa maadili na malezi mabovu kwenye msingi wa familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo ni nini tunacho sisi katika mapambano hayo? Tanzania ni nchi mojawapo nzuri sana katika kutengeneza sera, miongozo na mikakati, lakini ni lazima nikiri hapa na ninyi ni mashahidi, *machinery* yetu ya Serikali, Wizara hizi za Kisekta, ni kutengeneza miongozo, ndiyo kama huu hapa mwongozo mwingine nimetoka kuusoma. Tuna mwongozo mwingine ambao unahusiana na masuala ya malezi, uendeshaji wa vikundi vya wazazi vya malezi na matunzo ya mtoto wa Mei 25; tuna viongozi wa miongozo ya malezi na makuzi ya maendeleo ya awali ya mtoto kwa kuzingatia dini mbalimbali, hii hapa; tuna Kitini cha Wawezeshaji Kuhusu Majadiliano ya Mila na Desturi, hii hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, tuna mkakati kabisa wa kutokomeza ukatili ambao ni zao la mmomonyoko wa maadili Kitaifa kwa wanawake na watoto, watoto wa kiume na wa kike. Kwenye Mashirika Yasiyo ya Kiserikali tuna miongozo vilevile na mingine sijaibeba, shida yetu ni wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzoefu wangu wa kufanya kazi Serikalini miaka yote mpaka nimekuwa Mbunge, tumetengeneza Sera ya *Decentralization by Devolution,* ambapo Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tumepeleka wataalam kule. Tuna Maafisa Utamaduni tumewaweka pale ma-*custodian* wenye dhamana ya masuala ya maadili, tuna

wataalam wa Sheria, wa Maendeleo ya Jamii, wanaoshughulika na Habari, kila mtaalam yupo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto yetu moja, ambayo ninaomba niikiri hapa, ili tushirikiane ni miongozo hii. Huenda katika baadhi ya maeneo inawekwa kabatini, lakini tuna *machinery* yetu ya Serikali za Mitaa inayoendesha vikao rasmi, ambavyo vinaanzia ngazi ya kata *(WADC)* na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kule kwenye kata ndiyo Wenyeviti, tuna Kamati za Baraza la Madiwani na *Full Counsel* nimefuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona vipaumbele vya ajenda mbalimbali bado ni changamoto. Ili tuweze kutoka hapa tulipo tufikirie hata kuja na Sheria ya Maadili sasa, ambayo itatekelezwa na kufungamanisha mambo yote ya maadili huko mbele ya safari. Ni lazima tukubaliane kufanya ajenda ya maadili na mmomonyoko wa maadili kuwa kipaumbele katika halmashauri zetu, kwenye majukwaa yetu rasmi ya kuweka ajenda za vipaumbele mezani. Vinginevyo utamkuta Afisa Utamaduni anafanya mengine, hana mkakati aliouwasilisha, lakini hoja za vipaumbele zimepita na kwa kawaida bajeti itakwenda na vipaumbele vilivyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe, tumefanya kazi ya kuandaa hii miongozo, tumeisambaza, tushirikiane kufanya mapinduzi ya ajenda kwenye *machinery* zetu, ili mikakati yetu kwenye halmashauri zetu ifuate *local context* pale walipo, tutaweza kutoka kwa haraka. Hata hayo mambo ya malezi na makuzi watayasikia kwa haraka, masuala ya kuna Sheria gani watasikia kwa haraka, masuala yote ya kuhusu kwamba, tuvaaje, mila na desturi ziweje, tuongee vipi, watayasikia kwa haraka badala ya kubakiza kwenye sera hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mdogo, mambo ni mengi. Ningependa kusema machache kuhusu hoja za Kamati, tumezipokea; na kuhusu masuala ya maendeleo ya vyuo vyetu kuwa ya ubia, ndiyo. wakati muafaka umefika wa kufikiria hizi

hosteli zetu zijengewe pamoja na ushirikiano wa Sekta Binafsi ziweze kuwa nzuri, ili mapato haya yaongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ameongelea tena suala linalomuumiza sana kuhusu ushirikishwaji wa wanaume katika masuala yote ya Wizara hii. Nimhakikishie, tumeanza vizuri, Wizara hata haikuwepo miaka iliyopita, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya jambo kubwa kuileta hii Wizara akaanza na hawa wanawake, ambapo changamoto ilikuwa inaelemea sana, lakini kadri tunavyokwenda tunaona kwamba, takwimu zinabadilika, wanaume pia, wanakatiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie, kwenye mikakati yote ya kutetea watoto wa kike kuanzia kwenye madawati ya ulinzi shuleni, kwenye hayo Mabaraza ya Watoto, Sheria yenyewe ya Watoto, Mabaraza na Madawati ya Vyuoni ni watoto wa kiume na wa kike. Hata Iringa, 19 Novemba, mwaka jana 2024, nilienda kwenye Kongamano la Wanaume kwa siku yao ya Wanaume Duniani, Tarehe 19 Novemba. Huu ni mwanzo wa safari ya kufika kule, kutengeneza vizuri mchango wa wanaume na kuzifanyia changamoto zao vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kitabu changu cha Hotuba nimeonesha pale kwenye Ukurasa wa 55, Aya ya 104, inayosema, "tuna sekta nyingine zinatoa mikopo vilevile, ambayo inahusisha wanawake na wanaume. Mfano, kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, mifuko hii 75 ikijumuisha 63 inayomilikiwa na Serikali na mifuko 12 iliyo chini ya Sekta Binafsi hadi Aprili 2025, mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 3.5 imetolewa, ambapo kiasi cha shilingi trilioni 1.7, sawa na 49%, imetolewa kwa wanawake na kwa upande wa wanaume zilitolewa shilingi trilioni 1.8, sawa na 51%."

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha kwamba, kuna mtandao mpana wa upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa wanaume pia, siyo kwa wanawake pekee yao. Kutokana na changamoto za mila kandamizi zinazowaathiri zaidi wanawake

ndiyo zilitengenezwa programu chache, kwa ajili ya kuwanyanyua hawa wanawake waende kwa kasi zaidi, lakini kama vile haitoshi Dkt. Samia Suluhu Hassan akaona hapana, isiwe kesi, ninatengeneza Mfuko mwingine wa wafanyabiashara ndogondogo ambao unahusisha mtu mmoja-mmoja na wala siyo kikundi, wanawake na wanaume. Takwimu zilizoko hapo za Machi, zilikuwa ni kama shilingi milioni mia moja na kitu zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi kwenye eneo hili, *record* inasema tayari wafanyabiashara ndogondogo 601 wameshapata mkopo wenye thamani ya shilingi bilioni 1.1, lakini kuna maombi 2,092 yanaendelea kuchakatwa yenye thamani ya shilingi bilioni 3.5. Leo tumeomba shilingi bilioni 12, wakitupitishia ina maana Mwaka wa Fedha unaoanza Julai, wanaume wafanyabiashara ndogondogo kumekucha kuchere, nawakaribisha waje wajisajili, wabebe fedha, Wizara yao imewakumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ni mengi, lakini nimeyapokea, tutayaandika na tayari yameshaandikwa hapa, tutayahariri na kuyawasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache sana, ninaomba kutoa hoja, tupitishiwe bajeti yetu tukatekeleze.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa, imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante. *(Makofi)*

Katibu.

**27 MEI, 2025**

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 4,516,293,405
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 941,735,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...................Sh. 1,411,233,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.................................Sh. 718,604,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*........................................................Sh. 414,657,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*........Sh. 638,589,000
Kifungu 1007 – *ICT Unit*....................................................Sh. 588,189,000
Kifungu 1008 – *Legal Service Unit*................................Sh. 588,017,981
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 490,489,000
Kifungu 2001 – *Community Development Institutes*..........................................Sh. 15,613,737,000
Kifungu 2002 – *Community Development*................Sh. 1,812,158,000
Kifungu 3001 – *Gender Development*......................Sh. 1,738,516,000
Kifungu 3002 – *Children Development*.....................Sh. 1,256,618,000
Kifungu 3003 – *Special Groups*...................................Sh. 1,761,482,000
Kifungu 4001 – *Non-Government Organizations*.....Sh. 2,982,859,614
Kifungu 5001 – *Social Welfare Division*....................Sh. 13,642,519,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**27 MEI, 2025**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...................Sh. 7,731,456,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*............Sh. 90,000,000
Kifungu 2001 – *Community Development Institutes*...........................................Sh. 1,200,000,000
Kifungu 3001 – *Gender Development*......................Sh. 1,920,000,000
Kifungu 3002 – *Children Development*.....................Sh. 2,500,000,000
Kifungu 3003 – *Special Groups*................................Sh. 10,500,000,000
Kifungu 5001 – *Social Welfare Division*......................Sh. 3,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yako imemaliza kazi.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninaomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako likikaa, kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi, ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji; kwamba, Bunge Sasa likubali Kupokea, Kujadili na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wenu, Katibu Mkuu na Wataalam hongereni sana. Bajeti yenu imepita vizuri sana na mkatekeleze maelekezo mliyopewa na Mheshimiwa Rais. Wizara hii mna majukumu makubwa sana na nchi inawategemea ninyi.

Nimeona michango ya Wabunge mingi sana kuilaumu Serikali kwenye maeneo ya malezi; malezi hasa ni jukumu la mzazi, Serikali inaweka tu urataribu wa kisheria. Huwezi kuilaumu Serikali wakati wewe mwenyewe mwanao wa miaka 12 unamnunulia *iPhone* ya shilingi 4,000,000 akajioneshe shule na wala haina *parental guidance* au *control,* kwenye simu, anafanya anachokitaka. Kwa hiyo, Serikali isipewe lawama, lawama ni zetu sisi wazazi wenyewe.

Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na wananchi, wazazi, wake kwa wanaume, tulinde maadili ya watoto wetu, ili wawe viongozi bora kwenye Taifa letu la kesho.

Mheshimiwa Waziri, bado kuna maadili ya ulevi holela mitaani, ni kazi Serikali, lakini vilevile kazi ya ninyi, mkazie. Kwa sababu, pombe hizi, visungura vinauzwa sasa hivi maeneo ya hovyo hovyo tu mitaani, hazina *control* wala nidhamu. Vijana wakianza kulewa nguvu kazi ya Taifa itapotea. Waheshimiwa Wabunge, niwaombe sana, tushirikiane katika kutetea mambo haya na kuliweka Taifa letu katika maadili mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.02 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 28 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*